

# *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

BUNGE LA TANZANIA

-----  
MAJADILIANO YA BUNGE

-----  
MKUTANO WA KUMI NA TATU

Kikao cha Tano - Tarehe 4 Novemba, 2013

(Mkutano Ulianaza Saa Tatatu Asubuhi)

D U A

*Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali, tunaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu, atakayeuliza swali la kwanza ni Mheshimiwa Gaudence Kayombo, kwa niaba yake naona Mheshimiwa Mwambalaswa unaweza kumwulizia!

Na. 53

**Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbinga Kuwa Mamlaka Kamili**

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA (K.n.y. MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO)** aliuza:-

Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbinga umekamilisha vigezo vyote kuwa Mamlaka kamili ya Mji:-

Je, ni lini Serikali itaridhia na kutekeleza ahadi hiyo ya Mheshimiwa Rais?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Gaudence C. Kayombo, Mbunge wa Mbinga Mashariki, kama ifuatavyo:-

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI)]*

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, mwaka 2010, Mheshimiwa Rais, aliahidi kupandisha hadhi Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbinga kuwa Halmashauri ya Mji. Ahadi hii ilitokana na ukweli kwamba, Mamlaka hii imeonekana kukua kwa kasi, kwa maana ya ongezeko la watu na shughuli za kiuchumi na kijamii na hivyo Serikali inaona ipo haja ya kuipandisha hadhi ili kuingiza dhana ya Mpango Mji kwa lengo la kuzuia ukuaji holela, kuchochea ukuaji wa uchumi na kuboresha huduma za jamii.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, mchakato wa kuupandisha hadhi Mji wa Mbinga bado unaendelea na ofisi yangu bado haijapokea maombi kutoka Mkoa wa Ruvuma. Tunamwomba Mheshimiwa Mbunge, ashirikiane na Uongozi wa Mkoa ili kuharakisha mchakato wa kuupandisha hadhi Mji wa Mbinga. (*Makofii*)

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri. Pamoja na hayo nina swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbinga, inafanana kabisa na Mamlaka ya Mji Mdogo wa Makongorosi Wilayani Chunya, ambayo nayo upo katika mchakato wa kuwa Mji Mdogo kamili, kufuatana na ahadi za Mheshimiwa Rais:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha kuipa Mamlaka kamili Mamlaka ya Mji Mdogo wa Makongorosi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, kama ifuatavyo:-

Mchakato wa kufanya Mji wowote kuwa Halmashauri ya Mji au kugawanywa kwa Wilaya au Kata, kwa kiasi kikubwa kunategemea Mamlaka za Serikali za Mitaa zenyewe, Halmashauri, Mkoa pamoja na Ofisi ya Waziri Mkuu. Kwa hiyo, kwa sasa hivi sina nafasi ya kuweza

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

*[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI)]*

kusema ni lini, kwa sababu bado mchakato huo katika ngazi ya Mkoa wa Mbeya haujakamilika na kuletwa katika Ofisi yetu.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa pia katika Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo katika Tarafa ya Sasawara, Kata ya Lusewa, tuliomba Mji Mdogo Serikalini. Vigezo vyote tumeshatimiza na maombi hayo yapo katika Ofisi ya TAMISEMI:-

Je, Serikali imefikia wapi kutamka rasmi mamlaka ya Mji Mdogo Kata ya Lusewa?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Vita Kawawa, Mbunge wa Namtumbo, kama ifuatavyo:-

Napenda nimhakikishie kwamba, litakapokuwa tayari suala lake tutalishughulikia, lakini mpaka ninavyozungumza, suala linalohusu Mji wa Lusewa halijafika mezani kwangu. Kwa hiyo sina uhakika kama kweli lilishatoka katika Mkoa wake. Ninachomwomba, tukitoka tuwasiliane ili tuone na tuweze kujua limefikia wapi au limekwama wapi.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba tuendelee, kwanza miji inazidi kuongezeka. Sasa twende kwa Mheshimiwa Moses Machali, swali linalofuata.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibiwa kwa swali langu, ningependa niwafahamishe Wananchi pamoja na Waheshimiwa Wabunge, juu ya hali ya Mheshimiwa Dkt. Mvungi; ni kwamba, nimetaarifiwa na Mheshimiwa Mbatia, ambaye yuko Hospitali ya Muhimbili kuwa, anaendelea vizuri na Madaktari wanajitahidi kuweza

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. M. J. MACHALI]

kupigania afya yake. Kwa hiyo, waondoe wasiwasi, naamini atapona.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya mafupi, naomba swali langu namba 54 lipatiwe majibu. Ahsante.

Na. 54

### **Uhitaji wa Watumishi Katika Hospitali ya Wilaya ya Kasulu**

**MHE. MOSES J. MACHALI** aliuliza:-

Wastani wa Watumishi wa Afya katika Hospitali ya Wilaya ya Kasulu ni 600 lakini kwa mujibu wa Taarifa ya *DMO* watumishi waliopo sasa ni 186 ambaao ni wachache sana:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza watumishi kwenye Hospitali hiyo?

**SPIKA:** Pamoja na taarifa nzuri, lakini siyo utaratibu. Mheshimiwa Waziri wa Nchi, majibu!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Moses J. Machali, Mbunge wa Kasulu Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua upungufu wa Watumishi wa Sekta ya Afya Nchini. Hivyo basi, iliona ni vyema kuwa na mkakati maalum wa kuajiri wahitimu wote wanaomaliza Vyuo Vikuu vya Afya.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu kwa sasa ina jumla ya watumishi 359 wa kada mbalimbali za afya, wakiwemo Madaktari na Wauguzi, ambaao wanatoa huduma za afya kwenye Wilaya ya Kasulu. Hospitali ya Wilaya ina watumishi 206, Vituo vya Afya vina

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

*[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI)]*

jumla ya watumishi 52 na Zahanati zina jumla ya watumishi 101.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia umuhimu wa watumishi wa kada za afya, katika Mwaka wa Fedha wa 2012/13, Serikali ilitoa kibali cha kuajiri watumishi 41 wa Sekta ya Afya, ambapo hadi mwezi Oktoba, 2013 jumla ya watumishi 28 wa kada za afya wamesharipoti katika Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu.

Mheshimiwa Spika, Serikali inao mkakati wa kuhakikisha kuwa inadahili wanafunzi wengi katika Vyuo vya Afya pamoja na kuwalipia wanafunzi hao kupitia Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu. Aidha, Serikali huwapanga watumishi wote wa Sekta ya Afya moja kwa moja katika Halmashauri kadiri wanavyohitimu mafunzo katika vyuo. Serikali itaendelea kuajiri wataalamu mbalimbali wa kada za afya kadiri watakavyokuwa wakihitimu mafunzo na kufaulu ili kuondokana na upungufu mkubwa wa kada hiyo muhimu.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza:-

(i) Kwa kuwa katika Hospitali ya Wilaya ya Kasulu inaonekana tuna-*shortage* kubwa sana ya Madaktari hasa *Medical Doctors*, walikuwa wawili lakini wengine wamepelekwa kwenye Wilaya Mpya; na kwa kuwa madaktari walioko pale wakati mwingine wanaacha kuomba madaktari wa kutosha kutoka katika Wizara ya Afya kwa lengo la kutaka kulinda nafasi zao. Je, Serikali itakuwa tayari kutupatia Madaktari wa kutosha ikiwa kama ni ombi maalum ili kuweza kuziba pengo liliopo hivi sasa?

(ii) Katika Hospitali ya Wilaya ya Kasulu zipo changamoto nyingi kama ukosefu wa madawa wakati mwingine na hii inatokana na uzembe na vitendo vya wizi wakati mwingine; vimetokea na vingine tumeweza kudhihirisha. Wakati wa Bunge la Bajeti, niliombia *special*

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. M. J. MACHALI]

audit ya kuja kufanya ukaguzi kwenye Hospitali ya Wilaya, lakini ahadi zilitolewa kwamba, watafanya na hakuna ambacho kimefanyika mpaka leo hii, gharama za matibabu zimepandishwa. Je, Serikali itakuwa tayari kuititia Wizara ya TAMISEMI pamoja na Wizara ya Afya, kuweza kutupatia ile timu ambayo niliomba hapa Bungeni na mkaahidi kwamba mtaleta ili twende tukafanye *special audit*?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Machali, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, suala la kwanza kwamba, madaktari hawaombi madaktari wenzao kwa kulinda vyeo vyao, sidhani kwa sababu uchache ule unawaongezea wao mzigo mkubwa wa kufanya kazi. Katika hali ya kawaida, sidhani kama kuna daktari ambaye angependa afanye kazi za madaktari sita peke yake; kwa sababu bado atapokea mshahara mmoja na bado marupurupu yake yatabaki vilevile, hawezi kupokea ya madaktari ambao hawapo.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, suala la kuomba ikama siyo la madaktari wenyewe ni la Halmashauri. Napenda nikuhahakikishie kwamba, Wizara ya Afya na TAMISEMI, wote tunashiriki katika kuhakikisha kwamba, tunapeleka watumishi katika Halmashauri kwa mujibu wa ikama na kwa jinsi wanavyopatikana katika soko la ajira.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la *Special Audit*, sasa hivi ipo timu kule Kasulu ambayo inafuatilia masuala mbalimbali ya matumizi ya fedha na matumizi ya madaraka katika Mji wa Kasulu.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. M. S. KAKOSO]

Kwa kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda imegawanywa na kutoka Halmashauri ya Wilaya Nsimbo na Halmashauri ya Mji Mpya wa Mlele; na wote hao wamekuwa wakichukua wafanyakazi kutoka Halmashauri Mama ya Wilaya ya Mpanda na kufanya tatizo kuwa kubwa sana la ukosefu wa Madaktari katika Halmashauri ya Wilaya:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuleta watumishi wa kada ya afya kwenye Hospitali ya Wilaya ya Mpanda sambamba na Vituo vya Afya ambavyo kimsingi katika maeneo yote hata yaliyogawanywa bado kuna tatizo la ukosefu wa Madaktari? Serikali inaleta lini madkatari hao?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii nyongeza la Mheshimiwa Kakosi, kama ifuatavyo:-

Kuhusu suala la kupeleka Madaktari katika Halmashauri mpya na Halmashauri nyingine, napenda nimhakikishie kwamba, mara tu wahitimu wa kada ya afya watakapokuwa wamemaliza na tutakapokuwa tunapanga, maeneo mapya tutawapa kipaumbele cha pekee, kuhakikisha tunapunguza tatizo la upungufu wa watumishi.

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, nchi nzima maeneo mengi kuna matatizo ya upungufu wa Madaktari. Kuna maeneo mengi yenye vyuo, kwa mfano, Mwanza kuna Chuo cha Bugando na Bukumbi. Sasa kwa nini Serikali isitoe agizo kwa Halmashauri zote nchini zifanye jitihada binafsi za ku-partner na vile vyuo kwa mkataba ili waweze ku-train watu wengi kwa mkataba waende kufanya kazi kwenye hizi Halmashauri? Kwa nini Serikali isitoe agizo sasa Halmasahuri zote zifanye jitihada binafsi za ku-partner na hivyo vyuo kwa mkataba wapate watumishi?

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ezekiah Wenje, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyotangulia kusema kwamba, tunao mkakati wa kuhakikisha tunaondoa tatizo hilo na sasa hivi ninavyozungumza tunavyo vyuo vingi tumevianzisha na vingine tumevifufua. Sasa kusema Halmashauri tuziagize zikasomeshe, mimi nadhani kidogo itakuwa ngumu, kwa sababu tatizo siyo uwezo wa Serikali kusomesha, tatizo ni nafasi katika vyuo hivyo. Labda niziombe Halmashauri ambazo zipo jirani na maeneo hayo, kama zinao uwezo wa kutusaidia kutujengea mabweni na vyumba vyta madarasa, nadhani hilo litakuwa ni la busara na tutawawezesha Halmashaxuri hizo, zikijenga ambazo vyuo viro katika maeneo yao, tutawapa upendeleo kwa ajili ya udahili wa wanafunzi kutoka maeneo yao, ambao watamaliza na kufanya kazi katika maeneo yao.

Na. 55

### **Uwiano Katika Mpango wa Rasilimali Fedha**

**MHE. SYLVESTER M. MABUMBA** aliuliza:-

Tanzania ni moja kati ya Mataifa ambayo walijiwekea mikakati ili kutekeleza ipasavyo Malengo ya Milenia (*MDGs*); na kwa kuwa bado miaka miwili kufikia mwaka 2015:-

(a) Je, ni mikakati gani Taifa limejiwekea kuhakikisha kwamba rasilimali za Taifa zinagawiwa kwa uwiano ili kuliwezesha Taifa letu kuendelea kuwa moja?

(b) Je, baada ya 2015, Taifa linajiandaaje kuhakikisha kuwa uchumi wake unakua kwa maana ya *GDP*, na kubadilika kutoka uchumi wa sasa na kuwa Taifa lenye uchumi wa kati?

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

### **WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU) alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sylvester M. Mabumba, Mbunge wa Dole, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kuna vigezo mbalimbali vinavyotumika katika kuhakikisha kuwa, rasilimali za Taifa zinagawiwa kwa uwiano katika maeneo mbalimbali nchini. Vigezo hivyo ni pamoja na idadi ya watu, vipaumbvele vya Taifa na mazingira halisi kama vile maeneo ya pembezoni ambayo hayafikiki kwa urahisi au jamii zinazoishi kwa kahamahama kufuata malisho ya mifugo.

Mheshimiwa Spika, mgawanyo wa rasilimali za Taifa hugawanywa kwa kufuata maeneo makubwa yafuatayo:-

(i) Rasilimali zinazotengwa kwa ajili ya Miradi ya Kitaifa ambayo matokeo yake huwanufaisha Wananchi wote. Miradi ya aina hiyo ni kama vile miradi ya uzalishaji wa umeme ambao kwa kuboresha uchumi, kila mwananchi ananufaika.

(ii) Eneo lingine ni la Miradi ya Kitaifa ambayo inasaidia kuondoa vikwazo vya kiuchumi kama vile miundombinu. Aina hii ya Miradi ni kama vile reli, barabara, bandari na viwanja vya ndege. Kwa kuzingatia mazingira halisi kama vile maeneo ya pembezoni ambayo hayafikiki kwa urahisi, Miradi ya aina hii hugharimiwa Kitaifa, kwa ajili ya kukwamua maeneo husika. Miradi kama vile barabara zinazounganisha Mikoa na ujenzi wa miundombinu ya msingi inayopunguza gharama za uzalishaji na kufanya biashara, ni mifano mizuri ya Miradi hii. Aidha, Miradi hii pia huvutia uwekezaji wa sekta binafsi pamoja na kuunganisha masoko na kuwezesha Wananchi kuongeza kipato na kujajiri katika shughuli mbalimbali za uzalishaji.

(iii) Kwa upande wa Halmashauri za Wilaya, Miji na Majiji, fedha za maendeleo, zinagawanywa kwa

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU)]*

kuzingatia vigezo, kama vile idadi ya watu, ukubwa wa eneo, vifo vyta watoto chini ya miaka mitano, kiwango cha umaskini, umbali wa kupata huduma za kijamii hasa elimu, afya na maji. Vigezo hivi vinatumika kuhakikisha rasilimali za Taifa zinagawanywa siyo tu kwa uwiano mzuri, bali pia kupunguza tofauti za maendeleo baina ya maeneo husika.

(iv) Sheria na Kanuni zinazoongoza matumizi ya rasilimali za pamoja hususan ardhi, maji na misitu zinatumika kuhakikisha manufaa kwa Taifa zima na kwa namna ambayo ni endelevu.

(b) Mheshimiwa Spika, Tanzania ni miongoni mwa Mataifa 189 yaliyordhia Malengo la Maendeleo ya Milenia (*MDGs - 2015*). Majadiliano ya Kitaifa yaliyoendeshwa na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na *ESRF* mapema mwaka huu, kwa niaba ya Tume ya Mipango, yamebainisha umuhimu wa kuendelea kutekeleza *MDGs* baada ya mwaka 2015, pamoja na kutoa msukumo zaidi katika ubora wa elimu, tija katika sekta za uzalishaji, usimamizi makini wa rasilimali za nchi na kuimarisha mafanikio yaliyofikiwa katika utekelezaji wa *MDGs*. Ili kuhakikisha ukuaji wa *GDP* unaongezeka ili nchi ifikie hadhi ya nchi ya kipato cha kati mwaka 2025; Serikali itajielekeza kutekeleza Mpango Elekezi wa miaka mitano mitano kati ya miaka 15, ambao unatekelezwa kupitia mipango ya miaka mitano mitano. Lengo ni kuongeza uwekezaji katika maeneo ya kimkakati hasa miundombinu ya nishati na usafirishaji; kilimo; maendeleo ya viwanda; maendeleo ya rasilimali watu na ujuzi; na uendelezaji wa huduma za utalii, biashara na fedha.

**MHE. SYLVESTER M. MABUMBA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(i) Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri ameeleza kwamba, rasilimali zetu hugawiwa kwa kuzingatia vipaumbele vyta Kitaifa, maeneo ya pembezoni na hali za

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. S. M. MABUMBA]

kimazingira. Je, vigezo hivi vimetumikaje katika kusaidia maeneo ya Mikoa ya Lindi, Rukwa, Katavi, Shinyanga, Mwanza na Geita, ambayo kwa sasa bado inaonekana ni Mikoa ya pembezoni sana hata fursa za kimaendeleo hazionekani?

(ii) Kwa kuwa ameelezea Mheshimiwa Waziri kwamba, Malengo ya Milenia baada ya mwaka 2015, tutaendelea kutekeleza tena. Ningependa kujua kwa sasa Tanzania imefikia kiwango gani katika kutekeleza Malengo haya ya Milenia? Ahsante.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Sylvester M. Mabumba, kama ifuatavyo:-

Vipaumbele vyta Kitaifa ambavyo vimesaidia katika kukwamua maendeleo ya pembezoni na Mikoa aliyoitaja kama vile Rukwa, Kigoma, Mwanza na mahali pengine, ni kama ifuatavyo:-

Nimesema katika jibu langu la msingi kwamba, eneo ambalo linasaidia sana ni lile la miundombinu. Kwa mfano, katika Mkoa wa Rukwa, ambao kwa miaka mingi sana ulikuwa haupitiki na ingawa uzalishaji wake ni mkubwa, sasa tunawekeza katika kutengeneza barabara ambazo zitawawezesha Wananchi wa Rukwa, Kigoma na Ruvuma, kuweza kufikisha mazao yao sokoni. Kwa kweli bila kuwa na miundombinu, hata kilimo hakiwezekani kwa sababu hawawezi kufika sokoni, kwa hiyo, wanalima kwa wingi lakini hawawezi kupata maendeleo makubwa. Kwa hiyo, tumewekeza miundombinu katika maeneo hayo. Mikoa yote aliyoitaja, tunafikia kwa njia ya barabara.

Vilevile tunatengeneza reli kwenda katika Mikoa ya Kigoma, Mwanza na kadhalika. Siyo hivyo tu, lakini vilevile umeme ambao ni muhimu sana kwa ajili ya maendeleo, sasa unasambazwa katika maeneo yote. Katika mpango tulionao, tuna *grid* ambayo itaunganisha Mikoa ambayo

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU)]*

ilikuwa haijafikiwa, ikiwemo Rukwa, Kigoma, pamoja na Ruvuma. Kwa hiyo, mipango hiyo itasaidia sana kupanua uchumi katika maeneo hayo na kuwezesha uwekezaji katika maeneo hayo.

Kuhusu maeneo gani ambayo tumefanikiwa katika Milenia, kwa kweli tumefanikiwa katika maeneo mengi; kwa mfano, katika suala la kupunguza vifo vya watoto chini ya miaka mitano, kumekuwepo na maendeleo makubwa na upungufu wa vifo umekuwepo, ingawa tunapenda kuona ya kwamba, tunaendelea kupambana zaidi na jambo hili, kwa sababu hata akifa mtoto mmoja bado ni mtoto.

Yapo maeneo mengine; elimu kwa mfano, pamoja na kwamba, tuna matatizo ya kuboresha elimu kutokana na upanuzi mkubwa, lakini watoto wengi sasa wanasoma na moja ya Lengo la Milenia ilikuwa ni kuhakikisha watoto wengi wanaingia shulenii. Yapo maeneo mengi, Mheshimiwa Mabumba, nitakupa maelezo zaidi wakati wowote ukihitaji kuona kila kipengele cha Milenia tulichowea kutekeleza.

**MHE. KAIKA S. TELELE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Jirani zetu Kenya hapa kutokana na Katiba yao mpya wameanzisha Mfuko wa kusaidia maeneo ambayo yamekuwa nyuma kwa maendeleo kwa muda mrefu, wanaita *Equalization Fund*. Je, Serikali haioni kwamba ni muhimu tukaiga jambo hili kutoka kwa jirani zetu kwa sababu ni jambo la maendeleo? (*Makofii*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali moja la nyongeza kutoka kwa Mheshimiwa Mbunge wa Ngorongoro, kama ifuatavyo:-

Mimi nadhani ni jambo jema kujifunza mambo mema kutoka popote. Kwa hiyo, kama Kenya wao wameanzisha Mfuko wa namna ile, tutajifunza, tutausoma kwanza tujue makusudio yake ni nini na unakusudia kusaidia vipi. Kwa

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU)]  
hiyo, tunaweza vilevile tukajifunza kama tunavyojifunza  
katika sehemu nyingine Duniani.

**SPIKA:** Ahsante. Naomba tuendelee Wizara ya  
Katiba na Sheria.

Na. 56

### **Jengo la Mahakama ya Mwanzo Kibaha**

**MHE. SILVESTRY F. KOKA** aliuliza:-

Jengo la Mahakama ya Mwanzo kwenye  
Halmashauri ya Mji wa Kibaha ni bovu kabisa:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Jengo jipya  
la Mahakama hiyo ili liweze kutoa huduma zake sawasawa?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la  
Mheshimiwa Silvestry F. Koka, Mbunge wa Kibaha Mjini,  
kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kwamba, Jengo  
la Mahakama ya Mwanzo Kibaha Maili Moja ni bovu. Hata  
hivyo, Serikali kwa mwaka huu wa fedha imetenga fedha  
kwa ajili ya ujenzi wa Jengo la Mahakama ya Mwanzo Maili  
Moja - Kibaha. Mpaka hivi sasa taratibu za kumpata  
Mshauri Mwelekezi kwa ajili ya usimamizi wa ujenzi wa Jengo  
hilo zinakamilishwa ili kuwezesha ujenzi huo kuanza mara  
moja.

Mheshimiwa Spika, ni mpango wa Serikali kujenga  
majengo mapya katika Mahakama zote ambazo majengo  
yake ni mabovu na chakavu. Hata hivyo, kutokana na  
ufinyu wa bajeti uliopo, tutaendelea kujenga majengo ya  
Mahakama kadiri hali ya fedha itakavyoruhusu.

**SPIKA:** Ahsante, Mahakama kweli.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

**MHE. SILVESTRY F. KOKA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, lakini ninayo maswali mawili ya nyongeza.

(i) Katika Jengo la Mahakama ya Mkoa ndipo hapo vilevile Mahakama ya Wilaya inafanya shughuli zake; na jambo hili limeleta mkanganyo na kuchelewesha kesi kwa sababu vyumba vya Mahakimu kufanya kazi hii havitoshi; kwa maana sasa Mahakama ya Wilaya haina majengo, lakini vilevile samani na vitendea kazi ni duni sana. Je, Serikali ina mpango gani sasa wa kujenga Mahakama ya Wilaya na kuboresha vitendea kazi pamoja na samani katika Jengo hilo?

(ii) Kumekuwa na malalamiko sana kwa Watumishi wa Mahakama kutohana na masilahi yao mbalimbali ikiwa ni pamoja na fedha za sale, fedha kwa ajili ya nyumba (*In House Allowance*) au kulipia mapango; jambo ambalo linawafanya waishi katika maeneo ambayo ni hatarishi. Vilevile mazingira haya hufanya hata Idara ya Mahakama kwa namna moja au nyingine, kujihusisha kupokea rushwa na mambo mengine. Je, Serikali ina mpango gani kuhakikisha wanapata stahili zao ili kuboresha huduma ya Mahakama?

**SPIKA:** Ahsante na wengine ulizeni maswali kwa kifupi tafadhalii. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu!

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Silvestry F. Koka, Mbunge wa Kibaha Mjini, kama ifuatavyo:-

Kwanza kabisa, kuhusiana na ujenzi wa Jengo la Mahakama ya Wilaya ya Kibaha, napenda kumwarifu Mheshimiwa Mbunge kwamba, katika mwaka huu wa fedha, tutajenga Mahakama za Wilaya sita na Katika Mkoa wa Pwani, Mahakama ya Wilaya ya Bagamoyo ni mojawapo. Hali ya fedha ikiruhusu katika miaka inayokuja tutaangalia uwezekano wa kujenga Jengo la Mahakama

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

*[NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIAJ*

ya Wilaya ya Kibaha, lakini tunatambua changamoto walizonazo, kwa hiyo, hali ikeruhusu tutazingatia.

Kuhusiana na samani na vitendea kazi, tayari tumeshatangaza zabuni mbalimbali nchi nzima na pindi zabuni hizo zitapokamilika, basi tutanunua vifaa mbalimbali, samani na vitendea kazi kwa ajili ya Mahakama hizo.

Swali la pili kuhusiana na masilahi ya Watumishi wa Mahakama na kwamba wengi wamekuwa wakijilingiza katika vitendo vya rushwa. Kwanza kabisa, napenda kusema kwamba, rushwa ni adui wa haki. Nimekuwa nikisisitiza mara kwa mara hapa kwamba, kama kuna mtumishi katika Idara ya Mahakama, ambaye anaona hawezi kwendana na maadili ya Mhakama, basi ni vyema apishe. (*Makofi*)

Napenda kurudia tena, lakini pia niombe Waheshimiwa Wabunge mtusaidie, kupitia Sheria ya *Judicial Service Act*, Kifungu cha 40, kinaeleza kabisa kwamba, kuna Kamati mbalimbali za Maadili za kushughulikia nidhamu na maadili za Mahakimu. Kwa upande wa Mahakama za Mwanzo, Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo, nidhamu zao zinasimamiwa na DCs, lakini pia nidhamu za Mahakimu wa Wilaya na Mkoa zinasimamiwa na Wakuu wa Mikoa. Kwa hiyo, naomba na ninyi mtusaidie kufuatilia vikao hivi vya Kamati ya Maadili viweze kuketi mara kwa mara ili wale wote wanaojishughulisha na vitendo hivi vibovu, basi waweze kuchukuliwa hatua stahiki za kinidhamu.

Kuhusiana na masilahi, kwanza kabisa, katika masuala ya posho za nyumba, tayari suala hili tunalitambua na tumeshaanza kulifanyia kazi. Tumeshaanza sasa hivi kulipa Wasajili wote wa Mahakama na lengo letu ni kuhakikisha kwamba, tunalipa watumishi wote wa Mahakama. Kuhusiana na sare, vilevile tayari tumeshawaagiza Wasajili wote Wafawidhi katika ngazi za Wilaya, kuhakikisha wanatuletea orodha ili sare ziweze kupatikana hukohuko waliko.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba niilize Serikali, kwa sababu imekuwa ahadi ya muda mrefu sana ya kujenga Mahakama ya Mwanzo ya Nyamikoma iliyoko Kwimba.

*(Hapa mlilo wa simu ulisikika)*

**SPIKA:** Nimeshaagiza simu zinafungwa.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Tangu enzi za Mama Nagu, Mheshimiwa Celina Kombani, akaja *Chikawe One*, akaja *Chikawe Two*, sasa naomba tuambiwe ni lini hasa Serikali itajenga Mahakama hiyo ya Mwanzo Nyamikoma?

**SPIKA:** Nani mwenye simu azime aliko! Mheshimiwa Naibu Waziri majibu!

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ndassa, kama ifuatavyo:-

Kwanza kabisa ni kwamba, ahadi hii tunaifahamu na ni kweli imekuwa ya muda mrefu na amekuwa akitolea mfano wa Mawaziri mbalimbali ambao wamepita katika Wizara hii. Tulishajibu kwamba, hapatatokea *Chikawe Three* na wala hapatatokea *Kairuki Two* na katika mwaka huu wa fedha Mahakama hii ya Nyamikoma itajengwa.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Ukiuliza kwa kifupi, wengi itawafikia.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Kwa kuwa ahadi ya Serikali ya muda mrefu ya kujenga Mahakama Kuu Mkoa wa Singida mpaka sasa hajatekelezeka. Je, Serikali itakuwa tayari kutenga fedha katika bajeti ijayo?

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Diana Chilolo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Kwanza kabisa, napenda kutoa maelezo ya utangulizi ili ielewewe kwamba, ujenzi wa jengo lolote la Mahakama Kuu, unagharimu si chini ya takribani shilingi bilioni 6.5. Kwa hiyo, hali ya fedha itakaporuhusu, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa, tutajitahidi hali ya kifedha ikeruhusu katika Mwaka wa Fedha wa 2014/15, tutazingatia ujenzi wa Mahakama Kuu Singida.

**MHE. MCH. ISRAEL Y. NATSE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Naomba kumwuliza Mheshimiwa Waziri, Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya Karatu ilianza kujengwa kwa kasi sana, ghafla *ime-stop, kullkon;* nini kimetokea?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Natse, kama ifuatavyo:-

Kwanza kabisa, nampongeza kwa namna ambavyo anaafuatilia ujenzi wa Mahakama hii. Mimi mwenyewe nilifika na ndiye niliyehamasisha ujenzi huu wa Mahakama ya Mwanzo Karatu kupitia nguvu za Wananchi pamoja na Serikali ya Wilaya ya Karatu. Nini kimetokea; ni changamoto za hapa na pale, unajua Wananchi wakiwa wanachangia hali ya kifedha ikiwa inagotagota, ndiyo hayo yaliyotokea. Sisi pia kama Mahakama, tunaiangalia kwa karibu kuona ni kwa namna gani tunaweza kuongeza nguvu ili Mahakama hii iweze kumalizika mapema.

**MHE. MOZA A. SAIDY:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa Mahakama nyingi za Mwanzo na hata zile za Wilaya hasa katika Wilaya ya Kondoa, zipo karibu na makazi kabisa ya watu, jambo ambalo linasababisha

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. M. A. SAIDY]

ufanisi wa Mahakama kuwa ni kama kero. Je, Serikali inasemaje kuhusiana na suala hili?

**SPIKA:** Hilo swali ni geni kabisa, naomba ujibu tu!

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Moza Saidy, Mbunge wa Viti Maluum, kama ifuatavyo:-

Kwanza kabisa, azma nzima ya Serikali ni kusogezza huduma za Kimahakama karibu zaidi na Wananchi. Kwa hiyo, hatuwezi kukimbia Wananchi na kusema kwamba inaleta vurugu. Mahakama ni Mahakama, nidhamu zake zinaeleweka, kwa hiyo, nipende tu kumhakikishia kwamba, huo ndiyo utaratibu wenyewe, ni lazima ziwe karibu zaidi na Wananchi.

**SPIKA:** Ahsante. Naomba tuendelee na swali linalofuata. Mheshimiwa Rebecca Mngodo, atauliza swali hilo.

**MHE. REBECCA M. MNGODO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Wanawake wote wanaoonewa na kunyimwa haki zao hapa Tanzania, naomba sasa swali langu lipatiwe majibu.

Na. 57

## **Chama cha Mawakili Wanawake (TAWLA)**

**MHE. REBECCA M. MNGODO** aliluliza:-

Je, ni wapi Chama cha Mawakili Wanawake (TAWLA) hufanya kazi zake?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rebecca M. Mngodo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA]

Mheshimiwa Spika, Chama cha Mawakili Wanawake Tanzania (*TAWLA*), kilianza kazi zake katika Jiji la Dar es Salam, Mtaa wa Posta kwenye Jengo la Avalon. Kwa sasa Makao Makuu ya Ofisi zake yamehamishiwa kwenye Jengo la *TAWLA*, Kitalu Na. 33, Ilala Shariff Shamba, karibu na Hospitali ya Amana, Dar es Slaam. Aidha, *TAWLA* inazo Ofisi zake pia katika Jiji la Arusha, Dodoma na Tanga. Pia kwa maelezo zaidi, ningependa Mheshimiwa Mbunge afuatilie Tovuti ya *TAWLA*, [www.tawla.or.tz](http://www.tawla.or.tz).

**MHE. REBECCA M. MNGODO:** Mheshimiwa Spika, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(i) Kwa kuwa kwa maelezo ya Mheshimiwa Waziri, *TAWLA* inaendelea kufanya shughuli zake mijini hususan Dar es Salaam, Tanga, Dodoma na Arusha kuliko vijijini ambako asilimia kubwa ya wanawake wanateseka. Kwa mfano, Mama Ruth Timotheo anayeishi Msitu wa Tembo Meru, ambaye kesi yake ya kunyang'anywa ardhi kwa miaka kumi sasa hajamalizika. Je, wanawake vijijini waendelee kuteseka hadi lini?

(ii) Kwa kuwa wanawake wengi walioko Vijijini hawana elimu ya kutosha; je, pale wanapokuwa wameonewa au kunyanyasika wanawezaje kuvijua vyombo vinavyotoa msaada wa kisheria? (*Makof!*)

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Rebecca M. Mngodo, kama ifuatavyo:-

Kwanza kabisa, naomba ifahamike kwamba, *TAWLA* ni Shirika lisilokuwa la Serikali. Kwanza, hata suala hili lilivyokuja nilikuwa nacheka namtania Mheshimiwa Waziri wangu kwamba, itabidi nianze kueleza pale karibu na barabara ya vumbi, pale kwa mshona viatu ndipo ofisi zilipo. Hii ni *NGO*.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA]

Pili, kuhusiana na masuala ya elimu kwa wanawake mbalimbali wa vijiji na watu wengine wanaohitaji kujuu masuala ya kisheria, sisi kama Wizara tumejipanga, tutakuja na Sheria ya Huduma za Msaada wa Kisheria. Kama kila kitu kitaenda sawasawa, mwakani mapema sana tunatarajia kuwasilisha Sheria hii Bungeni. Lengo kubwa la Sheria hii kwa hivi sasa, masuala ya huduma ya msaada wa kisheria kuptitia kifungu cha tatu cha Sheria ya Msaada wa Kisheria kwa Masuala ya Jinai ya mwaka 1969, inatolewa tu katika makosa ya Mauaji na ya Uhaini.

Kwa hiyo, lengo letu ni kuja na Sheria hii tuangalie sasa ni kwa namna gani masuala mengine ya madai, ya mirathi, ya ardhi, pamoja na mambo mengine, ili basi wale wasiokuwa na uwezo waweze kupata huduma hii. Lengo kubwa pia ni Wizara kuangalia kwa namna gani inaratibu watoa huduma za msaada wa kisheria. Vilevile tunatarajia kuangalia ni kwa namna gani tunaweza kuwatambua rasmi sasa wasaidizi wa kisheria au *paralegals* ili waweze kufika katika sehemu zote nchini. Ahsante.

**SPIKA:** Naomba tuendelee na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundii. Mheshimiwa Catherine Magige, atauliza swali hilo!

Na. 58

### **Programu ya Kuongeza na Kuboresha Vyuo vya Ufundii**

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE** aliuliza:-

Tanzania inatekeleza Malengo ye Milenia pamoja na lengo la pili linalohusu upatikanaji wa elimu bora kwa wote na kwamba kufikia mwaka 2015 tunalazimika kupima utekelezaji wa lengo hilo ili kuona kama tunaendana na viwango vya Kimataifa:-

(a) Serikali ina mpango gani wa kuanzisha Programu Maalum hasa za ufundii kwa wanafunzi kama wale

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. C. V. MAGIGE]  
wa Kidato cha Nne waliofeli kwenye mtihani wa mwaka 2012?

(b) Je, Serikali haioni umuhimu wa kuongeza na kuboresha vyuo vya ufundi na kuweka mazingira rahisi kwa wanafunzi waliomaliza Kidato cha Nne kujiunga na vyuo hivyo?

### **NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Catherine Valentino Magige, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ilianzisha Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu Stadi (*VETA*) na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundu (*NACTE*) ili kusimamia na kudhibiti elimu ya ufundi katika ngazi mbalimbali za Elimu na Mafunzo ya Ufundu Stadi. Wanafunzi wanaojiunga na Vyuo hivi ni wale waliomaliza Elimu ya Msingi na Sekondari.

Mheshimiwa Spika, Serikali haina mpango wa kuanzisha Programu Maalum hasa za Ufundu kwa ajili ya kuwasaidia wanafunzi waliofeli kwenye Mtihani wa Kidato cha Nne mwaka mwaka 2012, bali imekuwa ikiwashauri wazazi au walezi kuwashawishi watoto wao kurudia Mtihani wa Kidato cha Nne. Kwa mwaka 2013, jumla ya watahiniwa 60,507 wa kujitegemea wamesajiliwa kufanya mtihani huo ambao unaanza leo na vijana hao 60,000 wanaendelea na mtihani. Kati ya watahiniwa hao, watahiniwa 3,578 wakiwemo wasichana 2,020 na wavulana 1,558, walifeli katika Mtihani wa Kidato cha Nne kwaka 2012, tayari wamejisajili kurudia mtihani huo unaanza leo.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa katika Vyuo vya Ufundu Stadi kuna programu za fani mbalimbali za muda mfupi na muda mrefu, ambazo wanafunzi waliomaliza Elimu ya Msingi na Sekondari wanaweza kujiunga kwa vile mafunzo yatolewayo katika Vyuo hivyo huzingatia stadi moja tu

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI]*

kama vile uashi, ufundi bomba, ushonaji, uchoraji, kilimo na mifugo. Sambamba na Vyuo vya Ufundi Stadi, kuna vyuo ambavyo vimesajiliwa na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (*NACTE*), vinavyotoa kozi mbalimbali za kuwapatia wanafunzi hao ujuzi katika fani mbalimbali za kada ya kati na kada ya juu (katika ngazi ya Cheti, Stashahada, Shahada na Shahada ya Juu) kama vile Ufamasia, Uhasibu, TEHAMA, Utalii na Ualimu. Baadhi ya Vyuo hivyo ni pamoja na Chuo cha Usimamizi wa Fedha (*IFM*), Chuo cha Elimu ya Biashara (*CBE*), Chuo cha Uhasibu (*TIA*), Chuo cha Magonjwa ya Akili Hospitali ya Mirembe, *Illembula School of Nursing, Haydom School of Nursing, Kilosa Clinical Officers Center, St. Marys Teachers' College* na *Capital Teachers' College*.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikiongeza na kuboresha Vyuo vya Ufundi na kuweka mazingira rahisi kwa wanafunzi ili waweze kupata stadi mbalimbali. Kati ya mwaka 2010 hadi 2012, Serikali kuitia *VETA*, imesajili jumla ya Vyuo vya Ufundi Stadi 75, sawa na asilimia 10.8 ya Vyuo 618 vilivyokuwepo. Aidha, katika kipindi hicho; jumla ya Vyuo 8, sawa na asilimia 3.2 ya Vyuo 248 vilivyokuwepo vilisajiliwa na Baraza la Elimu ya Ufundi (*NACTE*).

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

(i) Kwa kuwa kumekuwa na malalamiko ya muda mrefu kwamba wanaorudia mitihani wamekuwa hawatendewi haki katika usahihishaji na hivyo kupelekeea matokeo yao kuwa mabaya tofauti na wengine. Je, Serikali ina jitihada gani ya kuondoa kasoro hizi?

(ii) Kwa kuwa sasa kuna mapendekezo ya madaraja ya ufaulu; je, Serikali imeona hili ndilo suluhisho la mkanganyiko wa ufaulu uliojitekeza hapo nyuma?

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

### **NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:**

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Catherine Valentino Magige, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, nimpongeze Mheshimiwa kwa kulileta swali hili la nyongeza, hasa la malalamiko ya madaraja na hawa vijana wanaorudia. Nitoe ufanuzi kidogo; Mheshimiwa Spika, unipe dakika moja mbele ili angalau Watanzania waelewe japo tumeshaanza kutoa ufanuzi kwenye vyombo mbalimbali vya habari.

Mheshimiwa Spika, ye ye mwenyewe amesema kulikuwa kuna malalamiko na sisi baada ya kupata malalamiko hayo ndiyo maana tumekuja na majibu ya kusuluhiha malalamiko. Kwa mfano, wanafunzi hawa anaosema Mheshimiwa Mbunge, hawa wanaojitegemea, ni kweli huko nyuma *continuous assessment* zao zili kuwa hazifikiriwi na Baraza la Mitihani na hivyo walikuwa wanakosa kitu fulani; lakini kwa mwaka huu, kwa mitihani inayoanza leo, tumesema kwamba, tutachukua zile alama walipokuwa shulenii *40 to 60*. Maana yake 40 itakuwa ndiyo *continuous assessment* na mtihani wa mwisho utachukua alama 60 kama tulivyo-*calculate* kwamba kwenye *project* tutawapa alama tano, mtihani wa *form three* muhula wa kwanza alama tano na mtihani wa *form three* muhula wa mwisho alama tano na mtihani wa *mock* ambao wanasi mamiwa na wasimamizi wa nje tutawapa alama 10 na mtihani wa *form two* ambao unasi mamiwa na wasimamizi na mtihani wa kitaifa tutawapa alama 15; ili kumuwezesha mtoto anapokuwa *form one* mpaka *form four*, miaka mine, aonekane amefanya kitu fulani kule shulenii.

Ninajua Waheshimiwa Wabunge wote mmepitia Vyuo Vikuu, mtajua kabisa kwamba, *continuous assessment* hata kwenye Vyuo Vikuu ipo. Mwaka wa kwanza wanatunza zile alama zako, kwa hiyo, unakuta zinatunzwa 40 na mtihani wa mwisho una alama 60. Kwa hiyo, jambo hili tulilolifanya lisileté tena mkanganyiko bali ni katika

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI]*

kuendelea kuelimishana na Watanzania wataendelea kutuelewa.

Mheshimiwa Spika, swalii la pili, Mheshimiwa anauliza kwamba, je, kushusha haya madaraja ndiyo suluhisho la kuwaokoa vijana wanaokuwa wamefeli mitihani hasa wa mwaka 2012? Jibu ni la hasha, hatujashusha madaraja wala hatujaweka viwango tofauti na vilivyokuwa. Tumeongeza madaraja kuwatambua watoto kwamba, kulikuwa na mrundikano wa alama katika daraja moja. Kwa mfano, Baraza la Mitihani walikuwa wanatumia kwamba F inaanzia 0 – 34 lakini unakuja unajiuiliza na ukizingatia kulikuwa hakuna *continuous assessment* ambazo zinaingia pale, tofauti na Sera inavyosema kwamba kuwe na *continuous assessment* ya alama 50 kwa 50. Mtihani wa *continuous assessment* utunze alama 50 na mtihani wa mwisho alama 50, lakini sisi tumefanya *40 to 60*; sasa je, hawa wanafunzi waliokuwa wamepata alama 34 nao wamepata F?

Kwa hiyo, tumeanza kuzi-*grade* zile alama kwamba, tuweke madaraja yatofautiane kwa ngazi ya kumi kumi, lakini bado daraja la ufaulu litaendelea kuwa ni 40, maana yake 40 ndiyo ngazi ya kufaulu akipata alama C. Siyo kwamba Watanzania kama wanavyoandika kwenye mitandao na kwenye magazeti kwamba basi mwanafunzi akipata alama 19 ama 20 ndiyo amefaulu tunampeleka *form five*. Kwenye *selection* itakuja na mambo mengine, lakini katika kuyapanga madaraja tumeanza na F, tumeanza na E, tunakwenda C, B na kwenye B tumeweka na B+ ambayo hata Vyuo Vikuu ipo hiyo.

Naomba niwahakikishie Watanzania kwamba, tunafanya hivyo lakini ni katika kutoa ule mrundikano wa alama kwenye daraja moja. Labda hata hili ambalo lilikuwa limejitokeza mitaani kwamba labda tumefuta *division zero*, hatujafuta *division zero* itaendelea kuwepo. Ni mkanganyiko tu wa taarifa zilizokwuwa zimejitokeza kwamba kulikuwa na *division five*. *Division five* haipo ila kutaendelea kuwa na *division one*, *division two*, *division three*, *division four* na *division zero* kama kawaida. (*Makof!*)

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, naomba mlete Kauli ya Serikali, kwa sababu naona tunajibiwa tu. Tunaendelea na Mheshimiwa Selemmani Jafo, swali linalofuata!

Na. 59

### **Ukosefu wa Gari Idara ya Elimu Ukaguzi**

**MHE. SELEMANI S. JAFO** aliuliza:-

Idara ya Elimu Ukaguzi Wilayani Kisarawe haina gari kwa ajili ya kufanya shughuli za Ukaguzi jambo linaloshusha ari ya kufanya kazi kwa Maafisa Elimu Ukaguzi Wilayani.

Je, ni lini Serikali itaipatia gari Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe kwa ajili ya kazi za Idara ya Elimu ya Ukaguzi?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI**  
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Selemmani Saidi Jafo, Mbunge wa Kisarawe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kutoa usafiri kwa Ofisi zake za Ukaguzi wa Shule na kipaumbele ni kwa Halmashauri za Wilaya zenyet mazingira magumu kufikika kama ilivyo Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe.

Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe ilikuwa mionganoni mwa Wilaya za kwanza kabisa kupatiwa gari aina ya *Toyota Land Cruiser Hard Top*, lenye Namba za Usajili DFP 3065, lilitolewa na *UNICEF* mwaka 2006, lakini kwa bahati mbaya gari hilo liliibwa mwaka huo huo. Watuhumiwa wa tukio hilo walishaktiwa Mahakamani katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkao wa Pwani (Kibaha), (*Case No. RM/27/2007*), lakini waliachiwa huru baada ya kuonekana hawana hatia.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

**[NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI]**

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Idara ya Ukaguzi wa Shule ina jumla ya magari 112 kati ya 166 yanayohitajika katika Ofisi za Ukaguzi Kanda na Wilaya. Hivyo, kuna upungufu wa magari 54; 9 yakiwa ni kwa ajili ya Ofisi ya Ukaguzi wa Shule Kanda na 45 yakiwa ni kwa upungufu wa Ofisi za Ukaguzi wa Wilaya ikijumuisha na Wilaya ya Kisarawe.

Napenda kumhakikisha Mheshimiwa Mbunge kuwa, Wizara yangu itaendelea kununua magari ya kutosheleza kadiri fedha zitakavyopatikana na kuyasambaza katika Halmashauri ambazo hazina magari ikiwemo Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe.

**MHE. SELEMANI S. JAFO:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

(i) Pamoja na majibu ya ufanuzi ya Mheshimiwa Waziri, nilipenda kujua nini mpango wa Serikali (*time frame*), kwa sababu tuna miaka saba hatuna gari la ukaguzi pale Kisarawe; sasa nilitaka kujua kwamba nini mpango wa Serikali kuipatia Wilaya ya Kisarawe gari?

(ii) Kwa kuwa nilimwona Mheshimiwa Naibu Waziri akitembelea Wilaya mbalimbali katika suala zima la ukaguzi. Je, yupo tayari kuja Kisarawe kuhakikisha kwamba tunashirikiana kwa pamoja kuboresha elimu yetu Wilaya ya Kisarawe?

### **NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Selemani Saidi Jafo, Mbunge wa Kisarawe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli Mheshimiwa Mbunge anataka tutaje *time frame* ya lini tutapeleka gari Kisarawe, lakini tayari Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi imeshapata kibali kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu, cha kununua magari tisa, ambapo magari matatu yatapelekwa kwenye Ofisi za Kanda, hasa Kanda ya Kigoma kule Magharibi na

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

*[NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI]*

Kanda ya Kusini kule Iringa na Kanda ya Morogoro Kanda ya Kati.

Vilevile tunaо mpango wa *Global Partnership for Education (GPE)*, unaofadhiliwa na nchi wahisani mbalimbali. Idara ya Ukaguzi kwa kipindi hicho cha mwaka 2014/2015, tunatajia kupatiwa magari 36 yatakayogawiwa katika Ofisi za Ukaguzi ngazi ya Kanda na Wilaya. Hatua hiyo itawezesha Idara kukagua shule kwa ufanisi zaidi na Wilaya ya Kisarawe ndipo itakapopata gari kwa kutumia mfumo huo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swalı la pili kwamba nikatembelee Wilaya ya Kisarawe; Wilaya ya Kisarawe ni jirani na Dar es Salaam, kwa mwito wa Mheshimiwa Mbunge, Bwana Selemani Jafo, mimi nikuahidi tu kwamba, nitakuja. Vilevile nitakuja kuiona na shule ambayo wakati nikipitia swalı hili, nilikuwa naongea na Mkurugenzi wako akaniambia kwamba, umefanya juhudı kubwa kutoa milioni 36 kwenye Mfuko wako wa Jimbo umejenga Shule ya Mnegele, Kata ya Kibuta. Mimi nakupongeza sana na Waheshimiwa Wabunge na wengine tufuate mfano huu wa kutumia fedha za Mfuko wa Jimbo kuinua elimu kwenye majimbo yetu. Ahsante sana. (*Makof!*)

**MHE. HAROUB MOHAMED SHAMIS:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swalı la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu elimu ipo katika Mpango wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano na Idara hii ya Ukaguzi tunaiona kama inapwaya sana. Je, Serikali ina mpango gani wa kuiimarisha Idara hii ya Ukaguzi ili kuweza kujenga elimu bora katika nchi kwa ajili ya mpango huu ambaо tunaujadili uweze kwenda vizuri?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:**  
Mheshimiwa Spika, napenda kumjibu Mheshimiwa Haroub Shamis, swalı lake fupi la nyongeza kama ifuatavyo:-

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

### *[NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI]*

Ameitaka Wizara itoe mchanganuo wa namna gani ya kuiimarisha Idara hii ya Ukaguzi. Tunao mpango wa kuifanya Idara hii kuwa Mamlaka ili ijitegemee, iweze kupata mafungu peke yake, iweze kuimarisha Idara hii ya Ukaguzi. Kwa hiyo, nadhani ni mpango wa mwaka mmoja mpaka miwili, Idara hii itakuwa imeshakuwa mamlaka inayojitegemea.

**MHE. JOSEPHINE J. NGENZABUKE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa maeneo mengi nchini Idara ya Ukaguzi imekuwa ikipatiwa magari lakini inashindwa kuendesha magari hayo kutokana na ukosefu wa pesa na kupelekea shule nyingi nchini kutokufanyiwa ukaguzi ipasavyo na matokeo yake shule hizo kufanya vibaya. Je, ni lini sasa Serikali itamaliza tatizo hili ili Idara ya Elimu iweze kujitegemea? (*Makofii*)

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, napenda kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Josephine Genzabuke, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Kigoma, kama ifuatavyo:-

Kwanza, napenda kumhakikisha kwamba, Mkoa wake wa Kigoma ni mionganoni mwa Mikoa ambayo itapata magari ya Idara ya Ukaguzi; na kama nilivyo sema kwamba, watapata gari moja kwa ajili ya Kanda ya Kigoma; kwa hiyo, hilo hongera sana. Vilevile tutakapokuwa tunaleta gari hilo Kigoma, tutaweka na bajeti kwa ajili ya kununua mafuta ili ukaguzi wa shule Mkoa wa Kigoma uweze kufanyika.

Utakumbuka ni wiki tatu tu zimepita, mimi nilikuwa huko Kigoma kwa ziara ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, tumejifunza mambo mengi sana, tumetembea Wilaya zote za Kigoma na tumeona tabu iliyopo kwa ajili ya Idara ya Ukaguzi. Kwa hiyo, tutahakikisha kwamba, tutafanya kazi

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

*[NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI]*

kubwa kuokoa kutokana na mazingira yaliyopo kwa Mkoa wa Kigoma.

Na. 60

### **Chuo cha Maendeleo ya Wananchi**

**MHE. SAID AMOUR ARFI** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuendeleza Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Msaginya ili kiweze kutoa mafunzo ya ufundi stadi na stadi za maisha?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mbunge wa Mpanda Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Msaginya ni mionganii mwa vyuo 55 vinavyosimamiwa na Wizara yangu kwa madhumuni ya kutoa maarifa na stadi kwa Wananchi mahali chuo kilipo.

Mheshimiwa Spika, ili kutekeza azma ya Serikali ya kuhakikisha katika kila Wilaya kunakuwepo walau chuo kimoja kinachotoa mafunzo ya ufundi stadi, Serikali iliamua Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi vilivyopo katika Wilaya zisizo na Vyuo vya VETA viboreshwe ili viweze kutoa mafunzo ya ufundi stadi sanjari na mafunzo ya elimu ya Wananchi. Utekelezaji wa awamu ya kwanza ya mpango huo umehusisha vyuo 25 vya Maendeleo ya Wananchi.

Mheshimiwa Spika, wakati wa zoezi la kubaini vyuo hivi, Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Msaginya kilikuwa katika Wilaya ya Mpanda ambayo ilikuwa na Chuo cha VETA. Baada ya mgawanyo mpya wa Wilaya, Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Msaginya kipo katika Wilaya ya Mlele ambayo haina Chuo cha VETA. Hivyo, Chuo hiki

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO]*  
kimepangwa kuwemo katika awamu ya pili ya utekelezaji  
wa mpango wa maboresho wa Vyuo vya Maendeleo ya  
Wananchi.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kwa kutambua  
umuhimu wa Chuo hiki na hali halisi ya majengo na  
miundombinu iliyopo, Serikali kwa mwaka huu wa fedha  
imetenga shilingi milioni 290 kwa ajili ya ukarabati wa  
majengo ya Chuo hiki.

**MHE. SAID AMOUR ARFI:** Mheshimiwa Spika, pamoja  
na maelezo ya Mheshimiwa Waziri, nina maswali mawili ya  
nyongeza kama ifuatavyo:-

(i) Je, ni lini awamu ya pili itaanza na itachukua  
muda gani kukamilika ili Chuo hiki cha Msaginya kiweze  
kuanza kutumika?

(ii) Kwa kuwa Wizara yako ilikuwa imetenga  
fedha kwa ajili ya ukarabati kwa Mwaka huu wa Fedha  
wa 2013/14; napenda kujua ni kiasi gani cha fedha  
kimepelekwa na kazi iliyofanyika imefikia kiwango gani?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA  
WATOTO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili  
ya nyongeza ya Mheshimiwa Said Arfi, kama ifuatavyo:-

Awamu ya pili ya Maboresho ya Vyuo vya  
Maendeleo ya Wananchi, itaanza Mwaka wa Fedha wa  
2014/15. Ninapenda kukutaarifu Mheshimiwa Mbunge  
kwamba, katika Mpango wa Maendeleo ambao  
Mheshimiwa Wasira ameuwasilisha na tunaujadili,  
mojawapo ya eneo ambalo litatengewa fedha ni suala la  
kuboresha Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi kikiwemo  
Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Msaginya.

Kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Mbunge  
kwamba, wakati Mheshimiwa Wasira ana-conclude  
mjadala wake, kuhakikisha Vyuo vya Maendeleo ya

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO]  
Wananchi vinawekewa msisitizo ili itakapokuja hatua ya kutenga rasilimali fedha basi na chuo chako kiwemo.

Mheshimiwa Spika, suala la kiasi gani cha fedha kimepelekwa katika Chuo cha Msaginya, ni kwamba, hadi sasa hatujapeleka fedha, lakini nakuthibitishia kwamba, tutapeleka fedha kabla ya mwaka wa fedha kumalizika.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makof*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Ritta Kabati, utafuatiwa na Mheshimiwa Ntukamazina.

**MHE. RITTA KABATI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Kwa kuwa Serikali ilikuwa na mpango wa kikipandisha hadhi Chuo cha Maendeleo kilichopo Rungemba, Mkoa wa Iringa kutoka kutoa mafunzo ya Stashahada mpaka Shahada; je, ni lini Serikali itatimiza ahadi hiyo? (*Makof*)

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, ningependa kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Ritta Kabati, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Iringa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, bado tupo katika majadiliano ya kuhakikisha kwamba, tunapandisha hadhi ya Chuo cha Maendeleo ya Jamii cha Rungemba ili kuweza kutoa Shahada badala ya Stashahada, lakini kwa sasa hivi tumejikita katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru; na juzi Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii ilikitembelea ili kukipa hadhi ya kuwa Chuo Kikuu. Kwa hiyo, nikuthibitishie tu kwamba, hilo nalo liko ndani ya uwezo wetu.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makof*)

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

**MHE. DEOGRATIAS A. NTUKAMAZINA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa Chuo cha Maendeleo ya Wananchi (*Folk Development College*) cha Lemela Ngara kimechakaa sana kwa muda mrefu, *completely dilapidated*; je, Serikali inaweza kukifufua kikawa Chuo cha Ufundidi cha Wilaya?

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu!

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Deogratias Ntukamazina, Mbuge wa Ngara, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Ngara kipo katika Mpango wa Awamu ya Pili ya Maboresho ya Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi. Nami ninafurahi kwamba, Mheshimiwa Wasira, katika mpango wake, eneo ambalo amelisisitiza pia katika *Human Capital Development*, ni pamoja na kuboresha miundombinu na vifaa vya kujifunzia na kufundishia katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa wakati utakapokuja ku-*allocate resources*, baada ya kuitisha Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2014/2015, tuone ile *commitment* ya Mheshimiwa Wasira katika Mpango wa Maendeleo inakuwa *translated* katika fedha. Kwa hiyo, hilo ninaomba sana Waheshimiwa Wabunge mtusaidie itakapokuja sasa kujadili Bajeti.

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana.

**SPIKA:** Hakuna Mpango wa Mheshimiwa Waziri, isipokuwa kuna Mpango wa Nchi. (*Kicheko*)

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

Na. 61

### **Kukamilika kwa Mradi wa Gesi Mtwara**

**MHE. MBAROUK SALIM ALI** aliuliza:-

- (a) Je, ni lini Mradi wa Gesi Mtwara utakamilika?
- (b) Je, ni sekta zipi na kaya ngapi zitafaidika na Mradi huo utakapokamilika?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Mbarouk Salim Ali, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hivi sasa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (*TPDC*), ilimetangaza zabuni ya kumpata mshauri wa kufanya kazi ya kutathmini Athari za Mradi wa Mazingira na Jamii (*Environmental and Social Impact Assessment – ESIA*), upembuzi yakinifu (*Feasibility Study*), kusanifu miundombinu ya usambazaji wa gesi asili, pamoja na kusimamia kazi ya ujenzi wa Mradi. Kazi hii itafanyika kwa Mikoa ya Mtwara na Lindi na inatarajiwa kuchukua miezi sita baada ya kupatikana kwa mshauri.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya tathmini na upembuzi ndiyo yatakayoelekeza muda wa kuanza na kukamilika kwa Mradi wa Gesi katika Mikoa ya Mtwara na Lindi.

Mheshimiwa Spika, kama ilivyoelezwa hapo awali, Mradi wa Gesi kwa Miji ya Mtwara na Lindi hivi sasa upo katika hatua za awali za upembuzi yakinifu ili kupata mchanganuo wa idadi ya watumiaji na makisio ya awali ya mahitaji kwa sekta mbalimbali. Upembuzi huu unahusisha mchanganuo wa matumzi ya gesi asili viwandani, majumbani, katika taasisi na kwenye magari.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

**MHE. MBAROUK SALIM ALI:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Pamoja na majibu yake hayo, ninayo maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(i) Upatikanani wa gesi unaonekana kukaribia; na kwa kuwa tunahitaji kupunguza utumiaji wa mkaa ili kutunza mazingira yetu; je, kipi kianze; kutoa mafunzo kwa jamii au upembuzi yakinifu? (*Makofii*)

(ii) Inaonekana kwamba, ajira na shughuli zote za kiuchumi kwa sasa zimeelekezwa au zimewashirikisha zaidi watu kutoka nje. Je, ni lini shughuli hizo zitarudi kwa Watanzania? (*Makofii*)

**NAIBU WAZIRI WA NIASHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, utoaji wa elimu wakati wote imekuwa ndiyo shughuli ya maana na ya kwanza katika uendelezaji wa Sekta hii ya Gesi na kwamba, upembuzi yakinifu ni lazima ufanyike. Lazima pia hili nalo liende sambamba kwa sababu tunahitaji sasa kuanza kuitumia hii gesi, huku tukiendelea kuona umuhimu wa kutoa hiyo elimu kwa Wananchi. Haya yote ni muhimu kwa sababu matokeo yanahitajika haraka.

Mheshimiwa Spika, ajira zinawashirikisha wageni; ni kweli katika awamu hii ambayo sasa utealam zaidi unahitajika katika utafutaji na uchimbaji, bado sisi hatukuwa tumejenga uwezo kwa watu wetu kwa ajili ya kufanya shughuli hizo, ni wachache tu ndiyo amba wanashirikiana na hao katika *deep sea* katika utafutaji wa gesi.

Nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge kwamba, tunayo mikakati mingi tu ya kuhakikisha Wazalendo nao wanashiriki hasa tutakapoanza kuiendeleza gesi hii, ambayo kwa kiasi kikubwa bado tuko katika utafutaji na ujengaji wa miundombinu. Kwa yale maeneo ambayo

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI]

wazawa wanaweza wakafanya kazi, tutajitahidi sana katika *local content* kuhakikisha kwamba, wanapata umuhimu wa kwanza. (*Makof*)

**MHE. DAVID Z. KAFULILA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kupata nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, gesi ni sehemu kubwa sana ya uchumi na mwaka 2011 nikiwa Uholanzi, Kampuni ya *Shell*, ilionesha kwamba, ilishafanya utafiti wa uchumi wa Tanzania katika Sekta ya Gesi, *impact* ya gesi kwenye Uchumi wa Tanzania mpaka kufikia mwaka 2030. Ninaomba kujua Serikali hii imekwishakufanya utafiti wa mchango wa Sekta ya Gesi utaongeza Pato la Taifa kwa kiasi gani kufikia mwaka 2025 kama Dira ya Taifa? (*Makof*)

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa David Z. Kafulila, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri na lipo wazi kabisa kwamba, gesi itakuza uchumi wetu kwa kiasi kikubwa sana. Ni dhahiri kwamba, maeneo yatakayokuzwa zaidi, kwanza, upatikanaji wa nishati utasukuma kwa kiasi kikubwa maendeleo ya viwanda na mahusiano ya sekta nyingine kutokana na rasilimali hii.

Mheshimiwa Spika, kwa hesabu na kwa idadi, sina kumbukumbu nzuri, lakini kazi kubwa imefanywa na Wataalam wetu na tuna hakika *by 2030* tutakuwa na maendeleo makubwa na nchi hii itakuwa na maendeleo makubwa kama walivyo wenzetu wa Malaysia na nchi nyingine ambazo wamenufaika sana na gesi waliyoipata katika nchi zao. (*Makof*)

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaomba tuendelee na Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia.

Na. 62

### **Kuboresha Huduma ya Mawasiliano**

**MHE. ENG. ATHUMANI K. MFUTAKAMBA** aliuliza:-

Hivi sasa kumekuwa na malalamiko mahali pengi ya kukatikakatika kwa mawasiliano ya simu hasa ya *Tigo* ambayo ni moja ya wazabuni walioshinda kutoa huduma vijiji katika Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (*UCAF*):-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwaelekeza *Tigo* kuboresha huduma zao?

(b) Je, Serikali haiwezi kuweka utaratibu utakaowezesha kampuni za simu za mkononi kupokea mawasiliano kuititia mnara mmoja na kwa kufanya hivyo mawasiliano yaweze kupatikana huko Loya na Lutende Jimboni Igalula?

**WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Eng. Athuman R. Mfutakamba, Mbunge wa Igalula, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kumekuwepo na malalamiko kutoka kwa wateja kuhusu huduma isiyordihisha kutoka kwenye baadhi ya Kampuni za Simu. Katika kushughulikia suala hilo, Serikali kuititia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (*TCRA*), ilikwishaziagiza kampuni zote za simu ikiwemo Kampuni ya *Tigo*, kuboresha huduma zao kwa Wananchi na itaendelea kukumbusha utekelezaji wa agizo hilo. Aidha, utoaji wa huduma bora ni miongoni mwa masharti ya kisheria kuhusiana na leseni walizopewa watoa

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

*[WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA]*

huduma za mawasiliano na Serikali kuitia *TCRA* na zipo adhabu mbalimbali kwa kampuni zinapokiuka sheria hiyo.

Ili kuondoa utata katika taarifa za Kampuni za Simu zinazoonekana kuridhisha kinyume na malalamiko ya Wananchi, Serikali imefanya jitihada za kusimika mtambo wa *Telecom Traffic Monitoring System (TTMS)*, katika Ofisi za Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania. Pamoja na kusaidia uhakiki wa mapato, mtambo huo utaweza kupima viwango halisi vya ubora vinavyotolewa na watoa huduma ili hatimaye hatua za kisheria ziweze kuchukuliwa dhidi ya watakaoshindwa kutimiza viwango vilivyowekwa.

Mheshimiwa Spika, Bugne lako Tukufu lilitunga Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (*EPOCA*) mwaka 2010, ambayo imeweka utaratibu kuitia Kanuni za Miundombinu kwa Kampuni za Simu kuchangia miundombinu ikiwemo minara. Aidha, Kampuni za Simu zinaelewa umuhimu na manufaa ya kutumia mnara mmoja (*Infrastructure Sharing*), katika kusambaza huduma za mawasiliano kwa lengo la kuongeza tija kwa kampuni husika kulingana na matakwa ya Sheria ya *EPOCA* ya mwaka 2010 na Kanuni zake za mwaka 2011. Hata hivyo, ni vyema ikafahamika kwamba, minara ina ukomo wa kubeba vifaa vya mawasiliano (*Transmission Equipment*), ambazo ukizidi una madhara ikiwemo kuhatarisha usalama wa Wananchi na wakazi wa maeneo husika. Kabla ya kuchangia, kampuni husika hufanya tathmini ya kitaalam juu ya uwezo wa minara ili kuepuka athari hasi katika maeneo husika. Serikali inaendelea kuhamasisha Kampuni za Simu kutumia miundombiu ya mawasiliano ikiwemo minara ya simu kwa kushirikiana. Kwa kufanya hivyo, gharama za uendeshaji zitashuka na hivyo kuleta tija kwa makampuni ya simu na watumiaji wa huduma za mawasiliano kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuzingatia ushauri wa kutumia mnara mmoja kupeleka mawasiliano kwenye maeneo mbalimbali ya nchi, Serikali kuitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote, imeyajumuisha maeneo hayo ya Loya na Lutende huko Igalula katika ujenzi wa miundombinu

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA]*

ya mawasiliano katika awamu ya kwanza (*WB Phase 1*), unaotekelezwa kupitia Fedha za Benki ya Dunia, ambapo utekelezaji wa Mradi huo unaendelea kupitia kwa Kampuni ya Simu ya *MIC (T) Ltd. (Tigo)*. Jumla ya Dola za Kimarekani 372, sawa na shilingi za Kitanzania milioni 626.4 zimetengwa kwa ajili ya kupeleka mawasiliano katika Kata hizo.

**MHE. ENG. ATHUMANI R. MFUTAKAMBA:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri. Ninaomba kuiliza maswali mawili madogo ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(i) Wananchi wa Lutende na Loya, wanataka wajue tarehe ambayo Kampuni ya *MIC Tanzania Limited (Tigo)*, itaanza ujenzi wa minara hii ili wafanye sherehe ya uzinduzi?

(ii) Sasa hivi unapopiga simu hasa kwenda nchi za nje kutafuta Wawekezaji kuja Igulula hata kama mawasiliano hayakuunganishwa unakatwa shilingi 548 wakati wewe hukuongeza na wakati huo huo *Voda nayo* hata hailipi pango kule Goweiko; hii inakuwaje? Ninaomba majibu. (*Makofii*)

**WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, katika utaratibu wa kupeleka miundombinu ya mawasiliano katika Kata hizo mbili, kazi imeanza na mwishoni mwa mwezi huu kazi ya kuweka minara kwenye Kata hiyo itakuwa imekamilika.

Kunako mwanzoni mwa mwezi Januari, 2014 vifaa vya mawasiliano, *Transmission Equipment* vitakuwa vimekamilika na minara hiyo itaanza kuwashwa mwishoni mwa mwezi Januari, 2014 na Wananchi watapata huduma hiyo ifikapo mwishoni mwa mwezi Januari, 2014.

Swali la pili kuhusu kukatwa pesa kabla hujampata mtu unayemtafuta huko nje; kiutaratibu unatakiwa zikatwe pesa zako baada ya kupata *answer buzz signals* au sauti ya yule mtu unayemtafuta. Sasa kama unakatwa kabla

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

*[WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA]*

ya kupata hiyo sauti, hilo ni kosa. Ninaomba Mheshimiwa uwasiliane na Kampuni ya Simu, kama Makampuni ya Simu yatahindwa kurejesha hela yako, tafadhalii uwasiliane na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania, kama Mdhibiti na yeze atalishughulikia suala hilo.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ninaomba utulivu sijui kuna vurugu gani humu ndani.

**MHE. AGRIPINA Z. BUYOGERA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na ahadi ya muda mrefu ya kujenga Minara ya Simu katika vijiji vya mpakani. Ninataka kujua ni lini Vijihi vya Kitanga na Herushingo minara hiyo itakamilishwa?

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kumjibu Mheshimiwa Mbunge, swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Ni kweli kumekuwa na ahadi muda mrefu, lakini kwanza tuelewe uwekaji wa mawasiliano hasa mitambo inachukua muda mrefu, karibu miezi mitatu mpaka miezi sita. Sasa hivi tunatekeleza awamu wa kwanza ambayo inaendelea vizuri. Tunaamini itakapofika mwakani, kuanzia mwezi Januari, 2014 awamu ya kwanza yote itakuwa imekamilika. Sasa hivi tuna awamu ya pili ambayo *Tender* tumeshaitangaza na tunafungua wiki hii, ambapo baadhi ya vijiji vyako Mheshimiwa Mbunge vitakuwemo kwenye awamu hii.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda tulionao umekaa vibaya sana. Tunaendelea na swali linalofuata.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

Na. 63

### **Mamlaka Zinazosimamia Vivutio Vya Utalii**

**MHE. REBECCA M. MNGODO (K.n.y. MHE. JOSHUA S. NASSARI)** aliuliza:-

Njia mojawapo ya kuinua Utalii endelevu ni kujenga mahusiano mazuri kati ya Mamlaka zinazosimamia vivutio vya utalii na wananchi wa maeneo husika:-

(a) Je, ni jitihada gani zimefanywa ili kujenga mahusiano mazuri kati ya Wananchi wa Kata za Songoro, Maji ya Chai, Leguruki na Ngarenanyuki ambazo zimepakana na Hifadhi ya Wanyamapori ya Arusha na Mlima Meru?

(b) Je, ni hatua gani zilizochukuliwa kutatua migogoro ya muda mrefu kati ya Hifadhi ya Taifa Arusha na Wananchi wa Kata za Leguruki na Ngarenanyuki?

### **NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Joshua Samwel Nassari, Mbunge wa Arumeru Mashariki, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Hifadhi ya Taifa Arusha, inajenga mahusiano mazuri na Wananchi waishio katika Kata za Songoro, Maji ya Chai, Leguruki na Ngarenanyuki, ambazo ni miongoni mwa Kata zinazopakana na Hifadhi ya Taifa Arusha, kwa kutoa elimu ya uhifadhi na utunzaji wa mazingira kuititia ziara za kimafunzo, kutoa huduma za kijamii kama matibabu bure kwa Wananchi katika Zahanati iliyopo pale katika Hifadhi; usambazaji wa maji kwa ajili ya matumizi ya nyumbani na mashambani. Kwa mfano, Mto Ngarenanyuki, bomba la maji la Nkwasenga, bomba la maji la Songoro, Ngongongare, Ngurdoto na Kilinga na kuchangia Miradi mbalimbali inayoibuliwa na Wananchi. Katika kipindi cha kuanzia Mwaka wa Fedha wa 1996/97 hadi 2011/12, Hifadhi

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

*[NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII]*  
imechangia Miradi ya Maendeleo yenye thamani ya shilingi  
189,489,399.

Mheshimiwa Spika, hatua zilizochukuliwa na Hifadhi ya Taifa ya Arusha katika kujaribu kutatua migogoro katika Kata ya Ngarenanyuki ni pamoja na kufanya vikao mbalimbali na Kata na Vijiji vinavyohusika ili kuwaelewesha Wananchi ambapo mpaka kati ya hifadhi ya kijiji husika unakopita; kuweka alama za kudumu ambazo zinajulikana kama (*beacons*) hasa katika maeneo yasiyokuwa na alama za kudumu; kuhamasisha Jamii kuhusu umuhimu wa Hifadhi hiyo; kuchangia Miradi mbalimbali ya Jamii kama ujenzi wa madarasa ya shule za msingi, nyumba za Walimu, nyumba za waganga, samani za ofisi ya Kata, kutoa ajira ndogo ndogo zisizo za kiutaalam kwa Wanajamii wanaozunguka Hifadhi na vilevile kutoa ajira za kudumu kwa wale ambao wana uujuzi.

**MHE. REBECCA M. MNGODO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa mojawapo ya migogoro ya muda mrefu katika Wilaya ya Arumeru Mashariki kati ya Hifadhi na Wananchi wanaoishi katika Kata za Reguruki na Ngarenanyuki ni pale Wanawake wanapoingia katika msitu wa Hifadhi zillizopo karibu na Mlima Meru kuchanja kuni. Baadhi yao wanaposhikiliwa na Maaskari kwa muda na matukio ya kubakwa yametokea. Je, Serikali inalijua hilo na nini tamko lake kwa Maaskari hao wanaofanya vitendo hivyo viovu? (*Makof!*)

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rebecca Mngodo, kwa ufupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni marufuku kwa Askari ye yeyote wa Wanyamaporu kupiga Wananchi na ni marufuku kubaka, ni kinyume cha sheria. Wale ambao kwa sababu yoyote ile katika kutekeleza na katika kusimamia sheria ya halali

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII]*

ambayo tumeiweka kwa kutunza Hifadhi na kusimamia maeneo ya uhifadhi, endapo watajihusisha na vitendo vyatuvunja sheria ya nchi, sisi wenyewe tuko tayari kuwachukulia hatua.

Tumeendelea kuwakamata Maaskari ambao siyo waadilifu na ninaomba nilihakikishie Bunge lako Tukufu kwamba, Askari yeote ambaye atavunja maadili yaliyowekwa na Serikali katika kutekeleza kazi yake, tutamkamata, tutamwondo kazini na tutamfungulia mashtaka kisheria.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante na mimi kunipatia fursa ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa sasa hivi tunaanza kuona hali ngumu ya Wanyamaporini na Vivutio vikubwa vyatuvunja Wanyamaporini ni Tembo, Simba na Chui, lakini wenzetu kutoka Asia hasa China, wameingia katika zoezi gumu la kuhakikisha wanyama wetu wanatoweka. Nitatoa mfano; tulikwenda katika Katavi, Wachina wamekutwa wamechukua lori zima la Meno ya Ndovu na wakaachiwa. Hata jana tarehe 4 Novemba, 2013, uthibitisho tena Mchina amekutwa na Meno ya Ndovu 700, sawa sawa na kuuwa Ndovu 350.

Je, Serikali inatoa tamko gani kwa wenzetu kutoka Asia, kuwa wanatuletea fujo na kuhakikisha Utalii wa Tanzania unakufa? Je, Waziri anatoa tamko gani ndani ya Bunge hili ili Watanzania tuwe na faraja na hao wenzetu kutoka Asia? (*Makofii*)

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Riziki Lulida, kama ifuatavyo:-

Tuna tatizo kama nchi na suala kubwa sana la ujangili linaloendelea. Ninakubaliana sana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, kuna raia wa nchi za kigeni ambao tumewatia nguvuni na wengine tumewatia nguvuni hivi karibuni, kwa jitihada zinazotokana na mafanikio ya

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

*[NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII]*

operation ambayo imekuwa ikiendelea na kwa ushirikishwaji wa Wananchi, Maaskari wetu wa Wanyamapori na Vyombo vingine vya ULinzi na Usalama, kuhakikisha kwamba, hali hii ya kupotea kwa wanyamapori inatokomezwa.

Ninaomba niseme kwamba, zoezi hili ni gumu, zoezi hili linapaswa kuwa endelevu na zoezi hili Serikali haitaliachaa, kwa namna moja au nyingine, tunajipanga upya. Ningombaa nitoe wito kwa Wabunge na Wananchi wote kwa ujumla kwamba, tushirikiane katika kuhakikisha wanyamapori wa Tanzania watalindwa hasa kwa suala la kutoa taarifa ambazo zinasaidia sana kukamatwa wahalifu. Pia nitoe onyo kwa watu wanaodhani kwamba, nchi hii wanaweza kuja kama wageni, halafu wakajiingiza katika shughuli za kuvunja sheria zetu. Hatua ambazo tutazichukua ni kutomfumbia macho mtu ye yeyote aliyetoka katika Taifa lolote Duniani.

**SPIKA:** Ahsante, tunaomba tuendelee na swalii linalofuata, Mheshimiwa Mariam Nasoro Kisangi.

Na. 64

### **Msitu wa Mwandege, Vikindu na Mlamleni**

**MHE. MARIAM N. KISAGI** aliuliza:

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa Msitu uliopo Mwandege, Vikindu na Mlamleni kutokana na kukua kwa Jiji la Dar es Salaam na Mji mdogo wa Mkuranga?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kurudisha msitu huo katika Halmashauri za Mkuranga na Temeke na kubadilisha matumizi yake ili utumike kihalali kuliko sasa ambapo kuna ujenzi unaofanyika kinyemela?

(c) Je, Serikali inapata faida gani za ziada katika msitu huu zaidi ya uhifadhi wa mazingira?

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

### **NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Mariam Nasoro Kisangi, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c), kwa pamoja kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Spika, kuptitia Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania inasimamia uendelezaji wa msitu na imefanya na kuboresha yafuatayo:-

- Imepima na kusafisha mipaka na kuweka mabango ya kutambulisha eneo hili la msitu.
- Imeanzisha bustani ya miti au mimea (*botanical gardens*) ambayo itahifadhi uoto wa asili wa maeneo ya Pwani na uhifadhi wa viumbi hai.
- Imeongeza watumishi na vitendea kazi kwa ajili ya kulinda na kuhifadhi Msitu huo.
- Ujenzi wa Ofisi umeshaanza kwa ajili ya kuanzisha utalii ikolojia na ipo katika maandalizi ya kupanda miti katika mipaka na maeneo ya wazi ili kuboresha uoto huo wa asili.
- Wakala imetenga maeneo mazuri kwa ajili ya ufugaji wa nyuki na kuchimba mabwawa ya samaki.

Kutokana na juhudii zinazofanywa na Wakala, Serikali haioni umuhimu wa kuzikabidhi Wilaya za Mkuranga na Temeke na kubadilisha matumizi ya Msitu huu. Hii ni kwa sababu mpango uliotajwa hapo juu unaonesha nia njema ya Serikali ya kutumia msitu kwa matumizi halali na kwamba, Serikali itawaondoa watu wote wanaofanya ujenzi wa kinyemela ndani ya Msitu huo wa Hifadhi.

Mheshimiwa Spika, faida za ziada ambazo Serikali inapata katika Msitu huu ni zaidi ya uhifadhi wa mazingira kama ifuatavyo:-

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

### *[NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII]*

- Eneo la mafunzo ya uhifadhi na utalii ikolojia; kwa mfano, hivi karibuni aliyekuwa Kamanda wa Skauti Tanzania, Mheshimiwa Abdulkarim Shah, Mbunge wa Mafia, aliomba kushirikiana na Wakala wa Huduma za Misitu ili waweze kutumia msitu huo kwa mafunzo ya Wanaskauti Tanzania na sisi tupo tayari kushirikiana na wanaskauti nchini.

- Kuanzisha utalii ikolojia ambao utawashirikisha Wananchi wanaoishi karibu na msitu kwa lengo la kuwanufaisha kiuchumi.

- Katika mkakati wa ushirikishwaji, umetengwa Ukanda wa Ufugaji Nyuki ndani ya Hifadhi hiyo kwa ajili ya shughuli za ufugaji wa nyuki na uzalishaji wa makundi ya nyuki na pia kuchimba mabwawa ya samaki kwa manufaa ya Wananchi wanaouzunguka Msitu huo.

- Kuanzisha bustani ya miti au mimea (*botanical garden*) kwa ajili ya kutunza mimea yu miti hai ya Ukanda wa Pwani kwa ajili ya utafiti wa mafunzo.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ambayo nimeridhika nayo na nimeona ukweli aliyyoyasema yanaendelea kutendeka katika eneo hilo, lakini pia nina maswali mawili ya nyongeza.

(i) Kwa kuwa Serikali imeonesha juhudini kubwa ya kuendeleza msitu huo na kazi inaendelea na ninaomba iwe endelevu. Je, Serikali haioni sasa kuna haja ya kuanzisha makumbusho ya viumbe hai ili kusaidia Wanafunzi waweze kujifunzia na Walimu waweze kufundishia kuititia makumbusho hiyo?

(ii) Kwa kuwa walinzi wakuu wa Hifadhi hiyo ya Misitu ni Wakazi wa maeneo ya Mwandege, Vikindu, Churi,

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. M. N. KISANGI]

Mbagala na Mkuranga kwa ujumla. Je, Serikali inawasaidia vipi Wananchi wa eneo hili katika kukabiliana na changamoto zinazowakabili?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba ujibu kwa kifupi sina muda.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu kwa ufupi sana maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mariam Kisangi, kama ifuatavyo:-

Kwanza, tunamshukuru sana na tunampongeza kwa pongezi ambazo amezitoa, lakini nimhakikishie kwamba, ushauri alioutoa kuhusu makumbusho na mambo ambayo yanaweza yakasaidia Wanajamii na hasa Wanafunzi kuendelea kujifunza ni ushauri ambao naupokea.

La pili, jinsi ambavyo tunategemea Wananchi waendelee kufaidi ikiwa ni pamoja na wale ambao wanashiriki katika kuulinda Msitu huu na kuutunza ni kama nilivyosema awali kwamba, tunawaruhusu kwa mfano Wananchi kushiriki kuweka mizinga ndani ya hifadhi, tunachimba mabwawa ndani ya hifadhi, ambayo tunaamini yatatumika kama mabwawa ya kutunzia samaki ambao watawafaidisha Wananchi walio nje ya hifadhi hii na ninaamini hii ni sehemu ya ushirikishwaji wa jamii ambao ni endelevu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mchungaji Msigwa, swali fupi!

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa kuwa changamoto hizi za misitu ambayo ipo karibu na miji zimeleta shida kidogo kwa wakazi wa mijini. Changamoto hii inafanana na Manispaa ya Iringa ambayo kuna kitu kinadharia kinaitwa Msitu wa Kilolo, ambao kimsingi haupo. Kwa nini Wizara yako imeendelea kusucasua kuruhusu programu za Manispaa ya Iringa ziendelee kufanya kazi katika eneo hili ambalo msitu kimsingi haupo?

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba ujibu kwa kifupi!

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naomba njibuu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Mchungaji Msigwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tumelipokea hili suala la Msitu wa Kilolo, Wizara yangu kupitia kwa Halmashauri husika, kupitia kwa Mheshimiwa Msigwa na kupitia kwa Wadau wengine wa Iringa, wamelielezea sana hili suala. Ninaomba nimhakikishie tu Mheshimiwa Msigwa kwamba, tunaendelea kulifanyia kazi hili suala ili tufikie uamuzi ambao ni mwafaka.

Na. 65

### **Maoni ya Wananchi wa Kiloleni kwa Wizara ya Maliasili na Utalii**

**MHE. SAID J. NKUMBA** aliuliza:-

Wakazi wa Kata ya Kiloleni wamekuwa wakilalamika kuwa na eneo dogo la kilimo na eneo kwa ajili ya mifugo:

Je, ni lini maombi ya Wananchi hawa kwa Wizara ya Maliasli na Utalii yatazingatiwa?

### **NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Said Juma Nkumba, Mbunge wa Sikonge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua Kata ya Kiloleni kuwepo katika Wilaya ya Sikonge, Mkao wa Tabora, ambayo upande wa Mashariki inapakana na Msitu wa Hifadhi wa Nyahua Mbuga ambayo upande wa Kusini inapakana na Msitu wa Hifadhi wa Ipembampazi.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII]*

Msitu wa Hifadhi wa Nyahua Mbuga una ukubwa wa Hekta 679,896 na uliohifadhiwa na Tangazo la Serikali GN. No. 79 la tarehe 26 Machi, 1954 kwa ramani ya JB 175. Msitu huu unasimamiwa na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (*TFS*) na usimamizi wa kazi za kila siku hufanywa na Wataalamu wa Misitu waliopo katika Wilaya ya Sikonge.

Msitu wa Hifadhi wa Ipembampazi una ukubwa wa hekta 134,680.0 na ilitangazwa kwa Tangazo la Serikali GN. 345 ya tarehe 23 Machi, 1955 kwa Ramani Namba JB 179. Pia msitu wa Ipembampazi unapakana na Msitu wa Sikonge, ambao ni mali ya Wilaya na unasimamiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge.

Mheshimiwa Spika, umuhimu wa misitu hii ni moja, vyanzo vya maji vya Mito Nkwazi, Malingwe na Chona kutoka Msitu wa Nyahua Mbuga hadi maeneo ya tambarare ya Wilaya ya Igunga na Singida. Msitu wa Ipembampazi ni chanzo cha Mto Uruwa na ni hifadhi ya maji yanayotumiwa na wakazi wengi na mifugo katika Wilaya ya Sikonge. Msitu wa Sikonge ni chanzo cha maji ya mabwawa yaliyochimbwa Ulyanyana na Igigwa, kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji na maji ya Mji wa Sikonge.

Maeneo ya Msitu hasa kandokando ya mito, vilima na ardhi chepechepe ni muhimu kuhifadhiwa kwa ajili ya kuhifadhi bioanuwai ya aina mbalimbali za miti na mimea, wadudu na hata wanyamapori. Misitu mingi ni mapito ya wanyama wanaohama kutoka katika Pori la Akiba la Rungwa kwenda Msitu wa Ipembampazi na Mapori ya Wembele kwenda Mapori ya Inyonga Mashariki. Pia katika Misitu hii kuna vitalu vya uwindaji wa kitalii na kienyeji. Misitu hii ni muhimu kwa uvunaji wa mazao ya misitu na ni eneo nyeti kwa ufugaji wa nyuki na kuzalisha asali na nta ya miti ya miombo.

Mheshimiwa Spika, mwisho, usimamizi wa Misitu ya Hifadhi ya Mkoa wa Tabora ikiwemo hii ya Wilaya ya Sikonge, imekuwa na changamoto nydingi hasa za uvamizi ili kupisha shughuli nyagine za kibinadamu ambazo kwa kiasi

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

*[NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII]*

kikubwa, zimeathiri sana ubora na hadhi ya misitu husika. Hivyo, Wizara inatoa wito kwa Wananchi wote, kujiepusha na suala la kuomba kumega maeneo ya misitu iliyohifadhiwa kwa umuhimu wa hifadhi za maji na bioanuwai, kwa kuwa kuendelea kuharibu misitu kutasababisha janga kubwa la ugomvi wa maji kama tunavyoshuhudia baadhi ya migogoro iliyopo kati ya wafugaji na wakulima.

**MHE. SAID J. NKUMBA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali dogo moja la nyongeza.

Kwa kuwa kumekuwa na ongezeko kubwa la Wananchi katika maeneo hayo ya Mipaka ya Hifadhi na Vijiji; maana mipaka mingine imewekwa kabla ya Uhuru, lakini kwa kuwa maeneo mengi nchini yenye Mipaka ya Hifadhi na Vijiji, mengine yalishapoteza kabisa hadhi ya hifadhi na ongezeko la Wananchi kama nilivyosema. Je, ni kwa nini sasa Wizara isingekuwa na utafiti wa kina wa uhalisia katika maeneo yote nchini ambayo yanapakana na Hifadhi hasa kwenye Vijiji ili kuwahakikishia Wananchi ambao wamekaa wengine wanahangaikia ardhi na ardhi ipo ambayo imeshapoteza hadhi ya kuwa Hifadhi?

**SPIKA:** Naomba ujibu kwa kifupi sana, maana jibu lako lilikuwa refu mno!

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Nkumba, kwa ufupi kama ifuatavyo:-

Moja, tunakubaliana sana na Mheshimiwa Mbunge, kwa hoja yake ya kuwakilisha Wananchi hasa changamoto hii tunayoiona ya ufinyu wa ardhi ambayo imeyagusa maeneo mengi sana nchini.

La pili, ni maslahi mapana ya uhifadhi na masilahi mapana ambayo nchi yetu na vizazi vijavyo ni lazima vije vikute misitu hii ambayo sisi tumepewa wajibu wa kuitunza.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII]*

Ningeomba tu kusitiza kwamba; kwanza, lazima tutengeneze matumizi bora ya ardhii sehemu zote nchini ili maeneo ambayo yametengwa kama Hifadhi yaendeleee kubaki kama Hifadhi na yana faida lukuki ambazo kwa kweli sina haja hata ya kuzieleza hapa. Naomba kusema kwamba, Wizara yangu itashirikiana na Mheshimiwa Said Juma Nkumba, yeye mwenyewe, ikiwa ni pamoja na sisi kufika kuangalia haya maeneo, lakini tuhakikishe kwamba, maeneo yote ambayo yana migogoro inayofanana na hii yanapatiwa ufumbuzi endelevu.

Na. 66

### **Raia wa Kigeni Kuzagaa Maeneo ya Vijijini**

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU** aliuliza:-

- (a) Je, ni sababu zipi zinazopelekea raia wa kigeni kuzagaa hovyo katika maeneo ya vijijini na kushindania fursa kibashara na wazawa?
- (b) Je, kwa nini Serikali isiamuru raia hao kubaki katika maeneo ya miji mikuu tu?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO (K.n.y. NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Murtaza Ally Mangungu, Mbunge wa Kilwa Kaskazini, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuna sababu mbalimbali zinazowafanya raia wa kigeni kuingia nchini. Sababu hizi ni kama vile uwekezaji, wafanyakazi wa mashirika ya maendeleo na wategemezi wao (wanafamilia), wanaojitolea (*volunteers*), watalii na kadhalika.

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO]

Mheshimiwa Spika, sababu kubwa ni Sera ya Taifa ya Uwekezaji inayoruhusu mgeni kuingia nchini, kuwekeza mtaji wake katika eneo analoona atapata maendeleo ya Wananchi wake. Eneo hilo linaweza kuwa mjini au kijijiini, kutegemea ilipo fursa hiyo na ambayo huwa imetajwa na Serikali katika Mkoa husika kwa kutumia Kamati za Ushauri za Mkoa.

Mheshimiwa Spika, kwa makundi mengine ya wageni kama Wafanyakazi wa Mashirika ya Maendeleo, huombewa Vibali Maalum kutokana na shughuli wanazokwenda kufanya.

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kumwomba Mheshimiwa Mbunge na Wananchi kwa ujumla, kutoa taarifa za raia ye yeyote wa kigeni anayezagaa nchini bila kibali kwa Kamati ya Ulinzi na Usalama ili hatua stahiki za kisheria zichukuliwe dhidi yake.

Mheshimiwa Spika, Serikali hajaamuru raia wa kigeni kubaki mijini, kwa sababu Sera ya Uwekezaji iko wazi kuhusu fursa za uwekezaji zilizopo na aina ya uwekezaji unaohitajika. Hivyo, raia wa kigeni anapokidhi matakwa ya uwekezaji nchini, huwekeza ilipo fursa hiyo, iwe kijijiini au mjini, kwa kuwa nia ya Serikali ni kusambaza maendeleo na uwekezaji nchi nzima.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru.

(i) Ninapenda kujua Sera hii ya Uwekezaji imeundwaje kiasi kwamba haifanyiwi uhakiki kwa mitaji ya uwekezaji kwa wawekezaji hao kutoka nchi za nje kama mfano wa nchi zote duniani ikiwemo China, Marekani, Hong Kong na kadhalika. Imefikia hatua wafanyabiashara hao wanaoitwa wawekezaji, wameingia kwenye biashara ya uuza jibidhaa (*trading*), wamefungua maduka; huu ni uwekezaji wa aina gani? (*Makof*)

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. M. A. MANGUNGU]

(ii) Kazi ya ulinzi na usalama wa kulinda mipaka yetu ni jukumu la Vyombo vya Dola, leo hii Wananchi watawezaje kujua raia huyu wa kigani amepewa kibali cha aina gani! Hii inaonesha ni kiasia gani ambavyo Serikali sasa inataka kukwepa majukumu na kurudisha jukumu hili kwa Wananchi!

Sasa tamko la Serikali ni lini uhakiki wa wageni hao utafanywa kwa sababu sasa hivi kuna *operation* ya kuwaonda wageni *ime-base* zaidi kwa raia wa kigeni wa nchi zinazotuzunguka, hao wanaotoka mbali kwenye Mabara mengine kwa nini wanaachwa wanazagaa hovyo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI):** Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kujibu maswali vizuri sana na mimi naomba niongezee hasa kwa kujibu swalii hili la pili.

Mheshimiwa Spika, kufanya biashara siyo uwekezaji, uwekezaji ni kwenye kilimo, viwanda na maeneo mengine ya uzalishaji.

Pili, unapotaka kufanya biashara ni lazima uwe na leseni ya biashara na unapofanya mambo bila leseni ya biashara ni kosa. Kuna mamlaka zinazotoa leseni, nina hakika mamlaka hizi zinajua masharti na utaratibu wa kutoa leseni. Kwa hiyo, kama kuna wageni ambaa wanafanya biashara bila utaratibu hayo ni makosa.

La pili, uwekezaji wowote ni lazima ulete masilahi kwenye nchi ambayo inapokea wawekezaji. Inabidi tujipange vizuri, wawekezaji wanapotoka nje hata wale wa ndani, wanachotafuta ni faida kwa mtaji wanaowekeza. Vilevile nchi na Wananchi tujue sisi tunapata manufaa gani na faida gani na kwa hiyo, swalii la Mheshimiwa Mbunge ni la manufaa makubwa kwamba ni lazima tufanye kila wakati na kuona tunapata manufaa gani.

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI]

Kwa hivyo, Kituo cha Uwekezaji Taifa (*TIC*) tunakipa maelekezo kifuatilie wawekezaji wote kuona kwamba, mikataba inafuatwa na pili yale manufaa tulyokuwa tunayategemea tunayapata ili tuweze kujifunza kwa uwekezaji unaokuja na tuchukue hatua stahili kwa wawekezaji waliopo ambao hawawekezi kwa mujibu wa mkataba ambao umewekwa.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya sehemu ya kwanza.

### **NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA**

**MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Murtaza Mangungu, sehemu (a).

Kwanza nimshukuru Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Uwekezaji na Uwezeshaji kwa maelezo mazuri. Hata hivyo, niseme tu kwamba, Sera hii ya Uwekezaji imeundwa mwaka 1996 na Sheria yake ya mwaka 1997 na imeeleza kwamba, wawekezaji raia wa nje wanapitia *TIC* (*Tanzania Investment Centre*) wanapata vibali na pia wanapata Hati ya Ukaazi ya Daraja A pale wanapotimiza vigezo kupitia Kituo cha Uwekezaji (*TIC*).

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naona maswali yamekwisha na leo tuna muda mchache wa kufanya kazi zetu. Kwa hiyo naomba niwatambue wageni walioko hapa ambao ni:

Wanamichezo 50 kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi, wakiongozwa na Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Mheshimiwa Erick Minga (Diwani) pamoja na Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Allan Mgula. Naomba walipo wasimame. Ahsante sana. (*Makofii*)

Tunao pia Madiwani 20 kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Chunya, wakiongozwa na Mheshimiwa Makamu

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[SPIKAJ]

Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo anaitwa Mheshimiwa Bosco Mwanginde. Wako wapi hawa Waheshimiwa Madiwani? Ahsante, karibuni Waheshimiwa Madiwani. (*Makofii*)

Tuna wanamichezo 45 kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Kyela, eeh naomba wanamichezo kutoka Kyela wasimame kama wako ndani. Nafikiri watapata muda baadaye.

Kuna wanamichezo 32 kutoka Wilaya ya Biharamulo wakiongozwa na Afisa Utamaduni wa Wilaya, Bi. Esther Abel, wako wapi? Wanasema ni watumishi, nilidhani ni wanamichezo. Nadhani nao pia wamekosa nafasi humu ndani.

Pia tunao vijana 13 kutoka Makete wakiongozwa na Ndugu Erasto Mahenge ambaye ni Mwenyekiti wao, wako wapi hawa? Aah, ahsante. Karibuni sana. (*Makofii*)

Shughuli za kazi; Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii, Mheshimiwa Steven Ngonyani, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, leo Saa 7.00 mchana watakuwa na Kikao pale *basement*.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Uchumi, Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, leo Saa 7.00 mchana watakuwa na kikao katika Ukumbi wa Pius Msekwa 'B'.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, Mheshimiwa Dkt. Pindi Chana, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, leo Saa 7.00 mchana watakuwa na kikao katika Ukumbi Na. 231.

Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa Anna Abdallah, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba leo Saa 7.00 mchana watakuwa na kikao katika Ukumbi Na. 219.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[SPIKA]

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, Mheshimiwa Jenista Mhagama, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, leo watakuwa na kikao cha pamoja na Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) kujadili mchango wa Serikali katika Mfuko wa Akinamama na Vijana katika Serikali za Mitaa nchini, kitakachofanyika Saa 7.30 mchana katika Ukumbi wa Msekwa. Mtajua huko huko maana Msekwa ziko nyingi. (Makofi)

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu, Mheshimiwa Peter Serukamba, anaomba niwatangazie wajumbe wa Kamati yake kwamba, leo Saa 7.00 mchana watakuwa na kikao katika Ukumbi Na. 227.

Wengine hawakuchapa matangazo yao, nitayasoma kama yalivyo, lakini siku nyingine wachape.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mheshimiwa Dkt. Khamis Kigwangala, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake watakaopenda kuhudhuria kikao hiki wafike bila kukosa. Kikao kitafanyika Saa 7.00 mchana katika Ukumbi wa Msekwa baada ya kuahirisha shuguli za Bunge. Sasa hapa kuna Kamati mbili zinakutana Ukumbi wa Msekwa, kwa hiyo, muangalie mtakavyogongana na kuamua wenyewe huko huko.

Kiongozi wa Kambi ya *CUF*, Mheshimiwa Rashid Ali Abdallah, anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge wa *CUF* kwamba, watakatana leo Saa 10.00 jioni pale *basement*.

Halafu nina matangazo kutoka kwa Mwenyekiti wa Bunge *Sports Club*, Mheshimiwa Iddi Azzan, anaomba niwatangazie matokeo ya mchezo wa kirafiki uliofanyika siku ya Jumamosi wa Mpira wa Miguu na Mpira wa Pete. Kwa

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*  
[SPIKA]

upande wa Mpira wa Miguu, Bunge *Sports Club* walipata goli moja dhidi ya *Travel Ports* ambao walipata sifuri (0). Goli la mchezo huu lilifungwa na Mheshimiwa Dkt. Khamis Kigwangala na nyota wa mchezo alikuwa Sadifa Juma Khamis. (*Makofî*)

Mpira wa Pete, Bunge *Sports Club* walifunga magoli 24 dhidi ya Mahonda *Queens* kutoka Zanzibar waliopata magoli manne (4). Nyota wa mchezo alikuwa Mheshimiwa Eugen Mwaiposa. (*Makofî*)

Aidha, Waheshimiwa Wabunge mnaombwa kuhudhuria mazoezi kwa ajili ya maandalizi ya Michezo ya Mabunge ya Afrika Mashariki, yatakayofanyika mwezi Desemba nchini Uganda. Kwa hiyo, nawapongeza hawa Wachezaji nyota na wengine mshiriki kama tullvyosema, mashindano ya Afrika Mashariki yanakuwa magumu, kwa hiyo, mfanye vizuri ili safari hii mrudishe kikombe. Mwaka jana tulirudisha cha *Netball* tu, mwaka huu m jitahidi mrudishe vikombe vyote. (*Makofî*)

Baada ya kusema hayo, Mheshimiwa Said Nkumba!

**MHE. JUMA S. NKUMBA:** Mheshimiwa Spika, nimesimama kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7) inayosema: "Halikadhalika Mbunge anaweza kusimama wakati wowote ambapo hakuna Mbunge mwingine anayesema na kuomba Mwongozo wa Spika, kuhusu jambo ambalo limetokea Bungeni mapema ili Spika atoe ufanuzi kama jambo hilo linaruhusiwa au haliruhusiwi kwa mujibu wa Kanuni".

Mheshimiwa Spika, ni juzi tu Waheshimiwa Wabunge na Bunge lako Tukufu lilijadili kwa kina suala la dharura juu ya uonevu ambao wamefanyiwa wananchi wetu katika maeneo mbalimbali kuhusiana na Operesheni Tokomeza.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo jana na juzi Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Khamis Kagasheki

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. JUMA S. NKUMBA]

ameonekana akinukuliwa kwenye vyombo vya habari akisema kwamba, Wabunge wanasema sema tu ndani ya Bunge, lakini hawajali rasilimali za Taifa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, vile vile Mheshimiwa Waziri amesema kwamba hatishwi na maelezo ya Wabunge ya kumtaka ajizuzulu na ye ye hatoki mpaka maamuzi ya Rais aliye mteua. Sasa kwa kuwa ye ye mwenyewe Mheshimiwa Waziri ndiye aliye toa kauli ya kusitisha operesheni hii Tokemeza na kitendo cha kuwakamata Wachina ni zoezi tu la Serikali la kila siku ambalo linaweza likaendelea bila operesheni. (*Makof*)

Je, Mheshimiwa Waziri aliye toa kauli ndani ya Bunge na anatoka nje anabeza maamuzi ya Bunge, anakejeli Bunge, naomba Mwongozo wako kama jambo hilli linaruhusiwa. (*Makof*)

**SPIKA:** Waheshimiwa mmesimama kwa ajili ya nini?  
Hakuna, kufanyaje!

**MJUMBE FULANI:** Mwongozo!

**SPIKA:** Aah, tusiwe na Mwongozo, Mwongozo tu kila wakati.

Alichokisema Mheshimiwa Nkumba nadhani ni suala ambalo ningependa kusiwe na matumizi mabaya ya midomo, kwa sababu tukishakubaliana hapa, kwenda tena kusema vitu vingine ni kuwasho moto pale ambapo pengine ulikuwa unaendelea kuwaka vizuri. Nadhani ni matamko ambayo siyo makini. Tuendelee.

Si nimeshatoa Mwongozo. (*Makofi*)

Tuendelee Katibu!

## **HOJA ZA SERIKALI**

### **Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa kwa Mwaka 2014/2015**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunao wachangiaji wengi, lakini itabidi mjadala huu ufungwe leo. Sasa wengine watapata nafasi na wengine hawatapata. Ingependeza sana kama tusingekuwa tunajirudia rudia kwa sababu kama tukijirudia rudia Kanuni inasema ikifika mahali watu wanajirudia rudia tena ndiyo inakuwa mnafunga mjadala. Kwa hiyo, nitakuwa na wasemaji wafuatao;

Kamati ya Mipango, jamani naomba tusimame Kamati ya Mipango, nimesahau.

*(Hapa Wabunge walikaa kama Kamati ya Mipango)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba tukae. Samahani! Nilikuwa nasema leo ndiyo siku yetu ya mwisho, kwa hiyo, naomba wachangiaji wafuatao wajjandae. Nitamwita Mheshimiwa Stephen Ngonyani, Mheshimiwa Dkt. Kebwe Stephen Kebwe, Mheshimiwa Herbert Mntangi na atakuwepo Mheshimiwa Naomi Kaihula.

Tuanze na hao kwanza halafu tutaendelea. Mheshimiwa Stephen Ngonyani!

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kukushukuru sana kwa kunipa nafasi ili kuchangia huu Mpango wa Maendeleo. Nianze kwa kuipongeza Serikali kwa kazi nzuri ambayo wameshaanza kutuonesha, lakini vilevile nilikuwa na mapendekezo yangu ambayo nataka Serikali iyaone katika huu Mpango ambaa tunaujadili leo wa mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri Serikali ingemalizia mpango wa mwaka 2012/2013. Hii ingetusaidia sana kuujadili

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. S. H. NGONYANI]

Mpango wa 2014/2015 kwa sababu mambo mengi yamejadiliwa hapa, lakini hakuna hata moja ambalo limeanza kufanyiwa kazi. Kwa mfano, Mkoa wa Tanga, naona umesahaulika kabisa. Kuna bandari ya Tanga ile ya Mwambani inajadiliwa kila siku, lakini kutenda kwake inakuwa ni ngumu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna bandari ya nchi kavu pale Korogwe, alikuja Waziri kutoka Uganda akaungana hapa na Waziri wa Uchukuzi, tukaenda mpaka Korogwe, wakatupa maneno mazuri tukafikiria kwamba Serikali sasa imeamua kuwa na utendaji mzuri wa kazi. Cha kushangaza mpaka leo imekuwa kama ni hadithi, hakuna chochote kinachoendelea katika Mkoa wa Tanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tunajadili tu hapa reli ya kat, lakini ukichunguza si reli ya kat peke yake, hata reli ya Tanga - Arusha ilikuwa imeanza muda mrefu. Katika Mpango huu kuna mkakati gani wa kutengeneza hii reli? Kwa sababu reli ya Tanga – Arusha – Musoma ni muhimu sana, ndio maana barabara hizi hazidumu, zinaharibika kila wakati. Ningeishauri Serikali huu Mpango wa mwaka 2014/2015 hebu tumalize kwanza haya ambayo tumeshayaanzia kazi, ingetusaidia sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tunasema Kilimo Kwanza, hiki kilimo kwanza tunampelekea nani? Kama wananchi wa Mkoa wa Tanga hawana mahali pa kulima, hiki Kilimo Kwanza kinakwenda wapi? Tunazungumzia mashamba ambayo hayaendelezwi. Leo tunaomba Serikali mshughulikie masuala ya mashamba ambayo wananchi wengi wanataka kulima, lakini wakalime wapi, wakati wakilima huku wanapambana na wafugaji na ambao wote ni wakulima? Wakilima huku wanapambana na wenyewe mashamba, wakilima huku wanapelekwa Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipenda sana Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi, lakini hili tungelifanya kazi kwanza, kwa sababu tunayaongea hapa kila siku na tunayaachia hapa hapa, tukirudi hakuna anayekwenda

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*  
[MHE. S. H. NGONYANI]

kumuona Mbunge akihukumiwa na wananchi ambaye atawea kumsaidia, kila mmoja anabeba mzigo wake. Ili Serikali ioneckane inafanya haya mambo makubwa, ningeomba yale mambo ambayo tulikuwa tumeshayaanza yafanyiwe kazi rasmi ili wananchi waipende Serikali yao kama sasa hivi tunavyoipenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inaniuma sana, tumejadili mambo mengi sana hapa, lakini yanaishia ndani ya Bunge, hakuna chochote ambacho kinaendelea. Leo tunakwenda kujadili ya mbele wakati ya nyuma hatujayafanya? Hivi kuna mtu kweli anaweza kukuelewa huko nje? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba, kama kweli Serikali inatupenda hasa Mkoa wa Tanga, wasimamie kwanza bandari ya Tanga, bandari ya nchi kavu, wasimamie kiwanja cha ndege cha Tanga. Kiwanja cha ndege cha Tanga katika Mpango huu hakimo. Nimeona viwanja chungu nzima lakini kiwanja cha Tanga hakina maana, kwani ndege hazitui? Kwani wananchi wa Tanga hawataki ndege? Kwani wananchi wa Tanga hawataki kusafiri kwa ndege? Naomba kwanza haya yasimamiwe, yakisimamiwa haya sisi sote tutakuwa tunaiunga mkono mia kwa mia Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi, lakini kinyume cha hapo tutakuwa tunajidanganya, tutakuwa tunajidanganya sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Serikali sikivu ya Chama cha Mapinduzi, hebu yale mashamba ya kule Korogwe ambayo hayaendelezwi, ambayo wananchi kule wanazumbuliwa wapewe wananchi wafanye kazi. Yale mashamba ya chai, wakulima wa chai mpaka leo hii wanakatwa sh. 200 kila wanapokwenda kuongea na Serikali wakiomba zile fedha wanazokatwa ziongezwe, hazingezwi. Sasa leo hii tunaposema maendeleo ya miaka mitano ni yapi kama mkulima analima shamba lake, analiandaan mwenyewe, anavuna chai lakini kwenye kulipwa halipwi zile fedha zinazotakiwa? Tutakuwa tunawasaidia wakulima kweli? (*Makof*)

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. S. H. NGONYANI]

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi binafsi nimefurahia sana mipango hii, lakini sisi ni wepesi sana wa kuandaan mipango mizuri, lakini wanaofaidi ni wananchi wa nchi nyiningine. Kuna nchi jirani imechukua mipango kutoka Tanzania, leo hii imetushinda. Nchi jirani tu! Yaani sisi ni wepesi wa kupanga mambo, lakini wanaofaidika ni nchi za jirani, kwanini tusanzie kwetu? Kuna kizuzi gani hapa? Rais tunaye msafi, Mawaziri ni hao wazuri, hakuna tatizo hawa watendaji wa chini nyie mnawaachia wa nini? Kwa sababu kama watendaji wa chini mnawaachia wanafanya wanavyotaka matokeo yake ndiyo haya lawama. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali ya Chama cha Mapinduzi, hebu tumalizeni mipango ya mwaka 2012/2013; wananchi wa Mombo wapate mashamba, wananchi wa Mkoa wa Tanga, yale mashamba ya mkonge ambayo hayaendelezwi wagawiwe, mashamba ya misufi kule Korogwe ambayo yamekaa kwa muda mrefu hayana mtu wapewe wananchi, mashamba ya chai ambayo wananchi wanalima kila siku wanakatwa fedha yao walipwe. Nafikiri hili litakuwa ni wazo zuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisiwachoshe, kwa haya machache, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Dkt. Kebwe!

**MHE. DKT. KEBWE S. KEBWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia Mwongozo wa Mpango wa mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo maelezo machache ya kilio ya utangulizi kabla sijakwenda katika hoja. Naiomba Serikali siku ya Chama cha Mapinduzi, katika dharura ambayo imetokea katika Jimbo la Serengeti kuna ukame ambao haujawahi kutokea zaidi ya miongo mitatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukame huu hauna tofauti na uliotokea Ngorongoro na Monduli mwaka jana au mwaka juzi. Kwa hiyo *spell* hii ambayo imeingia Wilaya ya Serengeti

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. DKT. K. S. KEBWE]

imesababisha upungufu mkubwa wa chakula. Naomba Serikali, Wanaserengeti tuna asili ya kulima, hatujawahi kuomba chakula Serikalini, lakini katika mazingira haya yaliyopo, tunaomba chakula kiende, wananchi wauziwe kwa bei ya chini, bei nafuu kuliko ilivyo hivi sasa ambapo debe moja la mahindi ni sh. 18,000 hadi 20,000, bei ambayo kwa kweli ni ghali sana kwa wananchi wa kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, si hilo tu, kukithiri kwa tembo ambaao wanazunguka. Kuna kundi la tembo zaidi ya 50 wanaranda randa katika vijiji zaidi ya 20 ambavyo viko kando kando ya hifadhi. Wiki iliyopita katika Kata ya Isenye, Kijiji cha Iharara waliua ng'ombe na madhara mengine makubwa yanatokea, kama jana nimepata taarifa katika Kijiji cha Isarara, Kata ya pale Kisangura. Mazingira yote haya yanababisha upungufu mkubwa sana wa chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hoja nimepitia kitabu chote, kurasa zote ambacho kinapungua, naomba Mpango waitazame kwa makini, kwa sababu unavyokuwa na mwongozo ni lazima kuwe na *vital statistics* kuonesha kwamba ulifikia wapi katika kiwango cha maendeleo na vigezo vingine. Hata UNDP katika vigezo vya maendeleo huwezi kukosa *vital statistics* ikiwemo umri wa kuishi, vifo vya akinamama na watoto. Vigezo kama hivyo ni vizuri vinakuwa katika utangulizi ili unavyojielekeza katika kutengeneza Mpango, unajielekeza kupunguza vifo kwa kiwango kipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia ijaribu kuangalia mwongozo huu unatwambia kweli pato la Taifa limekua. Uzani wa kipato cha kila Mtanzania kutoka 800,000 kwenda 1,000,000 ina-sound vizuri katika masikio, lakini je, tafsiri yake iko wapi kwa wananchi wa kawaida. Kwa hiyo, kukua kwa Pato la Taifa kuendane na uhalisi wa maisha, maisha yanazidi kuwa makali kwa Watanzania wengi. Kwa mfano, tunaposema *per capital* imekwenda kwa milioni 1,000,000, hivi tafsiri ya yule mwananchi wa Serengeti anaitafsiri vipi na kiwango cha maendeleo hiki yeye anaona vipi? Angependa aone kwamba huduma za jamii anazipata kwa urahisi kadiri anavyohitaji.

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. DKT. K. S. KEBWE]

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia Mipango ambayo inajichomoza kwa mfano, *BRN*; *BRN* katika Mpango wa Miaka Mitano ambayo tuna –*operate* kwenda kwenye *Operational Plans* haikuweko. Kwa hiyo, ni vizuri ku-*harmonize* *BRN* na Mipango mingine ambayo tayari ilishakuwa *documented* kwenye *Five Year Plan*. Katika miaka mitano hii kwenda katika miaka 15 kwa maana ya 2025, haina *reconciliation*. Kwa hiyo, ni vizuri kuwe na uwiano mzuri ku-*capture* miradi kama hii na hii inatupa historia ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni vizuri tujifunze, mara nyingi tunapanga mipango, lakini dharura zinakuwa nyingi, katika Mipango vitu viwili lazima viangaliwe; *discipline* ya matumizi ni lazima iangaliwe na hapa ndio pale sasa tunaambiwa *TRA* wamekusanya, wamezidi malengo, lakini sasa utekelezaji wa mipango haupo, kwa sababu hakuna *discipline* ya matumizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine katika kupanga mipango ni vizuri mipango ile ambayo ni ya maendeleo izidi ile ya matumizi ya kawaida. Isiwe historia ya nchi yetu tunasema mipango kila mwaka, lakini inakuwa ni bajeti ya kutafuna, bajeti ya kula, bajeti ya matumizi. Kwa sababu *recurrent* inakuwa ni kubwa kuliko *development expenditure*, kwa njia hiyo hatuwezi kuendelea.

Mheshimiwa Spika, lakini ambacho tunakiona na mara nyingi Bunge hili tumepigia kelele suala la usimamizi, si zuri, tujaribu kuangalia mipango ambayo inajichomoza kwa kila mwaka, kunakuwa na viporo vingi, kwa sababu ya hali halisi ya usimamizi, mipango haiendi vizuri. Pia ile *value for money* katika miradi, tukipita katika maeneo mbalimbali kwa mfano, na-*declare interest* nipo katika Kamati ya TAMISEMI, tumepita katika maeneo mengi ya Wilaya na Mikoa, viporo vya miradi ni vingi mno. Kwa hiyo, nashauri katika Mwongozo huu wa Mpango ambao tunakwenda kuandaa 2014/2015 kusiwe na miradi mipyä, ni vizuri tujikite katika miradi ambayo ipo ili tuweze kuikamilisha ili twende katika miradi mingine.

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*  
[MHE. DKT. K. S. KEBWE]

Mheshimiwa Spika, Iakini pia mipango ambayo tumeisikia siku nyingi tangu miaka ya 60 katika awamu ya kwanza ni vizuri sasa iende kwa vitendo. Mara nyingi tumeambiwa kuna upembuzi yakinifu, kuna mikakati inaendelea, tupo mbioni, suala la reli ya kutoka Tanga-Arusha mpaka Musoma limekuwa ni wimbo na umezoleka kwa Watanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni vizuri wakati Mheshimiwa Waziri anahitimisha atwambie kuna mpango gani kuhusu reli ya Tanga-Arusha- Musoma. Si hilo tu katika uwanja wa ndege ambaao ulikuwa umepangwa kurahisisha usafiri katika nchi na nchi nyingi duniani ndivyo wanavyofanya, uwanja wa pale Musoma umechoka, umechakaa na ni mdogo na upo katikati ya Mji. Kwa hiyo, ni vizuri kujenga uwanja mwingine mpya, uwanja mkubwa ambaao utarahisisha usafiri katika Kanda ya Ziwa na hata Maziwa Makuu na kurahisisha utalii kwenda Serengeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika juhudhi ambazo Wilaya ya Serengeti tumefanya kujenga uwanja wa ndege *under PPP* na huyu mdau wa *Grumet Reserve*, ni vizuri Serikali iunge mkono kama ambavyo imeanza kwa kutoa kibali kwa bajeti ili kusudi kazi hii iende vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamshukuru huyu Mwekezaji tayari ameishatoa bilioni tano zipo kwenye Bodi tunangoja kibali cha Serikali. Kwa hiyo Wizara ya Mazingira tunaomba tupate kibali haraka na mipango ioneshe kwamba *PPP* tunajenga vipi ule uwanja ili uweze kwisha mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata Mheshimiwa Rais mara nyingi tukikutana akitembelea kule Serengeti anauliza tumefikia wapi. Kwa hiyo, ni vizuri suala hili ambalo litafungua sasa utalii katika Maziwa Makuu na hususan *Western Corridor* ya Serengeti tuweze kupata uwanja huo. Nina hakika hiyo ni kengele ya kwanza.

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. DKT. K. S. KEBWE]

Mheshimiwa Spika, suala la mchango wa utalii katika nchi yetu katika Pato la Taifa ni kidogo sana. Hatuwezi kubaki na wimbo kwamba Tanzania tuna vyanzo vizuri nya kitalii, ni nchi ya pili duniani badala ya Brazil. Sasa wimbo huu ni fursa, unatusaidia vipi? Kwa mfano, Pato la Taifa tunavyosema tumekwenda mpaka asilimia 17.2 ya *income*, bado hatujafanya chochote kwa vyanzo hivi ambavyo tunavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, utalii wa ndani hatuja-*capture* vizuri kwa takwimu ambazo tunazo, ni asilimia mbili tu ya fursa ambayo tunaipata katika utalii wa ndani. Sehemu hii tuifungue vizuri tuachane na kero ambazo zinasababisha kuongeza kodi. Kwa mwaka jana tulipiga kelele sana, lakini Serikali ikalazimisha kupilisha viwango katika mageti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati mbaya sasa hill lina-*operate* katika Mbuga ya Serengeti tu, hususan *Western Corridor* upande wa Mashariki kule kuna Ngorongoro ambayo ni Mamlaka, hawana viwango hivi, viwango hivi vilikuwa sh. 1,500, lakini ghafla vikaenda mpaka sh. 10,000 na tukapiga kelele katika Bunge lililopita, ikaenda kwenye sh. 5,000. Hata hivyo, sh. 5,000 kutoka 1,500 ni mzigo mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Mkuu alivyotembelea kule Serengeti katika Maadhimisho ya Bonde la Mto Mara ambako nchi ya Kenya na Tanzania tunashirikiana tulimweleza kuhusu suala hili. Kwa hiyo ningependa Serikali isitishe viwango vile mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Wizara ya Maliasili na Utalii wakati nachangia wakati wa Bajeti nilitoa onyo ambalo Wanaserengeti walinituma kwamba hatutaweza kuunga mkono bajeti ya Wizara kama itakuwa na mazingira hayo ambayo ni kandamizi kwa Wanaserengeti.

Mheshimiwa Spika, kwa suala nzima ambalo Wanaserengeti wamenituma, ni namna gani viwango vile ambavyo Serikali inawatoza viondoke kwa sababu wewe

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. DKT. K. S. KEBWE]

upo ndani Wilaya, unasafiri kwenye Wilaya yako halafu bado unatozwa, kwa kweli hata haiingii akilini.

Mheshimiwa Spika, kwa kumaliza suala zima la mipango upande wa afya ni vizuri tuanze kutazama, mtazamo wa dunia ulivyo. Kwa sababu tunavyokuwa na Vituo hivi vidogo vingi inakuwa ni *too costly* na kada zile wakati mwingine ukienda nazo unakuta kwamba hata mahitaji ya dunia sehemu zingine ukienda hawa Madaktari...

*(Hapa Kengele ya pili illia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante naona kengele imelia.

**MHE. DKT. KEBWE S. KEBWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaongeza kwa kuchangia kwa maandishi. Nashukuru sana. (*Makofii*)

**SPIKA:** Haya nashukuru. Nilimwita Herbert Mntangi atafuatiwa na Mchungaji Natse, halafu atafuatiwa na Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura na Mheshimiwa Rajab Mohamed ajiandae.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia leo katika Mpango huu wa Bajeti inayokuja mwaka 2014/2015. Nianze kwa kusema yafuatayo:-

Kwanza, tathmini ambayo imefanywa ya utekelezaji wa Mpango uliopita inaonesha upungufu katika maeneo yafuatayo:- Kwanza, miradi mingi haijakamilika na ipo nyuma ya wakati, kwa sababu zifuatazo:- Moja, ni kwamba kumekuwa na matatizo ya upatikanaji wa fedha katika utekelezaji wa miradi hiyo. La pili, kuna taratibu hizi za manunuzi zimekuwa pia zikichangia kuchelewesha utekelezaji wa miradi hiyo mikubwa. La tatu, kumekuwa na ucheleweshaji wa tathmini ya malipo ya fidia. Sasa kama

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. H. J. MNTANGI]

tathmini ya Mpango uliopita inaonesha upungufu huu mkubwa nini maandalizi yetu ya kuondoa upungufu huo ili Mpango huu unaokuja kwa hakika uweze kutekelezwa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika Mpango unaokuja una kitu kinachoitwa *Big Results Now (BRN)* kama huu tuliuona upungufu katika Mpango uliopita hatutauchukulia hatua ni wazi kabisa Mpango wetu wa BRN hautafanikiwa badala ya kuwa *Big Results Now* utakuwa *Big Failure Now*. Sasa lazima tujipange vizuri, lazima tutumie hekima na busara, tujipange vizuri tufanye kazi itakayoleta maendeleo mazuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wenzetu wa Zambia wametengeneza bomba la mafuta kutoka Dar es Salaam mpaka Zambia, sisi Watanzania tulikuwa na Mpango wa kujenga bomba la mafuta kutoka Dar es Salaam mpaka Mwanza ambapo ingesaidia sana katika kupunguza bei ya mafuta kwa watumiaji wadogo. Mpango huu umezimwa. Sasa hivi kweli kama tunataka kupunguza gharama kwa nini hturejeshi mpango huo ili kuchangia katika kupunguza bei ya mafuta kwa watumiaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo yangu ni kuurejesha upya mpango huo wa ujenzi wa bomba la mafuta kutoka Dar es Salaam kwenda Mwanza ili vile vile kupunguza athari kubwa ambazo tunapata sasa ya magari makubwa yanayobeba mafuta kutoka Dar es Salaam na kuendelea kuharibu barabara zetu, kwa nini mpango huu hatuutekelezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu Kenya wamejenga *pipeline* yao na wameshirikiana na Uganda. Sasa hivi bomba lile la Kenya linakaribia mwisho wa mpaka wa Kenya kuendelea kuingia Uganda ambapo Uganda tungeweza kuwasaidia kwa bomba la mafuta la kutoka Dar es Salaam hadi Mwanza. Sasa sisi kweli tunataka mabadiliko makubwa, lakini mambo ambayo tunatakiwa tuyafanye hatuyatekelezi.

Mheshimiwa Spika, lakini yapo mambo mengine katika utekelezaji wa miradi yetu, gharama ni kubwa. Kwa

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*  
[MHE. H. J. MNTANGI]

mfano, gharama ambazo tunalipa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ya Mpango ule wa dharura, hela tunazowalipa *IPTL, Aggreko, Symbion* ni hela nydingi kupita kiasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tuna mpango wa kuzalisha umeme wa Kinyerezi ambao ukianza Kinyerezi /, Kinyerezi //na Kinyerezi ///ni megawati 1,400 je, tuna mpango gani wa kuachana sasa na *IPTL* wakati tunazalisha megawati 1,400 kwa nini tuendelee kubaki na *IPTL* wanaotupa megawati 100 tu kwa gharama zisizokuwa na uhalali wowote. Gharama ni kubwa kupita kiasi. Kwa nini na tunajiandaa vipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu Serikali ije hapa na itwambie Mkataba wa *IPTL* unakwisha lini? Mkataba wa *Aggreko* unakwisha lini, mkataba ule wa *Symbion* wa dharura unakwisha lini ili waondoke baada ya sisi kuzalisha umeme unaotokana na mkakati huu ambao tumeupanga sasa.

Mheshimiwa Spika, matazizo ya upatikanaji wa fedha; mradi wa umeme wa Kinyerezi / umekwishaanza kutekelezwa na mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Nishati na Madini na tumekwenda pale. Tulipokwenda mwezi mmoja tu uliopita, tatizo hilo limezungumzwa na wale Wakandarasi waliopo *site* walikuwa wanasema wapo tayari kuondoka kwa sababu fedha hawajapata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunasema *Big Results Now*, fedha hakuna za kutekeleza mradi wa umeme, Wakandarasi wanataka kuondoka, hivi kweli tutafanikiwa! Hatuna maandalizi mazuri katika mpango wa upatikanaji wa fedha. Kwa hiyo tujitahidi katika kutekeleza hilo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini jambo lingine ni mpango na hili nalielekeza kwa Wizara ya Maji. Mheshimiwa Waziri wa Maji alikuwepo hapa asubuhi na nilimwandikia kikaratasi kuhusu mpango wa maji ambao ni ahadi ya Mheshimiwa Rais katika Wilaya ya Muheza, tunataka kuwa na uhakika fedha zinatengwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. H. J. MNTANGI]

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni tulikuwa na mpango katika Kanda ya Kaskazini ikiwemo Mikoa ya Tanga, Kilimanjaro na wenzetu wa Manyara wa Uwekezaji ambao tuliufanya na wawekezaji wengi walikuja pale katika Mkutano ule Tanga. Kitu kikubwa ambacho lazima kifanyike ni kwamba, lazima tuwe na miundombinu ya uhakika itakayowezesha kuvutia wawekezaji.

Moja, kati ya miundombinu hiyo, sawa ni barabara, maji, na kubwa ni umeme. Sasa haya mambo lazima tuyatekeleze. Kwa hiyo, tunaomba kuwa na uhakika kwamba, mradi wa maji wa Muheza kutoka Mto Zigi unakuwepo katika Mpango huu wa Bajeti na fedha zinatengwa ili mradi huo utekelezwe kwa uhakika. Hiyo ni ahadi ya Mheshimiwa Rais, ni lazima iheshimiwe na lazima itekelezwe.

Mheshimiwa Spika, lakini lingine pia Muheza tuna ahadi ya Mheshimiwa Rais ambayo ni barabara ya kutoka Muheza kwenda Amani. Naomba niseme kwamba kazi inayofanyika sasa ni nzuri kwamba barabara inaimarishwa. Lakini dhamira na ahadi ya Mheshimiwa Rais ni barabara hiyo kujengwa katika kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina uhakika mpango huo wa kuweka lami barabara hiyo utakuwepo katika bajeti hii. Kwa hiyo, hili nalo nalielekeza kwa Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu na nina uhakika ndani ya bajeti, fedha hizo kwa ajili ya kujenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami zinatengwa ndani ya bajeti hii inayokuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuendelee kuimarisha miradi ya uzalishaji wa umeme. Katika Wizara ya Nishati, mipango mizuri ipo, lakini je, itatekelezwa? Tumesema Kinyerezi moja, mbili na tatu ni megawati 1,400, lakini ukichukua na miradi mingine ambayo ipo katika mapendekezo uzalishaji utakuwa zaidi ya megawati 3,000, lakini je, tunasema kweli megawati 3,000 zitakuwepo kabla ya mwaka 2016?

*Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*  
[MHE. H. J. MNTANGI]

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama zitakuwepo itakuwa ni vizuri, na mpango wetu utaweza kufanikiwa, lakini kama hatutafikia viwango hivyo, ni wazi kabisa mipango yetu mingi itashindikana, Watanzania hatutapiga hatua. Kwa hiyo, tujitahidi tuboreshe bandari ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tuache mtindo ambao umewakatisha tamaa wawekezaji na umeikatisha tamaa nchi jirani na wengine wamekwishaanza kujitoa; rushwa iliyokithiri katika bandari yetu ya Dar es Salaam, lakini na vilevile huko barabarani magari yanakopita. Bila kuondoa matatizo hayo mizigo ambayo tumekuwa tukisafirisha kwa uhakika kwenda Rwanda na Burundi na DRC itapungua au itakwisha kabisa na wenzetu kweli watahamia huko walikokwenda kwa kutumia bandari ya Mombasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile Waganda walikuja na wakawa tayari kusaidia kuweka fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mpango wa ujenzi wa reli hii ya kutoka Tanga kuelekea Arusha na kwenda hadi Musoma, wenzetu Waganda walikuwa tayari, sisi Watanzania ambako eneo kubwa la hiyo reli itakuwa ndani hatukutoa.....

*(Hapa kengele ya pili illilia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Nakushukuru na naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante. Mchungaji Natse, atafuatiwa na Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura na Mheshimiwa Rajab Mohamed ajiandae.

**MHE. MCH. ISRAEL Y. NATSE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili nichangie katika Mpango wa Taifa. Kwanza, nilikuwa naangalia, sisi Watanzania Idara yetu ya Mipango imekuwa maarufu sana kuwa na Mipango mizuri, ambayo utekelezaji wake haufiki mwisho na hii mipango mizuri mingi imebaki kwenye makabati bila kufikia lengo kwa wahusika.

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. MCH. I. Y. NATSE]

Mheshimiwa Spika, nataka kuzungumza maeneo machache sana ambayo kwayo tumekuja na dhana ya *Big Results Now*. Moja ni juu ya Kilimo Kwanza. Nafikiri ni kweli tangu mwanzo kilimo ni mkombozi wa Mtanzania, lakini kilimo hiki kwa kuangalia tu hali ya hewa kutegemea mvua hatutafika mbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumezungumza hata katika mipango iliyopita kwamba tuondoke kwenye kilimo cha kusubiri mvua, twende kwenye kilimo cha umwagiliaji na mpango huu hauweki wazi dhamira ya dhati ya Serikali kuhakikisha kwamba, inatia nguvu kubwa katika kilimo cha umwagiliaji na kwa kuchagua maeneo na kuhakikisha kwamba maeneo kadhaa yatalisha nchi hii chakula na hata kuza ziada nje kama ambavyo wenzetu wanafanya, wakulima wachache wenye kuzalisha kwa nchi nzima na hata kuza ziada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapozungumzia juu ya kilimo hiki cha umwagiliaji, mabonde mengi yapo, imeshindikana kilimo hiki kuwa makini kwa sababu kuna jambo la hifadhi ya mazingira ambayo inaingiliana ili kuhakikisha kwamba vyanzo vya maji vinatunzwa sawasawa. Kumekuwa na uharibifu mkubwa wa mazingira katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano kule katika Bonde la Eyasi ambalo ni maarufu kwa wakulima wa vitunguu, mpunga na mahindi. Bonde lile lingesimamiwa vizuri *schemes ambazo zimejengwa*, zingine zimejengwa chini ya kiwango, zingesimamiwa vizuri zingezalisha vya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baya kuliko yote Bonde lile limevamiwa na watu wachache wenye tamaa ya utajiri wa haraka na kuharibu mazingira; kukata miti, kufungua mashamba kwenye vyanzo vya maji, lakini hakuna hatua inayochukuliwa. Kwa hiyo, niiombe Serikali bila kuonea aibu baadhi ya watendaji, maana haya yanafanywa na watendaji, yanafanywa na viongozi waandamizi wa Chama

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. MCH. I. Y. NATSE]

Tawala, bila kuonea haya ili kuweza kuwa na uhakika na kilimo cha umwagiliaji katika Bonde la Iyasi. Bonde lile lihifadhiwe kwa afya ya wananchi wote kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tunahitaji kuwekeza katika miradi michache ambayo tunaweza kupima ufanisi wake kuliko kuwa na miradi mingi na mwisho wa siku hakuna jambo ambalo linatupa matumaini. Kwa hiyo, niilombe Serikali tuwe na mipango ya uhakika ambayo inapimika na mwisho tupate matokeo yanayoitwa Matokeo Makubwa Sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikitoka kwenye kilimo, ni kweli kuwa, Mungu alipoumbad alikamilisha kazi yake siku ya saba kwa kumuumba mwanadamu, maana yake wanyama walikuwepo na maana yake mwanadamu alimkuta mnyama lakini mwanadamu alipewa kazi ya kutiisha viumbe vyote hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kusema nini? Nataka kusema kuwa, migogoro ya wakulima na wafugaji na Hifadhi zetu za Taifa hivi ni vitu vinavyohitajiana. Katika kuboresha kilimo tunahitaji kuangalia pia na hao wafugaji wawe wapi, hilo sitaki kulizungumzia kwa kuwa limezungumzwa na litawekewa utaratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye suala la hawa wanyamapor, tunawapenda na tunawahitaji. Nafikiri kinachokosekana kwetu Watanzania ni uzalendo wa kuipenda nchi yetu na *resources* zake, kwa sababu haiingii akilini kuona kuwa, kila siku tunatangaza vita vya ujangili unaoendelea katika Hifadhi zetu, naona hakuna dhamira ya kweli kwa Watanzania wote kwa ujumla hasa wale ambao wamepewa dhamana ya kulinda maliasili hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu haiwezekani leo tunasikia pembe za ndovu zimekamatwa kule na zingine kule na askari tunao. Ni kweli tunahitaji kuwa na dhamira ya kweli katika mambo haya. Ili tuweze kuwa na mpango, ili tuweze kuwa na rasilimali kwa maendeleo ya Watanzania.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. MCH. I. Y. NATSE]

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa natafakari hapa kuwa hata tukiunda hii Kamati Teule inakwenda kufanya nini, maana majibu ya haya mambo yote tunayo, wahusika tunawafahamu, haingii akilini kuwa tembo wameuawa *Selous*, wameuawa Ngorongoro na kwingineko na kwamba watu hawafahamiki, haingii akilini hata kidogo. Lakini kwa ajili ya taratibu na kutafuta ushahidi ni sawa na naafiki kuwa ni lazima tuwe na dhamira ya kweli ya Uzalendo kwa nchi yetu na mali zake hapo tutaweza kujikomboa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la umeme *Vijijini*; *World Bank* imechimba visima virefu Tanzania nzima, lakini naona mradi huu ambaao sasa tunasema *The Big Result Now* hauwezi kukamilika vizuri kama umeme hautakwenda katika maeneo haya, kwa sababu huko *vijijini* visima virefu bila umeme halna maana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maeneo mengi kama kule kwangu Karatu, maji yapo lakini namna ya kuyavuta hayo maji yaje juu wananchi watumie, ni kasheshe. Kwa hiyo, niombe Serikali tuweke nguvu zaidi katika maeneo hayo ili wananchi waweze kunufaika na tuone Matokeo Makubwa Sasa kule Karatu kwa maji. Ni kweli Matokeo Makubwa Sasa amekuja Waziri Mkuu, amekuja Waziri wa Maji, Naibu Waziri, lakini hatimaye hakuna maji. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi zimefanyika kweli ndogondogo za hapa na pale, lakini hakuna maji, tunataka kuona maji Matokeo Makubwa Sasa, kwa hiyo nafikiri *seriousness* katika kazi bado ni hitaji letu kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nzungumzie kuhusu elimu; tukitaka kuona Matokeo Makubwa Sasa tunahitaji kutengeneza mazingira mazuri ya shule zetu, ya Walimu na wanafunzi. Hilo litatusaidia kuhakikisha tunaona Matokeo Makubwa Sasa, kuwa wanafunzi watapata kile ambacho tumekusudia na Walimu watapata kile ambacho wanapaswa kupata na wafundishe vizuri.

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. MCH. I. Y. NATSE]

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusitegemee Matokeo Makubwa Sasa kama hatutaandaa mazingira bora kwa shule zetu hasa kwa Walimu. Tutabadiili viwango vyta kufaulu, tutafanya kila hali, lakini kama hatutatengeneza...

**SPIKA:** Mheshimiwa umepata *bonus* hii ilikuwa ya pili, *sorry!*

Sasa nimwite Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura ambaye atafuatiwa na Mheshimiwa Rajab Mohammed na Mheshimiwa Brigedia Ngwilizi ajiandae.

**MHE. MTUTURA A. MTUTURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii. Ukiangalia kitabu hiki cha Mheshimiwa Waziri, ukurasa wa 20 aya hii ya 34 inazungumzia vipaumbele vyta Taifa na hapa vipaumbele hivyo vyta kimkakati vimetanguliwa na Nishati, Barabara, Reli, Bandari, Usafiri wa Anga, Maji Safi na Maji Taka, Teknolojia na Habari. Najua kuwa kipaumbele cha Taifa bado elimu ni namba moja ingawa hapa hakijatajwa. Kwa hiyo, katika kuchangia kwangu nitazingatia hivi vipaumbele ambavyo vimetajwa hapa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muono wangu, naunganana na Waziri kabisa kuwa kipaumbele cha kwanza kiwe ni nishati, lakini badala ya kipaumbele cha pili kuwa barabara naishauri Serikali kuwa kipaumbele cha pili kiwe reli kwa sababu ya umuhimu wake kiuchumi katika nchi hii, kwa sababu tumeona barabara nyingi zinajengwa, lakini athari zinazopata barabara zile kutokana na kutokuwepo kwa reli ni kubwa na gharama kubwa sana za Serikali zimetumika katika kuzikarabati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kama kipaumbele cha pili kitakuwa ni reli, nadhani hata hizo barabara chache ambazo tumefanikiwa kuzijenga zitaweza kuimarika. Kipaumbele cha tatu kiwe ujenzi wa bandari na hasa bandari ya Dar es salaam kwa zile gati mbili gati namba 13 na 14. (*Makof!*)

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. M. A. MTUTURA]

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi kumekuwa na mkanganyiko kidogo kati ya Bandari ya Dar es Salaam na ile ya Bagamoyo, kwa kuzingatia kuwa sasa hivi tuko katika wazo la kuwa na *Big Results Now*, kwa maana ya Matokeo Makubwa ya Haraka Sasa, hatuwezi kupata Matokeo Makubwa ya Haraka Sasa hivi kama rasilimali chache tulizonazo tutazielekeza Bagamoyo ambako kunahitaji fedha nydingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naishauri Serikali kuwa waendelee na fikira zao za mwanzo za kujenga gati namba 13 na 14 na vilevile kujenga bandari ya nchi kavu ya kule Kisarawe ili ule mzigo ambao hauko tayari kuingizwa melini, basi uweze kulundikana kule Kisarawe. Naamini kabisa kuwa, Serikali itajenga uwezo mkubwa wa kuweza hata kujenga hiyo Bandari ya Bagamoyo na Bandari zingine za Mtwara pamoja na Tanga. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipaumbele cha nne kielekezwe kwenye barabara badala ya kuwa ni kipaumbele cha pili na cha tano kielekezwe kwenye maji safi na maji taka. Siyo siri mimi ni Mbunge wa CCM, lakini kutokana na hali iliyopo huko Vijiji ni sasa hivi na baadhi ya Miji katika nchi yetu maeneo ambayo Chama changu kitatafunwa sana ni eneo hili la maji. Naomba tuwe makini sana kwa miaka hii miwili ya bajeti tuliyobakiwa, tuhakikishe kuwa kero ya maji vijiji na kwenye Miji inaondolewa haraka iwezekanavyo, kinyume cha hivyo kazi yetu itakuwa ni kubwa sana huo mwaka wa 2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tujenge matumaini kwa wananchi juu ya kuwapatia maji safi na salama. Bahati mbaya maji hayana mbadala, usafiri una mbadala unaweza ukaamua kusafiri kwa ndege, kusafiri kwa treni, kusafiri kwa gari, kusafiri hata kwa miguu na baiskeli na bodaboda, lakini unapokosa maji hayana mbadala, huna pa kukimbilia. Kwa hiyo, tuwasaidie Watanzania wanyonge walioko vijiji ni katika kuhakikisha kuwa tunatatua tatizo la maji. (*Makofii*)

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*  
[MHE. M. A. MTUTURA]

Mheshimiwa Mwenyekiti, niangalie katika nyanja mbalimbali za uchumi; nchi yetu bado hajajitosheleza katika zao la sukari, tumekuwa na viwanda takribani vikubwa vine; Kiwanda cha Kilombero yaani Kilombero *onena two*, Mtibwa, kule Kilimanjaro na kule Kagera, lakini bado tuna maeneo mengi mazuri na makubwa ambayo yanaweza kuzalisha sukari nyingi ikatosheleza katika nchi yetu na bado tukaweza kusafirisha nje ya nchi. Maeneo hayo ni kama Bonde la Mto Rufiji na vilevile Bonde la Mto Ruvuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka ya nyuma tulikuwa na mpango wa kuanzisha shamba kubwa sana la miwa katika Bonde la Mto Ruvuma, lakini mpango huu umekwisha na hausikiki tena. Naomba sana Serikali aidha, kwa kutumia mashirika yake ya ndani kwa kuweka mazingira muafaka kwa wahisani, waje wafungue mashamba makubwa ya kulima miwa na kufungua kiwanda kikubwa sana cha sukari katika Bonde la Mto Ruvuma hususani katika Wilaya yetu ya Tunduru kwa sababu tunayo maeneo mengi ambayo Wakulima wanaweza wakapata zaidi ya hekari 5,000 za kuzalisha miwa na kufungua kiwanda cha kuzalisha sukari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna suala hili la ujenzi wa Bandari ya Mtwara na reli ya kutoka Mtwara hadi Mbambabay ili iweze kusafirisha makaa ya mawe pamoja na Chuma cha Liganga. Nimesikia minong'ono kuwa kuna wazo la kubadilisha wazo hili la kujenga hii reli ya kutoka Mtwara kwenda huko Mbambabay, kwa maana wanaona huenda isiwe na tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwahakikishie Watanzania wenzangu kuwa, tija bado ipo na itaendelea kuwepo kwa sababu dhamira ya kujenga reli hii ni kujaribu kufufua wazo ambalo Marais wetu waliotangulia akina Mheshimiwa Benjamin Mkapa na Rais wa Msumbiji na Malawi ili Ukanda huu wa Kusini mwa Tanzania na Kaskazini mwa Msumbiji na upande wa Mashariki mwa Zambia na Malawi wawewe kutumia usafiri ambao utawaleta tija.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. M. A. MTUTURA]

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitoka Malawi kuja Pwani njia fupi kabisa ni ya kuititia Mtwara. Wenzetu wa Malawi wanazimika kuititia Dar es Salaam kwa sababu hawana barabara mbadala, lakini reli hii ikijengwa tutapata mzigo mkubwa sana wa kutoka Zambia na Malawi ambao utapitia hapa, lakini vilevile Kaskazini mwa Msumbiji nao watanufaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi mionganoni mwa *Big Four* katika nchi yetu ni pamoja na Mkoa wa Ruvuma ambao unazalisha chakula kwa wingi sana, mahindi pamoja na Tunduru sasa hivi imejitokeza katika kilimo cha mpunga, Mikoa karibu yote ya Kusini wanategemea mchele kutoka Tunduru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama reli hii itakuwepo, uwezekano wa kusafirisha mahindi kwa njia ya treni mpaka Bandari ya Mtwara, halafu mahindi hayo yakasafirishwa nje ya nchi itawajengea uchumi ullo imara wananchi wetu wa Ukanda huu wa Kusini. Vile vile mzigo mkubwa sana utategemewa wa makaa ya mawe ya Ngaka pamoja na Liganga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba wazo hili la kujenga reli na siyo wazo la kuijenga reli, ni wazo la kufufua reli ambayo zamani illkuwepo, libaki palepale ili wananchi hawa wa kusini waweze kunufaika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, korosho za Tunduru sasa hivi hazinunuliki kwa sababu wanunuzi wengi wanashindwa kwenda Tunduru kununua kwa sababu wanasesma ni mbali. Reli ikiwepo wachuuzi wengi wa kutoka nje ya nchi watakuja kununua korosho Tunduru kwa bei nzuri kwa sababu usafiri wa bei nafuu wa reli hiyo ambayo tunaitarajia utakuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa fursa hii na naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante. Sasa nimwite Mheshimiwa Rajab Mohammed, atafuatiwa na Mheshimiwa Brigedia Ngwilizi na Mheshimiwa Pauline Gekul.

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru kwa kunipatia nafasi hii. Niseme tu kuwa, Watanzania tumekuwa mahodari sana wa kupanga mipango, tumekuwa mahodari sana katika suala la uandishi kiasi cha kuwa wananchi kwa sasa wanaanza kutupa majina ya ajabu ajabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kuna jambo kubwa ambalo linatafuno nchi hii, ambalo linakwaza maendeleo ya nchi hii, ambalo linasababisha matumizi makubwa ya Serikali kupanda kila mwaka, ambalo linasababisha hata wafadhili wetu kuanza kupunguza kasi yao ya kutusaidia, basi ni suala la nidhamu katika matumizi ya fedha za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimejaribu kukipitia kitabu kizima ambacho Waziri amekiwasilisha hapa sikuona maelezo ya aina yoyote ya mpango mkakati wa Serikali ambao unawenza kutushawishi na sisi kutoa mapendekezo yetu au kuungeza nyama katika mipango ile iliyozungumzia suala zima la nidhamu ya matumizi fedha za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima tukubali kuwa ndani ya nchi yetu, nidhamu ya matumizi ya fedha za Serikali imeshuka kwa kiwango cha chini kabisa, ni hali mbaya kabisa. Nenda katika taasisi zote, nenda katika Halmashauri zote nchini huko ndiyo kumeoza kabisa, nidhamu ya matumizi ya fedha za Serikali haipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hata kama tungeweka kipaumbele kimoja tu bila ya kuzingatia suala la nidhamu ya matumizi, basi hatuwezi kufanikiwa. Haya yote yaliyozungumzwa hapa, yaliyowekwa hapa, ni maelezo tu, lakini nidhamu ya matumizi ya fedha za Serikali hakuna na hili nataka nilithibitishe hata ndani ya Bunge lako angalia viti vya Mawaziri hapo, vitupu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wewe kwa mara mbili tumekusikia hapa unawaambia Mawaziri kuwa jamani kitu ambacho tunakiongelea ni kikubwa, ni mipango ya nchi, Mawaziri ni lazima muwepo ndani ya Bunge, msikilize

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. R. M. MOHAMMED]

michango, leo Mawaziri wale wanaohusika hasa wanatakiwa huu mpango wausikilize. Wasikilize maoni yetu sisi Wabunge, hawafiki hata kumi hapa. Kama wanabisha wanyanyue mikono hapa, kama watafika kumi hapa. Aibu, tena ni aibu kubwa, wallobaki ni Mawaziri wadogo tu, pengine sijui hata kama ndani ya Baraza la Mawaziri wanaingia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sijui hata tunafanya nini. Ikiwa kama leo Mawaziri ambao tunataka hii *Big Result Now* iweze kufanya kazi, wanashindwa kukaa hapa kutusikiliza. Nakubaliana na wananchi wanaosema kwamba, *this is Better Resign Now*, hawana sababu ya kuendelea kuwepo. Hii mipango tunapanga kwa ajili ya kuendesha nchi. Leo wao waingia mitini. Basi hata Spika hamumheshimu? Hata Spika? Ni aibu!

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la nidhamu ya matumizi ya fedha ningependekeza kwa Serikali kwamba, hiki ndio kiwe kipaumbele chetu cha kwanza. Bila ya kuwa na nidhamu ya matumizi ya fedha za Serikali, haya yote tunayozungumza kule kwetu tunaita *halindwa*, haitaleta tija yoyote. Leo wananchi wetu wote na hasa vijana wetu ambao sasa hivi wanamaliza shule. Wanachokijua wao ni kwamba, nipate kazi, kesho niwe na gari. Nipate nyumba nzuri ndani ya mwezi mmoja kwa sababu yeye anapopita mitaani, anasikia tu hii nyumba bwana ya kijana wa *TRA*, kaanza kazi juzi tu. Hili jengo ni la Waziri, hili jengo la...

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hii yote imetokana na nidhamu ya kutokuwa na nidhamu ya matumizi ya fedha za Serikali. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri au naionomba Serikali, hebu ituletee mpango wao mkakati na iwe ni kipaumbele cha kwanza, nidhamu katika matumizi ya fedha za Serikali. Kiundwe chombo kama wanataka tufanikiwe, ambacho kitakuwa kinashughulikia suala zima la nidhamu ya matumizi ya fedha za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *actually* matumizi tu, hata ukusanyaji wa mapato. *Trend* yetu inaonekana, katika kukusanya mapato. Safari hii tumeona katika mpango

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. R. M. MOHAMMED]

kwamba Serikali itakusanya *almost eleven trillion*, ni kidogo. Mheshimiwa Mbunge mmoja wa hapa Dole, aliwahi kutoa ushauri mwaka jana kwamba jamani hebu tuundeni Tume ikawachunguze hawa wakusanyaji mapato, kwani mapato mengi yanapotea. Hapa Taarifa inasema triliuni moja, lakini ni imani yetu kwamba zinazokusanywa, ni *twice* ya hii *trillion* moja, lakini zipo mifukoni mwa watu, kwa sababu ya kukosa nidhamu ya fedha za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende suala la miundombinu hasa suala la Bandari. Alizungumza Mheshimiwa Mtutura, Gati namba 13 na 14. Ikumbukwe kwamba, Gati hizi mbili ndizo zilizosababisha baadhi ya Mawaziri, kutimuliwa. Leo ni jambo la kushangaza humu kwamba imetajwa Gati namba moja mpaka namba saba, lakini imeachwa Gati namba 13 na 14 ambayo *feasibility study* yake ilishamalizika, Wakandarasi walishapatikana, fedha zile za mkopo tulizoambiwa zilikuwa tayari, *how come* leo mnatuletea Gati namba moja mpaka namba saba, kwamba ndio kwanza upembuzi yakinifu. Bila ya kutupa Taarifa za Gati namba 13 na 14.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna nini hapa? Au ndio haya maneno ya watu kwamba, yule Mchima mliompa Bagamoyo, ndiye ambaye kaingilia huu mchakato namba 13 na 14, kwa sababu kampuni ni ile ile. Tunaomba maelezo ya Serikali kuhusiana na Gati namba 13 na namba 14. Ili hizi kwa vile michakato yake ilishamalizika. Kwa nini zisianze Gati hizi mbili kwanza? Tunaanza kushughulikia namba moja na namba saba, Mwambani, Bagamoyo. Hebu tujribuni kuangalia na yale ambayo tunayazungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la kilimo. Katika Taarifa ya Waziri, anaeleza ekari ambazo kwa kweli hazijafanyiwa mchakato. Tulikuwa na Kilimo Kwanza, Serikali hebu ituambie kwanza tumekwama wapi kwenye Kilimo Kwanza? Tumepata mafanikio gani katika Kilimo Kwanza mpaka sasa hivi tunataka kuingia katika msamiati mwininge? Hebu tuambieni kwanza hiki Kilimo Kwanza tumefikia wapi ili tujue sasa tunaondokaje pale, tunakwenda katika msamiati

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. R. M. MOHAMMED]

mpya? Tusijaribu kuleta misamiati ambayo tunawachanganya wananchi. Tupeni taarifa kamili ya Kilimo Kwanza tumefikia wapi na tumekwama wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mmetupa taarifa za *TASAF*, kila Mbunge kakubaliana na taarifa za *TASAF* na kafurahia kabisa, lakini leo mnatupa kitu ambacho...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Brigedia Ngwilizi atafuatiwa na Mheshimiwa Gekul na Mheshimiwa Lowassa.

**MHE. BRIG. JEN. HASSAN A. NGWILIZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachozungumza hapa ni Mpango wa Maendeleo ya mwaka 2014/2015 ambao Mpango huu umezalishwa kutokana na Mpango wa Miaka Mitano 2011/2012 mpaka 2015/2016, ambao huo ndio utatupeleka kwenye mpango wetu wa 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ili tuendelee Watanzania tunakubaliana tunahitaji watu, ardhi, siasa safi na uongozi bora. Lakini hapo ndio mwisho wetu wa kufikiri. Huo ni mwanzo tu kwa ajili ya maendeleo ya watu. Lakini kwa ajili ya maendeleo ya nchi unahitaji vitu vingine vinne, niliwahi kuvisema naomba kurudia.

Tunahitaji miundombinu kwa maana ya *communicaton infrastructure*, iwe ni Reli, Barabara, usafiri wa Ndege, Maji na vile vile Teknohana (TEHAMA), yote hiyo imeingia kwenye mfumo wa usafiri. Hivyo kama hatutapanga katika mipango yetu ya maendeleo ili kufungua nchi yetu, basi tujue kwamba tunatwanga maji kwenye kinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nazungumza hivyo? Kwa sababu nchi kama hatujaiwekea miundombinu kuifungua, basi hakuna tofauti na yale ambayo yanawapata

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. BRIG. JEN. H. A. NGWILIZI]

ndugu zetu Wakongo. Kongo walipata uhuru kabla yetu na mpaka leo hii nchi haijaunganishwa kutoka kusini kwenda kaskazini. Nchi yetu hii mpaka sasa hivi tunazungumzia miaka 50 na zaidi. Bado hatujaleta mfumo rasmi wa jinsi ya kuunganisha. Ndio maana leo hii tunazungumzia reli ya katikana kwamba ni hiyo tu ambayo tunatakiwa kuiangalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasahau kwamba kuna reli ya Tanga, mpaka Arusha, mpaka Musoma; tuna reli kutoka Mtwara mpaka Songea mpaka Liganga huko Mchuchuma. Kwa sababu tupende tusipende tunaweza tukajidanganya kwamba kwa miaka hii, kumi na tano au ishirini, hatuhitaji hiyo reli, lakini katika miaka 50 inayokuja itabidi tujenge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa nini tungojee muda wote huo? Kwa nini tusijenge hivi sasa? Kama hatujengi reli hivi tunatazamia kile chuma cha Mchuchuma na Liganga tunakitoa vipi kule? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tuendelee, hayo mambo ya mawasiliano kwa njia ya reli, barabara, bandari ni moja. Tunahitaji nishati, nishati hiyo iwe inatokana na gesi, mafuta au maji, lakini bado tunahitaji nishati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa hivi tume-zero /insana sana kwenye suala la gesi. Lakini tunasahau kwamba maji vile vile ni chanzo muhimu cha umeme. Hapa sasa hivi tunazungumzia mazingira, tunaona kwamba, kwa sababu ya hali yetu ya mazingira na mabadiliko ya tabianchi, basi haitawezekana kutegemea maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile tunajua kwamba kwa muda mrefu tumekuwa tunazungumzia suala la bwawa la *Stigler's Gorge*. Sioni kokote likizungumzwa hili na *Stigler's Gorge* katika upembuzi yakinifu wake lilikuwa limekusudiwa kunywesha Bonde zima la Mto Rufiji. Bonde lile la Mto Rufiji bila *Stigler's Gorge* huwezi ukategemea kwamba utalinywesha, utakuwa unategemea maji yanayotiririka kwenye Mto.

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. BRIG. JEN. H. A. NGWILIZI]

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tunazungumzia suala la *Stigler's Gorge* vile vile katika Mpango yetu sikuona, tumezungumza sijui Bwawa la Kidunda, bwawa lile ni kwa ajili ya maji ya kunywa lile. Hakujazungumzwa suala la kujenga mabwawa kwa ajili ya kuhimili kilimo cha umwagiliaji. Tuna mabonde mengi, tuna uwezo mwengi wakujenga mabwawa yale lakini naona hilo katika Mpango huu liko *silent*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili uendelee unahitaji chuma kama kile ambacho tunacho Liganga na Mchuchuma. Bila Chuma huwezi ukafanya chochote, utategemea tu itabidi kuagiza chuma kutoka nje, lakini tunacho. Sijasikia mipango mahsus ya ku-*develop* Chuma chetu tulichonacho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho wa yote, tunahitaji sayansi na teknolojia kwa maana ya pamoja na elimu na kadhalika. Bila kuwatayarisha Watanzania katika *SNT*, hatuwezi ku-*meet deadline* hizi ambazo tumejiwekea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ili tuweze kutekeleza yote hayo, tunahitaji fedha, fedha hizo hatuna. Ndiyo maana naomba niungane na Kamati ya Bajeti, kwamba Serikali hajjaweza kutumia fursa ya kukopa. Ukurasa wa nane wa maoni ya Kamati unaeleza pale, kwamba Kamati inashangazwa na kitendo cha Serikali kusita kukopa ndani ya ukomo huu kwa ajili ya Miradi wa Maendeleo. Fedha ambayo imekopwa ya kiasi cha shilingi bilioni 118.6 ni pungufu kwa shilingi bilioni 161.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huo ndio ukomo ambao umewekwa Kimataifa, kwamba Tanzania tunaweza kukopa kiasi hicho. Kitu gani kinatufanya tushindwe kukopa wakati fursa hiyo ipo. Kwa hiyo, naomba kusisitiza kwamba, haitawezekana kufikia malengo ya huu Mpango wa Maendeleo kama hatutakopa. Kama hatutakopa maana yake tuendelee kutegemea Wafadhili na Wafadhili ndio hao tunuju wana ugumu wa kutoa fedha hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niingilie suala la majirani, tumelizungumza sana hapa. Kenya, Uganda, Rwanda

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. BRIG. JEN. H. A. NGWILIZI]

wanafanya hivi. Maoni yangu ni kwamba, wanafanya hayo kwenye nchi zao. Kenya, Uganda, Rwanda na majirani wote, wao ni majirani, tupende tusipende, jirani huwezi ukasema kwa sababu anafanya hivi humtaki akae pale, ataendelea kuwepo tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Sasa nimwite Mheshimiwa Gekul, atafuatiwa na Mheshimiwa Lowassa nafikiri na Mheshimiwa Batenga.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi ili nichangie machache yaliyopo katika Mpango uliopo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote niseme kwamba nchi yetu hajakosa mipango. Nchi yetu ni mahiri kuwa na Mipango, lakini *political will*, ukubali wa kisiasa wa viongozi tulionao ndio tatizo, kwa sababu tunaona katika kitabu alichotupatia Mheshimiwa Waziri deni la Taifa linakua kufikia trillioni 24.4 na mpango huo unatekelezwa kwa trillioni 8.9 wakati fedha za ndani ni trillioni 2.9.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unaona ni jinsi gani hata zile fedha chache tunazozikopa zinapotea kwa njia zipi. Kwasababu kama deni la Taifa linakua na tunakuwa na Mipango ya mwaka mmoja, miaka mitano hadi miaka mingapi, lakini hakuna *political will*. Hakuna usimamizi wa viongozi ambao wanapeleka fedha zikaenda kwa wakati na tukatengeneza mipango tuliyonayo, ni janga kwa Taifa na ni aibu kwa Taifa letu miaka 52 ya uhuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipaumbele katika Mpango huu tulionao, ni suala zima la miundombinu. Mimi kama Naibu Waziri Kivuli nilishauri katika mwaka wa Bajeti uliopita, tukazungumzia sana kuhusu bandari yetu ya Dar-es-salaam, tunakazungumzia ujenzi wa bandari unaoendelea Bagamoyo, lakini tukazungumzia jinsi ambavyo tunapanua

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. P. P. GEKUL]

hizi barabara na madhara yake au umuhimu wake kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishauri tena Serikali hii ambayo inaitwa sikiivu, lakini nina wasiwasi kwamba haisikii. Suala zima la wenzetu wa East Africa kujitoa, naomba msinibeze, ninyi ambao mpo katika madaraka na mmepewa nafasi hizi na Watanzania. Kwa sababu lazima tutapata mdororo wa uchumi, Bandari ya Dar-es-Salaam, wenzetu wameitenga, lakini wakati huo huo tunataka tupeleke vipaumbele hivi, tuendelee kujenga bandari Bagamoyo, mara Kisarawe mara wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niishauri Serikali mkatafakari kwa upya mawasiliano tuliyonayo na wenzetu na athari ya uchumi ambayo tunakwenda kuipata dhidi ya mipango hii tuliyonayo. Tuklendelea hivi usishangae uchumi wetu ukadorora na pato la Taifa likashuka, lakini wakati huo huo hatuko tayari ku-review mpango tulionao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaweza tukawa na mpango, lakini unapoanza safari, ukifika nusu ya safari lazima u-review na unapoona mambo hayaendi ni vizuri Serikali ikakaa chini na ku-review mipango tuliyonayo. Je, hii mipango tuliyotunga tangu wakati huo kuna sababu ya kuendelea nayo, kuna sababu ya miundombinu kuendelea kuwa kipaumbele au kuna mambo mengine lazima tuyaweke hata kama safari yetu ilikuwa miundombinu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishauri tu kwamba Waziri wa Ujenzi na uchukuzi wakae chini. Kwa mfano, kuna zoezi zima la Wizara ya Ujenzi kutengewa fedha nyingi sasa katika huu Mpango kwa sababu huu Mpango ndio unatupelekea kwenye Bajeti. Tuna fedha nyingi tunatenga karibu ya triliioni moja katika barabara zetu, lakini wakati huo upande wa uchukuzi unadorora. Nishauri wakae chini waangalie, kuna sababu ya Mheshimiwa Magufuli kuendelea kupewa fedha nyingi wakati Wizara nyingine ambayo inategemeana na hii inatengewa fedha chache.

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*  
[MHE. P. P. GEKUL]

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mpango huu tulionao upande wa barabara, nishauri Serikali kuna wale wananchi ambao walikuwa katika mita zilliongezeka katika kupanua barabara kutoka 22 zikafika mita 30. Wale wananchi sio wa Mkoa wangu wa Manyara tu ambao wanalamika kuhusu barabara inaunganisha Dodoma na Manyara. Wananchi wa pale Bonga hawajalipwa katika mita 30 muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inasema kwamba hii Mipango ni endelevu na hifadhi ya barabara itunzwe kwa mpango tulionao sasa wa nchi nzima. Tuangalie kwa nini tusiwape kipaumbele wale wananchi ambao wamekaa muda mrefu na wanaidai Serikali fidia kwa nini tusiwapatie fidia hizo? Naomba mkae chini Wizara hii mwangalie kwa mapana zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la maji vijijini. Wabunge wengi wamechangia katika hili, nishauri, mradi wa Maji wa *World Bank* umeshindwa. Tilitenga katika Bajeti iliopita zaidi ya bilioni 184 kwa maji vijijini. Mheshimiwa Waziri amesema kwamba ni asilimia 57 tu ya wananchi wanaokaa vijijini, wananchi milioni 22 ndio wana *access* na maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwa Mkoa wangu wa Manyara na kwa Mikoa mingine Mradi wa *World Bank* umeshindwa na ndio maana nasema lazima tuangalie nyuma tulipotoka, huku tunakokwenda tunafika au tunaendesha tu hili gari ilimradi lifike?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishauri sasa tusijifiche, Serikali isifanye *World Bank* kama kichaka cha kujificha dhidi ya matatizo ya wananchi ya maji. Tuangalie, tupange fedha zetu za ndani, vile visima ambavyo sasa *World Bank* wameshatujengea hadi hapo kwa mkopo ule, visima vina maji, tutenge fedha zetu tutandaze sasa mabomba maji yaende kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu kati ya Wizara ambayo inaongoza kwa maswali mengi Bungeni ni Wizara ya Maji. Hata tatizo la maji katika Jiji la Dar-es-Salaam

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. P. P. GEKUL]

Mheshimiwa Mnyika amekuwa akilisemea sana, lakini ni kwa nchi nzima. Kwa nini tuisitenge fedha zetu za kupeleka maji sasa vijijini kupitia visima hivi tukatenga fedha za kutandaza yale mabomba, haya maji yakafikia kwa wananchi. Badala ya Waziri kuja kila siku na kusema maji yamepatikana, visima vimechimbwa, lakini hayajawafikia wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali kwamba, tu-review mpango mzima wa *World Bank* ili hata haya maswali ya Wabunge yaishe kabisa, maji yapatikane kwa wananchi, vinginevyo ni janga kubwa kwa Serikali ya CCM.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la afya, kwa kweli bajeti ya Wizara ya Afya tuliyotenga *last time* katika mwaka wa bajeti ilikuwa zaidi ya billioni tisa kwa ajili ya kusafirisha wagonjwa wale ambao wanafuata matibabu nje ya nchi. Hivi tunavyoongea Wizara ya Afya ile bajeti imesha-*bust*. Tuna wagonjwa wengi tunawapeleka nje ya nchi wenye matatizo ya *cancer* na matatizo ya moyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali hivi ni mpaka lini tutatibu watu wetu nje ya nchi kwa miaka 52 ya uhuru? Ni kwa nini tuisitenge fedha kwa ajili ya kununua vile vifaa vinavyohitajika pale *Ocean Road*, kwa nini tusikate huu mrija wa kupeleka wagonjwa nje ya nchi, tutibiwe viongozi wote humu ndani ya nchi kama vile wananchi wanavyotibiwa hapa katika nchi hii. Naomba hili lifanyiwe kazi, vinginevyo ni aibu kwa Serikali yetu kwa miaka 52 ya Uhuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Utawala Bora, nimeona katika kitabu hiki Waziri akisema kwamba, miongoni mwa mambo ambayo ametoa kipaumbele ni ujenzi wa majengo ya *PCCB*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni juzi tu Rais wakati anahutubia Viongozi wa CCM hapa Dodoma akasema athari ya rushwa ndani ya Chama chake, lakini mnaona Maaskari barabarani wakichukua rushwa peupe, mabasi yote yanatoa shilingi 5000, shilingi 10,000, Viongozi

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*  
[MHE. P. P. GEKUL]

mnaafahamu, Mahakimu Mahakama ya Mwanzo wananyanyasa wananchi wetu, wanachukua rushwa waziwazi, PCCB hawafanyi kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa Mkoa wangu wa Manyara hawatusaidii kabisa, hatuna sababu ya kutenga fedha, eti tunajenga majengo ya *PCCB* wakati Mabaraza ya Ardhi yamejaa rushwa, Mahakamani rushwa, hospitalini, barabarani rushwa kweupe kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili halitakubalika na Wabunge tuungane, suala la *PCCB* kujengewa majengo mazuri wakati Walimu hawana nyumba za kuishi, wakati Polisi hawana nyumba za kuishi, wale wanaochukua rushwa na Polisi wanaongoza katika ripoti mbalimbali, lakini asubuhi tumeona kwamba, hata Mahakama za Mwanzo hazipo, kuna sababu gani ya kujenga ofisi za *PCCB* wakati wameshindwa kufanya kazi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, unakwenda kwenye uchaguzi rushwa inatolewa na sheria tumeitunga, unaita *PCCB* wanasema mpaka tuongee na Hosea! Kwa nini haya yanaendelea na sisi Wabunge tunatenga fedha kwa ajili ya kuwapa watu ambao wameshindwa kazi yao! Naomba hizi fedha za *PCCB* zikalipe posho za Wenyeviti wa Vijiji ambao mpaka sasa hawana posho, hizi pesa za majengo ya *PCCB* zikalipe mishahara ya Walimu, Madaktari, Polisi; rushwa nchi hii *PCCB* wameshindwa kuidhibiti. Naomba iondoke katika vipaumbele vyetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe, tunakwenda kwenye uchaguzi wa Serikali za Mitaa...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Nimwite sasa Mheshimiwa Edward Lowassa atafuatiwa na Mheshimiwa Batenga.

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. E. N. LOWASSA]

**MHE. EDWARD N. LOWASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuchangia mapendeleko haya ya Mpango wa Maendeleo, lakini nianze kwa kumpongeza Waziri na Tume ya Mipango kwa kazi nzuri mliyoifanya, hongereni sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekaa Bungeni hapa zaidi ya miaka 20, ni lazima nikiri kwamba Kamati yetu ya Bunge inafanya kazi nzuri sana. Sijawahi kuona toka nimekuwa Bungeni Kamati inayofanya kazi nzuri kiasi hiki kama ilivyofanya kwa wakati huu, hongereni sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikupongeze wewe mwenyewe kwa kuleta pendekezo la kuwa na Kamati ya Bunge ya Bajeti, ni wazo zuri sana na linazaa matunda mazuri sana, hongera sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, yamesemwa mengi, kwa hiyo utaniwia radhi nikirudia, lakini nianze na machache. Jambo la msingi moja lilolozungumziwa sana ni *resources* za kufanya kazi hii, je fedha zipo na kama zipo zinatumikaje na uzoefu huko nyuma umekuwaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Bunge imeeleza vizuri sana kwamba, kuna matatizo ya fedha kutotumika vizuri, kuna matatizo ya Tume ya Mipango kutosimamia fedha zikapatikana vizuri. Lakini la pili wamesema kuna vipaumbele vingi mno, kwa hiyo, utekelezaji wake unakuwa ni matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa nijikite kwenye suala la vipaumbele vingi mno. nadhani tungechagua vipaumbele vichache tukavismamia, tukavitekeleza. Tukiwa na vipaumbele vingi kwa wakati mmoja hatutekelezi vyote. Tuangalie nini kinawezekana, nini muhimu ambacho mkikianza kitakwenda kwa kingine. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mapendeleko machache, ningekuwa mimi ningeanza na kipengele cha ajira. Huwezi kuzungumza mipango bila kuzungumza habari ya ajira, huwezi kupanga mipango yejote bila kuzungumza

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. E. N. LOWASSA]

habari ya ajira. Kukiri kwamba kuna Watanzania wengi waliomaliza *form four*, waliomaliza *form six*, waliomaliza darasa la saba walipo mitaani hawana kazi, hawana ajira, tusipoangalia watakuja kula sahani moja na sisi, tusipowashughulikia. Siyo lazima yatokee yaliyotokea Kaskazini mwa Afrika, lakini tusipoangalia yatatuufika na sisi hayo hayo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, simwoni Waziri wa Fedha hapa, kwenye Mkutano wa *World Bank* mwaka huu walikaa kuzungumza habari ya m dororo wa uchumi Ulaya, nchi moja ambayo uchumi umedorora sana na Spain. Spain ikatoa mfano kwamba, walikuwa na *unemployment* inayofikia vijana asilimia 50, wakaamua bajeti yao na mipango yao ya kufufua uchumi wao inajikita kwenye *jobs created*, umezalisha ajira ngapi ndipo unapoju uchumi unakwendaje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikawa kila Mwekezaji anayekuja, anapewa sharti la kuwekeza katika ajira ya vijana. Katika miaka miwili, mitatu Spain imetoka kwenye matatizo hayo kwa sababu imeangalia suala la ajira. Ni lazima tuliangalie suala la ajira kwa umakini sana, ni muhimu sana. Mipango mingine haiwezekani bila kutazama suala la ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuwapongeza Mkuu wa Mkoa wa Tabora na Mkuu wa Wilaya ya Igunga, wameanza kuangalia suala la ajira ya Vijana. Inawezekana sana kila mmoja akiamua kulishughulikia, kila Wizara ikiamua kulishughulikia, linawezekana. Yule Mkuu wa Mkoa na yule Mkuu wa Wilaya wameamua kuchukua vijana waliomaliza Chuo Kikuu wamewatafutia mashamba, wamewatafutia trekta, wale vijana wanafanya kazi nzuri sana. Kwa hiyo inawezekana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, benki ya *CRDB* imeamua kushughulika na vijana ambao hawana *collateral*, wanachukua vyeti vya kumaliza Chuo Kikuu anapewa mkopo, ni hatua ya kutoa ajira kwa vijana. Kwa hiyo, pendelezo langu la kwanza, ajira ndio ingekuwa kipaumbele chetu cha kwanza.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. E. N. LOWASSA]

Mheshimiwa Mwenyekiti, pendekezo la pili ni elimu, ameisemea vizuri msemaji, tuangalie jamani mjadala huu juu ya elimu tusiupuuze, ilko tatizo la msingi katika elimu yetu. Hizi hatua zinazochukuliwa hazitoshelezi. Nilitegemea Kamati hii ingepata taarifa ile ya Waziri Mkuu iliyoolewa juu ya elimu kama ingetupa baadhi ya matatizo wanafanya nini ili tuangalie tunafanya nini. Haitoshi kuchukua wanafunzi wengi kumaliza Vyuo Vikuu wakati akienda kwenye *market* digrii ile haifai, haipo katika *market*. Unamfundisha ana digrii lakini kazi hamna. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu Wajerumani wanagawa digrii nusu na hawa walio na *skills* nusu, yule anayemaliza *Skills* ana hakika ya ajira, yule anamaliza Chuo Kikuu ana hakika ya ajira. Sisi wanaomaliza Chuo Kikuu hapa wengi hawana hakika ya ajira kwa sababu ya aina ya *education* tunayoitoa, *we are not imparting skills*. Kwa hiyo, ingekuwa ni maoni yangu, kipaumbele cha pili kingekuwa ni elimu, tuipe mkakati unaostahili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kelele zinazopigwa na wananchi juu ya elimu; inafaa tufanye mjadala nchini, tuzungumze, kuna tatizo gani na elimu yetu, tufanye nini cha uhakika. Tusipoangalia tutaachwa na Jumuia ya Afrika Mashariki, tutaachwa na *SADC*, tutaachwa na dunia, tutakuwa wababalishaji katika soko la dunia. Tuwasaidie vijana wetu, tubadilishe mfumo wa elimu, tuangalie tunaweza kufanya nini kizuri zaidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipaumbele cha tatu kwa maoni yangu, ni reli ya katii. Namsifu sana Dkt. Magufuli kwa kazi nzuri sana aliyoifanya ya barabara, lakini barabara zile zimeanza kuharibika kwa kasi ya hali ya juu sana. Nimetoka Singida juzi, inaharibika vibaya sana, ile ya Shinyanga inaharibika vibaya sana, kwa sababu malori yanayopita ni malori ambayo yanapaswa kutembea kwenye treni yanatembea kwenye barabara, barabara zinaharibika sana. Nawaomba muiangalie reli ya katii kwa haraka sana. (*Makofii*)

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*  
[MHE. E. N. LOWASSA]

Mheshimiwa Mwenyekiti, muda umekwenda, lakini suala lingine tuangalie suala la foleni Dar es Salaam, *it is nightmare!* Nakupongeza sana Dkt. Mwakyembe kwa kazi nzuri unayoifanya hongera sana, *keep it up.* (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini haitoshi jamani, muda wa saa tunazopoteza Dar es Salaam ukizipanga kwa ajili ya uzalishaji ni muda mrefu sana. Serikali haiwezi kukaa hivi hivi, *this is a disaster!* Haiwezekani mkakaa hivi hivi, mtafute njia ya kuangalia mnafanyeje foleni ya Dar es Salaam, sasa siyo kungoja, *it must be done now,* vinginevyo tunaharibu sana uchumi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho. ni ile *Presidential Implementation Unit.* Napongeza sana uamuzi wa Serikali kuanzisha *Presidential Implementation Bureau,* hongereni sana, lakini ningetaka mjiulize maswali machache, je, wana meno? Tatizo la nchi hii mnazungumza mambo, hakuna utekelezaji! (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazungumza lakini *discipline* ya Malaysia na hapa ni tofauti, hapa kuna Uswahili mwingi wa kukaa bila kutekeleza mambo, mnaamua lakini hamtekelezi. Kinatakiwa chombo ambacho kinaweza kufanya maamuzi magumu na yakawa maamuzi magumu yanayotekelzeza kweli kweli. Bila kujivisha joho la kufanya maamuzi kwa utekelezaji wakawa na *sanction* wanazoweza kufanya itakuwa ni kazi bure. Ni uamuzi mzuri, lakini usipoangaliwa itakuwa ni kazi bure, ni lazima wawe na meno ya kuuma. Mkishakubaliana mambo yafanyike. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani katika nchi kila mtu akawa analalamika, Kiongozi analalamika, mwananchi analalamika, Serikali inalalamika. Haiwezi ikawa ni jamii ya kulalamika, awepo mtu mmoja anayefanya maamuzi na anayechukua hatua. Bila kuchukua hatua tutaendelea kulalamikiana. (*Makofii*)

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. E. N. LOWASSA]

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, nirudie moja la Afrika Mashariki, tusigombane na Kagame na Uhuru na Museveni hamna haja, wameamua kwenda Sudan ya Kusini, sisi tunaweza kwenda East Congo ambako ni kuzuri zaidi. Tunachohitaji ni kufufua reli ya kat. Tukifufua reli ya kat. tutafanya vizuri zaidi kuliko wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. (*Makof*)

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Batenga, atafuatiwa na Mheshimiwa Moza Said.

**MHE. ELIZABETH N. BATENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili nichangie kidogo katika mjadala ulio mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ningekuwa nimepata nafasi, ningesema dakika tano zangu apewe Mheshimiwa Lowassa aliyemaliza kuzungumza sasa hivi kwa kuwa alikuwa anatupeleka vizuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mipango ni mizuri na nampongeza Mheshimiwa Wassira kwa namna alivyowasilisha, lakini pia nimpongeze Mwenyekiti wa Kamati yetu ya Bajeti. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mipango hii ni mizuri, lakini kama kila Mtanzania, nasema kila Mtanzania kwa sababu inaonekana kwamba watu wengi hawafanyi kazi kwa kadri ya uwezo wao wote. Kwa hiyo, Serikali ina kazi kubwa ya kuhamasisha watu kufanya kazi, kila mtu mahali alipo aweze kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muda mwingsi ofisi nydingi ukienda unakuta kila Ofisi ina TV, watu wana simu, mtu anaweza akawa ana simu mbili tatu, muda mwingsi sana

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*  
[MHE. E. N. BATENGA]

anaupoteza kwenye kupokea simu na kuongea na simu na kuangalia TV. Nakuwa na mashaka sana kama atakuwa na uwezo mkubwa wa kufanya ile kazi iliyomweka pale ofisi. Kwa hiyo, naomba matumizi ya TV, matumizi ya simu maofisini yaweze kupangiwa utaratibu ili kuwaruhusu watu waweze kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nizungumzie kuhusu miundombinu mingi ya nchi yetu ambayo mingi sasa hivi haifanyi kazi. Reli ya katи haifanyi kazi kwa uwezo wake wote, reli ya TAZARA haifanyi kazi kwa uwezo wake wote, hii inasababisha hata bandari kwa mfano, bandari ya Mwanza, bandari ya Bukoba, bandari ya Musoma na bandari nyingine kutoweza kufanya kazi kwa uwezo wake kwa sababu haipati mzigo wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono kwamba kwanza tutengeneze vile vilivyopo, reli ya katи itengenezwe vizuri na hata reli ya TAZARA iweze kutengenezwa ili kupunguza matumizi ya barabara kwa malori haya makubwa, kwa sababu barabara zinakula pesa nyingi na zinatengenezwa kwa bei kubwa, lakini baada ya muda inaharibika hivyo inabidi kufanyiwa matengenezo. Kwa hiyo, naomba sasa tujielekeze kwenye kutengeneza reli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie reli niliyoisoma katika ukurasa wa tisa wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri kwamba. kuna reli itatengenezwa kutoka Isaka kupita Keza kwenda Msongati. Sehemu ilipo Keza naifahamu kwa sababu ndiyo kwetu. Lakini jirani na Keza kuna mradi wa Kabanga Nickel/ambao umesuasua muda mrefu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakuwa wakati mwingine tunausikia wakati mwingine unapotea masikioni hatuusikii, sasa hatuelewi Serikali inafanya nini kwa sababu hii reli ambayo itatoka Isaka kupita Keza kwenda Msongati, Burundi wao wenzetu watakuwa wana nickel ya kusafirisha, sisi

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. E. N. BATENGA]

Tanzania tutakuwa tumenufaika nini na hii reli ambayo itapita katika maeneo yale ya Keza, Mgarama na kupita kwenda Burundi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali ioanishe mipango yake, Waziri wa Nishati nilisikia ametia sahihi mkataba wa kufua umeme eneo la Rusumo. Umeme huu wa Rusumo kama kweli utafanikiwa, lakini pia na reli hii inayokwenda Msongati itafanikiwa, basi Mradi wa Kabanga *Nickel* uanzeli na sisi hiyo reli iweze kutusaidia badala ya kwenda kusaidia wenzetu wa nchi jirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba wahusika wafanye hima kuhakikisha kwamba huu mradi wa Kabanga *Nickel* kama kuna matatizo, kama ni wawekezaji hawajapatikana, lakini pia hata miundombinu bado hajawa tayari, vitu vyote hivi viwe tayari ili maeneo yale na yenye yaweze kufaidi hayo matunda ya uhuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema hizo dakika zangu kama ningekuwa nimepanga vizuri, Mheshimiwa aliyenitangulia angeweza kuzitumia kwa mafanikio zaidi.

**MWENYEKITI:** Aliyetangulia hawesi kurudia ameshamaliza ulikosea. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Moza hayupo, Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga atafuatiwa na Mheshimiwa Diana Chilolo.

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nami ningependa kuchangia kidogo Mpango wa Maendeleo ya Taifa. Nikianzia na eneo la utawala bora, ningependa katika mpango huu ungetueleza wazi kwa sababu haukuingiza mpango wa uundwaji wa Mikoa mipyä, Wilaya mipyä, Halmashauri, Kata na Miji midogo.

Kwa hiyo, ili kuendana na mpango ambao unaweza ukakidhi vigezo, ni vyema hivi vitu vingeingia kwenye mpango; hii Mikoa, Wilaya, Kata zingeingia kwenye mpango kwa sababu tunapoamua kuanzisha utawala wa maeneo mapya hutumia gharama kubwa sana. Hivyo ningeomba mpango huu ungezingatia hayo, kwani katika mpango wa kuunda Mikoa mipyä tunahitaji ardhi, watu na rasilimali viende sambamba. Tusiangularie tu wingi wa watu bila kujua ardhi kama inaweza ikatosha na hii ndiyo inapekelea ugomvi baina ya wakulima na wafugaji kwa sababu tunaanzisha Mikoa mipyä, Wilaya mipyä, Kata mipyä bila kuzingatia ardhi. Je, matumizi yatakuwa yako sawa na mipango ambayo tumeenda nayo?

Kwa hiyo, ningeomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kufanya majumuisho aweze kuingiza huu uundwaji wa utawala mipyä katika mpango ambao ametuletea hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa hatizingatii hilo, ndiyo maana tumeshindwa kufikia malengo ya mpango kwamba matumizi ya kawaida yawe asilimia 65 na matumizi ya maendeleo yawe asilimia 35. Hapo hatutafikia kama hatutaweka mipango yetu vizuri ili tuweze kutoka tulipo na tusiwe na mipango ya kuandika bila utekelezaji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa niongelee kidogo suala la uvuvi. Katika uvuvi inachangia pato la Taifa asilimia mbili. Lakini kuna wavuvi zaidi ya laki tatu katika bahari, mito na maziwa makuu, wavuvi wanafanya kazi ya uvuvi. Pia tunapata tani zisizopungua 40,000 katika uvuvi huo. Lakini katika mpango nilikuwa na pendekezo dogo. Hao wavuvi wakubwa wa meli ambazo zinazokuwa katika bahari

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. M. A. KIMWANGA]

ya Hindi wanatozwa leseni tu za uvuvi. Mimi nilikuwa napendekeza hawa sasa walipe mrahaba ili nchi iweze kuijidesha na tuweze kupata pesa na tuweze kuepuka kuwasumbua wavuvi wadogo wadogo ambao wanasmuliwa bila sababu zozote za msingi. Kama hawa wavuvi wakubwa watalipa mrahaba, unaweza ukachangia kuendeleza wavuvi wadogo na wao wakaweza kukopeshwa kuititia mrahaba huo huo na wao wakaweza kujikwamua. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi Serikali inawabana zaidi wavuvi wadogo kwa kuwatoza leseni zaidi ya mara moja. Mvuvi mdogo anaweza akakata leseni katika Wilaya ya Illemela, lakini akiingia Wilaya ya Nyamagana tu, anaombwa leseni nyingine. Akate leseni nyingine au alipe faini au alipie ushuru. Akitoka hapo akienda Sengerema anaombwa tena leseni hiyo hiyo Lakini hawa wavuvi wakubwa hawalipi mrahaba, wanavua wanatumalizia mali zetu za asili kuanzia kwenye madini, mpaka kwenye uvuvi. Wao wanajiita tu wawekezaji, lakini ningependekeza katika Mpango huu wavuvi waongelewe kwa uwazi zaidi na wavuvi wakubwa walipe mrahaba ili wavuvi wadogo waweze kujikwamua na siyo kuangamizwa kila siku. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuongelea tena kuhusu suala la Vyuo vya VETA. Mpango unasema kwamba katika masuala ya elimu katika Vyuo vya VETA kufikia mwaka 2025 tutapata wahitimu ambao ni watalaan 635,000, lakini mpaka sasa tumeshapata watalaan 116,000 tu. Huu Mpango unaonekana unasuasua na kwa usuasuaji huu, hatutafikia malengo ya Mpango. Ni vyema sasa tukaangalia walimu katika Vyuo vya VETA, vitendea kazi katika Vyuo hivi na kuwajali wanafunzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba tumejenga Vyuo vya VETA, lakini Vyuo vingi tunajenga havina vitendea kazi, havina mabweni ya kulala wanafunzi; na tunafahamu kabisa wazi, kuna vijana wamemaliza Kidato cha Nne, kuna vijana wanamaliza Darasa la Saba wanajunga na VETA, lakini ukiangalia hata malazi yao, yaani

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. M. A. KIMWANGA]

hakuna mabweni. Vijana wengi wanatakiwa kwenda kukaa nje ya mabweni. Huu ni mwanzo wa kuwaachia watoto wengi uhuru wengine wakiwa wadogo ambaao wamemaliza Darasa la Saba, kujitegemea pasipo na sababu.

Sasa katika Mpango huu wangeongea wazi, pamoja na kwamba wataongeza Vyuo vya Ufundii, lakini waongee wazi kwamba wataongeza wataalam, wataongeza vitendea kazi, waweze kwenda sambamba na mpango wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ningependa kuchangia kidogo upande wa maji. Ni aibu kwa Mikoa ya Kanda ya Ziwa; pamoja na kwamba tunaambiwa kuna Mpango wa Miradi Mikubwa, lakini ni aibu upande wa Kanda ya Ziwa, mtu anakaa hata mita 200 haifiki eti naye ana shida ya maji. Huu Mpango ungekwenda vizuri ukaangalia wale watu walioko kando kando ya maziwa angalau iwe Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika na ziwa lingine lolote lile ili watu hawa wawewe kupata maji bila usumbu.

Kama Mpango hautawaangalia watu wanaokaa kando ya kando ya maziwa, hawa watu wanaokaa mbali zaidi, kwa mfano hawa wanaotaka maji ya Ziwa Victoria yaende Tabora, yatafika leo kama mtu anakaa kando ya ziwa hapati maji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tungewaomba, pamoja na jitihada ambazo Serikali inafanya, iongeze mara mbili ili tuweze kufika vizuri katika Mipango ambayo tunayoipanga. Siyo kupanga tu! Kikubwa tungeomba utekelezaji. Kwa sababu kama kupanga tumeshapanga sana, lakini utekelezaji ni hafifu. Tungeomba utekelezaji uende kwa kasi na Mpango wenyeewe tunaoujadili na pia tungeomba Waheshimiwa Mawaziri wasikilize haya waende wakayafanyie kazi ili tuweze kutoka hapa tulipo na tuweze kusonga mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Nilisema anayefuata ni Mheshimiwa Diana Chilolo, atafuatiwa na Mheshimiwa Pamba. Wengine nitawataja baadaye.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie nafasi ya awali kabisa kukupongeza wewe binafsi kwa kazi nzuri uliyofanya ya kuunda Kamati ya Bajeti ambayo ni Kamati mtambuka. Kwa kweli Kamati hii imeonesha jitihada za juu sana. Ninaamini kama Kamati hii tutaiunga mkono na tutaoa ushauri sambamba na Kamati hii, ninaamini sasa Bajeti ya nchi yetu itakwenda vizuri, italeta maendeleo kwa maslahi ya Watanzania. Mungu akubariki sana. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile nimpongeze Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana kwa kuleta mpango wa bajeti nzuri kabisa na naomba tu uwe tayari kupokea ushauri wa Waheshimiwa Wabunge ili uweze kuboresha mpango wako. Baada ya kupongezi hizo na kumpongeza Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti, sasa naomba nishauri baadhi ya mambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku zote kupanga ni kuchagua na sisi lazima tuwe watu wa kuchagua na vile vile unapochagua vipaumbele vyako katika kuandaa bajeti yako, lazima uangalie: Je, una uwezo wa kifedha kwa kiasi gani? Ni lazima sisi Waheshimiwa Wabunge tuisaidie pia Serikali, ni jinsi gani inaweza ikapata fedha. Ninaamini Serikali inashindwa kutekeleza mipango yake vizuri kwa sababu ya kuwa na fedha ndogo. Ndiyo maana kila wakati tunaambiwa sungura mdogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani Serikali haijaangalia vizuri vyanzo vyake vya fedha. Nilikuwa naongea na msomi mmoja Dar es Salaam wa Chuo Kikuu ambaye alifanya *research* kwa mitaa minne tu ya Dar es Salaam, pale Sinza, akaenda Makongo Juu, akaenda mitaa minne tu, akagundua kwamba endapo Serikali ingejikita kutafuta kodi ya nyumba tu zinazopangishwa pamoja na nyumba za biashara kwa mitaa minne tu, yule dada wa Chuo

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. D. M. CHILOLO]

Kikuu Dar es Salaam alipata Shilingi bilioni 28. Kama mitaa minne inaweza ikatoa Shilingi bilioni 28: Je, tukikusanya mapato hayo kwa Kinondoni nzima, tukienda llala, tukienda Temeke na nchi nzima kwa ujumla, tutakuwa na fedha kiasi gani? Ninaamini kabisa vyanzo vyetu tukiviboresha na tukavisimamia kwa kina, mipango yetu ya bajeti itakwenda vizuri. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata tukiamua kwamba sasa tunahakikisha tunapeleka umeme kwenye vijiji vyote, itawezekana kwa sababu tutakuwa na fedha. Hatuwezi tukawa tunaweka mipango bila kuwa na fedha. Namshukuru sana Mheshimiwa Lowassa hapa, ametoa mifano ya Igunga na Tabora ya DC aliyeamua kuwashika vijana wasomi, kuwapa ardhi na vitendea kazi, kuzalisha kilimo.

Ni kweli, ardhi yetu hatujaitumia vlivyo katika kilimo. Tunapita ardhi nydingi humo njiani tukitembea, unakuta hamna chochote kinachoendelea. Siyo hiyo tu, hata tukienda kwenye kilimo cha umwagiliaji, tumejikita kwa kiwango gani? Kimezalisha pato la nchi hii kwa kiwango gani? Tunapozungumza mipango, ni lazima tuzungumze: Je, fedha tunazipata wapi? Hebu tuangalie fedha, tuhakikishe tunazalisha fedha kikamilifu katika nchi yetu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge hawa wameshauri mambo mengi sana na mambo haya wameyaona katika nchi za wenzetu. Hivyo, naomba safari za Wabunge nje ya nchi kwenda kujifunza, bado Mheshimiwa Spika unatakiwa kuendelea kufanya hivyo kama unavyofanya sasa hivi, Waheshimiwa Wabunge waendelee kupata elimu ili waendelee kuishauri Serikali yetu. Unaweza ukaishauri Serikali yako kama na wewe unakuwa na upeo mzuri wa uelewa kwamba wenzetu katika mipango yao wanafanya nini? Wamefanikiwaje? (*Makofî*)

Mheshimiwa Lowassa ametoa mifano ya nchi mbalimbali ambazo zimefanikiwa. Sasa ni sisi Kamati yetu hii, lazima tuipe kipaumbele itembee, ijifunze ilete mipango hiyo katika nchi yetu. Tukifanya hivyo, nchi yetu ina uwezo kabisa

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. D. M. CHILOLO]

kuondoka katika nchi masikini na kuwa katika nchi yenye uwezo hata wa kati. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nataka niseme, ni kweli utekelezaji wa mipango yetu unakuwa duni kwa sababu hata wasimamizi wana mishahara duni. Kila mradi unaoanzishwa, mtendaji wa Serikali anahakikisha kwamba amemega hapo, amejenga barabara, amejenga na nyumba yake. Wanafanya hivyo kutokana na umaskini. Hebu katika mipango yetu tuangalie na mishahara ya watumishi, tuhakikishe nayo imekaa vizuri ili tutakapowapa majukumu ya kusimamia miradi ya maendeleo, waweze kusimamia vizuri na iweze kukamilika.

Mheshimiwa Spikia, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana, na ninaunga mkono Mpango huu. (*Makofî*)

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa kunipunguzia muda. Sasa nitamwita Mheshimiwa Pamba, atafuatiwa na Mheshimiwa Ritta Kabati na Mheshimiwa Augustino Masele atakuwa wa mwisho kuongea asubuhi hii.

**MHE. SALEH A. PAMBA:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati hii, kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia katika Mpango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mengi yameshazungumzwa. Kwa hiyo, itaonekana kama nayarudiarudia lakini kuna maeneo ambayo nitapenda yaweze kuwekewa mkazo hasa wakati wenzetu wa Tume ya Mipango watakapotuletea mpango kamili. Kwa sababu walichotuletea hapa ni mapendekezo tu ya maeneo mbalimbali ambayo yataingizwa kwenye Mpango.

Wakati nikitaka kufanya hivyo nataka nichukue nafasi hii kwanza ni-*declare* kwamba mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Bajeti ambayo iliuchambua Mpango huu kwa kina sana. Napenda nimpongeze Mwenyekiti wangu na Kamati nzima

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. S. A. PAMBA]

kwa ripoti nzuri ambayo imeletwa hapa ili kulisaidia Bunge lako. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna matatizo kidogo katika mpango huu hasa katika masuala ya uandishi. Ukiangalia kutoka ukurasa wa 13 mpaka wa 47 kuna maneno mengi ambayo yameelezwa humo ndani ambayo katika utaratibu wa kuandika wangeweza kuyaleta tu kwenye Jedwali na kuwa na *focus* zaidi katika Mpango wenyewe. Lakini ambalo nataka kulizungumzia limezungumzwa vizuri zaidi hasa katika eneo la ugharamiaji wa Mipango.

Mpango wetu huu tuliuandaa wa miaka mitano tunataka tutumie Shilingi triliioni 44, lakini hali halisi ni kwamba makusanyo yetu na mapato yetu ni Shilingi triliioni tano tu. Kwa misingi hiyo, maana yake ni kwamba mpango huu lazima urudi tena hasa ule mpango wa miaka mitano urudi tena ili tuweze kuangalia *resources* tulizonazo. Kwa hiyo, tuna *resources* kidogo. Kwa misingi hiyo, lazima turudi na kuweza kutoa vipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia katika Mpango huu ni kwamba tuna upungufu karibu Shilingi triliioni tatu kwa kila mwaka. Kwa hiyo, hatuwezi kuendelea kupanga mipango mikubwa wakati fedha zenyewe hazipo.

Wabunge wengi hapa kwamba kupanga ni kuchagua na ni kweli, lazima tufike mahali kwamba tuchague miradi michache ili kusudi kwa fedha chache tulizonacho tuweze kuzitekeleza. Kwa hiyo, napenda nishauri yafuatayo, kwa wenzetu wa Mipango wakati watakapokuja na Mpango. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza ambalo napenda kushauri ni kwamba tusiazishe miradi mipyä mingine. Tutekeleze miradi ile ambayo tunayo sasa hivi; na kama tunataka kuanzisha miradi mipyä basi tuwe na uhaka wa fedha, kama ni za ndani au ni za nje ili tuweze kusonga mbele. (*Makof*)

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. S. A. PAMBA]

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wa pili ambao nataka kuuzungumzia, ni kwamba ukipitia katika taarifa hii ambayo imeletwa na Serikali, utaona miradi mingi sana imekuwa ni viporo. Kwa hiyo, katika mpango unaokuja lazima kuwe na *commitment* ya Serikali ya kuhakikisha kwamba tunamaliza katika kipindi cha miaka miwili iliyobaki kabla ya uchaguzi, miradi yote viporo ili kusudi tuweze kujenga imani kwa wananchi na kuweza kusonga mbele. Hayo ni maeneo mawili ambayo nilifikiri ni muhimu sana katika kutekeleza Mpango wowote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuteleza Mpango kuna changamoto mbalimbali. Mipango yote hii tunayoizungumzia ya Shilingi triliuni 5.2 tunazungumzia juu ya *commitment* na tunazungumzia juu ya manunuzi. Asilimia 70 ya fedha za Serikali zinakwenda kwenye manunuzi na tumeona kabisa kwamba tunayo matatizo makubwa na Sheria ya Manunuzi. Mpango huu wote ambao tutaupitisha hautakuwa na maana kama hatutafanya marekebisho ya dhati kabisa katika *Procurement Act*. Naomba wenzetu wa Serikai kwamba ili tuweze kusonga mbele kwa *speed* tunayoitaka, walete Bungeni hata kwa *certificate* ya dharura tuhakikishe kwamba tunafanya mabadiliko haraka katika Sheria hii ambayo itakuwa ni kikwazo katika kutekeleza Mpango huu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Lowassa amezungumza vizuri sana na sipendi kurudia yale ambayo amezungumzia. Lakini moja nalo ambalo ni kikwazo pia, siyo Sheria bali ni maamuzi, *decision making*; uramu mkubwa ndani ya Serikali katika kutoa maamuzi. Miradi mbalimbali, miradi ya ubia kati ya Sekta Binafsi na Serikali na sekta nyiningine ya Umma inachukua muda mrefu sana. Watu wanazunguka kutoka Ofisi moja mpaka Ofisi nyiningine, *at the end of the day* hawapati maamuzi. Nchi haziendeshwi namna hii! Nchi zinaendeshwa kwa kutoa maamuzi ya haraka. Hao wenzetu tunaozungumzia kwa mfano Malaysia wanatoa maamuzi ya haraka, wanachukua *commitment!* Ukipewa madaraka ya kuongoza, toa maamuzi wenzako wakusahihishe kama umekosea.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. S. A. PAMBA]

Kwa hiyo, hayo ni maeneo ambayo yanataka kubadilisha *focus* na utendaji wetu ndani ya Serikali na kuhakikisha kwamba maamuzi yanatolewa haraka hasa maamuzi yanayohusu masuala ya kiuchumi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo ningependa kuzungumzia ni maeneo ambayo naona katika Mpango hayajapewa umuhimu. Katika mipango yote, eneo la kwanza ambalo lina *potential* kubwa lakini halijapewa umuhimu, halijapewa fedha ni eneo la uvuvi. Mchango wake ni 1% tu katika pato la Taifa. Mwaka juzi, mwaka jana, hakuna fedha zilizotolewa katika eneo hili. Wenzetu wa mipango mwende mkaweke fedha ili kusaidia sekta hii ambayo ina *potential* kubwa ya kuinua uchumi wetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo napenda nilichangie ni utalii. Nchi yetu imebarikiwa, wote tunajua na utalii ni eneo ambalo wewe unaweza ku-*tape* tu na kupata pesa pale, lakini hatutumii fedha za kutosha katika kutangaza utalii. Unatumia dola milioni 10 wenzako wanatumia dola milioni 100. Watakwenda kule ambako kumetangazwa! Nimeona bajeti ya utalii haitoshi hata kidogo. Kutoa tangazo katika CNN ni Dola milioni mbili. Wale mnaowaona Malaysia wanatangaza kwenye CNN na ma-Television ya Kimataifa ni gharama kubwa. Wapeni pesa za kutosha, watalii watakuja nchini. Tanzania ina vivutio ambavyo ni *unparallel*, huwezi kuvilinganisha na nchi yoyote duniani, lakini hatujaweka fedha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ambalo nataka kulizumgumzia ni kwamba Tanzania tumeingia katika uchumi wa gesi, lakini hakuna maandalizi. Hakuna maandalizi ya kuhakikisha kwamba, tunafaidika vipi na gesi hii? Katika miaka mitano ijayo Tanzania itaingia katika uchumi wa gesi; tunataka maeneo mawili yafanyiwe kazi haraka na yaletwe hapa Bungeni. Moja, Sera ikamilike haraka sana. Pili, mlete Sheria ya Gesi hapa Bungeni. Hatuwezi kwenda hivi hivi bila kujua kwamba nchi yetu itafaidika vipi, wananchi wetu watafaidika vipi katika *economy* hii ambayo ni kubwa sana hapa duniani. (*Makofii*)

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. S. A. PAMBA]

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo ni maeneo ambayo lazima yafanyiwe kazi haraka. Hatuwezi kuacha makampuni yaliyoko kule Mtwara yaka-*dictate*, yakatulazimisha kufanya mambo ambayo wao wanaendelea kwa sababu, Sera hakuna. (*Makofii*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa  
Mzungumzaji kwisha)*

**MHE. SALEH A. PAMBA** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja asilimia mia kwa mia. Ahsante sana nakushurukuru kwa nafasi.

**SPIKA:** Ahsante sana. Namwita Mheshimiwa Ritta Kabati, atafuatiwa na Mheshimiwa Augustino Masele.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu na kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa kwa Mwaka 2013/2014. Lakini kabla sijachangia, kwanza nikupongeze kwa kuteuwa Kamati ya Bajeti, Kamati ambayo imekuwa ikifanya vizuri sana na nikushukuru kwa kutuletea haya Mapandekezo ya Mpango mapema kabla hatujaanza kujadili bajeti. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma ukurasa wa 48 wa Kitabu cha Mpango, unaonesha maeneo ya kipaumbele katika mwaka 2014/2015, lakini utaona Mpango umejikita katika maeneo machache yanayoendana na programu ya *The Big Results Now (BRN)*, yaani matokeo makubwa sasa. Pamoja na hayo, ningependa kujua vigezo viliviyotumika katika kuchagua miradi ya vipaumbele. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa kabla ya yote nimpongeze Waziri wa Ujenzi, kwa sababu barabara nyingi sana zimejengwa; naipongeza sana Serikali. Tumetembea maeneo mengi sana na tumejionea jinsi ambavyo barabara zimejengwa. Hata katika Mkoa wetu wa Iringa kwa mfano barabara ya Mtera – Iringa, Mafinga – Iringa

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. R. E. KABATI]

ni kati ya barabara ambazo zimejengwa na Serikali yetu.  
(*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nina masikitiko makubwa sana kuhusiana na Serikali kutokutoa kipaumbele katika reli ya kati. Wabunge wengi sana waliochangia wameelezea kuhusiana na hii reli ya kati. Kwa kweli, naomba niungane nao kwamba, Serikali sasa itoe kipaumbele katika kujenga reli hii. Hii itasaidia kwanza kudumu kwa barabara zetu na vilevile itasaidia sana kukuza uchumi kwa sababu, tumekuwa tukitumia pesa nyingi sana katika kujenga hizi barabara na kufanya matengenezo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma ukurasa wa 53, Serikali katika mipango yake imesema, ili kuboresha eneo la utalii itaendelea kujenga miundombinu na kukarabati miundombinu ya usafiri, lakini haijaainisha ni maeneo gani yamepewa kipaumbele. Kwa mfano, katika Mkoa wetu wa Iringa ipo mbuga ya wanyama ya *Ruaha National Park*. Hii ni ya pili kwa Afrika kwa ukubwa. Mwaka 2012 nililetu swalii langu hapa kwamba hii barabara ni mbovu, miundombinu yake siyo mizuri na tuna imani kama hii barabara ingeimarishwa na kujengwa vizuri ile mbuga ya wanyama ingeweza kutusaidia sana katika utalii na ingeweza ikakuza kipato na ingeleta ajira kwa wana-Mkoa wa Iringa na Taifa kwa ujumla. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tuna kiwanja cha ndege, kiwanja ambacho kama kingepewa kipaumbele, kikajengwa kingeweza kusaidia watalii wengi kuja na kusaidia katika uchumi wetu. Sasa ningeomba Serikali iangalie, kama imeshasema katika mpango wake kwamba itajenga miundombinu katika maeneo ya utalii, basi ijenge miundombinu hiyo ya Kiwanja cha Ndege cha Nduli katika Mkoa wetu na vilevile iimarishe ile barabara inayokwenda katika mbuga za wanyama. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukurasa wa 53, wamezungumzia kuhusu elimu ya mafunzo na ufundi. Wamesema kwamba, mpango wa kuimarisha mafunzo kwa

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. R. E. KABATI]

kuongeza mbinu ya kugharamia elimu nchini. Naipongeza sana Serikali yetu kwa kuweza kutenga zaidi ya shilingi bilioni 306 ambazo walikidhi kuwapa wanafunzi 29,754 kati ya wanafunzi 31,649 ambaao ni sawa na 96%. Lakini vijana wetu wanakabiliwa na changamoto kubwa sana katika huu mkopo ambaao wanapewa katika vyuo vyao; wanafunzi kushindwa kupata mikopo hiyo kwa wakati, matokeo yake kumekuwa na vurugu vyuoni, migomo mingi, kisha wanaleta mpaka maandamano. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Wizara ya Elimu, hebu iliangularie hili suala kwa umakini mkubwa sana. Tunasikia uchungu sana tunapoona vijana wetu wanashindwa kuifikia ile mikopo. Ile *the Big Result* tutaipataje kama vijana hawa kutwa nzima wanafanya maandamano, wanafanya vurugu na Serikali imeshaamua kuwasaidia hawa vijana waweze kupata hii mikopo? Ningeomba Bodii ya Mikopo hii iangaliwe upya ili kuhakikisha kwamba wanafunzi wote wanapatiwa ile mikopo.

Tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwa ajili ya Serikali yetu; sasa hivi Mkoa wetu wa Iringa una vyuo vingi, zaidi ya vinne. Sasa tunajisikia vibaya kwamba tunapokuwa katika maofisi yetu, vijana hawa mara nyingi wamekuwa wakija wakinaka tuwasaidie ni jinsi gani ya kupata mikopo wakati ni haki yao ya msingi. Kwa hiyo, naiomba Serikali izingatie sana vijana wetu waweze kupatiwa hiyo ili waweze kuwa ndio wataalamu wetu, tunawategemea katika nchi hii; ndio Marais wetu Mawaziri wetu wajao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kitabu cha Mpango, sijaona kama imetengwa fedha kwa ajili ya *Researchers*. Sasa sijui bila utafiti tutaweka mipango gani? Ningeomba Serikali iangalie, itoe kipaumbele kwa watafiti wetu. Tunajua kwamba, tukifanya utafiti vizuri katika miradi mingi itatusaidia sana kuhakikisha kwamba tunapanga mipango mizuri ambayo inatekelezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante. Namwita sasa Mheshimiwa Augustino Masele.

**MHE. AUGUSTINO M. MASELLE:** Ahsante Mheshimiwa Mheshimiwa Mwenyekiti, ambaye ni Spika wa Bunge letu kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kutoa mchango wangu katika mpango huu wa Serikali yetu unaohusu maendeleo ya nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nami niungane na wenzangu kukupongeza wewe kwa kutuanzishia hiyo Kamati iliyo makini na ambayo kwayo imepelekea kuwepo na Mapendekezo mazuri ya Mpango wa Maendeleo wa nchi yetu. Hakuna nchi yoyote duniani ambayo imeweza kuendelea isipokuwa na mipango endelevu. Kwa ajili hiyo, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Nchi kwa kuweza kuja na Mpango wetu mzuri wa Maendeleo ambao kwa ujumla umesheheni mambo mbalimbali yaliyoko katika Vitabu vyake vyote viwili; kile kidogo pamoja na hiki kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu imejaliwa mambo mengi, ina rasilimali za kutosha. Mambo yaliyosalia ni ya namna gani tunavyoweza kujipanga na kuyasimamia. Mipango yote iliyolezwa katika Kitabu cha Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano na huu tunaoujadili kwa leo wa 2014/2015 ni mapendekezo ambayo yanatakiwa yapewe msukumo wa kipekee na zaidi sana upatikanaji wa fedha kwa wakati; maana tunapoendelea kuwa tunapanga halafu hatutekelezi, tutakuwa tunatengeneza madeni ambayo tutakuja kudaiwa mbele ya safari, hasa ikizingatiwa kwamba, kila baada ya miaka mitano kuna uchaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Reli ya Kati na Bandari ya Dar es Salaam ni suala ambalo haliepukiki. Tunapaswa kuhakikisha kwamba tunawekeza ipasavyo katika suala la bandari. Maana ukiangalia nchi za wenzetu, nchi za Uarabuni, nchi za Mashariki ya Mbali, zimeendelea kwa kuwekeza zaidi katika Bandari zao. Nasi Mwenyezi Mungu katika uumbaji wake ametujalia kuwa na vitu vyote vitatu; tuna anga, tuna maji, tuna ardhi. Kwa hiyo, tukiwekeza katika

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. A. M. MASELLE]

mambo yote haya matatu, nina uhakika kwamba tutapiga hatua kwa haraka sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la umeme. Nchi zote ambazo zimeendelea duniani hapa zimewekeza kwa kiwango kikubwa katika umeme. Nami niseme tu kwamba, tumshukuru Mungu kwa sababu sisi Waafrika alituumba na akatuweka katika Bara hili ambalo kimsingi halifikwi na yale majira mawili yenye hatari; wakati wa *summer* na wakati wa *winter*. Nchi za wenzetu wanaweza ku-survive wakati huo kwa kutumia umeme. Kukiwa na *summer* wanatumia umeme kuhakikisha kwamba wanapata baridi na wakati wa *winter* wanatumia umeme kuhakikisha kwamba wana-*heat* mazingira yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwetu sisi kwa sababu ya kutokuwa na haya majira, inawezekana ndiyo maana tumekuwa tukipuuzia namna ya kuzalisha umeme wa uhakika. Maana vinginevyo, nchi hii tungeweza kuangamia kama tusingekuwa tumejaliwa na Mungu kuishi katika nchi ambayo ina joto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba tu kwamba, pamoja na majaliwa haya ambayo Mungu ametusaidia tukawa na hali ya hewa nzuri, basi tujipe pongezi kwa kuwa na hiyo hali, lakini tujizatiti katika kuhakikisha kwamba, tunazalisha umeme ambao utatuhakikishia kwamba, tunawekeza masuala ya viwanda. Maana bila kuwa na umeme huwezi ukawekeza viwanda vya kuboresha thamani ya mazao ambayo yanazalishwa katika nchi yetu.

Kwa mfano, nchi yetu inazalisha pamba; kwa hiyo, upo uwezekano mkubwa tu wa kuwekeza viwanda vya nyazi na nguo. Tuna mifugo mingi tu ambayo na yenyewe inaweza ikawa ni chanzo kizuri tu cha kuwekeza katika viwanda vya bidhaa za ngozi, zikiwemo viatu na mambo mengine mbalimbali kama mikoba na vitu vingine. Vitu hivi tukivizalisha katika nchi yetu, tunaweza tukaviuza katika nchi za wenzetu na tukapata fedha za kigeni ambazo zinaweza zikaendeleza uchumi wetu.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. A. M. MASELLE]

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara nyingi nimekuwa nikiuliza hapa suala la kuanzishwa kwa Mamlaka ya Hifadhi za Wanyamapori; na Wizara ya Maliasili imekuwa ikiahidi kwamba itatuletea Sheria itakayounda hiyo Mamlaka. Sasa nashauri kupitia Mpango huu kwamba, suala hili lipewe kipaumbele, kwa sababu mimi ninakotoka tuna pori la akiba la Kigosi, lakini pori hili limeonekana halina maslahi kwetu kwa sababu ya ukubwa wake, lakini lina watumishi kama 30 tu, lakini miundombinu yake ni hafifu na wakati mwingine hata huu uhujumu uchumi unaofanywa na Wawindaji haramu na wenyewe unaathiri eneo hili ambalo kimsingi, kama lingeendelezwa, lingeweza kuchangia kwa vile lingevutia wawekezaji na watalii kutoka nchi za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie pia suala la kiwanja cha ndege cha Mwanza. Najua sasa hivi nchi yetu imeshakuwa na viwanja vyta ndege vyta Kimataifa vitatu; cha Songwe na kile cha Dar es Salaam pamoja na cha Kilimanjaro. Mimi nashauri kwamba, hata kiwanja cha ndege cha Mwanza na chenyewe kipewe kipaumbele kuwa kiwanja cha ndege cha Kimataifa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, kama inavyoonekana muda umekwenda, dakika tano hazitoshii mtu mwingine kuchangia. Tukaporudi, utaratibu wa jioni utakuwa kama ifuatavyo:-

Tutakopofika hapa atapewa nafasi Mheshimiwa Joseph Mbilinyi na Mheshimiwa Chiku Abwao dakika tano tano. Watafuatia na Mheshimiwa Mosi Kakoso na Mheshimiwa Michael Laizer. Hawa ndio watazungumza halafu baada ya hapo tunatoa nafasi kwa Mawaziri mbalimbali kujibu hoja zilizotokana na mjadala, halafu saa 12.30 tunampa nafasi Mtoa Hoja, atakuwa na muda mfupi uliobakia *ku-wind*.

Kwa hiyo, Bunge linarejea. (*Kicheko*)

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*(Bunge lilitrudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyokuwa nimeeleza kwamba tutakuwa na hawa Wachangiaji wachache kutoka kwa Wabunge halafu Mawaziri watajibu, lakini Mawaziri watakapo jibu watajibu kama Wachangiaji tu. Kwa hiyo, wana dakika zao kumi kumi kila mmoja. Halafu tatarudi katika mfumo wa Bunge, ndio Mtoa Hoja atapewa nafasi ya kujibu hoja. Sasa huo ndio utaratibu wa Bunge.

Kwa hiyo, hiyo ndio nafasi tutakayofanya mchana, kwa hiyo, kwa sasa sina tangazo lingine. Nasitisha shughuli mpaka saa 11.00 jioni.

*(Saa 7.00 mchana, Bunge lilitishwa hadi Saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilitrudia)*

*Hapa wabunge walikaa kama Kamati ya Mpango*

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kabla ya kusitisha shughuli za Bunge asubuhi, nilikuwa nimewataja wafuatao kama ndio wasemaji wetu wa kwanza; Mheshimiwa Joseph Mbilinyi atachangia dakika kumi na Mheshimiwa Chiku Abwao; Mheshimiwa Moshi Kakoso na Mheshimiwa Michael Laizer. Mheshimiwa Joseph Mbilinyi, dakika tano.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi kuchangia Mpango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naanza kupoteza kidogo *interest* ya *debate* za Bunge kwa sababu imekuwa sasa kama kila siku toka nimeingia hapa kwa mwaka wa tatu nasema vitu hivyo hivyo na nikisikiliza wenzangu, pia wanasema vitu hivyo hivyo. Kwa hiyo, tumekuwa humu ndani tunaongea mambo hayo hayo. Kwa sababu sasa hivi ni mwaka wa tatu toka nimeingia hapa nadai *ambulance* kwa

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. J. O. MBLINYI]

ajili ya Hospitali ya Rufaa Mbeya lakini kila mwaka naambiya kwamba bajeti itatengwa, bajeti itatengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumza maendeleo mimi naamini kwamba hakuna maendeleo bila watu kuwa na afya. Ile Hospitali pale majengo yake ni mazuri, nawapongeza *management* sasa hivi Hospitali ni safi katika Hospitali safi za nchi hii, lakini haina vifaa, haina *CT-Scan*, haina *MRmashine* ya kufanya vipimo vinavyohitajika vyenye hadhi ya Hospitali ya Rufaa. Mtu anapohitaji tu vipimo kama hivyo inabidi aangalie safari ya kwenda Dar es Salaam. Bajeti yenye we wanayopewa Hospitali ya Rufaa, unasikia Hospitali kama *KCMC* wanapewa zaidi ya bilioni 10, Rufaa nikiulizia unasikia wanapewa 1.5, 1.8 bilioni. Sasa unauliza kwamba ile Rufaa gani kama Mkoa wa Mbeya sasa hivi una watu wengi zaidi ya takribani milioni 2.7? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazungumzia maendeleo ya uchumi, kutanua bandari, lakini sisi Mbeya hatuna bahari, kwa hiyo, tunasema bandari ya nchi kavu.

Kwa mwaka wa tatu nimekuwa naiomba, nashukuru kwenye bajeti iliyopita Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe amatuahidi, lakini kwa sababu nimezoea kwamba ni vile vile, inabidi nitumie fursa hii kusisitiza kwamba ile *dry port* ni muhimu sana kwa uchumi na kama nakumbuka Mheshimiwa Sitta juzi wakati anazungumzia *network* ya reli na umbali na unafuu wa mizigo, unaona wazi kabisa hata sisi pale ile *dry port* ikianza kazi tutapunguza umbali kwa watu kutoka *Congona* watu wataendelea kuchangamsha uchumi wa Mbeya ikiwemo kwa Mheshimiwa Kaka Dkt. Mwakyembe kule Kyela. Kwa hiyo, natumia fursa hii kusisitiza umuhimu wa ile Bandari kupatikana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ile bandari haihitaji bajeti ya kujenga, inahitaji kibali tu na utaratibu wa kiserikali ili tuanzé kufanya kazi pale, ajira kutoka 40 sasa hivi tufikishe ajira 250/300 za *direct* kwa mujibu wa wataalamu wa pale wanavyosema.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. J. O. MBLINYI]

Mheshimiwa Mwenyekiti, michezo pia ni maendeleo, lakini kwenye Mpango huu sijaona wala sijasikia mtu akizungumzia michezo. Inaonekana kwamba bado hatuamini kwamba michezo inaweza ikachangia uchumi au pato la Taifa hili na pia hata kuchangia katika kutangaza utalii wa nchi hii. Lakini michezo bado imekuwa nyuma katika mijadala. Niwape *big up Mbeya*. Sisi Mbeya tunajitahidi na michezo, Chama chetu Mbeya *City* kule kinafanya vizuri, napata heshima hata ndani ya Bunge; nikikutana na Rais wa Simba, Mheshimiwa Rage ananiangalia vizuri kidogo, kwa kujuua tu kwamba ninakotoka kuna *Mbeya City*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kuwaasa vijana kule Mbeya kama Mbunge wao, wapunguze mizuka. Kushangilia kwa kurusha mawe siyo sehemu ya kushangilia, wataiharibu mizuka ambayo tayari imeshakaa sawa. Chama chetu kinakwenda vizuri, nchi nzima inajua sasa hivi kwamba Mbeya kuna *Mbeya City*, kwa hiyo, tutumie nguvu zetu katika kushangilia na kuendelea kuhamasisha timu yetu ili tuwe na *justification* ya kwa nini michezo ni kitu muhimu na inatakiwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la wamachinga naona bado kabisa limekuwa na utata. Bado kwenye Halmashauri zetu tunajadili kuondoa wamachinga hapa, kuwaondoa wamachinga pale bila kuja na mipango madhubuti. Nilikuwa China; wanasema kusafiri ni kujifunza.

Sasa tunakwenda nchi za watu kujaribu ku-*adopt* vitu vigumu ambavyo hatuviwezi, tunashindwa kuiga vitu vyepesi kama suala la kuangalia wamachinga wanafanyaje kazi. Nimekwenda *down town* Beijing, mmachinga anauza mahindi ya kuchemsha, Polisi anapita pale na hamna nchi yenye Polisi wakali kama China kwa historia; lakini kuna mama ntilie pale anauza samaki, anauza nini, kila kitu na hauoni uchafu ndani. Kuna mtu pale Mmachinga *down town* Beijing kabisa, anauza mahindi ya kuchemsha, hauoni Polisi anamsumbuwa, amepewa utaratibu wa usafi, elimu ya usafi, hauoni hata jani moja limedondoka chini, unakwenda sehemu...

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda  
wa Mzungumzaji kwisha)*

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** *Time is too short. Thank you very much. (Kicheko/Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chiku Abwao.

**MHE. CHIKU A. ABWAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ili nami nichangie hoja hii ya Mpango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa muda ni mdogo nitachangia hoja moja tu ambayo inatokana na pato la Taifa. Mheshimiwa Waziri katika kitabu cha Mipango ukurasa wa pili, amezungumzia kwamba pato la Taifa linakuwa na kwa nusu ya mwaka 2013 limeongezeka kuwa 7% toka 6.9%. Lakini ukiangalia hata ukuaji huu wa pato la Taifa bado ni mdogo, na kwa kiwango kikubwa haueleweki kwa wananchi walio wengi ambao ni maskini. Kwa hiyo, tunaendelea kulalamika na umaskini na hata ukisema kwamba kuna ukuaji wa pato la Taifa kwa wananchi wa kawaida wanaona kama vile ni mzaha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naona nichangie juu ya hoja hii kwa kuiomba Serikali, kwa kuwa sasa hivi kuna wanavyuo wengi wamesoma, wamehitimu vyuoni na wengi wamechanganyikiwa kwa kweli hawajui wafanye nini, kwa sababu ajira zimekuwa chache. Nafikiri umefika wakati sasa wa kuangalia huu mtaji wa nguvu kazi ya wanavyuo ambapo Serikali iweke mpango mahususi tu kwa makusudi kabisa kuwasaidia wasomi hawa kwamba wakimaliza Vyuo vyeti vyao viwe mitaji kwa sababu kutokana na hali halisi, hawakopesheki. Kwa hiyo, bila kuwasaidia kwa makusudi hawatakopesheka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ionekane vyeti vyao ndio mtaji wao na kwa kutumia wataalamu ambao najua tunao wengi tu Tanzania, wasaidie hawa wanavyuo kuandaa mipango kazi, waandikie michakato ya kazi hasa

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. C. A. ABWAO]

kuelekeza nguvu zao katika vijiji, wakaboreshe kilimo, wakopeshwe kule kwa kusimamiwa na wataalamu wetu ili waweze kuendesha kilimo na hii itasaidia sana kuboresha uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu hatuna shida katika ardhi, tuna ardhi ya kutosha. Kwa hiyo, wakisaidiwa wanavyuo hawa, wakapewa wataalamu ambao kwa kusaidiana nao wakawaandikia michakato ya kazi, *program* zao zikafanyiwa kazi kuhakikisha kwamba Serikali inakuwa nao kwa kuwafuatilia utendaji wao wa kazi, nina imani kabisa kilimo kitafanikiwa. Kwa Sera ya Kilimo Kwanza nadhani itakuwa ndiyo chanzo cha kuifanikisha zaidi.

Vile vile wanachuo watapata matumaini kwa kujua kwamba hata kama hakuna ajira, wataweza kuijari kwa njia hizo kwa sababu Serikali itakuwa nao bega kwa bega kuhakikisha kwamba wanapata mikopo na katika kuboresha kilimo pia itasaidia kwa sababu watapanuka zaidi, watakopa mashine za kusindika, watakuwa na viwanda vidogo vidogo na matokeo yake ajira zitaongezeka na uchumi utaongezeka kwa kiasi fulani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la wanachuo ni kubwa sana, kama Serikali haitaangalia kwa kina ni jinsi gani tutawasaidia vijana hawa, tutajikuta tunajiingiza katika matatizo makubwa. Mheshimiwa Lowassa siku moja aliyahi kusema kwamba vijana hawa ni bomu la *petrol*. Nami nakubaliana naye kabisa, ipo siku litakuja kulipuka, litatuletea maafa makubwa.

Kwa hiyo, tunawajibika kabisa kuhakikisha tunaweka mazingira mazuri ili wanavyuo waweze kufarrijika kwa kupata ajira kwa kusaidiwa na Serikali. Kazi pia wanapata kwa taabu, maana wanaambiwa wawe na uzoefu. Wana uzoefu wa kipindi gani? Mtu anatoka chuoni, atakuwa na uzoefu gani zaidi ya kwenda *field* kwa muda mfupi sana ambao bado unaonekana siyo uzoefu, kwa sababu anaangaliwa uzoefu wa kwamba awe ameajiriwa sehemu nytingine, ndiyo aende akafanye kazi sehemu nytingine. Bado ni tatizo.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. C. A. ABWAO]

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Serikali iangalie kwa kina hasa namna ya kutumia huu mtaji kwa sababu siamini kama Serikali ilivyoamua kusomesha wanavyuo, kukopesha wanavyuo mikopo haikuwa na lengo. Nafikiri lengo lilikuwa ni kuboresha maisha ya wanavyuo hawa, kuongeza uchumi wa nchi yetu na hasa kuondokana na hili tatizo la umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzangu wengi wameshazungumza, mimi nimeona dakika zangu tano nizungumzie hili suala moja tu la kuongeza ukuaji wa pato la Taifa ikiwa ni pamoja na kupunguza umaskini wa nchi yetu na kuwasaidia wanavyuo ambaao kwa kweli kwa sasa wamechanganyikiwa hawaelewi wafanye nini; elimu zao sasa imekuwa hazina thamani kwa sababu wanakosa namna ya kuzifanya kazi na kujiondoa katika janga la umaskini na shida ya ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haya machache nakushukuru. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, umejadili vizuri. Namwita Mheshimiwa Moshi Kakoso na atafuatiwa na Mheshimiwa Laizer.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Nianze kuchangia kwenye suala la bandari. Bandari ni kitu muhimu sana katika uchumi wa nchi inayokua. Bandari yetu ya Dar es Salaam bado kuna matatizo mengi ambayo yanahitaji kufuatiliwa kwa kina ili iweze kuwa na ushindani mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi ya kipekee kumpongeza Waziri husika Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe kwa kazi nzuri aliyofanya, lakini bado anahitaji kuzama kwa kina ili aweze kutatua matatizo yaliyopo ndani ya bandari ile. Unapoimarisha bandari, unasaidia uchumi wa nchi hii. Kuna kero ambazo zinafanya watumiaji wa bandari wawe na mashaka kutumia bandari yetu. Mimi naamini zile kero zikiondolewa zitasaidia sana kushawishi nchi zinazotumia

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. M. S. KAKOSO]

bandari ile mfano Malawi, Congo, achana na hii nchi ya Rwanda inayokuwa na matatizo; lakini tukiimarisha bandari yetu itasaidia sana kukuza uchumi kwa nchi tu ambazo zinatumia Bandari yetu; Zambia, Malawi, DRC na tukiimarisha bandari nyingine kama ile ya Mtwara, bandari ndogo ndogo za Ziwa Tanganyika zitasidia sana kukuza uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba hilo liangaliwe kwa kina na waliangalie kwa umuhimu wa aina yake ili tuweze kukuza uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni reli. Huwezi kuwa na uchumi mzuri kama reli haifanyi kazi. Maeneo mengi katika nchi zinazoendelea reli ndiyo kiungo muhimu sana cha uchumi wa nchi yoyote ile inayokuwa kiuchumi. Reli yetu ya kati ndiyo reli muhimu sana ambayo inaweza ikapunguza ughali wa maisha kwa Watanzania. Usafirishaji kwa njia ya barabara una gharama kubwa sana tofauti na reli. Mimi naamini tulkiimarisha reli ya kati inaweza ikachangia pato kubwa sana la uchumi wetu, lakini sambamba na hiyo reli ya kati bado kuna *branch* za reli ambazo zinahitaji kuimarishwa ikiwepo reli ya kutoka Kaliwa kwenda Mpanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wengi wa Wilaya ya Mpanda wanategemea sana huduma ya reli, lakini reli iliyopo kwa sasa halfanyi kazi vizuri na treni inayotumika bado ni chakavu. Kwa hiyo, tulikuwa tunaomba uimarishwaji wa reli ya kati sambamba na zile *branch* ziweze kuimarishwa katika hali iliyo bora ili ziweze kufanya kazi vizuri. Mimi naamini kama tutaimarisha reli hizi zikafika mpaka kule kwetu Mpanda na kukawa na mpango unaokamilisha kuweza kupeleka reli mpaka ukanda wa Ziwa Tanganyika eneo la Kalema, tunaweza tukapata kuitumia bandari ile ya Kalemie pamoja na bandari inayojengwa pale eneo la Kalema. Mimi naomba eneo hili liangaliwe kwa kina ili tuweze kusaidia uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo halijazungumziwa sana ni eneo la Sekta ya Uvubi. Tunalo Ziwa

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. M. S. KAKOSO]

Tanganyika ambalo halijafanyiwa uzalishaji mzuri kwenye maeneo ya ukanda wa ziwa kwa sababu hakuna vitu ambavyo vinasaidia ukuaji wa Sekta ya Uvumi. Nilikuwa naomba eneo hili liangaliwe na liweze kupewa umuhimu sana. Kukiwa na uvumi ambao unaweza ukavuliwa kisasa, tukatengeneza miundombinu, inaweza ikasaidia kukuza uchumi wa nchi, tena kwa Wananchi na pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Kilimo ni muhimu sana kwa maendeleo ya Taifa la Tanzania. Watanzania walio wengi wanategemea sana Sekta ya Kilimo. Lakini kwenye sekta hii bado hawajaweka fedha za kutosha. Wananchi walio wengi sasa hivi wanalima kilimo cha mazoea, bado Taifa linahitaji kuandaa wataalam wa kutosha ili waweze kuwasaidia wakulima wadogo wadogo ambao wataweza kuzalisha katika kiwango ambacho, kwanza watafukuza njaa; pili, watakuwa na pato la ziada kama wananchi lakini Serikali itanufaika na pato hilo la Taifa kutokana na mazao yatakayokuwa yanazalishwa hatimaye kuanza kuuzwa nje. Lakini kitu cha ajabu ambacho kwenye Sekta ya Kilimo kinaua kabisa uchumi wa wananchi ni mipango mibovu ya Serikali hasa ya kuagiza chakula cha kutoka nje kama vile mchele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania walio wengi wamepoteza rasilimali zao kubwa kwenye Sekta ya Kilimo na hatimaye kuacha kuwekeza kwa kiwango kikubwa kwa sababu mazao wanayozalisha wananchi walio wengi hayana soko na badala yake, Serikali inaingia katika vitendo vy'a ajabu vy'a kukopa wananchi mazao yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba Serikali iangalie sana na iwekeze fedha za kutosha, hasa kwenye ununuzi wa mazao. Watakapokuwa wananchi walio wengi watawapa motisha wakulima waweze kuzalisha kwa kiwango kizuri na hatimaye wakapata ziada itakayokuwa inakwenda nje. Lakini tofauti na ilivyo kwa sasa, wakulima wengi kile kilichozaishwa bado wanaidai Serikali kitu ambacho kinavunja moyo sana wakulima washindwe kufanya shughuli zao kwa nia nzuri.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. M. S. KAKOSO]

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini bado kuna matatizo ambayo Serikali inatakiwa iangalie na kuyarekebisha katika kipindi muafaka. Eneo hilo ni ugomvi kati ya wakulima na Serikali, hasa kugombania maeneo ya misitu na hifadhi. Karibu maeneo mengi sana Serikali imehodhi ardhi ambayo wakulima au wanachi walio wengi ambao shughuli zao wanazotegemea ni kilimo, hawana mahali pa kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ifike mahali iangalie kwamba Watanzania huko nyuma tulikuwa wachache, sasa hivi tumeongezeka na nina mifano tu kwamba katika Mkoa wangu ninakotoka Mkoa wa Katavi asilimia kubwa ya Mkoa ule ni mapori, hifadhi ya Taifa ya Katavi, *game Reserve*, kila kitu kilichopo pale, hasa misitu ni mali ya Serikali. Lakini wananchi wanazidi kuongezeka katika maeneo yale yale ambayo walikuwa wanafanya kazi toka kipindi hicho cha nyuma. Nalomba Serikali iangalie upya, ifike mahali ipanue wigo iwaachie wakulima maeneo na yaweze kufanyiwa kazi ili yaweze kuzalisha.

Kwenye suala la vijana, vijana ndio wanaotegemewa katika Taifa hili, lakini Serikali bado haijawekeza vizuri kuwasaidia kundi kubwa la vijana. Vijana wanahitaji kuandaliwa mazingira ambayo yatawasaidia kufanya shughuli zao pale wanapokuwa wanahitaji kwenye uzalishaji. Nilikuwa naomba Serikali iandae mpango maalum na kutenga fedha za kusaidia makundi ya vijana ambao wanapomaliza shule hawana shughuli za kufanya. Ni Serikali ikiandaa mazingira ambayo yatawasaidia vijana hawa ni imani yangu kuwa watakuza uchumi kwa sababu watakuwa wanafanya shughuli zilizo halali zinazowaingizia kipato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nilikuwa naomba nizungumzie suala la misamaha ya kodi. Ni vizuri Serikali iangalie misamaha ya kodi isiyokuwa na maana, lazima tuache kuifuta, vinginevyo tunaliingiza Taifa letu katika mazingira ambayo hayazalishi vizuri. Ni vyema tukaangalia hasa kwenye Sekta ya Madini, kuna misamaha mingi ya kodi ambayo hainufaishi Serikali au Taifa kwa ujumla. Ni vyema

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. M. S. KAKOSO]

tukaweka mikakati itakayosaidia kukuza uchumi na kudai kipato kikubwa kwenye sekta ya Nishati hasa ya Madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Michael Laizer.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie mpango huu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, kila nchi ina mipango, na usipokuwa na mipango kwa kweli hakuna utakachowenza kufanya. Lakini Mpango huu unastahili wananchi wenyewe wauelewe, waufahamu kabisa kwa sababu Mpango huu ni wa kwao. Kwa hiyo, ni lazima washirikishwe na ni lazima itatue matatizo yao na lazima waone faida ya mipango hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kila mwaka ina vipaumbele. Mwaka uliopita tulikuwa na kipaumbele cha barabara kwamba ni lazima barabara zijengwe na kweli naishukuru Serikali kwa sababu wamejenga barabara nyingi sana. Kuna barabara zinazounganisha nchi na nchi, Mikoa, Wilaya mpaka nyingine zinaunganisha Tarafa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tuangalie kwa sababu wakati mwagine kuna miradi inafanyika chini ya kiwango na kupoteza fedha za wananchi.

Nikitoa mfano, barabara kutoka kwenda Arusha kwenda Namanga, imejengwa kwa muda wa miaka mine sasa. Lakini ukiangalia kabla hawajamaliza, eneo ambalo wamemaliza imeanza kubomoka. Sasa barabara hiyo imeanza tena upya kukarabatiwa kama mwanzo walipokuwa wakijenga. Mwanzoni waliweka madaraja madogo, sasa wamevunja tena wanaweka madaraja makubwa kana kwamba hawakuangalia kwenye mipango yao kwamba barabara hizo au madaraja hayo yanahitajika yawe makubwa.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. M. L. LAIZER]

Kwa hiyo, hiyo ni upotezaji wa fedha za wananchi. Kwa hiyo Serikali iangalie miradi kama hiyo kwa sababu hatutamaliza vipaumbele. Tuhakikishe kwamba vipaumbele tunavyochagua visiende mwaka mwingine, tumalize mapema kwa sababu kuna vipaumbele vingine ambavyo tumeviacha bila kuzifanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa kulizungumzia ambalo Serikali hawakuweka kwenye Mpango ni Kiwanda cha Magadi Soda, *Lake Natron*. Mheshimiwa Rais alipofungua Bunge hili alisema mwenyewe ni lazima tujenge Kiwanda cha *Lake Natron* kwa sababu magadi hayo yanakaa bila kutumiwa, bila kuwafaidia wananchi.

Vile vile Mheshimiwa Rais alipotembelea Wilaya ya Longido, allwaambia tena wananchi ni lazima katika kipindi chake Kiwanda cha *Lake Natron* kitajengwa ili wananchi vijana wapate ajira katika kiwanda hicho. Lakini sikuona katika Mpango huu, Serikali hawakuweka kabisa kwenye Mpango, naomba waweke kwa sababu bado inawezekana sasa, na ndiyo maana tunachangia Mipango hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia majirani zetu, hawataki miradi kubwa kabisa iliyoko mpakani, kila mradi wanapiga vita. Wanapiga vita mradi wa magadi, wanapiga vita barabara ya Mto wa Mbu, Engaruka, Lollondo na Mugumu. (*Makof*)

Ukiangalia barabara ya lami inayotoka Nairobi inaingia mpaka inafika Masai Mara. Haikuingia ndani ya Masai Mara lakini imefika Masai Mara, na sisi hatukusema kwamba tutajenga barabara ya lami ndani ya Serengeti. Jambo lingine ambalo wanapiga vita hata uwanja wa ndege wa Serengeti, na uwanja wa ndege wa Serengeti ni kilomita 17 kutoka Serengeti (hifadhi). Eti wanasema nyumbu watatupa mimba! Kitu cha ajabu, na sisi tunakubali! Sasa wenzetu wanatuzidi, wao wanapanga mambo yao wenyewe, lakini sijawahi kusikia Serikali ya Tanzania ikiingilia miradi ya Kenya. (*Makof*)

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. M. L. LAIZER]

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ninalopenda kuzungumzia; ukiangalia kila Mkoa una mahitaji au una zao lake. Wilaya yetu ya Longido, Monduli, Ngorongoro na baadhi ya Wilaya nyingine tunategemea mifugo. Lakini kwenye mipango hii haikuweka kabisa suala la mifugo. Sisi tunategemea Kiwanda cha *Kenya Meat Commission*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi ya asilimia 40 ya mifugo inayochinjwa pale inatoka Tanzania, mbuzi ni asilimia 60. Lakini Serikali ya Tanzania, sisi hatuna hata mapato tunayopata kwa mifugo inayokwenda kwenye kiwanda kile. Kwanini tusijenge kiwanda chetu Arusha? Mifugo ya Tanzania isipokwenda kwenye hicho kiwanda, kinafungwa. Lakini sisi tunakaa tu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa hili suala la viwanda vya nyama, vijengwe na kule kwetu Arusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni matumizi mabaya ya fedha za Serikali. Ukiangalia miradi ya maji, miradi inayoibuliwa ni fedha nyingi sana, kila mtu anashangaa, lakini Serikali haioni. Sijawahi kuona kwamba kisima kinachimbwa kwa Shilingi milioni 300, sijawahi kuona! Lakini kwenye utaratibu huu ipo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naomba Serikali hii itambue sasa kwamba mifugo inahitaji maeneo. Kwanini kuna maeneo ya wanyamapori na imetengwa kabisa? Kwanini kuna maeneo ya misitu na imetengwa kabisa? Kwanini kuna maeneo ya wawekezaji, nao wametengewa maeneo? Kwa nini kuna maeneo ya makaazi, lakini hakuna hakuna maeneo ya mifugo? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunataka mgogoro huu uishe na wafugaji wawe na imani na Serikali, hebu sasa tengeneni maeneo ya mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya vipengele ambavyo katika Taifa hili vimekuwa kero kubwa kwa wananchi ni maji. Hivyo, basi ningeiomba Serikali kuazimia mwaka wa fedha 2014/2015 kuwa Mwaka wa Maji kwa Taifa zima kwa kuhakikisha zaidi ya asilimia 75% ya nchi, wananchi wanapata maji, kwa kuwa hili linawezekana katika Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala kuruhusu maeneo ya mipaka (*borders*) kufanya kazi saa 24 tofauti na sasa, litasaidia kuongeza mapato katika Taifa, kutanua wigo wa ajira na soko kwa Mataifa ya karibu, hivyo nchi kuwa katika biashara muda wote. Mfano wa mipaka hiyo ni Tunduma ambayo kwa mwezi inaliingizia Taifa Shilingi billioni mbili. Hivyo, kuruhusiwa barabara hiyo kufanya kazi saa 24 itaongeza mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. ZARINA S. MADABIDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni suala zuri sana kujadili maendeleo ili kuweka mipango kabla ya bajeti. Lakini ingekuwa ni bora sana kama mpango ungetoa utekelezaji wa mwaka 2013/2014 ili jujikane wakati tunazungumza ya mwaka 2014/2015 tusirudie yaliyojitekelezwa mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vipaumbele ni vingi. Kwa upande wangu ningeweka miundombinu, Kilimo na Viwanda ndiyo vipewe msisitizo na sekta nyingine zipewe fedha za kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imefanya kazi kubwa sana kujenga barabara, lakini kwa sababu barabara zinabeba mizigo mizito sana, ni hatari, zitaharibika haraka kama tulivyoshuhudia kwa barabara nyingi. Nashauri yafuatayo:-

- (1) Reli zote ziimarishwe kwa kujengwa upya;

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. Z. S. MADABIDA]

- (2) Tusingubiri mfadhlili/mwekezaji ajenge, badala yake Serikali ijenge;
- (3) Ijengwe reli ambayo itakidhi mahitaji ya sasa na miaka 50 ijayo;
- (4) Kwa kuwa nchi yetu itakuwa na umeme wa kutosha, tujenge reli ya kutumia umeme ambayo itaenda kasi, asubuhi Dar es Salaam jioni Mwanza au Kigoma au Arusha na Mtwara;
- (5) Serikali isitegemee fedha ya bajeti kujenga reli, bali ifanye mkakati mahsusutu kutenga fedha za kutosha; na
- (6) Serikali kwa kutumia gesi yetu inakopesheka, tufanye mkakati huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kama inataka kutatua msongamano wa magari Dar es Salaam, ni lazima itanue daraja la Salender na Gerezani; itanue maeneo yote ya makutano, kuboresha na kutia lami njia za ndani ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *flyovers* zitasaidia, lakini tuelenze zinapita wapi. *Flyover* inayounganisha daraja la Kigamboni linasemekana kwenda *TAZARA*, lakini watu wengi kutoka Kigamboni wanaenda mjini na siyo *TAZARA*. Reli ya abiria ya Dar es Salaam inatumia injini za masafa marefu, tuwekeze kwa kuweka injini inayofaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tubadilishe mtazamo wa Kilimo, siyo kweli kwamba 75% ya Watanzania ni wakulima, bali ni waishio vijijini. Tuige Malaysia ambao walibadili msimamo wa nchi na kufanya 35% tu ndiyo wakulima, na hivyo kulima kwa tija na kuweza kuzalisha chakula na biashara. Ili kutoa ajira nyingi hasa kwa vijana, viwanda vingi vianzhishwe. Viwanda hivyo, viwe vidogo, vya kati na vikubwa, viwepo kote, vijijini hadi mijini.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. Z. S. MADABIDA]

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini mpango wa hivyo vipaumbele vitatu vitatoa maendeleo, ajira na kukuza uchumi wa nchi yetu.

**MHE. SABREENA H. SUNGURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami napenda Mpango wa Serikali uzingatia yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango uoneshe ni jinsi gani Sekta ya Afya itakomboa akina mama kutokana na vifo vya mama na mtoto, Elimu ya Afya ya Uzazi na ni jinsi gani itapunguza vifo hivyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kitengo vya Damu Salama ni vyema sasa katika mpango huu, Hospitali ya Tumbi ipewe mamlaka ya kisera kutunza damu yake yenyewe bila kutegemea kwenda Dar es Salaam kwenye Ofisi ya Damu Salama kipindi cha *emergence*. Hivyo watu wengi hupoteza maisha kutokana na *traffic jam* kutokea Kibaha hadi Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vyema mpango huu ujikite katika *special economic zone* kwa sababu fursa zipo, lakini kinachokosekana ni wawekezaji kuja kuwekeza. *Tanzania Investment Centre* iweke mikakati ya kuleta wawekezaji, hivyo kukuza uchumi wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, ni vyema Mpango huu uwekeze kwenye Sekta ya Maji, upatikanaji wa maji safi na salama na pia uwekaji wa mita kwa watumiaji ili waweze kulipa gharama halali kutokana na matumizi ili kuondoa migogoro mbalimbali inayopatikana katika maeneo ya Kigoma Manispaa na sehemu nyingine nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. YUSSUF HAJI KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii adimu kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuwa mionganoni mwa wachangiaji katika mada hii muhimu.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. Y. H. KHAMIS]

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2014/2015 ni muhimu sana kwa Taifa, kama mipango itakwenda sawasawa na usimamizi mzuri. Mimi binafsi ningependa Serikali ielekeze mipango yake katika uvuvi na hasa kwa wavuvi wadogo wadogo. Wavuvi wadogo wawezeshwe kwa kupewa elimu, wapatiwe zana za kisasa ili na wao waweze kuvua bahari kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango huu wa uvuvi wa bahari kuu ni muhimu kwa maendeleo na ajira kwa vijana wetu. Jambo muhimu ni mipango na usimamizi madhukuti. Sambamba na bahari, tunayo maziwa, mito na mabwawa. Vyote inapasa kusimamiwa na kuwawezesha vijana wetu katika uvuvi wa kisasa wenye tija na maslahi kwa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile Mpango huu uelekezwe katika Kilimo kwa mazao ya chakula na biashara. Wakulima wadogo wawezeshwe kwa vifaa kama matrekta, mbolea, mbegu bora pamoja na tafiti mbalimbali za kitaalam. Vijana wetu waliopitia JKT wapewe kipaumbele katika Mpango huu. Pamoja na mafunzo ya ulinzi ambayo wanapatiwa, lakini hufunzwa shughuli mbalimbali kama ufugaji, kilimo na fani nyingi nyinginezo. Kwa kuwa siyo rahisi kuwaajiri katika ulinzi wote, mimi nadhani ni wakati muafaka kuwakusanya vijana katika sekta ambazo wamejifunza, na Serikali iwawezeshe katika nyanja zote. Hii itasaidia ajira kwa vijana pamoja kuongeza uzalishaji na kukuza pato la Taifa.

Mheshimkiwa Mwenyekiti, mpango haujazungumzia maendeleo ya michezo ambayo ni muhimu kwa vijana na Taifa. Tanzania ni miongoni mwa nchi zilizokuja na hadhi kubwa kwa kuwa na wanamichezo wenye viwango hasa katika riadha, mpira wa miguu, mchezo wa ngumi na adhalika. Lakini kwa sasa michezo mingi imepotea na imekosa msisimko hasa Kimataifa. Hivyo mpango huu ungeangaliwa kwa upana kurejesha heshima ya Taifa letu. Kama tukijipanga vizuri, ukubwa wa nchi na wingi wa watu tulionao ni rasilimali tosha kujikomboa katika michezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, moja kati ya changamoto inayotukabili kama Taifa na kupunguza makusanyo/mapato ya Serikali ni misamaha ya kodi. Ni muhimu sana Serikali ikalichukulia kwa uzito wa pekee, kisha kulitafutia ufumbuzi wa kudumu. Ni aibu, ukosefu wa umakini kwa nchi, kutoa msamaha wa kodi kwa mwaka kwa kiwango ambacho ni asilimia 27% ya makusanyo yake ya mwaka na asilimia 4.3% ya pato la Taifa. (Rejea CAG 2013).

Mheshimiwa Mwenyekiti, wachambuzi wa uchumi (kama ilivyoainishwa na *Ripoti ya ESAUVP*) (2013, Pref. *Maliamkono et-al*) inabainisha wazi kwamba misamaha ya kodi ilikuwa muhimu kwa nia ya kuwavutia wawekezaji kipindi ambacho nchi haikuwa na miundombinu ya kutosha, changamoto ambayo kwa sasa inapungua kwa kiwango kikubwa. Inakuwaje badala ya misamaha ya kodi kupungua kwa kadiri miundombinu inavyoboreka, misamaha husika inaongezeka? Katika hatua nyingine, nyongeza kwa mwaka mmoja yaweza kuongezeka kwa 78%. (Kwa mwaka wa fedha 2010/2011 na 2011/2012, misamaha ya kodi iliongezeka toka triliioni 1.016 mpaka triliioni 1.8 mwaka 2012).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nchi ambayo inashindwa kutekeleza mipango ya maendeleo na (Mpango wa Taifa) kutohana na kuwa na ufinyu wa bajeti – kusamehe takriban triliioni mbili, ni mzaha na ukosefu wa umakini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muhimu Serikali ikaanza kushughulikia changamoto hii kwa kuhakikisha wanafanya mambo yafuatayo:-

(1) Kuweka ukomo wa misamaha ya kodi na kuhakikisha kuwa misamaha haitolewi zaidi ya kikomo kilichowekwa. Lazima ukomo ujulikane ili kuiwezesha Serikali kubaini miradi ambayo inahitaji misamaha na ambayo haihitaji;

(2) Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali akague misamaha yote ya kodi iliyotolewa ili kupima kama kuna matumizi sahihi ya fedha za umma;

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. H. J. MDEE]

(3) Utaratibu wa Kituo cha Uwekezaji Tanzania (*TIC*) wa kutoa misamaha ya kodi udhibitiwe/kusimamiwa ipasavyo. *TIC* akiwa kama mwangalizi wa Makampuni haya yaliyopewa misamaha, anatakiwa kujiridhisha kwamba motisha husika haitumiwi vibaya. Uzoefu umeonyesha kwamba ufuatiliaji husika huwa haufanyiki;

(4) Mamlaka wanayopewa Mawaziri (Mfano Waziri wa Madini) wakati wa kusaini Mikataba ya Madini (*MDA*) inayotoa vivutio vya uwekezaji, inatakiwa iangaliwe kwa jicho pana au kudhibitiwa;

(5) Serikali kusimamia utekelezaji wa sheria mbalimbali zilizotungwa na Bunge. Sheria ya Kodi ya Mapato (*ITA 2004*) kifungu cha 10 (3) inahitaji kwamba mikataba yote iliyosainiwa baada ya tarehe 1 Julai, 2004 kutopewa misamaha ya kodi. Licha ya kuwepo kwa kifungu hicho, Serikali imeendelea kusaini mikataba yenyе kifungu kinachoruhusu misamaha ya kodi;

(6) Sheria ya Kituo cha Uwekezaji (*TIC*) lazima ifanyiwe mabadiliko ili iweze kubainisha ukomo wa misamaha ya kodi; na

(7) Serikali itunge sera/iandae mwongozo wa kutoa misamaha, ambao unaelezea usimamizi na misamaha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya pili ni umuhimu wa Serikali na Kamati ya Bajeti kufanya kazi changamoto zinazozikabili Halmashauri nyingi katika kukusanya mapato, wakati kiuhalisia zina uwezo wa kukusanya zaidi ya kinachokusanya.

Ni muhimu kuhakikisha Halmashauri zote zinatakiwa kutambua vyanzo vyote vya mapato yao ya ndani (vyo kisheria), kisha kuwe na *database* ambayo itakuwa *updated* kila mara kwa kadiri mazingira yatakavyoruhusu. Hali hii itasaidia utaratibu unaotumika sasa wa Halmashauri kukusanya mapato kwa kubahatisha/kwa mazoea pasipokuwa na takwimu sahihi za walipa kodi.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. H. J. MDEE]

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inawajibika pia kutoa mwongozo/maelekezo kwa *TRA* kutoa taarifa sahihi za mapato ya mwaka ya Makampuni kwa Halmashauri ili kuwiwezesha kupata *service levy* iliyo sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo Serikali inatakiwa kuliangalia kwa umakini kama sehemu ya chanzo cha mapato ni ardhi kupitia Kodi ya Ardhi. Kifungu cha 33 cha Sheria ya Ardhi Na. 4 cha mwaka 1999, kinatamka bayana kwamba mwenye hati miliki pamoja na masharti ya vifungu vingine, inatakiwa kulipa kodi kama ilivyoelekezwa na Sheria ya Fedha za Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utafiti uliofanywa na Idara ya Uchumi, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, baada ya kupewa kazi husika na Wizara ya ardhi kuweza kubaini kama tozo mbalimbali (*land rent, fees, levies*) za ardhi au malipo mengine yanayotakiwa kutozwa kwa wamiliki wa mashamba, wanafanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utafiti husika uligundua kwamba kati ya mashamba 763 (ekari 902,403) yaliyotembelewa, ni mashamba 278 (36.45) tu ndiyo yaliyolipa kodi ya ardhi (2002) kama sheria inavyotaka. Wamiliki wa mashamba 432 (56.6%) waliohojiwa walikiri kwamba hawajalipa kodi husika. Lakini walipotakiwa kuonyesha uthibitisho (ushahidi wa risiti) kuonyesha kama ni kweli walikuwa wamelipa kodi husika, ni mashamba 102 yaliyoweza kuthibitisha. Hiyo imetuambia kwamba mashamba mengine 643 yawezekana kabisa hayakulipiwa kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hatua nyingine, iligundulika kwamba asilimia 43.47% ya wenye mashamba waliohojiwa walikiri kwamba hawajawahi kulipa kodi kabisa. Ikumbukwe kwamba hii ni sehemu ndogo tu ya mashamba yaliyotembelewa. Kodi hizi zingelipwa ipasavyo, ingesaidia kuongeza mapato ya Serikali kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka kufikia mwaka 2002, viwanja vyenye hati vilikuwa ni 995,000 tu. Sasa kama kigezo

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. H. J. MDEE]

cha kutozwa kodi ni kuwa na hati miliki, na kwa kuwa viwanja vyenye hati miliki ni vichache sana; tafsiri yake ni kwamba Serikali inakosa mapato mengi sana kwa sababu tu hajagundua umuhimu wa ardhi katika mipango yake. Lazima mtazamo huu mgando ubadilike. Ardhi na upimaji wa ardhi ina kila sababu ya kuchukuliwa kwa uzito wa kipekee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukisimamia nidhamu ya kutoza kodi kwa wamiliki wa mashamba, itafanya watu wawe na nidhamu ya kutumia ardhi kwa uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kodi za majengo, hili ni eleo ambalo Serikali hajjalifanya kazi vyta kutosha. Likisimamiwa ipasavyo, litakuwa na mchango mkubwa sana katika pato la Serikali.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata nafasi ya kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kuelezea mpango mpya wa maendeleo, swali la kujiuliza ni kwa kwamba, kwa kiasi gani mpango wa mwaka 2012/2013 umetekelizwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la reli, barabara zetu kwa kiasi kikubwa zimetengenezwa kwa lami, lakini barabara hizi haziwezi kudumu kwa muda mrefu kwa sababu bado malori yenye uzito mkubwa yanazitumia barabara hizo kusafirisha mizigo badala ya kusafirisha kwa mabehewa ya treni. Imekuwa ni hadithi sasa Treni ya *TAZARA*, Reli ya Kati na Kaskazini; ni lini Serikali itaamua kuchukua maamuzi magumu na kubomoa reli zote na kuweka za kisasa za mwendo wa kasi, ukizingatia tayari umeme wa uhakika Serikali imeshaanza kuishughulikia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu deni la Taifa. Katika Mpango wa Taifa, Serikali inatueleza kuhusu ukuaji wa pato la Taifa kwamba umekua kwa asilimia 7.0% ukilinganisha na 6.9 mwaka 2012. Lakini hapo hapo deni la Taifa la ndani na nje limeondgezeka kwa Shilingi trillioni 24.49. Haiingii akilini

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. L. F. OWENYA]

kwamba deni ni kubwa kuliko bajeti ya nchi, halafu wataalam wanatueleza uchumi unakua. Utakuaje? Ndiyo maana maendeleo mengi hayafanyiki. Kumekuwa na matatizo ya kuiba kila sekta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano, Kilimo cha Umwagiliaji. Kilimo hiki hakiwezi kukamilika bila kuchimba vizima vya maji vya kutosha kila mahali. Mradi wa maji vijijini bado ni tatizo, vijiji vingi havijafanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee Jiji la Dar es Salaam. Jiji letu hili ndiyo kioo cha nchi yetu, lakini mpaka sasa hivi wakazi wa Dar es Salaam hawana maji safi na salama kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Mpaka leo hii baadhi ya wakaazi wanachota maji ya chumvi na machafu kutoka baharini. Hii ni hatari. Lazima tuwe na watu wenye afya ili kuwa na nguvukazi imara. Kwa kutumia maji yasiyo salama, magonjwa ya milipuko ya kuhara, *typhoid* na kadhalika hutokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu usafiri wa anga, niipongeze Serikali kwa kukarabati viwanja vingi vya kurukia na kutua ndege sehemu nydingi nchini. Je, Serikali sasa ina mikakati gani ya kuhakikisha Shirika letu la ndege ATCL linafufuka kama njia ya maendeleo na kuliongeza pato la Taifa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utalii, ningependa kujua, ni kwa jinsi gani mpango huu umejikita katika kuendeleza utalii endelevu wenye kujali mazingira ikiwa ni pamoja na kuongeza na kupanua vivutio vya utalii? Naomba majibu.

**MHE. SALOME D. MWAMBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mpango huu, maeneo mengi hayapewi kipaumbele katika utekelezaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la maji bado ni tatizo. Ahadi ya visima 10 bado haijakamilika. Mpango huu unasuasua. Nashauri Serikali ijitahidi kuchimba visima vifupi

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. S. D. MWAMBU]

ili wakati wa mvua viweze kusaidia kupunguza tatizo la maji vijijini. Wilaya ya Mkalama, vijiji vingi havina visima; wanatumia maji yasiyo salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano Kata za Msingi, Miganga, Mwangeza, Mwanga, Iguguno, Ibaya, Ilunda na Nduguti. Huu ni mfano tu wa baadhi ya Kata katika Jimbo la Iramba Mashariki, Kata ambazo hazina maji. Naishauri Serikali kuwa, visima vifupi bado vinahitajika katika Jimbo langu. Hivyo, Serikali iziwezeshe Halmashauri kupata fedha za maendeleo za kutosha ili ziweze kuchimba visima vifupi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali ione umuhimu wa kuweka mawasiliano, mitando ya simu isambazwe nchi nzima, kwani kasi ya kusambaza inasuasua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa elimu, Serikali izidi kuongeza bajeti ya Wizara ya Elimu. Pia uchambuaji wa mikopo izingatie watoto ambao hawana uwezo na wanaotoka katika mazingira magumu (maskini).

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali ipeleke umeme katika Wilaya zake mpya. Kasi iongezeke ili iweze kusukuma shughuli za maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. MAHMOUD H. MGIMWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naishukuru sana Serikali kwa kuleta Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2014/2015. Kwanza, naanza kwa kuzungumzia bajeti ya mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makusanyo ya robo mwaka 85.7% mpaka sasa yanatokana na mapato ya ndani, na asilimia 32.4% yanatokana na mapato ya nje. Hii inatoa taswira kuwa Serikali inashindwa kutekeleza majukumu yake. Mfano, Wizara ya Maji mpaka sasa imepatiwa Shilingi bilioni 43, kati ya Shilingi bilioni 157.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. M. H. MGIMWA]

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2012/2013 Serikali ilipanga bajeti ya Shilingi triliuni 15, mwaka 2013/2014 Shilingi triliuni 18 na mwaka 2014/2015 Shilingi triliuni 20. Kila mwaka kumekuwa na ongezeko la matumizi, lakini miaka yote imeshindwa kufikia malengo yake na pia imeshindwa kuainisha vyanzo vya mapato. Ni vyema safari hii Serikali ikaainisha vyanzo vya mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Mipango ni "*think tank* ya Serikali". Imefanya vizuri katika maeneo mengi, lakini sasa imekuwa kero kwa kuchelewesha baadhi ya miradi ambayo tayari imeshapitishwa na Bunge kwa kisingizio cha kuhakiki. Mfano, mradi wa Kurasini (*Logistic Hub*) na kusababisha fidia katika *KMO* kuwa kubwa kutoka bilioni 60 hadi bilioni 94.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wakati muafaka sasa kwa Serikali kuangalia upya Sheria ya Manunuzi ambayo inaleta gharama kubwa, mianya mingi ya rushwa na udanganyifu mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imefanya vizuri katika maeneo ya miundombinu na hasa barabara, lakini bado Serikali inahitaji kuongeza nguvu katika eneo la reli ambalo ni nyeti sana kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tutajielekeza zaidi katika reli, kutasaidia kupunguza gharama za usafiri, ambazo *automatically* zitasaidia kupunguza gharama za uzalishaji mali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukuaji wa pato la Taifa kwa asilimia 6.9% - 7.0% ni kweli katika nusu ya mwaka, lakini kuna maswali ya kujuliza: Je, ukuaji wa pato la Taifa umekwenda sambamba na kuondoa umaskini? Je, matabaka ya walio nacho na masikini yameongezeka?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumuko wa bei umeshuka, lakini ungeshuka zaidi kama umeme wa uhakika ungekuwepo na kwa bei nafuu.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. M. H. MGIMWA]

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile tungeimarisha zaidi usafiri wa reli kuliko wa barabara. Serikali isitishe uagizaji wa mchele toka nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wakati muafaka sasa wa Serikali kutueleza mikakati yake ya kulipa madeni ya wazabuni wa ndani ambao wamepoteza mwelekeo sababu ya Serikali. Ni mikakati gani Serikali imeweka kwa ajili ya kudhibiti deni la ndani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado Serikali imeshindwa kutekeleza kwa uhakika miradi ya maji na umeme vijijiini. Ni vyema sasa Serikali ikatatua tatizo la umeme, ambalo limesababisha hasara kwa viwanda vingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali bado haina dhamira ya kweli ya kuanzisha Benki ya Wakulima ambayo itakuwa mkombozi kwa wakulima hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu viwanda, Serikali imenyamaza kimya kuhusu EPZ – Bagamoyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. SILVESTRY F. KOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na kupongeza Mpango wa Maendeleo ya Taifa. Niseme kuwa mipango ni mizuri, lakini uwezo na utekelezji wake unaenda ukisuasua sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kuwa ikibidi tupunguze vipaumbele ili tuwe na vichache tutakavyoweza kuvikamilisha kwa muda mfupi, tarajiwa na kukidhi mategemeo ya wananchi vyema kuliko vingi ambavyo vinasusua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mojawapo ya vipaumbele kabisa katika Jimbo langu la Kibaha Mjini na nchi kwa ujumla ni maji safi na salama. Katika mipango ya Serikali ni pamoja na utekelezaji wa miradi ya maji katika vijiji/mitaa 10 na kazi hii imeanza.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. S. F. KOKA]

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kusikitisha ni jinsi ambavyo walishajitahidi hata kuchangia asilimia wanazostahili na wakandarasi walishaanza kazi *site*. Lakini fedha hazipatikani za kutosha na kwa wakati, jambo ambalo linatishia hata Wakandarasi kuacha miradi na kuongeza gharama za ujenzi wa miradi hii. Swali la kujuliza, fedha za bajeti zilipangwa tena mapema kabisa, zimekwenda wapi au hazijakusanya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi mkubwa wa maji Ruvu Juu uliotajwa ukurasa 24, katika kitabu hiki cha Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2014/2015, ni muhimu sana kutoa huduma hii ya maji safi na salama kwa Miji ya Kibaha. Lakini cha kusikitisha, ahadi hii ambayo ilitakiwa ifanyiwe utekelezaji toka mwaka 2012, bado hadi leo Novemba, 2013 hata dalili za kuchimba mtaro wa bomba hazijawepo, na huku wananchi wakitaabika na kusikia ahadi tunazowapa kutoka Serikalini. Tunaomba Serikali sasa itoe kipaumbele katika mradi huu ili wananchi wapungukiwe na kutaabika na ahadi ya Serikali itimie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maendeleo yoyote yale na mtaji wa kwanza kwa binadamu ni ardhi tuliyopewa na Mwenyezi Mungu. Wananchi walio wengi wana maisha duni na rasilimali kuu walionayo ni ardhi, na Serikali ilishaanzisha mpango wa kuwasaidia wananchi kurasimisha na kufanya ardhi za wananchi ziwe na dhamani tambulika waweze kuitumia kujiletea maendeleo. Hii ni pamoja na Mkurabita. Mradi huu wa Mkurabita umeishia vitabuni na magazetini tu. Ukienda vijijini hata kwenye Kata, wananchi hawaelewii mpango huu wa Serikali. Wito wangu, naomba sasa Serikali itoe utaratibu maalum na kuelimisha wananchi kuhusu Mkurabita ili wananchi walio wengi waweze kufaidika na rasilimali hii muhimu katika kujiletea maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu sasa imeingia katika miradi mikubwa ya utafiti na uchimbaji madini, utafiti na uchimbaji wa mafuta na gesi; na tayari kuititia Makampuni makubwa ya shughuli hizo duniani, yameshagundua gesi Mtwara, Lindi na Kilwa.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. S. F. KOKA]

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jitihada za Serikali kushirikisha Watanzania, bado hatujaweza kuwa na sera nzuri zaidi ya kuwezesha Watanzania na hasa Makampuni ya wazawa kuwa sehemu ya biashara hii kubwa na yenye faida kubwa. Pamoja na kuhimiza Makampuni ya Kitanzania kutoa huduma katika Makampuni haya, yaani "*Supply of Goods and Services*", bado Makampuni ya Mafuta na Gesi yanakuja na Wakandarasi wao. Tunaomba Serikali iweke bayana sharti la kuwapa Makampuni ya Kitanzania yenye uwezo na ushindani kipaumbele katika kutoa huduma mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, bado tunaishauri Serikali iweze kuweka utaratibu wa kuwashawishi na kulazimisha Makampuni makubwa yatokayo nje kuwekeza kwenye mafuta na gesi, yaweze angalau hata kutoa asilimia kidogo ya ubia na Makampuni ya ndani, hata 5% tu. Hii itaweza kujenga uwezo mkubwa kwa Makampuni ya Kitanzania na kuweza jamii kufikiwa haraka na kwa ukaribu maendeleo ya kiuchumi yatokanayo na miradi hii mikubwa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. CHRISTINA L. MUGHWAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata fursa hii ili nami niweze kutoa maoni yangu katika Mpango wa Maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu imekuwa ni hodari sana kuandaa mipango ya maendeleo ambayo matokeo ya utekelezaji wake hayaonekani wazi. Tumekuwa na mipango mingi, mfano MKUKUTA, MKURABITA, Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano, na sasa *Big Results Now*, na kadhalika. Hivi kweli kati ya hizi zote, ni mpango gani hasa tunaoufuata? Je, upi ulifuta mwagine, na ni sababu zipi zilizopelekea kuanzisha mpango au sera mpya bila kueleza sababu za kutokutekelezwa kwa sera yningine?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa tupo katika mwaka wa tatu wa utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Miaka

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. C. L. MUGHWAI]

Mitano, lakini cha kushangaza katika taarifa yake, Serikali hajaeleza ni kwa kiwango gani mpango huu umetekelezwa hadi sasa? Kiasi gani cha fedha kimetumika, na miradi gani bado hajatekelezwa na itakamilika lini? Kiasi gani cha fedha kinatarajiwa kutumika na kitatoka wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuja na mpango ama sera ya Matokeo Makubwa Sasa. Hivi kweli matokeo haya makubwa yatakujae iwapo fedha za maendeleo zilizotolewa kwa robo ya mwaka huu ni asilimia 11 tu? Ni wakati upi ambapo Serikali itajali mpango wake wa maendeleo kwa kuutengea fedha za kutosha za utekelezaji kama mpango wenyewe unavyoelekeza?

Mheshimiwa Mwenyekiti, imefika wakati sasa Serikali yetu iheshimike kwa kutenda na siyo kwa idadi ya mipango tullyonayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. MESHACK J. OPULUKWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mpango ujao naomba Serikali iweke mkakati muhimu wa kumaliza tatizo la kulipa fidia kwa wananchi wa kigamboni (*New City*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Serikali iweke mikakati ya kutosha kuweka mipaka maeneo yote yanayozunguka hifadhi zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MHE. RACHEL M. ROBERT:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendeleko ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa yanatakiwa kuainisha malengo mahsus ya kila mwaka kutokana na vipaumbele. Kuna tatizo la kuweka vipaumbele visivyokuwa na *specific targets*, ambavyo mwisho wa siku mpango unakuwa mgumu kutekelezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna matatizo ambayo yanahuisha au yanachangiwa na vyombo vinavyotekeleza

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. R. M. ROBERT]

mpango huu ambavyo havisimamiwi ipasavyo katika utekelezaji wake katika mpango wa kila mwaka. Kuna haja sasa ya Serikali kuhakikisha inasimamia kwa karibu sana vyombo hivi ili viweze kuleta tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri sana mpango wa maendeleo ukalenga kujibu au kutatua tatizo kubwa la umasikini kwa kila Mtanzania, ukizingatia zaidi ya Watanzania milioni 40 hawana kazi zinazoeleweka. Kitendo cha mipango kama hii kuishia kwenye makaratasi kunaleta manung' uniko makubwa na hasa kama hayatakelezwa kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumuko wa bei hauendani kabisa na kipato cha Mtanzania. Vijana walio wengi wamekosa ajira na huku thamani ya Shilingi ikizidi kushuka. Tofauti ni kubwa sana kati ya aliyenacho na asiyenacho. Hii inatokana na pengine pesa zinatumiliwa vibaya na watu wachache bila kuchukuliwa hatua. Kwa mtaji huu sasa kila siku tutakuwa tunapoteza muda kuandaa mipango kila mwaka isiyotekelzeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi imekuwa mingi sana na kibaya zaidi mingi haijatekelezwa, na hata kama imetekelzeza, basi ni kwa kiwango cha chini kabisa. Pesa nyingi za umma zinapotea huku walengwa wakikosa huduma muhimu kama afya, maji na miundombinu ya barabara na hata nishati ya umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Serikali kuendelea kutekeleza miradi ya maji ilioibuliwa katika Programu ya Matokeo Makubwa Sasa, bado kuna changamoto nyingi sana katika baadhi ya miradi. Kama mradi wa *Lake Victoria* ambao sasa unatoa huduma katika Miji ya Shinyanga na Kahama, kuna malalamiko mengi ambayo wasambazaji wanalazimika kutoza bili kubwa za maji ili kukidhi gharama za uendeshaji.

Maheshimiwa Mwenyekiti, tatizo ni kwamba Serikali haitoi ruzuku ili mradi kama huu usimumuize mtumiaji wa mwisho, na hata kama inatoa ruzuku, basi haitoshi.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. R. M. ROBERT]

Upatikanaji wa maji vijijini ni mdogo, kwani fedha nyingi zinapotea katika kuchimba visima ambavyo havitoi maji. Je, Serikali haioni kuna haja ya kupima kwanza sehemu inayotakiwa kama kuna maji? Lakini pia kwa nini Halmashauri zisifanye kazi hiyo zenyewe bila kutoa kazi kwa Wakandarasi ambao wamekuwa wakilipwa pesa nyingi na kuacha visima havitoi maji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango unaeleza utaongeza upatikanaji wa matumizi ya pembejeo, zana za Kilimo na huduma za ugani. Lakini mpaka sasa bado kuna tatizo kubwa la ucheleweshaji wa pembejeo kwa wakulima, na matokeo yake wakulima wanauziwa kwa bei kubwa sana na wafanyabiashara wanaoleta pembejeo zao kwa wakati. Serikali iangalie suala hili kwani wakulima wamekuwa wakipata hasara sana kutokana na ucheleweshaji wa pembejeo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma za ugani bado zinalegalega, kwani Maafisa Ugani waliopo hawatoshi na hivyo kusababisha Kilimo kisicho na tija, na mazao yanakuwa ni hafifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la afya bado ni kitendawili. Pamoja na mipango mizuri, Serikali bado ina kazi kubwa kuhakikisha miundombinu na upatikanaji wa huduma za afya na ustawi wa jamii. Bado hospitali nyingi nchini hazina madawa, vifaa na hata Madaktari wa kutosha. Kama vitu hivi hakuna, hata iletwe mipango yenye asali, bado tutakuwa hatujamaliza tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushiriki wa sekta binafsi kuwekeza kwa wingi katika huduma za afya nchini, bila kuzisaidia ni kuziongezea mzigo zisizouweza kuutua. Kuna umuhimu sasa kuhakikisha kama ni ruzuku, basi iende kwa wakati katika Hospitali hizi binafsi na za Mashirika ya Dini kuweza kutoa huduma nzuri kwa jamii zinazoizunguka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa 48 unaonyesha maendeleo ya kipaumbele katika mwaka 2014/2015. Lakini mpango umejikita katika maeneo machache yanayoendana na program ya *Big Results Now*. Ningependa kujua ni vigezo gani vilitumika katika kuchangua hiyo miradi ya kipaumbele? Pamoja na hayo, ningependa kuzungumzia mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imejitahidi sana kujenga kwa kiwango cha lami barabara nyingi sana nchini zikiwemo za Mkoa wetu wa Iringa, zikiwemo za Mtera – Iringa, Iringa - Mafinga; na mikoa mingi sana imefunguka kwa sasa. Lakini inasikitisha sana kuona bado Serikali hajatilia umuhimu mkubwa sana katika uimarishaji wa Reli ya Kati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua kuwa hili lilishakuwa eneo la kipaumbele, lakini siku zote halitengewi pesa ya kutosha. Najua uimarishaji wa Reli ungesaidia sana hata hizi barabara nyingi tulizozijenga kudumu na uchumi wa nchi hii ungekua kwa kasi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nzungumzie kuhusu Utalii. Ukurasa ule wa 53, inasema: "Serikali ili kuboresha eneo la utalii nchini, itaendelea kujenga na kukarabati miundombinu ya usafiri katika maeneo ya utalii." Lakini hajaainisha ni maeneo yapi? Kwa mfano, Mkoa wetu wa Iringa una mbuga ya *Ruaha National Park* ambayo ni ya pili kwa ukubwa Afrika, lakini barabara inayoelekea huko mpaka leo haipo kwa kiwango cha lami. Kiwanja chetu cha Ndege cha Nduli bado hakijapewa kipaumbele, hakijulikani lini kitakarabatiwa. Ni imani yangu kama miundombinu hii ingepewa kipaumbele katika mpango huu, ungeweza kusaidia sana kukuza ajira na pato la Mkoa wetu na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine kuhusu Elimu naMafunzo ya Ufundu. Katika ukurasa wa 53, Serikali inategemea kuimarisha mfumo wa kuongeza mbinu ya kugharamia elimu nchini. Naipongeza Serikali kwa kuweza kutenga zaidid ya Shilingi bilioni 306 ambazo waliokidhi vigezo vyta kukopeshwa ni wanafunzi 29,754 kati ya wanafunzi 31,647

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. R. E. KABATI]

ambao ni asilimia 96%. Lakini zipo changamoto ambazo zinapelekea wanafunzi kushindwa kupata mikopo hiyo kwa wakati, kisha kuleta vurugu, migomo na kisha maandamano vyuoni. Baadhi ya kezo hizo ni:-

- (i) Maafisa kuchelesha taarifa za *batch* za mikopo za wanafunzi;
- (ii) Mfumo mzima wa mtando wa (*OLAS*), mtandao upo chini sana (*network*); na
- (iii) Wengi wao hawajui matumizi ya mfumo huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma Taarifa ya Bodi ya Mikopo katika mitando ya tarehe 23 Oktoba, 2013, imebainisha changamoto hiyo kuwa zaidi ya wanafunzi 6,364 taarifa zao hazikukamilika licha ya Bodi hiyo kutoa muda wa ziada wa wiki mbili, ni wanafunzi 3,151 tu ndio waliweza kukamilisha taarifa zao kwa usaili kwa asilimia 48% na wengine asilimia 52% hawakukamilisha taarifa, aidha kukosa taarifa, wakiwemo hata wanafunzi wa Mkoa wa Iringa. Kwa hiyo, tunaitaka Serikali iangalie upya hii Bodi ya Mikopo, ikiwezekana ifumuliwe na tunaweza kubani mengi zaidi ya hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Vyano vya Mapato ya Ndani; katika ukurasa wa 57 unaonesha jinsi Mpango huu utakavyoendelea kutumia vyano vipyta vilivyopendekezwa na Bunge na pia itabuni vyano vingine. Ningombwa wakati Waziri atakapokuwa anajibu, basi atupatie ufanuzi kwamba hivyo vyano vipyta ni vipi na vyano vilivyobuniwa ni vipi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. MARIAM R. KASEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kuchangia hoja ya Mapendeleko ya Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2014/2015 kama ulivyowasilishwa hapa Bungeni.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. M. R. KASEMBE]

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mambo mengi ya msingi yaliyopo katika mpango, yapo pia mambo muhimu ambayo hayakutajwa katika mpango huu. Kwa kuwa Mpango huu ndiyo dira ya bajeti ya mwaka 2014/2015, nimeona ni vyema nikaanza kuikumbusha Serikali kwamba katika llani la Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, tuliahidi kwanza ujenzi wa Reli kutoka Mtwara hadi Mchuchuma, kazi ambazo hadi hivi sasa hazijaanza na katika Mpango huu haimo: Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kuwa ujenzi huu wa reli unaanza kabla ya mwaka 2015 ili kuendana na utekelezaji wa llani yetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, reli hii ni kiungo muhimu sana, kwani hali ya uchumi katika Mkoa wa Mtwara inakua kwa kasi sana kutokana na gesi iliyogundulika mkoani humo. Lakini hata hivyo, katika mapendekezo ya Mpango uliowekwa Mezani umeonesha kuwa kutakuwa na mwendelezo wa upanuzi wa Bandari ya Mtwara na bandari huru. Hivyo ni dhahiri kwamba Ujenzi wa Reli ni muhimu sana ili kuweza kusaidia usafirishaji wa mizigo ambayo itakuwa inapitia katika Bandari hii. Hivyo ni msingi kabisa ujenzi wa reli hii uingizwe katika mpango huu wa utekelezaji, uanzo kabla ya mwaka 2015 ili kutimiza ahadi ya llani ya Uchaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo napenda kuikumbusha Serikali, pamoja na kwamba imeelezwa katika Mpango huu, ni ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Kusini ambayo inajengwa Mtwara, lakini kwa kasi ndogo sana. Hospitali hii ni muhimu sana katika kanda hii, kwani ongezeko la watu ni kubwa sana; na kwa kuwa hali ya uchumi inakua, tunatarajia kwamba kutakuwa na viwanda ambavyo pia vitaongeza idadi ya watu. Hivyo, umuhimu wa uharaka wa ujenzi huu ni muhimu sana.

Naiomba Serikali kwamba mpango ambao umepangwa na ujenzi wa jengo la mapokezi na Idara ya Wagonja wa Nje, bado itakuwa ni hatua ndogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naiomba Serikali kuangalia namna ambavyo wanaweza kuweka kwenye

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. M. R. KASEMBE]

mpango, ujenzi wa jengo la kulaza wagonjwa, kwani ikumbukwe kuwa hii ni Hospitali ya Rufaa, na wagonjwa wanatoka mbali na wengine ni wagonjwa waliojiweza. Hivyo, haitawasaidia sana kama watakuwa wanatibiwa katika wodi ya nje. Pia ikumbukwe kwamba Ujenzi wa Hospitali hii ni wa muda mrefu sana, lakini unakwenda kwa kususua sana. Hivyo, naomba mpango huu uelekeze nguvu zake katika ujenzi wa hospitali hii muhimu kwa wakazi wa Kanda ya Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. DEOGRATIAS A. NTUKAMAZINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuunga mkono hoja, na kwa kumpongeza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Mahusiano na Uratibu) - Mheshimiwa Stephen Wasira na Tume yake ya Mipango, kwa kazi nzuri ambayo wameianzisha ya kusimamia uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema wakati nachangia kwa kusema kwamba tatizo kubwa ambalo Serikali haina budi ilishughulikie na ikiwezekana ilitatue, ni kuleta uwiano mzuri kati ya mipango inayoandaliwa na utekelezaji wake. Tuondoe *imbalance* hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni kwa Serikali kusimamia kikamilifu ukusanyaji wa mapato kwa kuipatia *TRA* viwango (*targets*) vya juu. Pia kwa maoni yangu, Tume ya Mipango ina wataalam wazuri, bado *capacity* ya Hazina kusimamia makusanyo ya mapato ni mdogo. Pia *mindset* ya Watendaji wa Hazina inatakiwa ibadilike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali iwezeshe MKURABITA iweze kurasimisha mali na biashara za wanyonge waweze kulipa kodi. *The informal sector which is a sleeping giant should be tapped.* Mimi nitaendelea kuwa Yohana Mbatizaji, kwa kupiga kelele nyikani (*voice in the wildness*) kuhusu umuhimu wa Serikali kuwa *serious* na suala la kuinua hali ya wanyonge (wazawa) kwa kuwa na sera ya upendeleo (*preferential treatment*) kwa wazawa – kama ilivyo katika nchi za Malaysia, Zimbabwe na *South Africa*.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. D. A. NTUKAMAZINA]

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo siri kwamba uchumi wetu uko mikononi mwa Watanzania wenyе asili ya asia, kama inavyokuwa Malaysia, uchumi wao ulikuwa mikononi mwa Wachina. Lakini Waziri Mkuu – Mahadhir Mohamad katika miaka ya 1980 alibadilisha hali hiyo kwa kuanzisha sera za upendeleo kwa wazawa, na sasa *indiginous Malayswana-compete* na Wachina katika biashara bila wasiwasi.

Mheshimiwa Spkika, kama Tume ya Mipango itasimamia utekelezaji wa miradi ya vipaumbele, naishauri Tume isaidie kujenga *capacity* ya Idara za Mipango katika Halmashauri zote waweze kuwa na uelewa wa mipango na umuhimu wa utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee kuhusu Utawala Bora. Viongozi wengi Serikalini hawako *serious*, hawajibiki ilia wanafurahia vyeo kujinufalsha. Siyo kama zamani wakati wetu. Kuna mmomonyoko wa maadili ya viongozi mkubwa sana. Katika hali hii ya *leadership crisis*, kweli tutasimamia miradi na kupata *Big Results Now?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kwamba tukamilishe ujenzi wa Uongozi *Institute* ili viongozi wote wa juu wapigwe msasa kwa kupewa *leadership skills* na *the ABC of Management*. Lakini pia wapewe mazoezi ya kijeshi, kama tulivyokuwa tunafanya *Kivukoni College* zamani, ili kujenga nidhamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema katika mchango wangu jana kuwa Serikali iwe *serious* katika kuwekeza katika Hospitali zetu za Rufaa kwa kujenga vituo vya kushughulikia magonjwa makubwa kama Magonjwa ya Moyo, Figo na Saratani ili kuokoa fedha nyingi zinazotumika kuwapeleka wagonjwa nje ya nchi. Hii itakuwa ni pamoja na kununua vifaa tiba vya kutosha. Pia kuwamotisha Madaktari Bingwa wasikimbie kutafuta kazi katika nchi nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mipango ya Maendeleo *should address* matatizo sugu ya Maji na Umeme. Hivyo

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. D. A. NTUKAMAZINA]

ndivyo vichocheo halisi nya maendeleo ya uchumi. Tatizo la maji ni kubwa sana, *we should be very serious about it.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, mimi binafsi huwa nawaogopa wawekezaji. *They are very sophisticated in terms of technology and management systems.* Wanaweza wakatuibia kwa urahisi. *The Government should regulate the private sector without stifling it.* Private sector iwe mhimili, lakini Serikali iongoze uchumi. Nadharia ya "Invisible Hand" tuwe waangalifu nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. DAVID Z. KAFULILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nafasi ya Tanzania kwa Afrika na mwenendo wa biashara duniani baina ya wakubwa wa dunia Ulaya, Marekani na China, inapaswa kutengenezewa mkakati. Mpaka sasa USA na Ulaya inaitazama Tanzania na South Africa kama *strategic countries* kwa uchumi wa Afrika. Hivyo, Serikali iwe na mkakati mpana katika eneo hili badala ya kubaki kuwa inashirikishwa tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafasi ya BRELA katika uchumi wa soko ni muhimu sana kwa sababu wawekezaji wa ndani na nje wote wanategemea sana ufanisi wa BRELA. Bahati mbaya sana BRELA imeoza, haiendi na wakati na imekuwa kero na inasababisha usumbufu mkubwa kwenye biashara hasa katika maeneo ya *Trade Mark, licence* na kadhalika. Nashauri ifumuliwe na kusukwa upya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, agenda ya maji ipewe msukumo katika utekelezaji. Maji ni kero namba moja kwa mujibu wa utafiti wa *Synovate 2009*. Ziwa Tanganyika lina asilimia 17% ya *fresh water* duniani na bado Tanzania ni nchi ya 11 kwa kuwa na mito mingi duniani. Lazima utolewe msukumo maalum kwa Mkoa wa Kigoma na nchi nzima hakuna maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania itumie nafasi yake ya mahusiano na China kukabili changamoto ya vijana wengi

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. D. Z. KAFULILA]

kukosa ajira kwa sababu ya kukosa ujuzi. Nashauri tujenge vyuo vya kutosha kama mpango maalum ili vichukue vijana wengi kwa kuwapatia ujuzi (*skills*) kuititia vyuo vya kati vinavyotoa vyeti na diploma. Hii ni elimu muhimu sana katika kujenga Taifa la watu wanaojitegemea. China wamefanya vizuri katika eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafasi ya *Stock Market* kwa uchumi wa soko. Soko la Mitaji ni nguzo muhimu sana katika kuwafanya wananchi washiriki uchumi wao, uwazi wa kodi na hivyo kuongeza mapato ya Serikali na kupunguza tatizo la mlingano wa ushiriki wa wananchi katika uchumi wao. Mpaka sasa *Domestic Market Capitalization* ni asilimia 10% ya *GDP* wakati nchi kama Kenya, *Domestic Market Capitalization* ni asilimia 40% ya *GDP*. Mpaka sasa tangu tubinafsische mashirika zaidi ya 300, lakini mashirika yaliyokuwa *listed* katika *Stock Market* ni 11 tu. Ni muhimu Serikali ihakikishe kuanzia mashirika yote ambayo Serikali inamiliki kwa asilimia fulani, yawe *listed* katika *Stock Market*. Tumezungumza Bungeni muda mrefu kuhusu mashirika hayo kuwa *listed*, lakini Wizara ya Fedha na Wizara zingine hakuna utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Hifadhi ya Jamii. Moja ya changamoto kubwa inayokabili watu wengi na hususan wazee, ni tatizo la huduma ya hifadhi ya jamii. Naishauri Serikali isisitize formula moja kwa Mifuko ya Hifadhi kwa maslahi ya jamii. Mifuko hii iunganishwe, uwe Mfuko mmoja kwa urahisi wa usimamizi. Zaidi Serikali itenye fedha kuchangia wateja kutoka sekta isiyo rasmi kama njia ya kuwahamasisha kujiunga na Mifuko ya Hifadhi. Bado Tanzania ina asilimia ndogo sana (asilimia 6%), ya wananchi wake waliopo kwenye Mifuko. Rwanda, Serikali inachangia asilimia 50% kwa wajasiriamali waliopo kwenye Mifuko. Sisi tuanze walau na asilimia 10%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hoja ya bima kwa wananchi. Bima ni eneo muhimu sana kwa ustawi wa uchumi na maisha ya watu. Mpaka sasa *insurance penetration ratio* ni asilimia 0.9%, ukilinganisha na nchi kama Kenya ambayo ni asilimia 2.6%. Serikali lazima iwe na mpango wa kuhakikisha

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. D. Z. KAFULILA]

sekta ya bima inakua na yenyewe Serikali iwe mstari wa mbele kuonyesha mfano. Mpaka sasa magari yote ya Serikali hayana bima. Nashauri magari yote ya Serikali yakatiwe bima. Majengo yote ya Serikali hayana bima, nashauri majengo yote ya Serikali yakatiwe bima. Huu utakuwa mfano mzuri na utaongeza uwezo wa *NIC*. Pia kwa kuwa kuna makampuni mengi ya kigeni nchini yanayokata bima kwa makampuni ya nchi zao, naishauri Serikali iweke utaratibu kuhakikisha makampuni hayo ya bima ya nje lazima yashirikiana na makampuni ya ndani kuhakikisha Serikali inatambua mapato ya makampuni hayo na hivyo kupata kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utawala bora bado ni changamoto kubwa. Mawaziri wengi hawatimizi wajibu wao. Mipango ni mingi na mizuri. Utaona nchi zingine zinatekeleza mipango tullyobuni Tanzania, lakini bado nchi yetu tulio buni mipango hiyo tumeshindwa. Kuna umuhimu wa kupitia upya Sheria ya Utumishi wa Umma kwa sababu kuna vizuizi vingi vinavyomlinda mtumishi, matokeo yake kuwa chanzo cha uzembe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kwanza kumpongeza mtoa hoja kwa mpango mzuri aliouwasilisha ambao umeainisha mambo kadhaa yatakayotiliwa mkazo kwa mwaka 2014/2015 kwa ajili ya maendeleo ya Taifa letu. Binafsi nimevutiwa na mapendekezo yaliyowasilishwa na niseme tu kuwa naunga mkono hoja hususan katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utalii. Katika maelezo yake, Serikali imesema kuwa inakusudia kujenga na kuboresha vivutio vya utalii nchini. Hili ni suala la msingi sana. Ingawa muda wa utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2013/2014, unaonyesha kuwa idadi ya watalii wanaokuja nchini imeongezeka na kufikia 1,077,058 mwaka 2012 bado idadi hii ni ndogo mno ukilinganisha na vivutio tulivyo navyo na pia uwezo tulio nao. Ni vyema mamlaka

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. C. V. MAG/GE]

zinazohusika zikaongeza idadi, juhudhi, maarifa na ubunifu katika kutangaza vivutio hivyo tulivyo navyo ili watalii waongezeka. Kuongezeka kwa watalii ni kuongezeka kwa pato la fedha za kigeni, kukua kwa ajira kwa wananchi wetu na kuongezeka kwa mapato ya kodi pamoja na faida nyingine nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Tanzania tukijitapa kwa watalii milioni moja kwa mwaka 2012, Malaysia ambako ndio tumejifunza Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa (*Big Results Now*), mwaka huohuo walipokea watalii milioni 24.6 na kupata dola bilioni 1.8! Dubai, Falme za Kiarabu, nchi ndogo kabisa, walipata watalii milioni 9.3 na kuingiza dola bilioni 4.6 kwa mwaka 2011. Hata majirani zetu Kenya wametupita kwa idadi ya watalii. Tunahitaji kuongeza bidii katika hili ili tunufaikie ipasavyo na sekta ya utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu rasilimali, nimesoma pia katika mapendekezo haya ya Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2014/2015 kwamba changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa 2012/2013 ni pamoja na ufinyu wa rasilimali fedha, hususani upatikanaji wa mikopo ya kughamramia miradi. Tatizo la ufinyu wa rasilimali fedha linaweza kuongezeka kama hatutazingatia ushauri wa Kamati ya Bunge ya Bajeti kuhusu mapendekezo haya kwamba sasa Serikali irejee katika utaratibu ambao ilikuwa ikiutumia katika kipindi cha kabla ya mwaka 1994/1995 wa *Capital Budget* kwa kukopa kutoka Taasisi kadhaa za fedha ili kuendesha bajeti na mapato yanayopatikana yakalipie madeni. Hii itasaidia kuondokana na tatizo la rasilimali fedha na pia kuwezesha miradi mbalimbali ya Serikali kutekelezwa kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuondokana na tatizo la rasilimali fedha, nashauri pia Serikali iongeze vyanzo vipyaa vyaa mapato badala ya kuendelea na utaratibu uleule wa kodi kwa wafanyabiashara na watumishi kama chanzo kikuu. Aidha, ni vyema pia Serikali ikaangalia namna ya kupunguza matumizi yake ya kawaida ili fedha zitakazookolewa hapa zitumike kwa matumizi ya maendeleo.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. C. V. MAG/GE]

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo naona Serikali inapaswa ijipange upya katika mapendekezo haya ni suala la ajira. Nimesoma kwa kuridhika namna wahitimu toka Vyuo vya Elimu ya Juu wanavyoongezeka. Hata hivyo nimekuwa najiuliza kuwa iwapo kasi ya ongezeko hilo la wahitimu linaendana na nafasi za ajira zilizopo katika soko?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vyema Serikali ikaweka mikakati madhubuti katika suala la ajira kwa kutoa fursa kwa sekta binafsi kuajiri zaidi. Aidha, natoa wito pia kwa vijana wenzangu kwamba wazingatie uwezekano wa kujajiri binafsi na pia Serikali katika mapendekezo iweke mikakati ya kuwasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mikopo, nimeona pia katika mapendekezo haya, mpango na mikakati ya Serikali kwa maendeleo na ustawi wa wanawake. Naipongeza Serikali kwa kutoa fedha kuisaidia Benki ya Wanawake Tanzania ambapo kwa mwaka 2012/2013, Serikali ilitoa shilingi bilioni 1.1 na kuiwezesha Benki hiyo kufikisha mtaji wa shilingi bilioni 8.2 na hatimaye Benki hiyo kufikisha utoaji wa mikopo kwa wanawake wajasiriamali 10,607.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hatua hizo, nashawishika kuamini kwamba bado mapendekezo haya yanahitaji kuboreshwa kumsaidia mwanamke hususan wa vijiji. Nashawishika kuamini kwamba wanawake wengi waliofaidika na mkopo ni wale walioko mijini. Hivyo basi, Serikali ijipange kuisaidia Benki ya Wanawake ili kuweza kuwafikia wanawake wa vijiji ambao ndio wengi na wenye uhitaji zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. SUSAN L. A. KIWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kitabu cha Mpango, ukurasa 13, 2.2.1(ii), utekelezaji unaonyesha kufungua Ukanda wa *SAGCOT* kwa barabara ya Kidatu – Ifa – Lupilo – Malinyi – Londo – Lumecha/Songea, ni vizuri. Hata hivyo, pamoja na Serikali kuahidi kujenga barabara ya Ifakara – Mlimba kwa kiwango cha lami, pia

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. S. L. A. KIWANGA]

Mlimba – Taweta – Madeke/Njombe ili kufungua barabara ya Kilombero - Njombe ambapo ndilo eneo linalozalisha mpunga na *cocoakwa* wingi na ndiko kwenye mradi mkuwa wa *KPL*. Sijaona mahali popote kwenye Mpango huu inapozungumzia kuhusu barabara hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maji, Mpango umezungumzia upatikanaji wa maji katika Jiji la Dar es Salaam katika miradi mbalimbali ukiwemo na mradi tarajiwa wa Bwawa la Kidunda liliopo Morogoro Vijijini. Hata hivyo, Mpango hauzungumzii chochote kuhusu kupeleka maji ya Bwawa la Kidunda katika Wilaya ya Morogoro na Manispaa ya Morogoro ambapo kuna tatizo kubwa la maji. Hivyo naishauri Serikali iboreshe Mpango kwa kuingiza usambazaji wa maji Morogoro na Manispaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali iingize kwenye Mpango, Mradi wa Maji wa Mji wa Ifakara kwenye chanzo vya Kiburubufu ambapo andiko la gharama ya mradi huu limeshafikishwa ofisi ya Waziri na Naibu Waziri. Sababu za kusitiza mradi huu ni kutokana na ongezeko la watu katika mji huo, takriban 150,000; pia kuna Chuo Kikuu cha Madaktari Wauguzi, Tawi la Chuo cha SAUTI na vyuo vingine vidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango umezungumzia miradi mingi ya umwagiliaji, ambayo itatekelezwa katika Wilaya za Kilombero na Ulanga. Pamoja na nia njema hiyo, Mpango hauzungumzii ujenzi wa maghala katika Wilaya hizo. Pia hauzungumzii upatikanaji wa soko la mpunga, ambapo hivi sasa wakulima wa Wilaya hizo wamekumbwa na umaskini kwa kubaki na mpunga, hali ya soko na bei ya mchele imeporomoka; ambapo imesababishwa na Serikali kuleta mchele toka nje, pia kufunga mipaka kwa mchele kutouzwa nje. Wakulima wa mpunga wako kwenye hali mbaya, wameshindwa kulipa mikopo, kufanya maendeleo ya watoto wa shule na makazi na kadhalika. Wananchi wa Kilombero na Ulanga wanasubiri Kauli ya Serikali hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa mpunga – Ngalimia, Morogoro wa hekta 31,500; umeathiri wananchi wa

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. S. L. A. KIWANGA]

Kata ya Mlimba, Wilaya ya Kilombero, Kijiji cha Miembeni. Mradi na mipaka inaonyesha karibuni eneo la kijiji linalotumiwa kwa kilimo, linaingia kwenye mradi huo. Hii italeta athari kubwa kwa wananchi wa Mlimba na Miembeni. Hivyo, naishauri Serikali ikarekebishe mipaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Mpango uone haja ya kuishauri *TRA* kukopesha mashine za risiti. Nashauri kwamba kwa kupitia mashine hizo, wananchi wapewe motisha ambapo mwananchi atakayedai risiti kwa kila anachonunua na baada ya muda maalum na kiwango maalum kitakachopendekezwa; mtumiaji huyo atarudishiwa asilimia fulani ya pesa. Hiyo itazidisha ari ya kudai risiti kwa manunuzi na Serikali kupata mapato ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iachane na kodi sumbufo kama za kulipia laini za simu kwani watumiaji wengine hawana hata simu, bali laini tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. DKT. ANTONY G. MBASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kuchangia machache katika Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2014/2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna Taifa lolote litakaloweza kukuza uchumi wake, kuleta hali bora ya maisha kwa watu wake; kama hakuna mpango makini wa maendeleo uliowekwa na kuridhiwa na wananchi wake. Ili kuweza kufanikisha Mpango mzima wa Maendeleo, yafuatayo ni muhimu sana kuzingatiwa:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, kuwa na miradi michache inayotekelizwa badala ya kuwa na miradi ambayo haiwezi kutekelezwa. Hakika tumekuwa na miradi mingi sana ambayo haina ufanisi mzuri. Hii inatokana na kuwa na vyanzo vichache vyaa mapato na muda mwingine kutotolewa kwa fedha za miradi husika kwa wakati. Mara nydingi miradi hii hutekelezwa kwa ubora usiofaa, aidha kwa

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. DKT. A. G. MBASSA]

sababu ya muda wa utekelezaji kwisha au sababu ya uchache wa fedha. Napendekeza kuwepo na miradi michache ya kipaumbele na itekelezwe kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ni kupunguza matumizi makubwa ya Serikali. Suala hili limekuwa likijadiliwa au kuongelewa mara kwa mara lakini bila ya utekelezaji wowote. Suala hilo linajitokeza katika zabuni mbalimbali zinazotangazwa na Serikali kupitia Bodi za Manunuzi. Manunuzi haya hugharimu fedha nyingi sana na kuna tofauti kubwa sana baina ya bei inayotangazwa na bei halisi ya bidhaa kwa wanunuzi wa kawaida. Aidha, nashauri kupitia Bodi za Zabuni na Manunuzi kuwa makini katika kutoa zabuni hizo. Bodi zizingatie hali halisi ya bei iliyopo sokoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, Serikali kutotoa fedha kwa wakati. Imekuwa hali ya kawalda kwamba fedha nyingi za miradi kuletwa au kutolewa zikiwa zimechelewa sana. Taratibu za pesa pale zinapofika zimechelewa, taratibu za matumizi zisipokamilika, italazimu pesa hizo zirudishwe Hazina. Mbali na hayo, itabidi zifanyike semina na warsha mbalimbali ambazo nyingine hazina manufaa au tija kwa Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuondoa kero hii, nashauri pesa ziwe zinatolewa kwa wakati muafaka na kufanya kazi iliyokusudiwa. Kuwepo na utaratibu wa kumalizia miradi iliyopitishwa kabla ya kuanzisha au kupendekeza miradi mipyä. Hii itaondoa uititiri wa miradi ambayo haifanikiwi au kutekelezwa kwa manufaa ya wananchi ambao ndio walengwa hasa au ndio waibuaji wa miradi hiyo kulingana na fursa, vikwazo na mazingira yaliyopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni matumaini yangu kuwa hoja hizi zikizingatiwa, zitaboresha hali ya Mpango huu wa Maendeleo wa Taifa wa 2014/2015. Katika hilo, hakika utekelezaji wa mipango ya kipaumbele utazingatiwa na kupunguza utekelezaji wa miradi mingi inayofanyika chini ya kiwango na usimamizi duni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. MUSTAPHA B. AKUNAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango wa Maendeleo wenyе vipaumbele sitа kwa gharama ya shilingi trillioni 20 unawezekana kama yafuatayo yatatendeka:-

(1) Fedha zkipangwa, zikapatikana kwa muda wake;

(2) Wako wataalam mahiri wa kuongoza utekelezaji wake; na

(3) Serikali na Maofisa wake Wakuu – Mawaziri, Makatibu Wakuu, Wakurugenzi wa Idara mbalimbali, Wakuu wa Mikoa na Wakuu wengine watajali muda; yaani kuwahi kazini na kutoa uamuzi katika muda unaostahili. Kusive na uendeshaji wa Kamati – yaani hakuna uamuzi mpaka kikao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, Watanzania lazima wawe na tabia (*culture*) ya kazi. Watu waache uvivu wa kucheza *pool*, bao na kuliwa. Napendekeza kwamba pombe ya aina ya viroba ikatazwe na vijijini kuwe na masaa maalum ya kufungua baa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, Mpango huu ili ufaulu ni lazima uwe na “*monitoring*” ama “*evaluation mechanism*”. Ikitibidi kama hali imebadilika, kuwa na *midterm review* kukwepa miradi inayokwama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kuunga mkono hoja hii ambayo imeletwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Mahusiano na Uratibu).

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kuchangia hoja kwa kukubaliana na Mpango wa Serikali wa Matokeo Makubwa Sasa (*Big Results Now*). Matokeo Makubwa Sasa yanajikita katika maeneo mbalimbali yakiwemo barabara, madaraja na vivuko. Hata hivyo, naomba Waziri anipe

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. L. M. MNG'ONG'O]

majibu kwa nini barabara ya Musoma – Mugango hadi Busekela (*Majita Road*) haipo kwenye Mpango wa Serikali? Barabara hii ni klungo kwa Wilaya mbili, Wilaya ya Bunda kwenda Kwimba na Wilaya ya Ukerewe kwenda Visiwa vya Irugwe).

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii imo kwenye ahadi za Mheshimiwa Rais Kikwete wakati wa kampeni na pia Rais wa Awamu ya Tatu. Barabara hii ndiyo inayotegemewa kiuchumi na wananchi wa Wilaya ya Butiama, Tarafa ya Nyanje na wananchi wanaotoka Ukerewe kwenda Visiwa nilivyovitaja. Barabara hii ikijengwa kwa kiwango cha lami, itafungua uchumi wa Wilaya ya Butiama. Ni lini ahadi hii itatekelezwa kwa kujenga barabara hii? Bajeti ijayo lazima Serikali ihakikishe barabara hii inajengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya utalii ni muhimu, hivyo barabara ya Iringa – *Ruaha National Park* ikamilike kwa kujengwa kwa kiwango cha lami. Pia barabara iendayo *Kitulo National Park* kutoka Mufindi hadi Kitulo nayo ijengwe kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikopo kwa wanawake ni muhimu ili kupata mitaji. Banki ya Wanawake iwafikie wanawake Mikoani badala ya kuwa kwenye Kanda chache peke yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. BETTY E. MACHANGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna haja kubwa mpango wa 2014/2015 ulenge elimu. Hakuna Taifa limeendelea duniani bila wananchi wake kuwa na elimu ya kutosha. Tunaishukuru Serikali na wananchi kuchangia ujenzi wa shule za kata, ambazo zitakuwa mkombozi wa Watanzania kama tutaendelea kuwekeza katika shule hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ripoti ya *World Bank* ya 2004 ilianisha nafasi za kazi Tanzania zilivyochukuliwa na wageni kwa sababu ya elimu yetu kutokuweza kukidhi

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. B. E. MACHANGU]

mahitaji (*demands*) za soko la ajira. Mwaka 2006 tullijenga shule kila kata. Leo ni miaka saba na kiwango cha umaskini hakipungui kwa sababu elimu inayotolewa haina ubora wa kutosha (*quality education*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafiti zinaonyesha kwamba wanafunzi ambao wanaingia Vyuo vya Ualimu wanaingia na 'grades' ndogo na hivyo kuwa na uwezo mdogo katika yale masomo waliyosomea kufundisha. Wale wanaojiriwa na idara nyingine zisizo elimu, tafiti zinaonyesha kuwa wanakuwa hawana stadi za kazi zinazoridhisha waajiri; hivyo ajira nyingi kuchukuliwa na wageni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kujenga Taifa la watu ambao wameelimika, ambao wanaweza kutatua na kusimamia changamoto za maendeleo zinazolikabili Taifa hili; tuwekeze *heavily*kwenye elimu kwanza. *It is high time* Serikali ichoshwe na lawama za wananchi kuhusu elimu, ifanye kazi majengo machakavu ya shule, upungufu wa madawati, ukosefu wa maabara, ukosefu wa vitabu, vyumba vya Walimu, Walimu wa Sayansi na maslahi ya Walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ni kuongeza tija kwenye kilimo, hasa katika mazao yenye thamani kubwa. Zao la kahawa linaleta pato kubwa la Taifa. Ningetarajia Serikali ije na mpango kabambe wa kuboresha na kuendeleza zao la kahawa.

Wakulima wa kahawa wanalamikia bei kubwa ya dawa ya kahawa, ambayo kimantiki dawa hizi zilipaswa ziwe na ruzuku ili wakulima wapate motisha zaidi ya kulitunza zao la kahawa. Badala yake ruzuku imewekwa tu kwenye miche ya kahawa, ambayo hata hivyo wakulima wanaopata ni wachache. Iko haja Serikali ijue *Big Results Now* ni pamoja na *bumper harvest* ya kahawa kutoka Kilimanjaro, Kigoma, Mbeya, Kagera, Mbinga na kwingineko na siyo kwa Mkoa mmoja tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, liko pendekexo la kuhimili changamoto zinazotokana na mabadiliko ya tabia nchi.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. B. E. MACHANGU]

Tumeshuhudia ukame takriban miaka mitatu (3) kwa Ukanda wa Kaskazini (Manyara, Arusha na Kilimanjaro). Tumeshuhudia pia maporomoko ya udongo Wilayani Same na Mwanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafiti zilizofanyika Kimataifa za Sera za Chakula zilionya katika mukutano wake Berlin 2013 kuwa sera sahihi za kuzuia na kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi, nchi za Afrika, Kusini mwa Jangwa la Sahara, zitaathirika sana na kuongezeka kwa ukosefu wa ajira, kuongezeka kwa utapiamlo, upungufu wa mazao hasa ifikapo 2050. Tayari tafiti za mama na mtoto za 2010 zinaonyesha kwamba watoto wa Tanzania wameathirika na utapiamlo kwa asilimia 42%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, iko haja ya Serikali kuidhibiti hali hii kwa kuweka fedha katika utafiti, miundombinu vijijini, umwagiliaji, usimamizi wa uvunaji wa maji ya mvua na usambazaji maji. Pia fedha ziwekwe katika mpango kabambe wa kupanda miti na kulinda misitu yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutumia fursa ya ongezeko la watu nchini kuleta manufaa ya uchumi (*demographic dividend*) kwa kupunguza kiwango cha utegemezi/wafanyakazi. Kiwango cha uzazi (*fertility rate*) ya mama wa Kitanzania anayeweza kuzaa ni watoto 6 – 7. Taarifa za afya zinaonyesha kuwa wanawake 390 hufa kila mwaka, wakati wa kujifungua.

Sambamba na hilo, kiko kilio kikubwa cha uhaba wa Madaktari, uhaba wa Wauguzi, ukosefu wa magari ya kubebea wagonjwa pamoja na vifaa vingine kama *X-rays*, *Ultra Sound* katika Zahani na Vituo vya Afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkutano wa Kimataifa wa Maendeleo wa Idadi ya Watu (*ICPD*) uliofanyika Cairo (Misri) 1994 na mwingine uliofanyika Istambul mwaka 2012; ulikuwa na agenda zilizotaka nchi zote duniani kutekeleza maazimio ambayo ni pamoja na kupunguza na kuondoa vifo vya watoto, vifo vya mama wajawazito na kupunguza kiwango cha uzazi kwa kila mwanamke anayeweza kuzaa. Utekelezaji

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. B. E. MACHANGU]

wa maazimio haya hapa Tanzania, hasa katika eneo la maendeleo ya idadi ya watu, ni chini ya asilimia 20% kwa kipindi cha miaka 20.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kweli Serikali ina mpango wa kutumia idadi ya watu kupata *demographic dividend*, iko haja mambo tajwa pamoja na elimu, *gender equality*, ajira kwa vijana, *reproductive health*, *population structure*, *migration* na kadhalika ifanyiwe kazi. Serikali itenye kitengo kinachojitegemea katika Tume ya Mipango, kifanyie kazi maudhui ya maendeleo ya idadi ya watu (*population development*). Nchi nyingi zimeanzisha *commissions* za *population* na zimefanikiwa katika hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu nishati, Serikali iharakishe mchakato wananchi wapikie gesi. Gesi iingizwe kwenye nyumba kama umeme. Hii itasaidia sana wananchi kutokukata miti kwa ajili ya mkaa endapo bei ya gesi itakuwa ndogo ili mtu wa kipato cha chini aweze kununua. Mpango huu utaokoa misitu, utatunza mazingira, mapato zaidi yatapatikana katika sekta ya utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu viwanda, Serikali ifufue/itwae hati za viwanda vilivyobinafishwa ambavyo vimefanywa maghala. Kama *products* ambazo ziliikuwa zitengenezwe na viwanda hivyo zimepitwa na wakati (mfano Kiwanda cha Magunia, Moshi); basi mpango wa *PPP* uharakishwe kutungiwa Kanuni, tenda zitangazwe, sekta binafsi wakishirikiana na Serikali (Halmashauri/Wizara), waanzishe viwanda katika maeneo yenye fursa katika Wilaya mbalimbali nichini mfano maeneo ya *Big Six*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna sababu ya mahindi kusafirishwa kupeleka Burundi, Congo, Malawi na kadhalika badala yake viwanda vianzishwe ili viongeze thamani, wauze unga Congo, Malawi na kadhalika. Yapo maeneo yenye mifungo mingi, asali, matunda na kadhalika na yenyewe yaangaliwe kwenye suala zima la viwanda

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya uchumi. Ukuaji wa pato la taifa kwa asilimia 7% mwaka 2013, maeneo ya ukuaji ni pamoja na usafiri na mawasiliano (asilimia 18.4%). Hivyo, ni muhimu kuongeza usafiri – yaani barabara, viwanja vya ndege na mawasiliano, hususani katika maeneo ambayo hayana usafiri fasaha, hayana lami. Mfano barabara ya Njombe – Ludewa – Itoni na barabara ya Njombe – Ludewa – Lupingu. Pia mawasiliano huongeza uchumi na mzunguko wa fedha. Kuna maeneo mengi hayana mawasiliano ya simu. Mfano Mikumi, Ruaha, Mbuyuni (Kitonga), Ludewa, Lugurawa, Manda, Lupingu hakuna mawasiliano ya simu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muhimu maeneo mengi ya nchi yetu yakawa *accessible-communicated*. Barabara zikiwa mbaya, unatumia muda mrefu sana kusafiri na unachelewa kuzalisha. Usafiri ni muhimu, hivyo lazima gharama za usafiri ziwe za chini ili usafiri uwe ni huduma (*service*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna nauli za vijijini, wananchi wanatozwa bei kali sana. Sasa SUMATRA wapo Dar es Salaam tu. Je, nauli za ndege ni taasisi gani *in-control?* Mfano nauli ya ndege kutoka Dar es Salaam – Njombe – Dar es Salaam – Rukwa unaambiwa US\$ 500. Hii ni bei ya *return ticket* ya Dar es Salaam – Dubai (*Economy Class*) au Dar es Salaam- Nairobi. Usafiri unaongeza kipato kwa asilimia 18.4%. Iweje Tanzania hatuna Shirika la Ndege, kutwa tunawachangia KQ/SA/Emirates, siyo sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumuko wa bei umepungua kutokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa chakula. Sisi wananchi wa Mkoa wa Njombe (Wanging'ombe, Njombe, Ludewa) ni miongoni kwa watu tunaozalisha chakula kwa wingi. Hata hivyo, kutokana na barabara, wanaonunua zaidi chakula ni *FDR Serikali*.

Naomba kuuliza, kwa nini tunawakopa wakulima mahindi? Maana wao wakipeleka watoto shule inabidi ada zilipwe *immediately*. Pia ushuru wa mazao unacheleweshwa

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. DKT. P. H. CHANA]

sana kulipwa Halmashauri ya Ludewa. Sasa kwa niaba ya akina mama, wanaomba fedha za mahindi zilipwe mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mwenendo wa viwango vya riba, kwa mujibu wa Taarifa ya Bunge, mwenendo wa viwango vya riba za benki bado ni kubwa. *Interest* ya *Fixed Deposit* ni ndogo na *interest* ya *loan* ni kubwa. Sasa hivi tuna changamoto ya ajira katika nchi yetu. Kwa nini hizi benki zisikopeshe vijana? Mradi endelevu na zile fedha za mabilioni ya JK, *NMB* nilitarajia ziwe *revolving fund* hata leo watu wakakope, hususan vijana. Naomba ufanuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, akiba ya fedha za kigeni ukilinganisha na Deni la Taifa na misamaha ya kodi. Mpaka Julai, 2013 akiba ya fedha za kigeni ni US\$ milioni 4353.4 wakati mpaka Juni, 2013 Deni la Taifa ilikuwa ni bilioni 15.29. Je, Sera ya Misamaha ya kodi inasemaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, usafiri ni pamoja na madaraja. Daraja la Mto Ruhuhu, Daraja la Kivukoni – Kigamboni (Dar es Salaam), ni maeneo muhimu ambayo Serikali lazima iwe makini kutekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, reli ya kikanda, Serikali ina mpango gani kujenga reli kutoka Ludewa – Mchuchuma/Liganga hadi Makambako?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa 20, mradi wa makaa ya mawe Mchuchuma – Njombe. Mradi huu utakapokamilika unatarajiwa kuzalisha megawati 600. Napenda kujua ni lini unatarajiwa kuzalisha umeme megawati 600?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. GOODLUCK J. OLE-MEDEYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa ahadi za Rais. Kuanzia bajeti na Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2011/2012 hadi 2013/2014, nimekuwa nikiomba kuwa ahadi za Mheshimiwa Rais alizotoa kwenye Jimbo langu wakati wa kampeni za Uchaguzi Mkuu 2010 na pia kwenye ziara yake baada ya uchaguzi; ziwekwe kwenye Mpango wa Maendeleo na kutengewa fedha kwa ajili ya kutekeleza ahadi za Rais kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni miradi ya maji safi. Tarehe 17/9/2010, Mheshimiwa Rais akihutubia mukutano wa hadhara kwenye Uwanja wa Emaoi, aliahidi kuwa Serikali itaandaa mpango kamambe (*master plan*) wa maji kwa Halmashauri yote ya Wilaya ya Arusha na kutenga fedha kwa ajili ya utekelezaji ili ifikapo 2015, kero ya maji kwenye Wizara hiyo iwe ndoto.

Naomba kuwa chini ya *BRN*, Mpango wa Maji wa Halmashauri ya Wilaya ya Arusha utengewe fedha za kutosha ili kuondoa kero ya maji ambayo inaelekea kugharimu, siyo nafasi za uongozi tulizo nazo tu, bali shinikizo la damu linaweza kutupata na hivyo kutugharimu uhai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, barabara. Tarehe 17/9/2010, Mheshimiwa Rais aliahidi kuwa:-

(i) Atajenga barabara ya lami toka njia panda ya barabara kuu iendayo Nairobi na Ngaramtoni hadi Seliani *DDH*, Emaoi/Sambasha.

(ii) Barabara zote za Wilaya hiyo zitatengenezwa kwa kiwango cha changarawe ili zipitike mwaka mzima.

(iii) Tarehe 1/11/2012, Mheshimiwa Rais alipozindua Hospitali ya Wilaya ya Olturumet, aliahidi kuwa Serikali itajenga barabara ya lami toka Radio Habari Maalum hadi Hospitali ya Olturumet.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. G. J. OLE-MEDEYE]

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kulinda heshima ya Mheshimiwa Rais wetu, naomba barabara hizo ziwekwe kwenye Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2014/2015. Zitengwe fedha kwenye bajeti ya 2014/2015 ili ahadi hizo zitekelezwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, ujenzi wa reli. Ili kuboresha miundombini ya uchukuzi kwa ushoroba wa katи (*central corridor*) hadi kufikia nchi jirani za Burundi, Rwanda na Congo; nashauri reli ya katи ijengwe upya kwa *gauge* mpya. Reli hiyo itakapokamilika, itaongeza uwezo wa kusafirisha mizigo ya wawekezaji na nchi jirani na hivyo kuongeza tija katika uchumi wa Taifa letu. Aidha, kukamilika kwa reli hiyo kutapunguza uharibifu wa barabara kutokana na wingi na ukubwa wa mizigo inayobebwa kwa malori.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. VITA R. M. KAWAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri Stephen Wasira pamoja na Tume ya Mipango, kwa kuandaa Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo 2014/2015 na Mheshimiwa Waziri kuwasilisha vizuri sana kwa muhtasari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeelezwa kuwa juhudini nzuri zilizofanyika, zimesababisha kupungua kwa mfumuko wa bei na hii imetokana a ongezeko la mazao ya chakula (mahibndi, mpunga na mtama). Hii imejidhihirisha baada ya mavunzo ya mazao ya chakula hapa nchini. Ushauri wangu kwa Serikali, lisitumike suala la kupunguza mfumuko wa bei kwa kuagiza mazao hayo nje, ambapo inawaumiza wakulima, wanababaika na soko. Tutumie utaratibu huu kwa kununua na kuingiza sokoni chakula kinacholimwa nchini kwa wingi, lakini pia tuisiwakope wakulima mazao yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasema katika mipango yetu na hata katika mapendekezo ya Mpango huu, kuwa tunahitaji msukumo mkubwa katika kukuza sekta hii ya kilimo. Sekta hii ndio yenyeye kuajiri watu wengi, ndio Serikali inawekeza fedha nyingi katika pembejeo na mitando ya

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. V. R. M. KAWAWA]

umwagiliaji na sehemu za kuhifadhia mazao yanayonunuliwa na Serikali. Hata hivyo, inapofika suala la soko la mazao ya mkulima ili kukuza pato la mkulima na Serikali za Mitaa, Serikali Kuu:-

- (i) Inanunua kwa kukopa.
- (ii) Inafunga masoko ya mazao ili kuuza nje ya nchi.
- (iii) Inaagiza chakula kutoka nje ili kupunguza pato lao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Serikali itaendelea hivi, itakuwa ndoto kufikia mapema nchini yenye uchumi wa kipato cha kati cha Mtanzania cha Shs. 1,670,032/= – Shs. 6,500,000/=. Serikali inapoamua maamuzi ya kusaidia mtu aweze kuongeza pato, lazima ifungue milango yote; siyo tu kufungua mmoja na mwagine tunafunga. Ushauri wangu ni kwamba:-

- (i) Serikali iendelee kusaidia pembejeo za kilimo cha wakulima wa hali ya chini inavyopaswa.
- (ii) Inunue mazao kwa fedha taslimu.
- (iii) Ihakikishe maghala ya kuhifadhia mazao yao vijijini yanajengwa, kwani hata kama Serikali itashindwa kununua yatakuwa yamehifadhiwa vizuri vijijini na kupata soko lingine yakiwa salama na sivyo ilivyo sasa kwamba inasitiza kununua mahindi yao, wanabaki hawana pa kuyahifadhi, mvua zinaanza kunyesha, mlanguzi anakwenda kunua mazao kwa bei anayotaka yeye ya chini, mkulima anaona bora auze kuliko kuona mazao yake yanaharibika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imetueleza hatua inazochukua za kujenga maghala makubwa. Nawapongeza lakini mipango lazima pia ielekezwe katika *source* ya mazao hayo, kuwe na maghala ya kuhifadhia chakula. Ni lazima tumfikirie mzalishaji maskini – mkulima mdogo.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. V. R. M. KAWAWA]

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu gesi, naomba kuishauri Serikali kwamba tuanze mapema kuandaa Mpango, Sera na Sheria ya Mapato ya Gesi yatatumikaje. Mimi nashauri tuwe na Sheria ya Mapato na Matumizi ya Gesi yatakayokuwa *ring fenced* ili yaelekezwe katika miradi ya maendeleo maalum itakayosaidia Watanzania wote watakaoona matokeo ya haraka na itakayochochea kusaidia maendeleo yao.

Pia mapato ya miradi hiyo kusaidia kulipa mikopo tuliyokopa, kupunguza mzigo wa madeni tuliyo nayo. Mipango mingine ya kuendeleza vijana wetu kuwaelimisha ufahamu na ustadi, nao uendelee tena kwa kasi mno ili tuweze kuwa na wajuzi wengi katika eneo hili la gesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ili tuweze kuwekeza kifaida lazima pia sekta muhimu ziende pamoja katika kuwekeza ili kupata huduma wezeshi. Mfano maji, barabara na umeme katika maeneo ya miradi. Lazima tu-*combine* program zetu za sekta hizi na tusimamie, ziende sambamba ili kurahisisha uwekezaji na kutupa sisi pia “negotiation power” kwamba nasi tumewekeza kiasi gani kama Serikali katika eneo la miradi kurahisisha uwekezaji, hivyo, kuwa na nguvu katika majadiliano ya mgawanyo wa mapato ya miradi na wawekezaji kwa kuthaminisha uwekezaji na miundombinu yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. HAJI KHATIB KAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya uvuvi hapa nchini ni moja ya sekta inayoweza kuchangia zaidi katika kukuza uchumi na kupunguza umaskini kama ilivyoainishwa kwenye Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA) na llani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 – 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni kutokana na ukweli kwamba nchi yetu imebarikiwa kuwa na maeneo mengi ya maji baridi na maji ya bahari yenye rasilimali nyingi za uvuvi, ambapo shughuli za uvuvi hufanyika. Tanzania Bara ina

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. H. K. KAI]

Ukanda wa Pwani wenye urefu wa kilomita 1,424 na upana wa maili za majini 200. Eneo hilo la bahari limegawanyika katika maji ya kitaifa yenye upana wa maili za majini 12, sawa na kilomita za mraba zipatazo 64,000 na eneo la bahari kuu (*deep sea*) lenye upana wa maili za majini 188, sawa na kilomita za mraba zipatazo 223,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la maziwa makuu matatu ambayo ni Ziwa Victoria lenye kilomita za mraba 68,800 ambapo Tanzania humiliki asilimia 51% sawa na kilomita za mraba 35, Ziwa Tanganyika lenye kilomita za mraba 32,900 ambapo Tanzania humiliki asilimia 41% sawa na kilomita za mraba 13,489 na Ziwa Nyasa lenye kilomita za mraba 30,800 ambapo Tanzania humiliki asilimia 18.51% sawa na kilomita za mraba 5,700. Pia yapo maziwa ya kati na madogo 29.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na hali hiyo na iwapo kweli Serikali ina nia ya dhati ya mapendekezo ya Mpango huu wa Maendeleo wa Taifa, basi ni wakati sasa kuwawezesha wavuvi kwa kuwapatia mikopo ya fedha, kuwawezesha kitaalam pamoja na kuwatengenezea miundombinu ya kuwawezesha kupata vifaa vya uvuvi kwa bei nafuu. Iwapo Serikali itafanya hivyo kwa wavuvi, basi kwa kweli dhamira hii ambayo ni njema kwa wananchi na Taifa kwa ujumla wake, hasa kwa sekta hii ya uvuvi inaweza kufikiriwa. Iwapo itashindikana na kutokana na jinsi Serikali ilivyo jilabu juu ya jambo hili, itakuwa ni aibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha ajabu na ambacho kimekuwa kikiwavunja moyo na kuwakatisha tamaa kabisa wavuvi wa nchi hii hasa wale wavuvi wa eneo la Dar es Salaam (Minazi Mikinda Kigamboni), wavuvi ambao wanawezesha Mkoa wa Dar es Salaam na maeneo mengine kupata kitoweo cha samaki, wapo baadhi ya Watendaji wa Serikali na baadhi ya vyombo vya ulinzi huwasumbua wavuvi hawa na kuwanyanyasa, hata pale ambapo hawajavunja sheria. Baadhi ya vyombo vya ulinzi vinavyowanyanyasa wavuvi hawa ni *Police Marine* pamoja na JWTZ.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. H. K. KAI]

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile vyombo hivi kwa kuendeleza manyanyaso kwa wavuvi hawa, wakati mwininge huwafuata baharini na kuvifungasha vyombo vyao wavuvi hawa pamoja na kuwatishia na kuwapeleka *Police Marine* ambako wanapaki vyombo vyao. Ili wawaachie wavuvi hawa, ni hadi pale wavuvi hawa watakapotengeneza mazingira ya rushwa ndipo wanawaachia. Hii ni aibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, mwaka 2012 hadi kufikia mwezi wa sita (Juni, 2013), Serikali hajatoa leseni kwa wavuvi wa eneo la Dar es Salaam lakini *Police Marine* wanawalazimisha wavuvi kutoa leseni na hata pale wanaposema hatuna sababu kila tunapofuata kwenye ofisi husika tunaambiya leseni bado au vitabu vyao leseni hatujaletewa; wakati huohuo Watendaji wa Serikali ambao ni Maafisa wa *Fisheries* wanafahamu wanachoongea wavuvi na wanajua ni kweli leseni hazijatoka, unadhani ni nini maana yake? Ndiyo maana nikasema kwamba baadhi wanashirikiana na vyombo vyao ulinzi nilivyovitaja kuwatesa wavuvi na kuwanyanyasa. Vipi tutafanikiwa kwenye mpango huu wa Maendeleo wa Taifa? Hii ni aibu.

Mimi binafsi sifirkiri hata kidogo kwa kweli kama tutafikia kwenye Mpango huu mwema wa maendeleo ya Taifa, kama wapo Watendaji wa Serikali ambao hawana nia njema na mpango huu wa Taifa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ardhi, mara nyingi na kwa muda mrefu nchi yetu kumekuwa kukijitokeza matatizo na mizozo ya ardhi, jambo ambalo baadhi ya maeneo ya nchi yetu wananchi wamekuwa wakilalamikia maeneo hasa yale ambayo kuna wawekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kwanza kabisa napenda ku-*declare interest*, ni Mjumbe wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira. Kamati yetu hii tulifanya ziara ya kikazi katika Jimbo la Mufindi (la Mheshimiwa Kigola) ambako yupo mwekezaji anayemiliki Kiwanda cha Kutengeneza Karatasi (*Mufindi Paper Mill*). Kiwanda hiki kwa muda mrefu kina mizozo

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. H. K. KAI]

na waliokuwa wafanyakazi wa kiwanda hiki kabla hakijauzwa kwa mmiliki wa kiwanda hiki, kutokana na madai ya malipo yao na vilevile kwenye kiwanda hiki yapo malalamiko ya baadhi ya vijiji katika eneo hili wakidai kuporwa maeneo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Kamati yetu kupata nafasi ya kutembelea kiwanda hiki na kufanya mazungumzo na uongozi wa *Mufindi Paper Mill* na vilevile kukutana na wanakijiji cha Isaula ambao wanalalamikia eneo lao kuporwa na *Mufindi Paper Mill*; Kamati tulichobaini hatukuona matatizo ya ardhi, isipokuwa Kamati tulichokiona ni Sitofahamu. Kwa bahati mbaya sana Kamati ilichobaini ni mizozo, matatizo pamoja na sitofahamu. Yote hayo yanasaababishwa na Serikali inayoongozwa na CCM. Hii ni aibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa nini niseme Serikali hii inayoongozwa na CCM na inayojiita sikivu ndiyo inayosababisha? Kwa mfano, kutokana na madai ya waliokuwa wafanyakazi wa kiwanda hiki kabla ya kumilikiwa na *Mufindi Paper Mill*, Serikali na mmiliki wa *MPM* kwa mara ya kwanza walikaa pamoja kujadili juu ya tatizo hili na mmiliki wa *MPM* alikubali kutoa kiasi cha shilingi bilioni moja (1) kati ya shilingi bilioni tatu (3) wanazodai watu hao na zinazobakia ilipe Serikali, bahati mbaya Serikali ilishindwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, mmiliki wa Kiwanda cha *MPM* kwa sababu anataka mzozo huu umalizike, mara ya pili walipokutana tena na Serikali kuzungumzia jambo hili, mmiliki huyo alikubali fedha zote ambazo ni malipo ya wafanyakazi hao wa kiwanda hicho kabla hajamiliki yeye, fedha ambazo ni shilingi bilioni tatu (3) kuzilipa; isipokuwa tu alichohitaji ni *guarantee* ya Serikali vipi itamlipa fedha hizo lakini hadi sasa Serikali hii inayojiita sikivu imeshindwa. Hii ni fedheha na aibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu wanakijiji cha Isaula baada ya kuwasikiliza, walichotuambia wao hawana matatizo na mwekezaji kwa sababu walipokutana wao, wanakijiji na mwekezaji huyo kuzungumzia kuhusu eneo lao

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. H. K. KAI]

ambalo mwekezaji alipanda miti, mwekezaji alikubali kwamba alikosea na eneo hilo akawaachia wanakijiji. Isipokuwa wanakijiji hao tatizo wallilotulalamikia ni kwamba baada ya mwekelezaji kupanda miti katika eneo lao hilo, walilalamika Wizarani na Waziri alipeleka wataalam lakini hadi leo hawajapata mrejesho wa Serikali ama Wizara husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, rai yangu kutokana na mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa ili uweze kufanikiwa, ni vizuri sasa Serikali hii ihakikishe kila penye migogoro ya ardhi isimamie na kuimaliza kabisa na pale ambapo Serikali imewaaahidi wananchi, itekeleze ahadi hiyo.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2014/2015 yametaja miradi mbalimbali ya kitaifa. Kati ya miradi hiyo, uko pia Mpango Maalum wa Maji katika Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa uamuzi wa Baraza la Mawaziri wa mwaka 2011, Mpango huo utekelezaji wake ilikuwa mwaka 2013. Hata hivyo, kutokana na udhaifu katika utengaji wa rasilimali na kukosa uharaka wa utekelezaji hata kwa fedha ambazo zimetengwa, maamuzi hayo ya Baraza la Mawaziri hayatakuwa yametekelvezwa na kukamilika mwaka 2013. Aidha, Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano uliopitishwa Juni, 2011, sehemu kubwa ya miradi ilipaswa iwe imekamilika 2013/2014 na mingine imalizike 2014/15.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, Mpango tunaojadili sasa ufanyiwe marekebisho kwa kurejea Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano na michango yangu Bungeni 2011/2012 na 2013 na Hoja Binafsi niliyowasilisha tarehe 4 Februari, 2013. Aidha, Serikali itoe majibu iwapo kauli iliyonukuliwa kwenye vyombo vya habari tarehe 2 na 3 Novemba, 2013 na Waziri wa Maji, Mheshimiwa Prof. Jumanne Maghembe kuwa miradi ya Dar es Salaam itakamilika 2017, ndio ratiba mpya ya utekelezaji? Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Mahusiano na Uratibu). Mheshimiwa Stephen Wasira

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. J. J. MNYIKA]

atumie majumuisho kueleza ni lini hasa Mkutano na Rais juu ya Maji Dar es Salaam, kwa kuzingatia ahadi yake katika Mkutano wa Bunge la Bajeti kuwa "nikae mkao wa kula".

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Bunge hili kutambulisha wanamichezo mara kwa mara, michezo na burudani ni sekta ambayo haijapewa kipaumbele katika Mpango wa Miaka Mitano na hata katika Mpango wa mwaka tunaoendelea kuujadili. Hivyo, marekebisho yafanyike kwa kurejea Sera ya Michezo na Sera ya Utamaduni nchini na mipango mbalimbali na kuingiza michezo katika Mpango wa mwaka 2014/2015. Vipaumbele vya kuingizwa ni pamoja na kukuza vipaji na michezo kwa Serikali kushirikiana na Vyama vya Michezo vyote na Vyama vya Wasanii katika kutekeleza program za michezo na sanaa shulenii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Serikali iongeze nguvu katika kuwezesha ujenzi wa miundombinu ya michezo na burudani. Aidha, Serikali inayoongozwa na CCM irejeshe viwanja vilivyoohodhiwa na CCM ili vitumike kwa ufanisi kwenye maendeleo ya michezo na burudani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ya kitaifa ya sekta ya nishati. Ipo miradi ya umeme na ya gesi asili kati ya vipaumbele. Nishati ni chanzo cha ongezeko la gharama za maisha na athari kwa uchumi wa nchi. Hivyo, Serikali itoe majibu, sababu za Wizara ya Nishati kueleza inakusudia tena kupandisha bei ya umeme ikiwa ni siku chache baada ya Waziri wa Fedha kukutana na IMF na Benki ya Dunia (WB) Marekani Oktoba 2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ni kwa nini Serikali inafanya nyaraka za mikataba na ripoti za uendelezaji wa miradi ya gesi vinakuwa siri hata baada ya mimi kama Mbunge kuomba kwa Sheria ya Kinga, Haki na Madaraka ya Bunge?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya uchumi wa nchi hajjaweza kuongeza ajira rasmi na kuweka mazingira ya

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. J. J. MNYIKA]

kuwezesha ajira zisizo rasmi na hivyo kushindwa kuwezesha ufumbuzi wa matatizo ya ukosefu wa ajira, hususan kwa vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iwasilishe Bungeni Utafiti wa Ajira na Mapato (*Employment And Earnings Survey*) ya mwaka 2011 na kuharakisha kufanya tathmini ya nguvukazi (*labour force survey*) ili mipango na bajeti izingatie hali halisi. Novemba Mosi ni Siku ya Vijana Afrika, hivyo ni wakati muafaka Serikali kupokea mchango wa kuzingatia Mkataba wa Vijana wa Afrika ambao nchi yetu imeridhia, sasa uwekwe katika vipaumbele vyta Mipango ya Maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo ya Mpango, kipengele cha 2.3.11, juu ya kazi na ajira, kinaonesha kasi ya utekelezaji ni mdogo. Katika kifungu cha 3.3.14 kimesema kwamba katika mwaka 2014/2015 kutatekelezwa programu ya kukuza ajira kwa vijana. Hata hivyo, Serikali ikumbuke kwamba toka mwaka 1993/1994 palianzishwa Mifuko ya Maendeleo ya Vijana. Hata hivyo, pamekuwepo na udhaifu na ujisadi katika Mifuko hiyo na pia kiwango cha fedha kinachotengwa kimekuwa kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nyongeza kidogo ya mwaka wa fedha 2012//2013 ya shilingi bilioni 6.1 ni ndogo ukilinganisha na mahitaji ya mikopo na mitaji kwa vijana. Hivyo, kama ilivyofanywa kwa sehemu ya fedha za marejesho ya malipo ya Akaunti ya Madeni ya Nje (*EPA*), shilingi bilioni 40 kwenye Benki ya Rasilimali (*TIB*), Serikali ifuatilie zaidi ya trillioni moja zilizotolewa na kudhaminiwa wakati wa kunusuru uchumi (*stimulus package*) zielekezwe kwenye Mifuko ya Vijana na Wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Mwanasheria Mkuu wa Serikali atengue barua yake ya tarehe 16 Aprili, 2013 yenye Kumb. Na. AG CC/N.10/1 ili kuwezesha Muswada Binafsi wa Baraza la Vijana la Taifa uchapwe kwenye Gazeti la Serikali kwa kuwa utawezesha kuanzishwa Mfuko wa Maendeleo ya Vijana wenye usimamizi thabitii. Mwanasheria Mkuu azingatia kwamba Muswada niliowasilisha nilizingatia Ibara ya 135(2)

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. J. J. MNYIKA]

ya Katiba ya Nchi na hivyo haufungwi na mashafrti ya Ibara ya 99 ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, Serikali iwasilishe Bungeni taarifa ya utekelezaji wa wa Sheria ya Kuhamasisha Ajira ya mwaka 2004, ambayo imeielekeza Kamati za kuchochaea kazi na ajira kuundwa katika ngazi zote tano za utawala kuanzia kwenye Mitaa/Vijiji mpaka katika Serikali Kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, iwapo Serikali haitatoa majibu thabiti juu ya mchango wa Mpango wa Maendeleo kwenye maendeleo ya wanawake na vijana, ziada ya mapendekezo yaliyotajwa kwenye sheria kwa sasa ambayo haikidhi mahitaji, nitawasilisha Hoja Binafsi kwenye Mkutano huu wa Bunge kuhusu suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya uchumi wa nchi yetu hailingani na matarajio ambayo Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano uliweka, ambayo mapendekezo ya awamu tatu zilizotangulia kuanzia 2011 zilipaswa ziwe zimeyatimiza mwaka 2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2014/2015 ujikite katika kurekebisha kasoro ya ukuaji wa uchumi wa nchi, kuelezwu kuwa unakua huku uchumi wa wananchi ukishuka na kuongezeka kwa umaskini wa kipato. Pamoja na mfumuko na bei kushuka na kuwa tarakimu moja, bei za bidhaa na huduma hazijashuka. Hivyo, Serikali ielete ni kwa vipi Mpango huo utawezesha bei ya bidhaa kushuka kwa kuongeza uzalishaji na kurekebisha kasoro kupitia bajeti katika maeneo ambayo Sheria za Fedha 2011, 2012 na 2013 zimechangia ongezeko la bei?

Mheshimiwa Mwenyekiti, udhaifu wa miundombinu ya Jiji la Dar es Salaam iwe ni ya usafiri na usafirishaji, nishati, TEHAMA, maji safi na majitaka; ingekuwa na mchango mkubwa wa kupungua kero kwa wananchi asilimia 10% ya nchi na pia ingewezesha ongezeko la mapato kwa Taifa na hivyo kutoa mchango kwa maeneo mengine ya nchi. Kiwango cha fedha kilichotengwa, kilichotolewa na

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. J. J. MNYIKA]

kilichotumika kwenye utekelezaji wa miradi ya Kitaifa ya Jiji la Dar es Salaam kuanzia 2011 mpaka 2013 ni pungufu sana ya Jedwali la Mpango wa Miaka Mitano katika sekta husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, katika Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2014/2015 na bajeti ya mwaka tajwa - Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango, Wizara ya Maji na Wizara ya Fedha; irejee kipengele cha A.1.1.4 na kutenga fedha kamili kwenye miradi ya maji safi na maji taka kuziba pengo la upungufu wa miaka iliyotangulia na kuonesha kwa vitendo hatua za haraka za kuboresha upatikanaji wa miradi kwa kugawa kandarasi vipande kwa Wakandarasi tofauti kama inavyofanyika kwa barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, ili kupunguza msongamano kwa haraka pamoja na mradi wa Mabasi ya Haraka unaoendelea (*DART*), narudia kusisitiza kama iliyokuwa kwa mwaka 2011, 2012 na 2013 wakati wa michango yangujuu ya mipango na bajeti; Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango, Wizara ya Fedha na Wizara Ujenzi – zirejee kifungu cha A.1.2.1 na kutenga fedha za barabara za pembezoni za mchujo na barabara za mzunguko (*ring roads*). Kiasi kinachohitajika kwa kazi hii ni wastani wa fedha zisizopungua bilioni 100. Mpaka sasa kwa miaka mitatu, kiasi kilichotengwa kwa barabara hizo zilizotajwa kwa majina katika Jiji la Dar es Salaam hakijafikia hata robo (25%), na kiasi halisi kilichotolewa ni kidogo zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuongeza vyanzo vyaa mapato ya kutekeleza miradi, Serikali ipunguze misamaha ya kodi, ipunguze matumizi ya Serikali hasa katika ununuzi ambapo ghamama ambazo Serikali inanunua bidhaa na huduma ni 2% - 10% ya bei ya kawaida ya soko. Asilimia 40% ya ununuzi wa umma umekaliwa na ujisadi au ununuzi usio na thamani halisi (*value for money*) na hivyo kukwamisha miradi ya maendeleo. Ili kuongeza ufanisi wa ufuatilaji na tathmini, Serikali iwasilishe Bungeni mikataba yote ambayo Mawaziri waliingia kupitia Mpango wa Matokeo ya Haraka (*BRN*).

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuipongeza Serikali juu ya Mpango ulio mzuri, ingawa una changamoto kubwa na fedha ya kutosha kuweza kutekeleza miradi na mipango tuliyo nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naamini kuwa nchi hii ni tajiri sana na fedha haipaswi kuwa ni tatizo. Tunalo tatizo kubwa la kuweka vipaumbele vyetu, tunalo tatizo la *networking*, tunalo tatizo la ubinafsi, tatizo la kuwa ndani ya ‘box’ kwa kuamini kwamba maeneo fulani tu ya nchi ndiyo pengine yenye haki zaidi kuliko mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano, mradi wa mkaa/umeme Ngaka. Mradi huu ulianzishwa kwa nia ya kuchimba makaa ya mawe ili kufua umeme wa MW. 400. Uchimbaji wa makaa ya mawe unaendelea lakini uwekaji wa mitambo ya kufua umeme umekwama kwa miaka minne (4) sasa kwa kitu kinachoitwa majadiliano kati ya ZAWCOM na TANESCO bado hayajakamilika. Wakati huohuo nchi ina upungufu mkubwa wa umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, TANESCO inatumia Sh. 4.5 billion kwa siku ili kuzalisha umeme, US cts 45 – 50 badala ya US cts 7 – 10. Hizo fedha za siku moja zingeweza kabisa kuifanya TANESCO ijenge *power station* pale Ntunduwaro Mbinga na kupata umeme wa nafuu. Kwa nini Tume ya Mipango na Wizara ya Fedha hailioni hilo? Kwa nini mradi huu wa kimkakati haupewi fedha na Serikali na ushiriki wa Serikali ni mdogo mno. Kwa hiyo, fedha zipo, swali ni kwamba tunazitumia wapi? Wananchi wakilalamika, Serikali inatumia nguvu kubwa kuwanyamazisha. Hivi Serikali haina njia nzuri ya kuongea na wananchi wa Ntunduwaro kama inavyoongea kwa ustaarabu na wawekezaji Wazungu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, miundombinu, licha ya mradi mkubwa wa makaa ya mawe, Ruvuma ni Mkoa unaozalisha chakula kwa wingi. Usafirishaji wa makaa ya mawe unafanya kwa malori na chakula vivyo hivyo. Barabara hizi ni za vumbi, hivyo kuleta madhara makubwa. Suluhisho (*short term*) ni kuweka lami barabara ya Kitai –

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. G. C. KAYOMBO]

Ruanda – Lituhi. *Midterm* ni kujenga reli toka Mtwara – Songea – Mbinga – Mbamba Bay pamoja na tawi toka pale Kitai kwenda Ruanda (Ntunduwaro) Lituhi ili kubebe makaa ya mawe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni yangu ni kwamba nchi yetu ina madini mengi ya aina mbalimbali. Serikali iwe na mpango madhubuti wa namna ya kuvuna madini yetu kwa faida ya Watanzania hasa wachimbaji wadogo wadogo, kama wachimbaji wa *Saphire* katika Wilaya ya Mbinga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bei ya mazao ya Kilimo. Serikali iharakishe programu ya kuhakikisha wakulima wa mazao ya biashara kama kahawa, pamba na korosho wanafaidika pale bei za mazao hayo zinapoporomoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *CARMATEC* imefanya kazi nzuri ya kubuni na kutengeneza trekta. Sasa Serikali iiwezeshe kuzalisha matrekta hayo. Halmashauri za Wilaya zinaweza kuhusishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. HAMAD ALI HAMAD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kitabu cha Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa (uk. 2) (kif. 1.2) aya ya 2, inasema na imeonesha kukua kwa pato la kila mtu kwa mwaka 2012. Kwa maeleo hayo, pato hili lilikuwa wastani wa 2847. Hata hivyo, shabaha ya Mpango (uk.11)(a), kuongeza pato hadi asilimia 7.1 ambapo pia Mtanzania atakuwa anapata pato chini ya Shs. 4000. Hii ni kuwakebehi wananchi. Kama bado shabaha ya mpango ni kuendelea na kupata mlo mmoja usiokamilika, hapa hatuwezi kuwa na maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ni ya wakulima, wafugaji, wavuvi na wafanyakazi. Kwa muda mrefu sasa, Serikali imekuwa ikilizungumzia tatizo la wakulima na wafugaji bila kulipatia ufumbuzi wa kudumu tatizo hili na hali inaashiria matatizo endelevu baina ya wakulima na wafugaji. Wavuvi

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. H. A. HAMAD]

wanapata shida kubwa toka Serikalini kwa kushurutishwa vifaa vyta kisasa ambapo Serikali haijioni kuwa ina wajibu wa lazima wa kuwawezesha wavuvi hao.

Pia Serikali inalalamika kuwa samaki wanaibiwa lakini hadi leo haina mpango wowote wa kuwa na meli zake za kuvulia samaki hao kwa maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, linaloonekana kwa Serikali ni kuwaonea wananchi ambao wameshindwa kuwatengenezea mazingira mazuri ya kuweza kujiedeleza na kukuza vipato vyao. Jambo hilo la Serikali kushindwa kuwa na mpango madhubuti wa kufanya makundi haya kufanya harakati zao kwa amani na wao hawataweza pia kuunga mkono Mpango wa Serikali wa Maendeleo, wakijua kwamba Serikali hiyo hiyo ndiyo inayoua kwa risasi mifugo yao lakini pia ndio wanaochoma moto nyavu za wavuvi bila utaratibu mbadala wa Serikali kwa makundi haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Serikali inaonekana kushindwa kufikiria njia mbadala ya kuwawezesha makundi haya kuweza kujiedeleza, Serikali sasa inatumia nguvu isiyo ya kawaida kujihami kwa kuwanyanyasa wananchi, kuua mifugo yao na kadhalika badala ya kuwa na mipango mizuri itakayowasaidia watu wetu. Hatuwezi kufikia maendeleo tunayoyataka, maana tunasema tu bila kuwa na utekelezaji wa tunayopanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya uchafuzi wa mazingira, Serikali itilie maanani na ichukue hatua ya dhati ya kuhakikisha kwamba nishati mbadala ya gesi inawafikia wananchi katika maeneo yao mbalimbali na kwa bei nafuu ili kuondoa au kupunguza wimbi lililopo la ukataji miti kwa ajili ya mkaa wa kupikia. Jambo hili litasaidia kupunguza uchafuzi wa mazingira utokanao na ukataji wa miti na uchomaji wa mkaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.  
Ahsante.

**MHE. SHAFFIN A. SUMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Kwanza, naipongeza Serikali kwa kazi nzuri na mpango mzuri iliyouleta Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha muhimu hapa ni kuhakikisha kwamba maelezo yote yanatekelezwa. Hata hivyo, kutokana na mfumo wa *cash budget*, ratiba ya mipango haiendi sawia na kalenda. Ni bora Serikali ikaona uwezekano wa kupata mkopo wa muda mfupi wakati tukisubiri *TRA* ikikusanya mapato. Pia *TRA* inatakiwa ijipange vizuri zaidi kukusanya mapato kwa sababu ni wafanyabiashara 1.7 milioni tu wanaolipa kodi Tanzania, jambo ambalo linahitaji kufanyiwa kazi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna makampuni mengi Dar es Salaam ambayo hayalipi kodi ipasavyo na chanzo cha tatizo hilli ni kupidisha bidhaa nyingi bandarini bila kulipiwa ushuru. Bado mtandao wa walaji upo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali pia isiachie miradi ya maendeleo iliyopo. Kwa mfano, zao la tumbaku linaingiza pato kubwa katika Taifa letu. Hata hivyo, wakulima walio wengi Mkoani Tabora bado wanatumia jembe la mkono ila wanazalisha sana tumbaku. Kwa sasa wananchi hao wanahitaji msaada na msukumo mkubwa kwa sababu fedha walizokuwa wanadai kupitia Chama cha Msingi, hazipo na tena zimeshaibiwa. Naishauri Serikali ili Isipoteze mapato makubwa, ione namna ya kuwalipa fedha zao ili zao la tumbaku lisidorore.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iharakishe mchakato wa kufufua reli ya kati ili kupunguza mfumuko wa bei wa kila mara, ambao unatokana na bei ya mafuta kupanda kila mara. Hata hivyo, tumbaku yote inayozalishwa Tabora inaweza kusafirishwa na reli kupelekwa Morogoro, soko la usafirishaji lipo, ni Serikali tu yenyewe inajichelewesha lakini pia reli ya kati ni tegemeo kubwa kwa nchi za jirani. Soko lipo, sisi wenyewe tu hatulioni.

Mheshimiwa Spika, bandari ya Tanga ina umuhimu

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. S. A. SUMAR]

wa kipekee. Tunaweza kutumia bandari zetu kutuliza mbio za wenzetu wa Kenya. Leo wao wanajivunia bandari ya Mombasa na wanajua kabisa kuwa pamoja na kwamba sisi Tanzania tuna fursa nzuri zaidi kuliko Kenya lakini tumelala sana. Muda umefika, tuamke sasa tutekeleze yale yote tunayoyapanga. Ahsante.

**MHE. DKT. DAVID M. MALLOLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kupata nafasi hii ili nami nitoe mchango wangu wa maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo cha umwagiliaji. Enzi za Ukoloni, mabwawa mengi sana yalichimbwa hapa Dodoma Mjini. Mabwawa haya sasa yamejaa tope na kukosa uwezo wa kutunza maji mwaka mzima. Serikali ielekeze nguvu zake katika kuchimba tope za mabwawa haya, hasa yale ya Hombolo, Vikonde, Makutupora, Mbalawala na Mkalama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji haya yatasaidia sana kilimo cha umwagiliaji wa mboga-mboga kwa matumizi ya idadi kubwa ya wananchi na wanafunzi wa Vyuo Vikuu vya Dodoma (itachukua wanafunzi 40,000) na Vyuo vya St. John, CBE, Chuo cha Mipango, Chuo cha Hombolo na kadhalika. Maji haya pia yatasaidia kunyweshea mifugo yetu na umwagiliaji wa mashamba makubwa ya zabibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda (Kiwanda cha Zabibu). Dodoma Mjini inahitaji kiwanda kikubwa cha zabibu. Wananchi wamekata tamaa na kilimo cha zabibu. Hakuna soko na hakuna kiwanda cha zabibu. Ni wakati muafaka sasa Serikali itamke kama wananchi waendelee na kilimo cha zabibu au kama waache kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zao la zabibu ndiyo ukombozi pekee wa kiuchumi wa watu wa Dodoma. Kwa vile zao hilo linakubaliana na hali ya hewa na uhaba mkubwa wa mvua ambao husababisha njaa kila mwaka hapa Dodoma. Wananchi wakiuza zabibu, wanapata hela, watanunua chakula, watajenga nyumba bora,

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. DKT. D. M. MALLOLE]

watasomesha watoto na kufanya mambo mengi ya kimaendeleo. Tunaomba jibu la soko na kiwanda kikubwa cha zabibu kwa ajili ya wakulima wa zabibu Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa miaka iliyotangulia na huu wa sasa, ni mizuri sana. Sina wasiwasi kwa Mpango huu wa 2014/2015. Tatizo ni utekelezaji. Kuna mambo ambayo yanaleta utata kwa wananchi kuhusu uchumi wa Taifa:-

(a) Kukua kwa pato la Taifa, kwani hawaoni tofauti na miaka iliyopita.

(b) Mfumuko wa bei za bidhaa na huduma ya jamii, inawanyima wananchi kuona unafuu wa kupungua au kushuka kwa mfumuko wa bei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Longido ni Wilaya ya wafugaji kwa asilimia 95%. Uchumi wao waliopewa na Mwenyezi Mungu ni mifugo, wanyamapori na magadi kwenye Ziwa Natron. Katika mambo haya mataku, hakuna mikakati iliyowekwa au mpango mzuri ili wananchi na Taifa zima wafaidike. Napenda kuikumbusha na kueleza Serikali kuhusu uchumi ambao tunao, lakini wanaofaidika ni Wakenya tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, mifugo (ng'ombe) wote wa Wilaya ya Longido na Ngorongoro wanauzwa Kenya kwa sababu huko ndiko kuna Kiwanda cha Nyama (KMC) ambapo wanachinja ng'ombe 500 kwa siku (asilimia 60 ni ng'ombe wa Tanzania). Kenya hawawezi kujitosheleza, wakikosa mifugo wa Tanzania watafunga kiwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, hakuna utaratibu wa Tanzania kupata ushuru wa mifugo wanaokwenda kuuzwa Kenya, wanapitishwa njia za panya. Nilitegemea Kiwanda cha Nyama kingejengwa Arusha ili Watanzania wapate soko

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. M. L. LAIZER]

Ia mifugo na Serikali kupata mapato ya mifugo wengi wanaouzwa Kenya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutowekwa Kiwanda cha Magadi kwenye Mpango. Kwa masikitiko makubwa, nashangaa kutowekwa Kiwanda cha Magado Soda ya Lake Natron Soda Ash kwenye Mpango. Rais, Mheshimiwa Jakaya M. Kikwete alipofungua Bunge hili mwaka 2010, alisema ni lazima kijengwe kiwanda hicho. Tena alipofanya ziara Wilayani Longido, aliwaambia wananchi kwamba hatatoka madarakani kabla ya kiwanda hicho kuanza. Hii ni ahadi ya Rais mwenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa kuna vita ya kiuchumi kati ya Kenya na Tanzania. Wakenya wanadai ujenzi wa Kiwanda cha Magadi – umbali wa kilomita 30 kutoka Ziwa Natron utaharibu mazingira ya Ziwa hilo na mazalia ya Flamingo wakati wao wamejenga cha mita 300 tu kutoka Lake Magadi. Wanaendelea na uzalishaji, hao Flamingo wanaingia mpaka kiwandani. Baraza la Madiwani wametembelea Kiwanda cha Magadi Soda Kenya, wakawakuta hao ndege ndani ya kiwanda. Wakenya wanapinga kiwanda kwa vile magadi kwetu ni mengi, wala siyo ya kuchoronga kama walivyochoronga huko Engaruka; ni ya kukusanya tena kwa wingi sana. Eneo la mazalia ya Flamingo ni kilomita 50 toka eneo la kiwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakenya wanapinga barabara ya Arusha – Loliondo – Mugumu kwa sababu watalii watafika Mbuga za Serengeti na Ngorongoro bila kutumia ndege. Barabara itarahisisha usafiri bila kutumia gharama kubwa. Wakenya wanapinga ujenzi wa Kiwanja cha Ndege Serengeti – umbali wa kilomia 20 toka Serengeti. Mbuga ya North Mara, barabara ya lami inafika kwenye mbuga. Kwa nini iwe nongwa ikifika Mugumu au Loliondo, ambapo siyo ndani ya Mbuga?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mgawanyo wa keki ya Taifa. Kwa hili, baadhi ya maeneo wanakosa pesa za miradi hasa Wilaya ya Longido. Kila bajeti wanayopanga

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. M. L. LAIZER]

hawapati fedha, hawajawahi kupata zaidi ya asilimia 27%. Matatizo ni mengi, hata kwenye Mipango ya mwaka huu 2014/2015, hatutegemei chochote. Naomba ujenzi wa Kiwanda cha Magadi Soda – Lake Natron uwekwe kwenye Mipango ya mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Mnada mkubwa wa Mifugo ujengwe pamoja na Kiwanda cha Nyama Arusha. Tanzania waweke utaratibu mzuri unaoeleweka wa kupeleka mifugo Kenya na kulipa ushuru Tanzania, kuliko kwenda kulipa Kenya tu. Nategemea kama mtaangalia ukweli bila upendeleo, mtakubaliana na mchango wangu. Tatizo la wapangaji ni upendeleo, hili ndiyo tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, Mungu awabariki sana.

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hali na mwenendo wa uchumi wa dunia ni kweli siyo wa kuridhisha kutokana na sababu mbalimbali pamoja na mabadiliko ya tabianchi. Hata hivyo, ukiangalia rasilimali zilizopo Tanzania pamoja na vivutio vya kitalii tulivyo navyo, ni dhahiri kwamba bado Tanzania inayo fursa kubwa zaidi ya kukuza uchumi wake. Kasi ya ukuaji wa uchumi wa Tanzania haiendani kabisa na hali ya kipato cha mwananchi na rasilimali tulizo nazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali ama kwa kutumia wataalam wake wa ndani au hata wa kutoka nje (*consultants*) kukaa na kuangalia upya mifumo na mipango yetu ya kiuchumi (*environmental reform*), pia kuangalia upya baadhi ya sera zetu. Ni imani yangu kwamba majawabu yake yanaweza kutuondoa hapa tulipo na kupiga hatua nyiningine mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuangalia mifumo yetu, hivyo ni vyema kupata mrejesho wa tathmini ya kina kuhusu mradi wa "Kilimo Kwanza" kwani ni jambo la kushangaza kuona kwamba Kilimo kinachangia asilimia 1.4% ya pato la Taifa, ilhali eneo letu la kilimo ni kubwa. Maeneo

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. R. M. MOHAMMED]

kwa ajili ya upatikanaji wa maji ya umwagiliaji yapo, maziwa makubwa yametuzunguka na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado Serikali hajachukua dhamira ya dhati katika eneo la Uvuvi. Katika taarifa ya Serikali hakuna sehemu ambayo Serikali imeonesha imejipangaje sasa katika bahari na maziwa tuliyonayo kukuza uvuvi na namna ya kuboresha wananchi wake wa Kanda ya Ziwa, *Lake Tanganyika*, *Lake Nyasa* na wa Ukanda wa Pwani watakavyoweza kuwasaidia ili kuwa na uvuvi wa kisasa wenye tija zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni aibu iliyo wazi kwamba hivi sasa uvuvi unachangia asilimia 2% tu katika pato la Taifa ilhali uvuvi pekee iwapo utaendelezwa, unaweza kuchangia asillmia 3% ya pato la Taifa. Naishauri Serikali kuandaa mazingira endelevu na yaliyo wezeshi ili sasa ijikite katika uvuvi wa bahari kuu. Sambamba na hilo, kuimarisha ulinzi katika eneo hilo ili kuzuia meli zilizo nyingi kutoka nje ya nchi yetu kutokuendelea kuiba rasilimali ya samaki tuliyonayo katika bahari kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala la makusanyo ya kodi, bado mianya ya ukwepaji kodi hajapatiwa udhibiti ulio bora. Pamoja na hilo bado katika ngazi ya Halmashauri, utaalam na ubunifu wa kuibua vyanzo vya mapato ni mdogo. Pia hakuna udhibiti mzuri wa ukusanyaji wa mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeshauri Serikali kuiboresha Tume ya Mipango kirasilimali ili watu wawewe kushuka katika ngazi ya Halmashauri ili kuzisaidia badala ya wao kubaki ofisini na kutia miongozo tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, ni vyema sasa Serikali ikasitisha uanzishaji wa Halmashauri mpya nchini ili kwanza ikae ifanye *evaluation*. Ni dhahiri miradi mingi ya Serikali iko katika mamlaka za Serikali za Mitaa, lakini tija yake imekuwa ni dhaifu sana.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. R. M. MOHAMMED]

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwezo wa Halmashauri zetu kuijendesha hivi sasa kwa kutumia mapato yao ya ndani hayazidi asilimia kumi. *Average* hii si hali nzuri hata kidogo. Ni vyema Serikali kupeleka nguvu za kitaalam kwenye Halmashauri zetu katika kusimamia mapato na miradi ya maendeleo ili ilete tija. Hivi sasa Halmashauri zimejaa madeni na zipo kwa ajili ya kusubiri ruzuku kutoka Serikali Kuu tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. SYLVESTER MASSELE MABUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango huu wa Maendeleo wa Taifa ni sehemu ya utekelezaji wa Dira ya Taifa ya mwaka 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kuna nia safi ya kutaka kufikia malengo ya Dira ya Taifa, ni wakati muafaka sasa tuviangalie upya vipaumbele vyetu kwani si kila tulichokianisha kwenye mpango ni kipaumbele. Nijuavyo mimi, kipaumbele ni kitu ambacho kikitekelezwa kitachangia kukua kwa sekta zingine pia kwa wakati badala ya kutekelezwa kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba ya Mheshimiwa Waziri imeonesha vipaumbele vya miundombinu ya reli, barabara, umeme, maji; vilevile sekta za kilimo, afya, elimu, madini, bandari na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo yaliyoordheshwa hapo juu yanahitaji kuangaliwa upya. Mfano, kati ya reli na barabara, kipi kiwe kipaumbele cha kwanza. Reli ni muhimu kwa usafiri wa uhakika ambaao pia utaziwezesha barabara zetu kupata *relief* ya mzigoo mkubwa unaosafirishwa na ambaao huziharibu barabara zetu mara kwa mara. Mapato yatokanayo na usafirishaji wa mzigoo, yataongezeka na ajira nydingi zitapatikana.

Mpango unapaswa kuonesha namna tutakavyokabiliana na *Traffic Jam* katika miji mikubwa hapa nchini. *Traffic Jam* imepunguza *efficiency* na *productivity*. Hali hii inaathiri sana uzalishaji na ukuaaji wa uchumi.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. S. M. MABUMBA]

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya umeme ni muhimu sana kwa uchumi wa nchi yetu. Je, Serikali imejipanga vipi katika kuwapatia umeme wananchi walioko mijini na vijiji? Tukifanikiwa kuvitekeleza vipaumbele hivi, hata sekta za elimu, maji na afya zitaweza kuboreshwa. Vinginevyo shule na hospitali zitaendelea kutokuwa na umeme wa uhakika hata maabara hazitafanya kazi. Sekta ya Kilimo bila ya umeme, reli na barabara; haiwezi kukua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali kuviangalia upya vipaumbele vyetu. Naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

**MHE. ZAYNAB M. VULLU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina mpango wa kuanzisha Benki ya Wakulima. Je, Serikali imejipanga vipi katika kuviwezesha vikundi mbalimbali na hata wakulima wadogo wadogo na hasa wa vijiji? Itawafikia vipi?

Wanawake na vijana ni mionganoni kwa wakulima ambao wanahitaji kuwezeshwa. Je, Serikali imejipanga?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vyema mikopo hiyo isiwe na riba kubwa sana.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia kwa kushauri juu ya nini kifanyike ili tuweze kukuza uchumi wa mtu mmoja mmoja (*Individual Economy*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, inashangaza na huwa najiuliza ni nini hasa kazi ya Wizara ya Mipango na Uvuu pamoja na Wizara ya Kilimo? Tumeendelea kushuhudia migogoro mingi kati ya wafugaji na hifadhi, wafugaji na wakulima, wafugaji na watu katika makazi yao. Mgogoro huu kwa kiasi kikubwa wanaathirika wafugaji ambapo hivi karibuni tumeshuhudia *Operation Tokomeza* ambayo kwa hakika ililenga kutokomeza Watanzania maskini huku ikiwaacha walengwa.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. E. N. MATIKO]

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja bila *operation* ya kutokomeza, *operation* ya uwindaji haramu/wawindaji haramu; lakini siyo kuwaonea wananchi na kuwageuza kitega uchumi chao. Mfano, *operation* iliyoanza Mkoani Mara tarehe 14/10/2013 ambapo tumeshuhudia wananchi wakichomewa nyumba pamoja na mali zao zote, wakipigwa na wengine kuuawa. Mfano Mzee Peter Maseya Marwa wa Kijiji cha Mvito aliyechukuliwa nyumbani kwake na siku ya pili yake walimrudisha wakiwa wameshamuua kwa kipigo kichwani. Tumeshuhudia ng'ombe, mbuzi na kondoo wakitokomezwa na hiyo *operation* tokomeza. Kiukweli ni fedheha sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesoma mpango, lakini kwa masikitiko makubwa sijaona mpango madhubuti wa kumwinua mkulima, mfugaji na hata Mtanzania mwingine ambaye si mkulima wala mfugaji. Tumeshuhudia wafugaji wakitozwa jumla ya Sh. 180,000/= kwa ngombe, wasipokuwa nazo zinapigwa risasi na au kupigwa minada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza kwamba Wizara ya Mifugo na Uvuvi ijkite zaidi katika *Livestock Management*, tofauti na sasa ambapo tumejikita hasa katika *Veterinary Issues* tu. Wizara ina wajibu na kutaka kujua kuna mifugo mingapi na iweze kukuza kiwango cha ubora cha mifugo/ufugaji (*quality products*). Ili hii ifanikiwe inabidi Wizara na huu Mpango uzingatie kuwapatia wafugaji maeneo mbadala ya kulishia mifugo yao, (kibidi hata zero grazing). Kutoa elimujuu ya ufugaji bora na siyo bora kufuga, kwamba ili ufugaji uwe na tija (*productivity*) ni lazima tuzingatie *quality* na siyo *quantity*. Tuwe na Maafisa Mifugo ambao watahakikisha tunakuwa na *breedings* zitakazotoa mazao bora, pia Wizara ihakikishe upatikanaji wa maji kwa ajili ya mifugo. Hii itasaidia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wakati sasa Wizara Mama/mtambuka kwa maana ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Kilimo; Ardhi, Nyumba na Makazi pamoja na Wizara ya Maliasili, zikae na kupata/kutafuta ufumbuzi wa jinsi gani tutakuwa na ufugaji wenye tija, kilimo chenye tija, makazi

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. E. N. MATIKO]

bora na hii itatoa fursa ya ukuaji wa uchumi kwa kila Mtanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wakati sasa wa kuwa na mipango madhubuti ambapo kilimo na ufugaji zinatakikana zitegemeane (*compatible*). Mfano wafugaji/mifugo itatoa mbolea na ardhi yenye *tilling* kwa ajili ya wakulima. Wakati huo huo wakulima (*farmers*) watatoa ardhi/malisho kwa ajili ya mifugo yao kwa muda huku wakifuatilia malisho mahali pengine. Hili likitekelezwa vizuri, ardhi kwa ajili ya ufugaji itatuondolea jangwa na kuongeza rutuba kwenye ardhi/udongo; na hivyo kutoa fursa za kiuchumi, vilevile itatoa maendeleo na kuwepo (*coexistence*) ya mifugo, kilimo chenye tija na ulinzi imara wa hifadhi zetu (*wildlife*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, kwa kifupi kabisa napendekeza miundombinu ya reli kutoka Bandari ya Dar es Salaam hadi Chalinze ambapo tutaanisha bandari kavu Chalinze. Hii itasaidia sana kupunguza msongamano wa magari ambaao unazorotesha uchumi wa nchi yetu, kwani muda mwingi unapotea katika foleni, unaweza kukaa zaidi ya masaa matatu (3) au matano (5) toka Dar es Salaam hadi Chalinze. Hii ni sababu ya kuwepo na malori ndani ya Jiji hadi Chalinze. Reli itasaidia sana kutatua hili tatizo sambamba na uboreshaji wa reli ya kati na ile ya kutoka Tanga hadi Musoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tunahitaji mkakati utekelezwe wa kuondoa kero ya maji hasa kwenye Majiji kama Dar es Salaam. Hii ni aibu sana.

**MHE. ROSWEETER F. KASIKILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa afya hii. Nikushukuru na wewe kwa nafasi hii ya kupokea mchango wangu wa maandishi. Pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana hii, Katibu Mkuu na Watendaji wote walioandaa Mpango huu wa 2014/2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kitabu cha Mpango, ukurasa wa 49 – 53 vimeorodheshwa vipaumbele sita

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. R. F. KASIKILA]

ambavyo vina shughuli (*activities/vipengele*) 41 ambavyo utekelezaji wake kwa kufikia viwango vya kuridhisha/kufikia malengo kutahitaji fedha nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuanzia ukurasa 53 – 56 yameorodheshwa maeneo mengine 15 (*refer kitabu*), lakini si kwamba haya maeneo yatacaa *dormant*, nayo pia yatahitaji fedha nyingi tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa uzoefu, mipango imekuwa ikipangwa, lakini utekelezaji wake umekuwa duni; na hii imepelekea kuwa na viporo vingi, lakini yote haya yamekuwa ni kwa sababu ya ufinyu wa bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Matokeo Makubwa Sasa (BRN – *Big Results Now*) ya Mpango huu yanahitaji fedha. Niishukuru Serikali kwa ujenzi wa barabara zinazounganisha mikoa, lakini Bajeti ya barabara inayotengwa kwa Halmashauri kwa ajili ya barabara za vijiji ni chini ya asilimia 10% katika ya asilimia 30% wanazotengewa, lakini hii ni kwa ajili ya ufinyu wa bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ratiba ya Vikao vya Bajeti ilibadilika na kuanza Aprili – Juni ili Wizara, Taasisi, Halmashauri, Manispaa na Majiji yaanze kupewa fedha (mafungu) ili waanze utekelezaji robo ya kwanza ya mwaka husika wa fedha. Lakini hadi sasa (Oktoba) baadhi ya Wizara na Halmashauri hazijapelekewa fedha, ni kwa ufinyu wa bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhaba uliokithiri wa watumishi, wataalam, madawa, vitendanishi, vifaa tiba, lakini na ukamilishaji wa majengo ya Zahanati na Vituo vya Afya ambavyo wananchi kwa nguvu zao wamejitatihidi kujenga, lakini ufinyu wa bajeti husababisha uhaba huo na kutokamiliha majengo hayo ikiwa ni pamoja na nyumba za watumishi wa shule za msingi, maabara za sekondari na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni yangu katika hili na kwa sababu fedha zinakuwa hazitoshii, natoa maoni kuwa

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. R. F. KASIKILA]

vyanzo vipyta kwa mapato vibuniwe vyenye mapato makubwa vikijumlishwa na vyanzo vilivyopo sasa; ukusanyaji wa mapato kwa uaminifu na weledi ufanyike. Kila anayepaswa kulipa kodi na alipe. Kodi ikusanywe kwa ukamilifu na fedha itakayokusanya itumike kwa kadri ya mpango (miradi).

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni wakati muafaka wa Kamati za Kudumu za Bunge (Kamati Mtambuka) wakati ujao wa Vikao vya Kamati vya Maandalizi ya Bunge la Bajeti, Kamati ziombe Wakuu wa Mikoa na Halmashauri katika mipango yao waoneshe majedwali yanayoonesha vyanzo kwa mapato, vya zamani na vipyta; mafanikio na changamoto katika ubunifu wa vyanzo na ukusanyaji mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. NASSIB SULEIMAN OMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naunga mkono Mpango huu wa Maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya uchumi ya nchi yetu imeimarika sana. Kama wanavyosema wataalam kuwa katika kipindi cha miaka kumi uchumi wetu utaushinda uchumi wa Kenya. Kadhalika baada ya ugunduzi wa Gesi, Mafuta na Madini; uchumi wa Tanzania utakaribia uchumi wa nchi za Kiarabu kama Dubai katika kipindi cha miaka 20. Jambo muhimu ni kusimamia mipango yetu ya maendeleo. "Big Results Now" ni jambo muhimu sana kwa nchi yetu. Vipaumbele sita vilivyopendekezwa kama vitasimamiwa vizuri, nchi yetu itapiga hatua kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukuaji wa uchumi hauendani sambamba na kupungua kwa umaskini nchini. Hivyo, ukuaji wa uchumi lazima ulenge vijijini ambako hali za kimaisha za watu wetu ni mbaya. Kilimo ndiyo mwokozi wetu. Pembejeo, viuadudu, mbegu na matrekta lazima vipatikane kwa wakati ili wakulima wetu waweze kuongeza uzalishaji wa mazao ya kilimo.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. N. S. OMAR]

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuwapatia vijana na akinamama mikopo yenye riba na masharti nafuu ili wengi waweze kupata mkopo kwa azma ya kupunguza umaskini.

**MHE. REBECCA M. MNGODO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hali halisi ya maisha ya Watanzania, Mpango wa Maendeleo haujaweza kurahisisha au kusaidia kufanikisha maendeleo katika maeneo yale ambayo yako nyuma kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ingawa mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo yanaonesha kwamba pato la Taifa limekua kwa kiwango cha asilimia 7.0% ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 6.9% mwaka 2012, lakini ukuaji huo hauonekani katika maisha ya Mtanzania wa kawalda. Sekta zilizokuwa na viwango vikubwa vyta ukuaji ni pamoja na usafiri na mawasiliano kwa asilimia 18.4%. Ukuaji huo wa pato katika sekta ya Mawasiliano haumgusi mwananchi na wala haujaweza kumsaidia katika kujikwamua kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba, miundombinu yaweza kuwa kipaumbele katika mpango huu. Lakini tunahitaji nguvu kubwa katika mageuzi ya maendeleo katika uboreshaji wa reli. Reli ni njia pekee ambayo yaweza kurahisisha usafirishaji wa bidhaa mbalimbali za biashara na chakula kwa bei nafuu na ni usafiri wa uhakika katika kurahisisha usafirishaji kutoka nchi moja kwenda nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nguvu kubwa ielekezwe katika kujenga reli imara za kisasa kwa kutumia uwekezaji mkubwa ambao faida zake zitaonekana kwa kipindi kirefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nchi kama yetu ambayo elimu haijapewa kipaumbele kwa miaka mingi, jambo ambalo limepelekea kuzalisha Taifa lisilo na utamaduni wa kufanya kazi kwa bidii, badala yake tumetegemea Mataifa makubwa kwa kuwa omboaomba na kuwakopa kila mara.

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[MHE. R. M. MNGODO]

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza elimu ipewe kipaumbele. Taifa likiwa na wananchi walioelimika katika maeneo mbalimbali, sekta nyingine zitaendelea kwa urahisi kwani tutakuwa na watalaam wetu wenyewe na tutakuwa na watu wenye kujali muda wa kazi na wenye kufanya kazi kwa bidii na hivyo kuwa na ustaarabu wa kulipa kodi kutokana na kuelimika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchumi wetu unaweza kukua, kwa kuwa na watu wenye afya. Suala la afya halijatupiwa macho. Uchumi hujengwa na watu wenye afya nzuri. Wasomi wazuri wenye afya nzuri hujenga uchumi imara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. ANNAMARYSTELLA J. MALLAC:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango huu ni mzuri kama utatekelezwa kama ulivyokusudiwa, lakini napata wasiwasi kwa sababu mipango ni mingi na bado inakwenda taratibu kwa kusuasua. Mfano, Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza na suala la Elimu. Mpango kwa kuusoma tu ni mzuri, kiutekelezaji unaona kwamba:-

(a) Nyumba za Walimu hakuna. Walimu wanaishi katika mazingira magumu;

(b) Watoto wanasona huku wakikaa chini, madawati hayatoshi na miti tunayo;

(c) Walimu hawatoshi; na

(d) Shule za Kata hazina Maabara. Je, tutawapataje Wanasyansi kwa kusoma nadharia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija kwenye Kilimo; tunaelewa wazi Kilimo ni uti wa mgongo na ndiyo ajira kwa Watanzania wengi na tulihamasishwa sana kujikwamua kupitia:-

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. A. J. MALLAC]

- (a) Kilimo cha Kufa na Kupona; na
- (b) Siasa ni Kilimo na sasa Kilimo Kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na wananchi kujituma, Serikali imekuwa ikichelewesha upatikanaji wa pembejeo kuititia Wakala wa Pembejeo. Mbolea inakuja kwa kuchelewa, inakuta mkulima amepanda mazao bila mbolea ya kupandia, vivyo hivyo ya kukuzia. Maafisa Kilimo hawana tabia ya kuwazungukia wakulima kutoa elimu ya namna ya kulima kilimo bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo cha tumbaku; tumbaku ni zao linalochangia kuingiza pato la Taifa. Lakini wakulima hawa wamekuwa wakicheleweshewa pesa za mauzo mpaka misimu miwili mkulima hajalipwa pesa yake. Je, pembejeo anunue na nini? Pia je, hayo ni maisha bora kwa kila Mtanzania?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali kusimamia Vyama vya Ushirika viweze kumjali mkulima na kutoa huduma ya pembejeo kwa wakati, pia kusimamia bei nzuri na masoko kwa mkulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maji; suala la maji katika kuleta uhai na kusukuma maendeleo, ni suala nyeti sana katika Mpango huu. Mpaka sasa tuna miaka mitatu ya Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano ambao utasambaza maji vijijini na kuhakikisha wananchi hawatembe mwendo mrefu kufuata maji, lakini mpaka sasa wananchi wanatembea umbali mrefu sana kutafuta maji na wengine vijijini wanakunywa maji ya madimbwi wakichangia na wanyama. Hii imesababisha ongezeko la maambukizi mapya ya UKIMWI kutokana na wanawake kubakwa wanapofuata maji umbali mrefu. Naomba Serikali itambue hili na kuweka mazingira mazuri ya upatikanaji wa maji ili wanawake wasibakwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Utawala Bora. Utawala bora ni nguzo katika kusimamia maendeleo yenye

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. A. J. MALLAC]

mafanikio. Bila utawala bora, nidhamu ya kazi hakuna na mafanikio ya maendeleo hayapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utawala tulionao ni wa kutumia nguvu na usiozingatia haki za binadamu wala heshima ya mtu. Wananchi sasa hivi wanaishi maisha ya wasiwasi, woga na hofu. Viongozi hawana nidhamu wao kwa wao, hawaheshimiani, hawana upendo, hawathaminiani, wamejawa chuki na fitina mahali pa kazi na kuchafuana. Hali hii inahamia mpaka kwa wananchi wa kawaida wanaoongozwa. Upendo na heshima vimepungua, na chuki na fitina ndivyo vimeshika nafasi. Ndiyo maana sasa hivi kumekuwa na matukio ya mauaji ya kinyama na kumwagiana tindikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali:-

(i) Idumishe amani kwa kusositiza upendo mionganoni mwa jamii, ikianzia kwa viongozi; na

(ii) Ipambane na rushwa kwa dhati, kwani rushwa ni chanzo cha chuki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, napenda kumalizia kwa kusema kwamba rasilimali watu ithaminiwe. Nchi bila watu hakuna kazi wala miundombinu. Kwani watu wanauawa hovyo na askari wetu, kila kukicha ni risasi za moto kwa wananchi kwa kosa dogo tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ikae chini itafakari nini hasa tunahitaji nchini. Suluhisho la tatizo nchini siyo kupiga risasi, siyo kuchoma nyumba na mifugo na mali za wananchi. Ni kurudisha nyuma Taifa na kuwatia umaskini wananchi. Ahsante.

**MHE. CYNTHIA H. NGOYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naomba kuipongeza Serikali kwa kuandaa Mpango mpya wa Serikali kwa mwaka 2014/2015. Naomba kuchangia hoja hii katika maeneo machache kama ifuatavyo:-

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. C. H. NGOYE]

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wazi kabisa uchumi wetu hutegemea kilimo, maliasili na mifugo, lakini tumeacha mambo muhimu ambayo yanapaswa kuzingatiwa ili sekta hizi zichangie maendeleo endelevu hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumzia kilimo kwa hakika ni lazima tuzungumzie kilimo cha umwagiliaji ambacho kinaweza kufanyika mwaka mzima. Tatizo kubwa ninaloliona ni mipango yetu kutoliweka suala la hifadhi ya mazingira na hasa hifadhi ya vyanzo vya maji kwa uzito mkubwa. Ni lazima Wataalam wetu wa Mipango waanze kuliona suala la mazingira kama jambo la lazima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tutaendelea kuliacha suala la mazingira kama *agenda* isiyo ya umuhimu, mipango ya kKilimo Kwanza au mpango wa *SAGCOT*; haina maana yoyote, haina uendelevu wowote. Ni matumaini yangu na nashauri mpango huu uweke bayana program za upandaji miti kwa kila Kaya, kuhifadhi vyanzo vyote vya maji, misitu yote ihifadhiwe ili tuwe na uhakika wa upatikanaji wa mvua za uhakika kwa ajili ya kilimo na mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mifugo; ni muhimu Serikali yetu ianze kuiga mfano wa namna nchi nyininge kama Namibia wanavyofanya. Kuna haja ya kila Mkoa kutenga maeneo kwa ajili ya mifugo tu, ambako kutajengwa mabwawa ya maji kwa ajili ya mifugo, kupanda nyasi za mifugo na wafugaji watengewe maeneo hayo. Wafugaji wenyewe wataamua kuwa na idadi ya mifugo kulingana na ukubwa wa maeneo waliyopewa. Uzururaji wa mifugo hautakuwepo tena na kuondokana na mapigano kati ya wakulima na wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la amani na utawala bora, ni lazima yaangaliwe kwanza. Hakuna mpango wowote wa maendeleo utakaowezekana kutekelezeka iwapo wananchi hawana usalama wa uhakika. Mipango ya kusimamia usalama wa nchi yetu ianze kuangaliwa kwa makini sana ili vyombo vyetu vifanye kazi vikiwa na amani bila vikwazo.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. C. H. NGOYE]

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mipango ya Maji; hakuna njia yoyote itakayofanikiwa wala miradi ya kuwa endelevu kama mipango ya hifadhi ya vyanzo vya maji itapuuzwa na wafugaji, wakulima na wawindaji. Upatikanaji wa vyanzo vya fedha una njia nyingi katika nchi yetu, hasa kama tutaziangalia sana hifadhi zetu za wanyama, ambayo ni maeneo ya kitalii. Hata hivyo, utalii mwingine ambaeo ni wa milima, maua na kadhalika. Maeneo hayo hayajaangaliwa kwa karibu ili yatoe mchango wa kiuchumi hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naishauri Serikali ijikite zaidi katika kuwawekea mipango mizuri ya maendeleo Wanawake na Vijana, kwani haya ni makundi muhimu kiuzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo machache, naunga mkono hoja hii.

**MHE. FATUMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda kupongeza kwa Mpango, kwani Mpango umetaja mambo mazuri na yanayomgusa mwananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niongelee juu ya jinsi ya kuendeleza uchumi nchini ili kukuza uchumi wetu:-

- (1) Kuendeleza elimu nchini.
- (2) Kuendeleza maji – maji ni muhimu.
- (3) Kuendeleza kilimo – chakula ni muhimu.
- (4) Nishati na madini – ili kuendeleza viwanda.
- (5) Utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo haya matano (5) yatakuza uchumi wetu. Tuna rasilimali za kutosha sana ambazo ni nyenzo za kuendeleza uchumi huo. Tujiipange, tuendeleze ili tufufue uchumi wetu. Naomba kuwasilisha.

**MHE. MILTON M. MAHANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naunga mkono hoja hii, lakini ningependa nizungumzie suala la mikakati ya kukuza ajira nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze Serikali kwa kuainisha mikakati na program za ajira zitakazoshughuliwa na Serikali mwaka 2014/2015.

Hata hivyo, uzoefu unaonesha kwamba, Wizara ya Kazi na Ajira inayosimamia programu hizi za ajira huwa haipewi fedha za maendeleo kwa ajili ya kutekeleza programu na mikakati hiyo.

Kwa mfano, mwaka huu (2013/2014) Wizara hii imepata sifuri kwa miradi ya maendeleo. Kama program na mikakati ya kukuza ajira iliyooneshwa kwenye Mpango huu halitapangiwa fedha za maendeleo ya kuitekeleza, tutakuwa hatuoneshi umuhimu wa kushughulikia tatizo hili kubwa la ajira kwa vijana.

Aidha, Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango umeeleza kwamba Serikali itatekeleza tafiti za hali ya nguvukazi na hali ya utaalam nchini.

Pia kwenye maelekezo ya uandaaji wa mipango na bajeti 2014/2015, *MDAs* wametakiwa kujaza fomu za uzalishaji wa ajira kwenye maeneo yao. Mambo yote haya yanahitaji uwezo wa kifedha na nyenzo ili Wizara ya Kazi na Ajira iweze kufuatilia, kutekeleza na kubaini ukuzaji wa ajira hadi ngazi ya chini ya Halmashauri za Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara pia imeshindwa kutekeleza na kukamilisha mradi wa *Labour Market Information System (LMIS)* kwa ukosefu wa fedha za maendeleo. Ni matumaini yangu kwamba mwaka 2014/2015, Wizara ya Kazi na Ajira itaanza kupewa kipaumbele kinachostahili kuliko sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. DKT. MAUA ABEID DAFTARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na pia naomba kuchangia ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Dira yetu ya Maendeleo ya 2025 ni kuendeleza ujenzi wa uchumi wa kisasa na Taifa linalojitegemea. Na Serikali imeweka vipaumbele vya kutekeleza katika Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (5) ambavyo ni miundombinu, kilimo, viwanda vinavyotumia malighafi za ndani na kuongeza thamani, maendeleo ya rasilimali watu na ujenzi na uendelezaji wa huduma za utalii, biashara na fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Kilimo bado haijasimamiwa kisawasawa. Upo umuhimu wa kukuza kilimo kuanzia ngazi ya familia, kwa familia kuwezeshwu kupata ardhi ya kutosha ya kilimo, wakopeshwe pembejeo za kilimo, elimu bora kwa wakulima na ufuatiliaji thabiti wa Mabwana na Mabibi Shamba. Uingizaji wa *power tillers* dhaifu hazikusaidia sana wanyonge, bado wananchi wengi wanatumia jembe la mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, uingizaji wa mbegu mbaya za mahindi kumeathiri sana kilimo cha mahindi, Arusha na Nyanda za Juu. Vituo vya Utafiti wa Mazao mbali mbali vinahitaji sana kuboreshwa. Watafiti wapatiwe zana na vifaa na pia kupewa motisha. Aidha, kufufuliwa kwa maeneo ya utafiti na watafiti kupewa nafasi ya kwenda kupata mawazo mapya ya kitafiti toka nchi nyiningine. Matokeo ya tafiti mbalimbali kurejeshwa kwa wakulima kwa lengo la uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Sekta ya Uvuvi. Ni sekta isiyo na wenywewe. Wavuvi wanavua kwa bahati na si kisayansi. Wanaofaidika ni wavuvi wa bahari kuu wenye vifaa. Nao hawa wana matatizo ya rasilimali zetu za samaki kwa kuwavua samaki wakubwa na hasa wadogo na kuwatupa baharini wakati tayari wamekufa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna *monitoring system*

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. M. A. DAFTARI]

yoyote wanayofanyiwa wawekezaji wakubwa, badala yake wavuvi wadogo wadogo ndio wanaoandamwa na makundi mbalimbali. Ni vyema wavuvi wadogo wadogo wasaidiwe kupata unafuu wa kodi kwenye nyavu, mashine za boti; na pale wanapobahatika kununua mbaao za kuchonga majahazi/boti za uvuvi. Wavuvi wadogo wadogo wanachangia sana uchumi wa nchi yetu, wawezeshwe. Tunashukuru kufutwa kwa kodi za nyuzi, ile haileti *impact* kubwa kwa wavuvi wetu wadogo wadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Uchukuzi; reli zetu zinahitaji kuboreshwa na ikiwezekana kuongeza matawi ili zisaidie uchukuzi kwenye maeneo ya uzalishaji mali. Tunang'ang'ana na kuboresha barabara, na kusahau kuwa iwapo reli itaboreshwa kubeba mizigo mizito, barabara itapata nafuu na itadumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea kusema kwamba sioni mantiki kwa reli zetu kuchangia *Road Toll* ya barabara. Huyu ni mpinzani wake, iweje leo reli ife kwa kunufaisha barabara? Mabilioni ya fedha yatokanayo na *road toll* ambayo reli inachangia kwa barabara siyo haki. Reli na barabara zote zina umuhimu wake na zote zipewe Kipaumbele sasa. Ujenzi wa reli ya Dar es Salaam – Isaka, sasa tufikirie reli hiyo iende Burundi kwanza badala ya Rwanda. Waache Rwanda wajenge reli yao na Uganda na Kenya na Sudan. Kwanza Rwanda haituhitaji Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Viwanda; napenda kujua ule uamuvi wetu kutaka Viwanda vyetu vya Pamba kutengeneza nyuzi na kuuza nje badala ya kuuza pamba safi, umefikia wapi? Je, ule uamuvi wetu wa kubangua korosho hapa hapa nyumbani badala ya kupeleka korosho zetu raw umefikia wapi? Yote hayo ni maamuvi yenye tija, ila hayakutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara kwa kazi nzuri na pia kwa Bunge kuunda Kamati ya Bajeti ambayo inafanya kazi nzuri ya kuisaidia Serikali mambo mengi.

**MHE. NAOMI A. M. KAIHULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa Mwenyezi Mungu kwa kunipatia afya njema na wasaa huu wa kuweza kuchangia Mpango huu.

Kwanza, Mheshimiwa Mwenyekiti, yahusu suala la kukua kwa uchumi na kuhusu kuongezeka kwa pato la wastani kwa kila mtu kwa kiwango cha asilimia 17.9%. Jambo hili bado halijajibu utata wa viulizo vyta wananchi kwamba mbona ongezeko hilo haliendani na hali halisi ya kipato cha wananchi wa hali ya chini ambao pato lao linazidi kiushuka hata kuwa chini ya dola moja kwa sasa hivi? Hii inaonesha jinsi gani mipango hii siyo shirikishi. Matokeo yake ni kuwepo kwa takwimu kwenye maandishi yasiyowalenga wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, Mpango huu pia haukuchukulia kwa umakini sekta muhimu kama viwanda na biashara, ambazo ikiwa zingepangwa vizuri kwa kufufua viwanda muhimu viliviyohujumiwa na Serikali ya CCM, basi ajira zingeongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Serikali hii haijaona kuwa kuna umuhimu wa kuanzisha na kuendeleza viwanda vyta kusindika na kufungasha vyakula kwa ajili ya kuwapa wananchi nafasi ya kufungua na kupenyeza masoko ya majirani zetu ambao wengi wao wana uhitaji wa vyakula na sisi Mungu katukirimia tunu hiyo. Kuongeza thamani kwa mazao ya kilimo kwa kuyasindika na kuyafungasha, kungepunguza adha kubwa ya wananchi kudodewa na mazao yao ya kilimo. Manufaa makubwa ambayo yanepatikana ni kupunguza utegemezi wa mazao haya kwa nchi za jirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la utegemezi haliangaliwi kwa umakini. Mpango haujaonesha jitihada za makusudi za kuondokana na utegemezi wa misaada toka nje na mikopo kutokana na washiriki kutoka nje. Kwani kusema kweli haina faida kihivyo iwapo mipango madhubuti ya kuwa na sera nzuri za kuondoa misamaha ya kodi inayotolewa kiholela kwa wawekezaji kwa kisingizio rahisi cha vivutio vyta wawekezaji. Tatizo siyo misamaha ya kodi, bali ni

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. N. A. M. KAIHULA]

udhaifu wa utangazaji wa vivutio hivyo katika Balozi za Tanzania na ukosefu wa elimu ya uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utawala Bora; suala hili pia ni muhimu katika utekelezaji na mafanikio ya Mpango, lakini Mpango huu haujatilia maanani sana. Mpango unapaswa kuzingatia mkakati wa kuwashughulikia wahujumu wa uchumi ambao idadi yao inaongezeka kwa kasi. Mfano, viongozi na wataalam ambao wanatayarisha mipango hafifu na mikataba hafifu kwa ajili ya faida zao binafsi au kwa ajili ya manufaa binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia haujaonesha jinsi gani *grand corruption* inayoendelea sasa hivi na inayoathiri uchumi kwa sehemu kubwa, inaweza kudhibitiwa. Mfano, wauaji wa tembo, mikataba mibovu ya madini, gesi, urani na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango usipange ukiwa na itikadi za watawala vichwani. Hili litasababisha mpango kushindwa kabisa kuanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Deni la Taifa halioneshi kupungua.

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naiunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi kwa kuwa ina maslahi makubwa kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyo ada kwamba, kupanga ni kuchagua na Tanzania kama Taifa, tunavyo vipaumbele vingi katika kuhakikisha nchi yetu inapiga hatua katika kuelekea kwenye maendeleo kama Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Nchi pamoja na Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango kwa kuja na vipaumbele vichache ambavyo vina mchango mkubwa katika ukuzaji wa uchumi wa nchi hii. Sekta zilizoainishwa kama vipaumbele ni pamoja na:

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. A. M. MASELE]

- (i) Miundombinu;
- (ii) Kilimo;
- (iii) Viwanda vinavyotumia malighafi za ndani kuongeza thamani;
- (iv) Maendeleo ya Rasilimali watu; na
- (v) Uendelezwaji wa huduma za utalii, biashara na fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hakika kuwepo kwa Mipango ya Maendeleo ni jambo moja na kuwepo kwa ufuatiliaji wa dhati wa mipango yenye na ndipo wazo la kuwepo kwa falsafa ya Matokeo Makubwa Sasa (*Big Results Now*) lilibuniwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza pia hatua ya kuanzishwa kwa *Presidential Delivery Bureau*. Kwa kuwepo kwa kitengo hiki ni jambo la kheri na naishauri Serikali ione uwezekano wa kuwashirikisha Watanzania walioonesha ubunifu mkubwa na kuzifanya taasisi zao kufanya vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iwajumuise katika *Presidential Delivery Bureau*. Watu hao ni kama akina Dkt. Ramadhan Dau wa NSSF, Nehemiah Mcchechu wa Shirika la Nyumba na Dkt. Kimei wa Benki ya CRDB. Watanzania hawa wameonesha kuwa na vipaji, akiwemo pia Ndugu Mfugale wa TANROADS. Wazalendo hawa wachache wameonesha uwezo mkubwa wa kuziongoza taasisi zao na kwa jinsi hiyo watamshauri Mheshimiwa Rais pamoja na Tume ya Mipango kuhusu mpango wa Matokeo Makubwa Sasa (*Big Results Now*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, naishauri Serikali ichukue hatua za makusudi za kuajiri wataalam mabingwa wa kutoka Mataifa yaliyoendelea; mabingwa hao wawe ni

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. A. M. MASELE]

wale waliothibitika kutoa michango katika Mataifa mbalimbali. Ni dhahiri kuwa Mataifa yanayopiga hatua kwa haraka kama Korea Kusini, Malasyia na Uchina, yamekuwa na Tume za Mipango kama ya kwetu na zikatumia mbinu za kupata wataalam kutoka nchi zilizoendelea. Mifano ni mingi, ikiwemo pia nchi ya Iran.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utajiri wa nchi yetu unatuweka katika nafasi nzuri ya kuweza kuwa na ushawishi wa kupata wataalam mabingwa kutoka nchi zilizoendelea, cha msingi hapa ni kuwalipa mafao mazuri. Ukiwepo mkakati kabambe wa kuwepo kwa *Presidential Delivery Bureau*, nina imani kubwa kuwa nchi yetu itakuwa tayari kuhakikisha kwamba teknolojia mbalimbali zinazopatikana duniani kote tunaweza kupata kwa aidha:-

- (a) Kuomba Mataifa yaliyoendelea yatupatie.
- (b) Kuhakikisha tunatenga fedha kwa ajili ya kununua teknolojia husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina imani na Serikali ya CCM kwamba, ni siku na zaidi sana niishauri kuwa mchakato wa uchimbaji wa Makaa ya Mawe na Chuma kule Liganga na Mchuchuma ili kuhakikisha nchi yetu inafanikiwa katika Mapinduzi ya Viwanda na kuikabili biashara ya vyuma chakavu inayotishia uwepo wa miundombinu ya nchi yetu inayohujumiwa na watu wasiokuwa na nia njema na nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Sasa nawaita wafuatao: Mheshimiwa Simbachawe na atafuatiwa na Mheshimiwa Saada Salum, Mheshimiwa Eng. Lwenge, Mheshimiwa Goodluck Ole-Medeye, atafuatiwa na Mheshimiwa Adam Malima, halafu Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi nianze kwa kuunga mkono hoja ya Serikali ya Mipango ambayo ni mapendekezo kama hatua ya mwanzo ya bajeti ya mwaka unaofuata wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ingawa nilitegemea kupata mawazo ya nini tufanye, lakini hapa kwa kiasi kikubwa nitajikita kwenye yale ambayo yamesemwa na Waheshimiwa Wabunge ambayo kwa kiasi kikubwa hapa ni kutoa taarifa ya baadhi ya mambo ambayo pengine hayaeleweki vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Sekta ya Nishati na Madini limezungumzwa sana suala la utayari wa Serikali juu ya uchumi wa gesi na hapa imesemwa sana juu ya utayarishwaji wa Sera ya Gesi na Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kulitaarifu Bunge lako Tukufu na Watanzania kwa ujumla kwamba mchakato wa Sera ya Gesi umekamilika na Sera ya Gesi imekamilika tangu tarehe 10 Oktoba, 2013, na kinachosubiriwa sasa ni maandalizi ya sheria. Ingawa yalikuwa yanaenda sambamba na utayarishaji wa Sera hii; maandalizi ya sheria ambayo na yenewe inabadilika kwa kiasi kikubwa, kwa hiyo, mchakato huo baada ya muda na wenyewe utakamilika ili kwanza tutayarische sera ndiyo baadaye tutayarische sheria. Hali kadhalika gesi *master plan* na yenewe itafuata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zoezi hili limechukua muda mrefu kwa sababu ya umakini tunaopaswa kuwa nao katika kutumia rasilimali hii. Tumejifunza kutoka kwenye nchi mbalimbali maana rasilimali hii sisi siyo wa kwanza duniani, nchi mbalimbali zimegundua rasilimali hii, lakini tumejifunza na huko kuna mazuri na mabaya ya kujifunza na ndiyo maana sisi tumejitahidi kuhakikisha kwamba hatufanyi kosa katika jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo limezungumzwa sana na Waheshimiwa Wabunge juu ya

**Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)**  
[NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. G.  
B. SIMBACHAWENE)]

Sekta ndogo hii ya gesi ni suala zima la ushirikishwaji wa Watanzania. Ushirikishwaji wa Watanzania hapa umezungumzwa katika nyanja mbili. Moja, imezungumzwa katika nyanja ya ushirikishwaji katika ile *local content* kwamba Watanzania nao wanashiriki vipi katika uchumi wa gesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa hatuwezi kusema kwa kiwango ambacho tumegundua gesi tulioigundua sasa kwamba tuko kwenye *full implementation*, kabisa ya kusema kwamba sasa tunazalisha na tunatumia zao hili ambalo tumelipata. Kwa hiyo, sasa bado tuko kwenye hatua ya awali sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, gesi tulionayo kwa sasa ni ile ya Songsongo ambayo inatumika kuzalisha umeme ambayo tunazalisha Dar es Salaam, lakini na ile ya *Mnazibay* ambayo tunamla kuzalisha umeme tuna ozalisha kule Mtwara na ambao umesambazwa katika Mkoa wa Mtwara. Gesi nyingine iko kwenye kina kirefu na bado haijaanza kutumika na itachukua muda kwenda kuitumia hiyo. Kwa hiyo, nichukue nafasi hii kuwaambia Waheshimiwa Wabunge kwamba hatujachelewa, ila haraka yetu pia inapaswa tuwe makini sana kuhakikisha kwamba hatukosei. Hatujachelewa bado, hii rasilimali bado, pengine zaidi ya miaka mitano ijayo ndipo tutakapoanza kuitimia rasilimali hii vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini eneo la pili, lilikuwa ni suala la ushirikishwaji wa Watanzania katika utafutaji na uchimbaji wa gesi. Vyovoyote utakavyosema, suala hili linahitaji mjadala wa kutosha. Unaposema kuwashirikisha Watanzania katika uchimbaji na utafutaji, Serikali imeweka Shirika la *TPDC* ambalo ni Shirika la Umma la Watanzania wote kwamba litutazamie na lilinde maslahi yetu, Watanzania wote. (*Makofii*)

Sasa unaposema sekta binafsi, sijui ni kikundi cha watu, lazima hapa uje na jibu useme kabisa ni nani huyo tumpe? Uje useme kabisa, tunampa nani kwa niaba ya Watanzania? Serikali yenye weimeona *TPDC* ndiyo itachukua rasilimali ile.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. G.  
B. SIMBACHAWENE)]

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu uko hivi: Serikali kuititia Wizara Nishati na Madini inatoa leseni kwa *TPDC*, *TPDC* wanamtafuta mbia, wanashirikiana naye, kwa kuwa *TPDC* inawakilisha Watanzania wote, wanashirikiana na hiyo kampuni nyingine itakayokuwa imekuja kuwekeza au Makampuni ya kuja kuwekeza na pale *TPDC* inakuwa inatunza *share* za Watanzania kati ya asilimia 65 hadi 75. (Makof)

Sasa unaposema Watanzania lazima waingie katika sekta hiyo, washiriki katika kuchimba na kutafuta, lazima uwe pia *specific kwamba tunampa nani kwa niaba ya Watanzania?* Hapa lazima Watanzania wakubali kwamba mpeni fulani, lakini ukisema tu hivi halafu ikabakia hewani hivi, kidogo inakuwa ni vigumu sana kueleza hili jambo. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine lilirozungumzwa hapa ni *launching* ambayo imefanyika ya tarehe 25 Oktoba, 2013. Tumefanya uzinduzi huu. Uzinduzi huu hauna maana nyingine yoyote zaidi ya kuweka tu kusema jamani sisi tuna vitalu vya gesi, vipo. Kwa mujibu wa sera hii ambayo iko tayari, tumewakaribisha wawekezaji wa ndani na wa nje washiriki katika kuingia kwenye mnada huu wa vitalu, hakuna aliyezuiwa, wote wanaruhusiwa. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama *exceptions* zinatafutwa, basi tujadiliane hapa tu-discuss tuseme *exceptionals* hizo zimkumbe nani, nani apendelewe, hilo ni jambo lingine. Lakini kwa maana ya sera, sisi tunesema Watanzania, na wasio Watanzania washiriki katika zoezi hili. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, limezungumzwa suala lingine la umeme katika Wilaya mpya. Wilaya mpya ambazo hazina umeme ni Wilaya 13. Katika Wilaya hizi 13, tayari Wakandarasi wameshapatikana na sasa hivi tunapoelekea ni kuanza kwa utekelezaji wa miradi hiyo ya Wilaya hizi 13. Wilaya hizi zinajulikana, ni Wilaya ya Chemba, Kyerwa, Mlele,

*Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*  
[NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. G.  
B. SIMBACHAWENE)]

Uvinza, Kakonko, Buhigwe, Momba, Nanyumbu, Kalambo, Mkalama, Nyasa, Busega na Itilima. Huku Wakandarasi wameshapatikana, tunaenda kwenye utekelezaji.

Kwa miradi ya *REA* kwa ujumla ambao tulisema kwamba utekelezaji wake utatuchukua katika mwaka huu wa fedha na utaanza, Mikoa mingine imepata Wakandarasi lakini Mikoa mingine kumi haijapata Wakandarasi na mchakato unaendelea, mwisho wa mwezi huu tunaweza tukakamilisha mchakato wa kupata Wakandarasi ili kuweza kutekeleza miradi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, limezungumzwa suala la bomba la mafuta kutoka Dar es Salaam hadi Mwanza. Bomba hili tulifika hatua nzuri akapatikana kampuni inaitwa *Nuru Oil* ambao walisema watajenga hilo bomba lakini pia watajenga na *refinery*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kusuasua huku kunatufanya tufikirie upya wazo hili la kuiachia hii kampuni na tuone namna nytingine. Lakini wazo hili bado liko pale pale. Ni muhimu sana kwa uchumi wa Taifa kuwa na bomba hili la mafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine lilirozungumzwa ni umeme unaotokana na makaa ya mawe wa Ngaka. Tuko katika hatua ya *negotiation* katika *PPA* kati ya *TANESCO* na wenzetu wa *NDC* wakishirikiana na hiyo kampuni, mbia wao na hali ya mazungumzo inaenda vizuri ingawa wanachobishania pale ni bei za umeme, tutaona namna ya *ku-speed up* hilo zoezi. Aidha, Liganga na Mchuchuma, mkandarasi yuko *site* anaendelea na mgodi wa Kiwira ni kwamba *STAMICO* wameshakabidhiwa, mchakato unaendelea ili waweze kupata mbia ili waweze kuendesha mgodi ule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekaa hapa Bungeni miaka saba, nimejifunza sana namna ya michango ya Wabunge na namna ya kufanya ili Bunge liweze kuwa na ufanisi. Ni lazima tujikite sana kwenye kanuni zetu. Kanuni ya 94, inasema, Serikali italeta mpango na baadaye Wabunge watachangia na kuishauri Serikali. Lakini kwa kiasi kikubwa

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. G.

B. SIMBACHAWENE)]

nimeshuhudia hapa zaidi sana ni kulaumiwa, kusemwa, sasa hata hatupati ule mchango ambao tingesema tuuchukue kama Serikali ili tuweze kuboresha huu mpango ambao umekuja ambao ni mapendekezo. (*Makofi*)

Nichukue nafasi hii kuwaomba Waheshimiwa Wabunge kama wana mawazo mazuri bado fursa ipo na Serikali sisi tutaendelea kupokea, Wizara yangu ya Nishati na Madini tutaendelea kupokea mawazo yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, dunia hii changamoto zipo, zilikuwepo enzi ya mitume wote, enzi ya Yesu Kristo na changamoto zilikuwepo na matatizo hazikwisha akaja Muhammad, matatizo hayakwisha na mpaka tutamaliza sisi matatizo hayatakwisha. (*Makofi*)

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha  
kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Sasa unatuambia akina Muhammad, imekuwaje? Mheshimiwa Saada Salum, atafuatiwa na Eng. Lwenge.

### **NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA MKUYA SALUM):**

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nashukuru kwa kupata fursa hii ya kuweza kuchangia hoja ambayo tumeiletu sisi kama Serikali ya Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo mwaka 2014/2015.

Aidha, katika mchango wangu vilevile nitajikita katika kutoa ufanuzi wa hoja mbalimbali ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge. Kimsingi hoja zote ni *valid* na tutajaribu kwa uwezo wetu kuchukua mawazo mapya ambayo yametolewa na Waheshimiwa Wabunge kwa ajili ya kuboresha utendaji kazi wetu Serikalini na pamoja na utekelezaji wa ufanisi wa bajeti hii ya Serikali.

Kulikuwa kuna hoja ya utaratibu huu wa *Cash budget* ambayo tunatumia sasa hivi *as against* utaratibu wa *Capital*

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. S. M. SALUM)]

Budget ambao tulikuwa tukitumia kabla, miaka ya nyuma ya 1995/1996 na kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti pamoja na Waheshimiwa Wabunge, tutakumbuka kwamba, katika miaka ya 1995/1996 wakati Serikali inaendelea kufanya mageuzi ya kiuchumi na ya kifedha, Utaratibu wa *Capital budget* ndiyo ambao ulikuwa ukitumika. *Concept* nzima ya utaratibu huu ambao Waheshimiwa Wabunge wengi wamesisitiza kwamba, kwa sababu ya matitizo yaliyopo kwenye *cash budget*, turudi kwenye utaratibu wa *capital budget*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tuchukue fursa hii kujikumbusha hali ilikuwaje wakati tulipokuwa tukitumia utaratibu wa *capital budget*. Kwa muda huo Bunge lilikuwa linaidhinisha mapendekezo ambayo yameletwa na Serikali, mapendekezo ya mipango pamoja na fedha zake. Bunge linaidhinisha matumizi ya taasisi za Serikali kutumia kama vile ambavyo imependekewa katika mpango yao, bila kutilia maanani kiasi ambacho Serikali itawenza kukusanya kutoka vyanzo vyake vya ndani na vyanzo vya nje. Kwa maana hiyo tukiondoka hapa, muda huo ilikuwa ni kwamba, haya kila Taasisi iende ikatumie *according to* vile ambavyo imepanga na imeidhinishwa na Bunge.

Utaratibu huu iliingiza Serikali katika madeni makubwa. Kwa nini? Kwa sababu, Wizara inapotoka hapa bajeti inakuwa imeshaidhinishwa. Wakati huo kila Wizara ina *account* yake Benki. Kwa hiyo, kwa sababu ilikuwa Hazina ina-issue ile ex-chequer, kwa hiyo, kila Taasisi ilikuwa na uwezo wa kutumia kutohana na kile ambacho killidhinishwa hapa na Bunge, bila kujali ni kiasi gani kama Serikali tungeweza *collect*. Muda huo Serikali iliingia katika madeni makubwa, kwa sababu Taasisi zinatumia bila kujali kile ambacho kitapatikana, bila kujali miongozo ya bajeti, bila kujali kitu kingine chochote. Taasisi zilikuwa zinatumia kutohana na mahitaji yake, lakini hatuja-*consider* mahitaji ya nchi nzima au uwezo wa nchi nzima kuweza kukusanya mapato ya ndani na ya nje. Kwa hiyo, utaratibu huu iliingiza Serikali katika deni kubwa.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. S. M. SALUM)]

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengi wetu ambao tulikuwepo, *at least* sisi ambao tumesoma katika *documents* mbalimbali, kuna ripoti mbalimbali zimetayarishwa, tuliona kwamba Serikali iliingia sana kwenye madeni makubwa wakati huo. Ndiyo maana ikasababisha Serikali hii ya Tanzania kuingia katika ule mpango ule wa *Highly Indebted Poor Countries (HIPC)*. Sababu mojawapo ilikuwa ni utaratibu wa kutumia *capital budget*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mageuzi hayo yaliendelea, Serikali kwanza tulikuwa katika *Structural Adjustment Program*, tukaingia *HIPC* na mpaka sasa sasa hivi tuko katika utaratibu huu wa *PS*/kwa sababu tuna-guide ule mlolongo wetu wa matumizi ili uende na kile ambacho kinapatikana. Nadhani hii ni *logic*.

Waheshimiwa Wabunge, naomba mtu-support katika hili, kwa sababu ni utaratibu ambao tumefanya kuiwezesha nchi sasa iweze kutumia kwa kile ambacho inakipata, kile ambacho inaweza kukusanya na kile ambacho tunaweza kukopa kutoka kwa washirika wa maendeleo.

Kwa hiyo, hiyo ilikuwa ni nia njema sana ya Serikali. Kwa hiyo, tunaomba Waheshimiwa Wabunge mtu-support katika hili. Tuna nia njema, tunataka mipango ya mendeleo tuitekeleze, lakini kwa sababu tunakuwa *constrain* na mapato.

Kwa hiyo, sasa hivi tunaelekea huko, na nawaomba Waheshimiwa Wabunge sasa tujitahidi kwa pamoja sote tuweze sasa tu-guide kujua *mechanism* nzima ya kuweza kutumia kutokana na kile ambacho kipo katika nchi na kile ambacho tunaweza kukopa katika kutoka kwa mashirika ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa kuna suala lingine ambalo Wabunge walikuwa na wasiwasi sana kuhusiana na Deni la Taifa. Deni la Taifa limekua. Hii haina ubishi na kutoka mwaka jana mpaka mwaka huu deni la Taifa limekua kwa kiasi cha *dollar billion* 1.39. Kwa nini?

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. S. M. SALUM)]

Kwa sababu tukikumbuka Waheshimiwa Wabunge ni kwamba, deni la Taifa lina-constitute vilevile madeni ambayo yalichukuliwa miaka ya nyuma. Kwa hiyo, madeni ambayo yaliyochukuliwa miaka ya nyuma; miaka ya 1930, miaka 1940 hususan concessional loans ndiyo zina-mature sasa hivi. Kwa hiyo, ingawa tunalipa na ingawa tunaendelea kukopa, lakini tukumbuke vilevile tunalipa deni ambalo huko nyuma lilichukuliwa kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo. Kwa hiyo, tusiwe na wasiwasi sana kwamba deni la Taifa linakua, halikui kwa sababu tunachukua cash na tunatumia, lakini lina-constitute vilevile mikopo ambayo ilichukuliwa miaka ya nyuma na sasa hivi ina-mature na ndiyo ambayo tunaendelea kulipa pamoja na mikopo mingine ambayo tunagharamia miradi ya maendeleo. (*Makof!*)

Waheshimiwa Wabunge, kitu cha msingi hapa, tushirikiane kuhakikisha kwamba Serikali inachukua mikopo kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo. Wengi wetu tumemponeza sana Dkt. Magufuli kutokana na kuona barabara nyingi sasa hivi zinapitika, zimejengwa. Tujue kwamba barabara zile zimejengwa. *It goes a long side with* hata hiyo mikopo ambayo tunachukua. Tunachukua mikopo, tunaingiza kwenye miradi ya maendeleo ikiwemo barabara ambazo Waheshimiwa Wabunge tunashukuru kwamba wengi wenu mmeipongeza Serikali katika hili, kwa hiyo tuone vilevile ni jinsi gani Serikali inakopa na inaingiza fedha za mkopo katika miradi ya maendeleo ikiwemo barabara. (*Makof!*)

Wengi wetu hapa tumelisimamia suala la reli, lakini tukumbuke kwamba Serikali itakapomaliza mchakato wake wa fedha, mchakato wa ku-mobilise hizo resources, tujue deni la Taifa litakuwa, lakini kitu cha muhimu, tunaelekeza kwenye miundombinu ya reli ambayo italeta tija. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa kuna eneo lingine, Waheshimiwa Wabunge wamepigia kelele kuhusiana na huu ukomo ambao umewekwa na IMF na Benki ya Dunia. Tumeona kwamba hii labda ni kuinyima fursa Tanzania kukopa mikopo mikubwa ya kibashara ili kugharamia miradi

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. S. M. SALUM)]

ya maendeleo. Hili nalo ni eneo lingine ambalo Waheshimiwa Wabunge lazima tulizingatie. Tunapokopa lazima kunakuwa kuna vigezo veya kukopa. Kwa sasa ukomo ambao tumewekewa katika kukopa vyanzo vyetu ni asilimia moja ya pato la Taifa. Kwa nini iwe ni asilimia moja ya pato la Taifa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Benki yoyote inaweza ikamkosesha mwananchi wa kawaida lakini ikaikopesha Serikali, kwa sababu ndiyo mkopeshaji ambaye tukiingia kwenye mikopo ile ya *TB's* ndio yenyeye uhakika zaidi. Sasa kama tutakopa zaidi ya kiwango cha asilimia moja, kutokana na *measurements* mbalimbali, tutaikosesha *private sector* kuweza kukopa kwenye vyanzo veya ndani, maana *banks* ni za kibishara. Maadam Serikali imetoa *TB*, kila mtu anakwenda ku-*invest* kwenye *TB*. Mwananchi wa kawaida, vikoba, wakulima, watakuwa hawana nafasi ya kukopa katika Mabenki kwa sababu pesa yote sasa imekuwa *invested* kwenye *TB* zao.

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha  
kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA MKUYA SALUM):**  
Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa Lwenge.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya mimi niweze kuchangia mapendekezo ya mpango wa maendeleo wa mwaka 2014/2015. Kwanza, kabisa nampongeza Mheshimiwa Wasira kwa kuleta Mpango mzuri ambao naamini kabisa unatekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza Waheshimiwa Wabunge wasiwe na wasiwi kusema tunapanga vitu vingi. Siku zote lazima u-*think big*. Ukitaka kufanikiwa, uwe na

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[NAIBU WAZIRI WA UJENZI]

malengo makubwa. Huwezi kuanza na malengo madogo halafu utegemee kufanikiwa.

Waheshimiwa Wabunge, sasa kwa sekta ya miundombinu, ukipitia llani ya Chama cha Mapinduzi, kuanzia ukurasa wa 72 mpaka 78, zimeandikwa barabara nyingi sana hapa. Sasa hapa huwezi kuiacha barabara kwa sababu tumewaaahidi wananchi kwamba barabara hizi zote tutazitengeneza. Ndiyo maana tumetengeneza utaratibu; kwanza tumeanzisha huo Mfuko wa Barabara ili tuwezeshe barabara nyingi zilizoko Mikoani. Barabara kilometa 33,000 ni barabara kuu na barabara za Mkoa ziweze kutengenezwa kwa ajili ya fedha ambazo una uhakika kwamba zipo na wengi mnasema barabara za *TANROAD* ni nzuri, ni kwa sababu tunao Mfuko unaotengeneza barabara hizo. (*Makof*)

Sasa tukianzia kwenye llani, ni kwamba toka mwaka 2005, Rais wetu Mheshimiwa Jakaya Kikwete alipoingia madarakani alianza na hii *Big Results* ambayo inazungumzwa leo, akaamua kuzishambulia za nchi hii, ili kuunganisha mikoa yote. Lengo lilikuwa Mikoa yote iunganishwe kwa barabara za lami. Kwa hiyo, ndiyo maana kilometa zinazojengwa sasa hivi ni nyingi sana, karibu kilometa 11,891, hazijapata kutokea kwamba zinajengwa kwa wakati mmoja. Sasa katika hizi barabara tumeziweka katika maeneo makuu matatu. Kwanza, tunazikarabati barabara zile ambazo zimeshapita muda wake. Kwa sababu barabara huwa zinasanifiwa kwa miaka 20. Sasa barabara ikitumika zaidi ya miaka 20 kwa vyovyyote vile, na ili upate *economic rate of return* inayotakiwa, lazima uifanyie ukarabati.

Kwa hiyo, kwanza llani imetuagiza tuzifanyie ukarabati barabara zile; pili, tuzitengeneze barabra nyingine mpya; na tatu, tuzifanyie upembusi yakinifu. Kwa hiyo, kuna makundi haya matatu makubwa. Sasa tulivyoanzisha mwaka huu wa fedha uliokwisha 2013; huu mpango wa matokeo makubwa sasa, tumeweka miradi 25 inayohusiana na barabara. Kwanza, tunataka tushughulikie miradi inayoondoa msongamano wa Bandari ya Dar es Salaam ili kufungua uchumi wa nchi. (*Makof*)

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[NAIBU WAZIRI WA UJENZI]

Kwa hiyo, miradi yote inayoanzia Dar es Salaam Bandarini mpaka kuunganisha na nchi jirani, ukianzia na *central corridor*, ndio tumeweka kipaumbele. Kwa sasa hivi tunataka tupanue barabara, kwa mfano kuanzia bandarini pale mpaka Tazara, badala ya kuwa njia mbili ziwe njia tatu. Kwa hiyo, tunasema ni njia sita. Halafu kutoka pale *TAZARA* mpaka *Air port*, pia tunapanua zinakuwa tatu tatu kila upande.

Kutoka pale *airport* kwenda mpaka Pugu, tunapanua kuwa njia sita vilevile. Ukitoka Pugu unaunganisha na *Morogoro Road*, nayo tunakwenda na njia sita; halafu ukitoka pale Mbezi unaunganisha na Bunju hii njia ya Kawe kwenda Bagamoyo nayo tunapanua kwa njia sita. (*Makofi*)

Kwa hiyo, unakuta kwamba, barabara hii pamoja na *ku-congest* Bandari ya Dar es Salaam, lakini pia utapunguza msongamano wa Dar es Salaam, kwa maana ya kwamba magari mengine yataweza kwenda *Airport*, hayana haja ya kupita katikati ya Mji. Hilo la msongamano wa Jiji la Dar es Salaam Waheshimiwa Wabunge wamelisema kwa nguvu sana, tunaafiki ni kweli msongamano upo lakini Serikali imeshaanza kuchukua hatua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hii miradi ambayo inaendelea, mradi wa mabasi yanaoyoenda kwa kasi, ni mojawapo katika miradi ambayo tutapunguza msongamano. Lakini pia Japan wamekubali kujenga *fly over* pale *TAZARA*, Japan pia wamekubali kujenga *fly over* nyingine ya Ubungo. Tunaendelea na mipango ya kujenga *fly over* ya pale Magomeni, Morocco na pia Wachina wamekubali kufadhili ili kupanua *Surrender Bridge*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naamini kabisa kwa maana ya msongamano wa Dar es Salaam, hatua zipo na tumeweka kwenye *big results*, naamini kabisa tunahitaji rasilimali fedha kama Shilingi billioni 531, kuweza kutekeleza miradi ya *Big Results*. Tunapozungumza habari za fursa za kuichumi, kuna wengine wamezungumza kwamba tungefanya barabara chache, lakini naamini kabisa

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[NAIBU WAZIRI WA UJENZI]

tumetengeneza nchi hii katika Kanda tisa kuunganisha. Maana barabara huwezi ukatengeneza kipande kimoja halafu ukaacha kipande kingine. Tunazungumza maisha bora kwa kila Mtanzania, maana yake kila mmoja apate fursa za kiuchumi na kijamii. (*Makofii*)

Kwa hiyo, kuna barabara nyingine inawezekana hawalimi, lakini wanafuga, au pengine kuna hospitali kubwa. Kwa hiyo, kila mahali unakuta barabara ni muhimu ijengwe. Ndiyo, maana unakuta tumeshika nchi nzima. Kama kuna eneo ambalo unadhani kuna Watanzania wengi mmepongeza ni katika Sekta ya Barabara kwamba tunafanya vizuri.

Naomba mtuunge mkono ili tuweze kuendelea na mipango hii iliyopo. Tunataka tuunganishe Mikoa yote ya Tanzania kwa barabara za lami za uhakika na hivyo kazi inaendelea kwa kasi kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna barabara zinazounganisha nchi jirani. Hizo pia ziko kwenye mpango katika hizi kilomita 11,174 zinazoendelea, na tumeziweka kwenye mpango na zinashughulikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nijibu baadhi ya hoja ambazo Waheshimiwa Wabunge wamekuwa wakichangia. Nianze na suala la msongamano wa Dar es Salaam nimeshalielezea. Lakini niseme habar ya barabara ya ndungu Somanga naona Waheshimiwa wawili, watatu wamezungumza kwa uchungu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli barabara ya Ndunu – Somanga, mkandarasi huyu amesuasua lakini kimkataba, tulimpa mpaka Desemba, 2013 kumaliza. Mpaka sasa kilometra 40 za rami ameshamaliza kati ya kilometra 60. Yaani ukichukua *over roll progress* ya Mkandarasi yule, amefikia asilimia 90% ya Mkataba ule. Naamini kabisa kazi hii itakwisha. Kwa sababu asipomaliza, ikifika Desemba

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[NAIBU WAZIRI WA UJENZI]

tutaanza kumkata *liquidated damages*. Maana tunatoza tozo kwa ucheleweshaji wa kazi hiyo.

Eneo lingine ambalo Mheshimiwa Mbunge mmoja amezungumzia ni suala la kupunguza Mfuko wa Barabara kuchangia huduma za reli. Naomba niwarejeshe kwamba, sheria inasema kwamba, fedha ambazo zinatengwa kwa ajili ya Mfuko wa Barabara zinakuwa ni kwa ajili ya Mfuko wa Barabara, hakuna vinginevyo.

Naomba sana kama kuna mawazo mapya ya kutaka fedha hizo ziingie kwenye mfuko mwengine, basi ni suala la kubadilisha sheria hii.

Waheshimiwa wengine wamezungumzia habari za barabara za Mikoa. Mimi niwahakikishie kwamba, kwa sababu tuna fedha za Mfuko wa Barabara, kazi yake kubwa ni kufanya matengenezo. Asilimia 90% ya fedha za Mfuko wa Barabara ni kufanya matengenezo, asilimia kumi ni miradi ya maendeleo.

Kwa hiyo, pamoja na hizi kilometra 11,000 tulizozungumza kuna baadhi ya maeneo katika Mikoa tunajenga barabara za lami kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara, ile asilimia kumi ambayo imeruhusisha kisheria, lakini kwa sehemu kubwa tunataka fedha hizi zifanye kazi ya matengenezo. Kuna baadhi ya Wilaya bahati nzuri niseme hapa kwamba, fedha za Mfuko wa Barabara wamezitumia kwa kazi ambayo siyo ya barabara.

Sasa kwa mfano umeweuka fedha barabara halafu unakuta mtu anazitumia fedha zile kwa kuendea semina ambayo haihusiani na barabara, hiyo kitu hairuhusiwi.

Kwa hiyo, hiyo naomba tukubaliane kwamba fedha za mfuko zitumike kwa ajili ya barabara ili wananchi wote waweze kufaidika kwa maendeleo ya kazi ambayo inaendelea. (*Makof!*)

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[NAIBU WAZIRI WA UJENZI]

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii ya Mpango wa Maendeleo. Naomba sana tufikirie kikubwa ili nchi yetu iweze kwenda haraka katika kunusuru maendeleo ya nchi hii. Ahsante. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Sasa namwita Naibu Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, Mheshimiwa Adam Malima.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu na nikushukuru wewe kwa kuniruhusu kuchangia hoja hii kwa niaba ya Waziri wa Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitambue nafasi ya pekee na michango ya Waheshimiwa Wabunge ambayo mingi sana imejikita kwenye suala la kilimo hasa kwa kutambua nafasi ya pekee ya kilimo na wadau wake katika maendeleo na mustakabali wa Taifa hili kwa leo na kwa huko mbele tunakokwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuzielezea hoja hizi vizuri, natarajia kwamba Mheshimiwa Waziri wa Nchi atazifafanua baadaye zaidi. Naomba tu kusema kwamba, kila mara tunapozungumza, tunasema Tanzania *is an agricultural based country*; na zipo nchi za namna tatu; kuna *agricultural based*, kuna *transforming countries* na kuna *organized*. Sisi Tanzania *is an agricultural based*. Sasa sisi tukisema *as an agricultural based country, we have 70% of our population*, yaani asilimia sabini na zaidi ya Watanzania ambao wanategemea moja kwa moja uchumi wao kwenye Sekta ya Kilimo.

Sasa kwa upande wa Tanzania kimahesabu, kwa watu milioni 45 walioko leo, tunachosema ni kwamba watu milioni 32, wanategemea uhai wao kutokana na uchumi huu wa kilimo. Kwa maana hiyo, ifikapo mwaka 2025, tukisema tutakuwa na Watanzania milioni 60, Watanzania milioni 42 watakuwa wanategemea Sekta ya Kilimo moja kwa moja. Maana yake nini?

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHRIKA]

Maana yake ni kwamba, kwa wale milioni 42 wanaozalisha kwa ajili ya milioni 60 wote, ni lazima maandalizi yao yaanze kufanyika leo. Maandalizi ya kwenda huko mbele ya kuhakikisha kwamba nchi yetu hii, *is self sustaining country* kwa maana ya chakula, yanaanza kwa mipango kama hii ambayo Serikali na Tume ya mipango wameileta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme jambo moja; katika michango ya Wabunge, mimi najua kabisa, nimeiangalia ile hotuba ya Mpango wenyeewe, ule Mwongozo wa Mpango ukurasa 51 unatoa vipaumbele, unatoa na changamoto zilizokuwepo.

Nilichoewa mimi, ni kwamba Waheshimiwa Wabunge walikuwa wanasesma, pamoja na maelezo yale yaliyokuwemo kwenye vitabu, lakini maelezo yale yalikuwa yanaonekana kama *business as usual*; kama maelezo ambayo wamesoma kwenye mipango ya mwaka jana na mwaka juzi na mwaka majuzi.

Waheshimiwa Wabunge, walikuwa wanataka maelezo ya kina zaidi ili utekelezaji wa mipango hii uende ukufaishe wakulima na Watanzania moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme tu kwamba nimeilewa ile tafisiri, kwa sababu kwenye uchumi mwaka 1992, *Norman Lamont* Chancellor of *Shark* wa Uingereza, aliambiwa pamoja na kwamba, uchumi wetu unakua, hatuoni Waingereza.

Sasa Eddie George akiwa Gavana wa *Bank of England*, wakabaini usemi unasema: "*a feel good factor.*" Kwa hiyo, Watanzania pamoja na kwamba wanatudai kwamba uchumi wetu unakua, sasa wanataka kuiona ile *feel good factor.* (*Makof*)

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[NAIBUWAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA]

Kama asilimia 70 ya Watanzania wako kwenye kilimo, lazima mipango yetu hii ijielekeze kwenye kutafuta ufumbuzi wa namna ya kuwapa Watanzania hawa *feel good factor* ya kuona kwamba maendeleo haya na wao kule chini yanawafikia. Kwa hiyo, hayo tunayapokea kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge na tumekaa na wenzetu wa upande wa Tume ya Mipango na Wizara ya Fedha, Jumamosi na jana Jumapili, tumekubaliana kwamba mipango hii pamoja na utekelezaji wake izingatie haya kwa sababu ndiyo Wabunge wamedai kwa niaba ya Watanzania. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo lazima tuliweke mbele katika kutathmini kilimo cha Tanzania, ni kwamba kilimo cha Tanzania ni *small holder farming* ambayo kwa kiasi kikubwa, mkulima wa Tanzania ni mwanamke. Mwanamke ndiyo mhimili wa kilimo cha Tanzania na kwa maana hiyo mwanamke ndiyo mhimili wa uchumi wa Tanzania, *it is the fact.* (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo ambalo tumelizungumza na tumekubaliana kwamba ni lazima twende tukatengeneze mikakati ya makusudi kwamba ile mikakati ya msingi, ambayo inabadilisha kilimo, kwa maana ya *transforming agriculture, access to finance* (uwezeshaji), lazima iwe na nafasi maalum ya kuzingatia mchangi wa mwanamke na vijana ili huko mbele tutakakokwenda tusiwe kama tunakwenda kama vipofu tu tunaongozwa, hilo jambo moja. Kwa maana hiyo, tunakamilisha kwa mwaka huu suala la Benki ya Kilimo na pawe na *window* maalum kwa ajili ya vikundi vyा akina mama na vyा vijana. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni miundombinu, hatuwezi kutoka hapa tulipokuwa bila ya kuwa na miundombinu maalum ya kilimo na kwa Serikali hii, jamani tukubaliane wanaosema, wanaobeza kama hamtaki kuona, ndiyo hivyo tutafanyaje, lakini kuna suala la *Rural Roads, Rural Energy, Rural Water*, miradi ya *irrigation* inatusumbua kwa sababu kwa kiasi kikubwa miradi ya umwagiliaji imekuwa haipati usimamizi mzuri. Tumepitisha Sheria Bunge liliopita na ninyi wenyewe Wabunge mmeridhia,

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

*[NAIBUWAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA]*

tunapitisha mradi wa umwagiliaji wa shilingi bilioni moja, halafu bado haufanyi kazi, lazima mtu awajibike kwa sababu zile ni fedha za umma. Sasa kwa utaratibu huu, tunakubaliana kwamba mpango huu unaweka mikakati ambayo inapewa nguvu ya kisheria ya kuhakikisha kwamba mikakati yetu ya kilimo inapata utekelezaji mzuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala lingine ambalo limezungumzwa, nalo ni suala la masoko ya mazao. Wakulima wamezungumza kwa uchungu kwamba saa nyingine tunapitisha mikakati, wakulima wanahamasika, wanalima, wanazalisha zaidi lakini mazao yanakuwa hayapati soko. Haya yanaendana na yale mawili, kwa maana ya uwezeshaji, ambao siyo suala la uwezeshaji tu kwa wakulima wakubwa lakini pia, mpango huu unataka kujikita ili hii sekta ya fedha iwe na uwezo wa kuwafikia wakulima wa kat. Hata hivyo, suala la masoko, lina Wizara mbili sasa, lina Wizara ya Viwanda na Biashara na sisi Kilimo, Chakula na Ushirika, tumekubaliana kwamba tulitengenezee mkakati maalum ili masoko ya mazao ya kilimo isiwe ni tatizo tena kwa wakulima. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo Waheshimiwa Wabunge wamelizingumzia na tumelisikia, ni suala la kuhakikisha kwamba wakulima wanahamasika kweli. Kwa mfano, kama sasa hivi tunajua tuna tatizo kubwa la ushirika, ambapo kwenye maeneo mengi ushirika umechangia kudumaza hamasa ya kilimo kuzalisha zaidi kwa maana ya *surplus*. Mtu anazalisha kile kinachomwezesha yeye tu kula na familia yake, hazalishi zaidi, kwa sababu hana motisha, anazalisha na ushirika unamuumiza. Tumepitisha Sheria ya Ushirika hapa na sasa tumekubaliana kabisa kwamba katika misingi hii, ushirika hautatumika tena kama chaka la watu kuhujumu wakulima. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, katika yale ya jumla ambayo nilitaka kuyasema ni *access to technology*. Hakuna mabadiliko ya kilimo yasiyozingatia mchango wa sayansi kwenye kilimo. Tumefika hatua, tuna watu kwa makusudi wanahamasisha watu kutumia mbegu mbovu,

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[NAIBUWAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA]

dawa za ajabuajabu, kwa sababu wao wana misingi ya biashara mle ndani. Tuna watu ambao kwa sasa hivi kwa mfano kwa zao la korosho, kama dunia nzima wanatumia *sulphur* ya maji, dawa ya maji ya kupulizia, sisi bado tunatumia *sulphurya* unga. Dunia nzima wanatumia pamba *hybrid*, sisi bado mpaka leo tunataka tutumie mbegu zile za pamba za kienyeji na watu wanataka kuandamana Kahama, Shinyanga kwa sababu ya kutumia mbegu hizo wakati mbegu hizo ziliachwa kutumiwa huko duniani miaka zaidi ya 40 niliyopita. Haya ni mambo ambayo lazima tukubaliane ndugu zangu, kwamba sisi kama ni nchi ambayo ni *agricultural based* na uchumi wetu unaegemea hapo, lazima tutengeneze utaratibu wa kuhakikisha kwamba sayansi inakuwa ni msingi wa maendeleo ya kilimo na hakuna maendeleo ya kilimo bila utafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tulichosema, ni kwamba kwa kiasi kikubwa kwenye mpango huu, utatenga kiasi cha fedha maalum kabisa ambazo zitakwenda kwa ajili ya utafiti na ugani, kwa maana ya kuwapatia wakulima wa Tanzania elimu ya kilimo cha kisasa. Hatuwezi kuendelea, hata kama mtu unalima na jembe la mkono, lakini bado kuna vitu vya msingi ambavyo vinakuwezesha kutoka kwenye gunia nne kwa eka moja ya mahindi, kwenda kwenye gunia 20, wakati wenzetu duniani wanalima mpaka gunia 40.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, haya ndiyo mambo tunataka tupeleke na mpango huu kwa kiasi kikubwa unaunga mkono haya na Waheshimiwa Wabunge mmesisitiza kwamba pawe na mabadiliko makubwa katika Kilimo cha Tanzania. Naomba niseme tu kwamba pia katika Serikali ni mkakati wa kuondokana na huu ukuaji wa asilimia 4.3 kila mwaka, twende kwenye wastani wa ukuaji wa asilimia sita katika sekta ya kilimo. Tukifika hapo, tuna matarajio kwamba wakulima walio wengi, wale asilimia 70, watafikiwa na maendeleo haya kwa maana ya ile *feel good factor* ambayo tunaitarajia, kila mtu aone kwamba tunavyokwenda uchumi unakua lakini na sisi wote kwa pamoja tunakua.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[NAIBUWAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKI]

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako mambo ambayo lazima tufanye na ninaomba niwasihii Waheshimiwa Wabunge, kwenye mpango huu utakaokuja, kuna mambo kwenye kilimo lazima yatabadilika, kwa mfano, suala la pembejeo, mwaka huu tumeweka shilingi bilioni 120 lakini tumefikia kaya laki laki nane, lakini fikra ni kufikia kaya milioni mbili. Ili tufikie kaya milioni mbili, lazima tuweke zaidi ya shilingi bilioni 200, lakini tukiweka shilingi bilioni 200 kwenye pembejeo, maana yake lazima tutoe shilingi bilioni 100 kwenye kitu kingine, *that is the art of budgeting*. Kwa hiyo, naomba niwasihii tu Waheshimiwa Wabunge kwamba tumesikia vipaumbele vyao lakini tutakapofika mwezi wa pili na hiyo rasimu itakapokuja, tutambue kwamba kupanga ni kuchagua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Profesa Anna Tibaijuka, dakika ni 10.

### **WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA**

**MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza kabisa, naomba nimpongeze mtoa hoja kwa mpango mzuri ambao tumeuona hapa mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa sekta ya ardhi nichangie tu kwa kusema kwamba na sisi tumejipanga, hasa kuziwezesha zile sekta ambazo zina kipaumbele katika kutekeleza mpango huu ambao uko mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sekta ya ardhi ambayo ni sekta mtambuka, ni wazi kwamba watekelezaji wengi, sekta mbalimbali inakuwa vigumu kwenda mbele bila sisi kuwa tumeshawawezesha kufanya hivyo. Kwa hiyo, tulivyojipanga sisi, tunaangalia ardhi kwa misingi mitatu. Kwanza, kuna ardhi za vijiji, ambazo pia hujumuisha ardhi za hifadhi. Tatizo kubwa ambalo totalishughulikia katika mwaka huu, ni kujaribu kuondokana na migogoro ya ardhi. Wachangiaji wengi hapa wamegusia, kwa sababu kunakuwepo na mgongano, *pressure* ya matumizi ya ardhi

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI]

kati ya wakulima na wafugaji, kati ya hifadhi na wakulima na kati ya watumiaji mbalimbali wa ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu tumejaliwa ardhi kubwa, lakini pia kama wote tunavyotambua, Mwenyezi Mungu pia ametujalia sisi wenyewe tunaendelea kuongezeka. Kwa hiyo, kila mwaka tutakuwa tunaona kwamba kuna *pressure* ya ardhi, eneo linakuwa dogo, sisi tunaongezeka, lakini ardhi haiongezeki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sekta ya kilimo kama alivyomaliza kuchangia Mheshimiwa Malima hapa, tunahimiza sana utumiaji wa kisasa wa ardhi. Sisi kama wapangaji wa ardhi, tunatambua matumizi bora ya ardhi, lakini tunapopanga matumizi bora ya ardhi, hapohapo tunahimiza uhifadhi wa ardhi, lakini pia teknolojia na mapinduzi ya kilimo na ufugaji. Hasahasa, nikijikita kwenye sekta ya ufugaji, jambo ambalo tumelizungumza sana katika Bunge hili ni kwamba ufugaji wa sasa hivi, kwa sisi kama wapangaji wa matumizi ya ardhi, tunahimiza ufugaji wa kisasa. Ufugaji wa kuhamahama, unaanza kuitwa na wakati. Ni jambo gumu sana lakini bila kulitambua hili, itakuwa vigumu kuondokana na migogoro ya ardhi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naposema umepitwa na wakati sina maana kwamba tuache kufuga, lakini nina maana kwamba tuache kuhama na mifugo. Sasa hivi, asilimia 70 ya kitoweo tunakipata kwenye mifugo ambayo haihami. Asilimia 70 ya nyama inayouzwa Tanzania haitokani na wafugaji wanaohamahama au *pastoralists*, inatokama na *mixed farmers* yaani wale wakulima mseto, wanakuwa na mifugo, wanakuwa na mazao, hao ndiyo tunawategemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunafanya kazi kwa karibu sana kama sekta mtambuka na wenzetu katika Wizara ya Mifugo, kuboresha nyasi. Ili ufuge bila kuhama, lazima ufanye mambo matatu. Lazima uwe na maji ya kutosha pale ulipo, ni lazima uzuie magonjwa ya mifugo na pia lazima uwe malisho yaliyoboreshwa. Sasa ukishafanya

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI]*

mambo hayo matatu, huna tena haja ya kufugafuga, utakuta heka moja ya malisho inaweza sasa kubebe ng'ombe wengi zaidi, inaitwa *carrying capacity*. Katika jambo hili tunajikita hasa kwa kutoa elimu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine ambacho tumejikita nacho sasa ni *tension* au tuseme migogoro kati ya Miji inayokua, matumizi ya makazi na ya wakulima. Sehemu nydingi za Miji inakua kwa kasi, Mji kama wa Dar es Salaam unakua kwa kasi na sasa hivi ndiyo tuna mpango wetu Kabambe wa Mji Mpya wa Kigamboni. Mji Mpya wa Kigamboni tumeupa kipaumbele kabisa na tunapiga hatua nzuri. Katika Mji Mpya wa Kigamboni tunatarajia kwamba tutaweza kuongeza wakazi wa Kigamboni kutoka takribani 100,000 tulio nao sasa hivi tunatarajia kufikisha watu kama laki nane au milioni moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kusudi uweze kuwa na Mji wa watu milioni moja, ni lazima upange Makazi vizuri, lakini upangajji Mji siyo Kigamboni tu, ni Tanzania nzima. Kwa hiyo, Wizara inaweka kipaumbele kwa *Dar es Salaam Master Plan*. Tunataka Mji yote mikubwa iwe na *master plan*. Sasa hivi tumejitahidi, Halmashauri zimejitahidi kupima viwanja lakini maelekezo tuliyotoa ni kwamba ukipima viwanja bila kuwa na *master plan*, unakosea maana yake unaweza ukafanya makosa ukajikuta kwamba bomoabomoa haitaisha. Kwa hiyo, suala la kupanga makazi linakuwa jambo muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wachangiaji wengi wamezungumzia mambo *specific*, hapa yamesemwa katika Bunge kwa mfano, mchangiaji kutoka Tanga, kuna suala la mashamba ya Mkoa wa Tanga, ambayo kusema kweli katika Mikoa yote ya Tanzania yenye mashamba makubwa Tanga inaongoza na wananchi wa Tanga wala siyo siri, wengi wao wanahitaji ardhi hizi zirejeshwe kwao kusudi waweze kuzitumia. Mchakato wa kurejesha ardhi hizi unaendelea, tulipofikia tunahitaji habari zaidi kutoka kwa Halmshauri na Wilaya mbalimbali za Tanga ili tuweze kwenda mbele. Kuna

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI]

mashamba mawili ambayo sasa hivi tumeshafikisha kwa Mheshimiwa Rais, tunasubiri uhaulishaji. Kwa mfano, Shamba la *New Korogwena Kibaranga Farm*, hili liko Muheza. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu nyingine nyingi ambapo tumekuta pia migogoro kati ya wakulima na hifadhi, nadhani mnaona na sisi tunafanya kazi pamoja na wenzetu wa Maliasili kuhakikisha kwamba hifadhi itakuwa ya binadamu lakini pia hifadhi ya wanyama. Kwa hiyo, katika matumizi ya ardhi sisi tunatafuta *balance* kwamba kila kitu ni cha lazima, lakini lazima zaidi wananchi wawe na ardhi ya kutumia. Sasa wananchi hawawezi kuwa na ardhi ya kutumia kama wenyewe pia hawaendi mbele, hawaendi na teknolojia. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sekta yetu ingawaje sisi siyo *core sector* katika *Big Results Now*, lakini sasa hivi tumekaribishwa na Mheshimiwa Rais kuingia katika Baraza la utekelezaji la *Big Results Now*. Hii ni kutohana na kutambua kwamba bila matumizi ya ardhi kupangwa, bila mipango ya ardhi kuwepo, itakuwa vigumu kwenda kwa kasi ambayo tunaihitaji. Katika hili, niseme kwamba sasa hivi tunajaribu kufanya kazi na sekta nyingine hasa za miundombinu na uchukuzi tuwe tunapanga kwa pamoja. Kwa sababu tusipopanga kwa pamoja, wakati mwingine unaweza kujikuta uko kwenye juhudhi bila maarifa. Kwa mfano, katika sekta ya usafirishaji, kuhakikisha kwamba tunapopanga barabara, zitakidhi viwango? Nimefurahi sana kusikia wachangiaji wengi leo mkizungumzia sekta ya reli. Sisi tunatambua kwamba pia sekta ya reli itatusaidia, kwa sababu barabara zinachukua sehemu kubwa ya ardhi. Kuna sehemu nyingine ambapo ukifika, unakuta ni milima na kadhalika inaweza kuwa vigumu kuitisha barabara kubwa zinazotosha. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kwamba Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, suala la nyumba hatujalisahu. Shirika letu la Nyumba linaendelea lakini mimi hapa ni Waziri wa Nyumba, siyo Waziri wa *National Housing*. Kwa hiyo, tunahimiza sana Halmashauri sasa hivi

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI]

kupanua mawazo na kwenda mbele ya *National Housing* kwamba Halmashauri zetu zihimizwe kuwa na *Council Housing*. Huwezi kutatua, huwezi kuwa na makazi bora kama unategemea Shirika moja. Kwa hiyo, katika sekta ya ardhi utaona kwamba mwaka huu tutakuwa tunaboresha nyumba zetu za tembe, hizi za kienyeji, tuwe na nyumba bora na hizi hazitaweza kujengwa na Shirika la Nyumba ambalo linaendelea kufanya kazi nzuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, suala la fidia. Wizara ya Ardhi imejikita katika kuleta fidia endelevu. Sisi hatutaki fidia ambayo ...

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)*

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Sasa tumwite Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe.

**WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza, naunga mkono hoja na vilevile nianze kwa kumpa pole mdogo wangu mpendwa Mheshimiwa Joseph Mbilinyi, Mbunge wa Mbeya Mjini. Amedai *ambulance* kwa miaka mitatu bila mafanikio, hata mimi kaka yake Mbunge wa Kyela nilidai *ambulance* kwa miaka kama mitatu bila mafanikio lakini nikagundua Serikali ina mambo mengi ya kuhudumia, nikajinyima kidogo, nimenunua *Noah*, nimeikabidhi Hospitali ya Wilaya ya Kyela. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, huo ni ushauri wa bure tu. Ubunge si kufoka tu, kulalama na kulaumu, tenda. Hata ukinunua Bajaji mbili, nina uhakika kabisa wana Mbeya Mjini watathamini mchango huo kuliko ngonjera za kulalama. (*Makofii*)

**MBUNGE FULANI:** Safii!

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

**WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Anna Abdallah, anataka kujua kwa nini ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Mtwara haujitokezi katika mpango huu. Naomba tu niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba kutokana na shughuli ambazo zinafanyika Kusini mwa Tanzania, Kiwanja cha Ndege cha Mtwara, tutakijenga na kitakuwa Kiwanja cha Kimataifa chenyе ukubwa sawa na Kiwanja cha Julius Nyerere na ujenzi kama mambo yote yataenda vizuri utaanza mwaka ujao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari tuna Kampuni kubwa ya Kichina inaitwa *AVIC International*/kisherikiana na Kampuni ya Shapriya ya Tanzania, wameshafanya *feasibility study* kwa fedha yao wenyewe na vilevile *preliminary design*. Vyanzo vyta fedha ya ujenzi vimeainishwa, kuna Mashirika makubwa mawili ya Bima tayari yamejitokeza kudhamini mkopo huo, *SINO SURE* ya China na *ATI* ya Afrika. Kazi ya kitalaam inayoendelea sasa hivi ni kuhakikisha kuwa fedha ya mkopo kwa mradi huo inaendana na mahitaji yetu na vipaumbele vyetu na vilevile ina masharti nafuu yanayobebeka.

Mheshimiwa Sylvester Mabumba, anaishauri Serikali kukipanua Kiwanja cha Ndege cha Kigoma ili kihudumie na nchi za jirani. Kiwanja cha Ndege cha Kigoma, pengine kwa faida ya Waheshimiwa Wabunge, ni mionganii mwa viwanja saba, ambavyo tulishavifanyia upembizi yakinifu na usanifu wa kina kutokana na fedha ambayo tulikopa kidogo Benki ya Dunia kama dola laki nane na dola laki nne tukatoa sisi wenyewe. Ni Kiwanja ambacho kipo pamoja na viwanja vingine vyta Arusha, Bukoba, Shinyanga, Sumbawanga, Tabora, ambavyo viko katika ngazi mbalimbali ya utekelezaji, lakini Kiwanja cha Mafia ambacho kipo kwenye kundi hilihili vilevile, chenyewe tumeshamaliza kimeanza kupokea ndege. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulishaanza ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kigoma, ambacho *runway* yake ingekuwa mita 1800, kwa kuweza kupokea ndege ndogo za katikati, lakini kutokana na hoja hizo za Waheshimiwa Wabunge na ukweli kwamba Kigoma imekaa mahali

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[WAZIRI WA UCHUKUZI]

ambapo inaweza kuwa kiungo muhimu katika usafiri wa anga ukanda wa Afrika Mashariki na Kati, Serikali ikaamua kurefusha *runway* ya Kigoma kwa mita zaidi ya 1300, ili kiwanja hicho sasa kiwe na barabara ya kurukia na kutua ndege yenye urefu wa mita 3,100 kuwezesha ndege kubwa aina ya *Boeing, Embraer, Airbus* yenye kubeba abiria zaidi ya 150 kutua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapema mwaka huu Benki ya Dunia ilikubali kutupa pesa Dola Milioni tisa ili tuweze kurefusha hicho kiwanja kwa hiyo mita 1300 na wakatupa masharti ya kwamba ifikapo mwezi Machi, tuwe tumeishawalipa wananchi wa Kigoma fidia ya shilingi bilioni moja 1.5. Tukajitahidi, tumelipa hiyo pesa na Benki ya Dunia ikatuma ujumbe wake Kigoma kwenda kuhakikisha kama fidia ililipwa. Tuliwapokea kwa shangwe nyangi lakini pakatokea maandamano mafupi pale yaklongozwa na kijana mmoja anayeitwa kwa jina la Bukumbura, wakidai wamepunjwa. Vijana wenyewe tulikuja kugundua hawana hata viwanja pale, kwa kutegemea tu kwamba Benki ya Dunia ni Benki ya Dunia inaweza ikawa na pesa za ziada. Benki ya Dunia ime-withdraw pesa yake kwenye mradi huo, kwa hiyo, Kiwanja cha Ndege cha Kigoma, kitabakia mita 1,800 kutokana na hayo maandamano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii kumpongeza sana Mkuu wa Mkoa wa Kigoma – Kanali Mstaafu Machibya. Yeye ilimuuma sana, nani ametushika shati huyo, akamtafuta huyo kijana lakini baadaye akaamua kumpekuwa, akagundua huyo kijana anatumia majina matatu. Yeye ni Bukumbura *a.k.a.* Erick Fundi Rugeze, *a.k.a.* Eric Nyandwi na kwamba kiongozi huyo wa maandamano ya siku hiyo siyo raia wa Tanzania ila raia wa Burundi. Tumempeleka Mahakamani, siwezi kuendelea zaidi ya hapo lakini *runway* ya Kigoma itabakia mita 1,800, tutakapopata pesa baadaye tutaongeza. (*Makofi*)

Mchungaji Peter Msingwa na Mheshimiwa Rita Kabati, wanataka ukarabati wa Kiwanja cha Ndege cha Nduli, kilichopo Iringa, uonekane kwenye Mpango. Mbona suala

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[WAZIRI WA UCHUKUZI]

hili tumeshalieleza mara nyingi sana hapa Bungeni kwamba tumeshapata fedha kutoka Benki ya Dunia na sasa hivi tumeshapata *approval*, tumeshaanza tayari upembuzi yakinifu katika viwanja 10 vilivyopo nchini ambavyo tutaanza ndani ya mwaka huu wa fedha na *immediately there after* tuanze ujenzi wa viwanja hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanja hivyo mbali na kiwanja cha Nduli cha Iringa, tuna Kiwanja cha Musoma, sijui kama Mheshimiwa Dkt. Kebwe, yupo, unasikia hapo? Tuna *Lake Manyara*, tuna Moshi, tuna Tanga, Mheshimiwa Stephen Ngonyani unasikia hilo? Tuna Lindi, tuna Kilwa Masoko, tuna Songea, tuna Njombe na Singida. Kwa sababu za kimsingi kabisa, tumeingiza vilevile kiwanja cha ndege ya Simiyu kwenye mchakato huu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Deogratius Ntukamazina, anataka Shirika la Ndege la *ATCL* ianze sasa kuruka na ameenda mbali kwa kusema nchi ndogo kama Rwanda inawezaje kuwa na ndege nyingi na sisi hatuna? Nataka kusema kwamba kupanga ni kuchagua, sisi na jirani zetu hao unaowataja wote tulipata pesa kutoka *African Development Bank (ADB)*. Wenzetu waliamua kununua ndege, sisi tukaamua kujenga barabara kutoka Iringa kuja Dodoma na kutoka Minjingu kwenda Singida. Kwa hiyo, baadaye tutanunua tu hizo ndege. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la *ATCL*, wameliongelea wengi, kwa upande wa Serikali, kazi kubwa kwanzia ni kusafisha mizania ya *ATCL* na tumeshafanya hivyo. Sasa hivi *ATCL* inapendeza kweli na inawatamanisha watu wengi ndani na nje ya nchi, wanataka sasa ubia na *ATCL*. Kwa sasa tuna mazungumzo na Kampuni moja ya Oman na vilevile tuna mazungumzo na Kampuni kubwa ya China ya Ndege ya *AVIC International* na tutawataarifu matokeo ya majadiliano haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Eugen Mwaiposya, Mheshimiwa Dkt. Kebwe, Mheshimiwa Ngonyani, Mheshimiwa Dkt. Kikwembe, Mheshimiwa Peter Serukamba,

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[WAZIRI WA UCHUKUZI]

Mheshimiwa Ismail Aden Rage, Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mheshimiwa Masele na Mheshimiwa Kakoso na wengine, wemeongelea sana suala la reli. Naomba niwajibu kwa ujumla kwamba, ukiachia reli ya TAZARA, tunao mtandao wa reli wenye urefu wa kilometra 2,707 na madaraja 5,123. Vyote hivi vina umri wa miaka 108. Tumeanza kazi kubwa kama *short measures* kuondoa hizo reli zilizochakaa na kuweka mpya. Mpaka sasa tumeweza kutandika reli mpya kilometra 634, tumejenga madaraja mapya yanayoweza kuhimili mzigo mkubwa zaidi ya madaraja 183. Tunao pia mpango wa muda mrefu nao ni kujenga reli kuanzia Dar es Salaam mpaka mpakani mwa Rwanda na Burundi kwa *standard gauge*, upana zaidi ili iweze kubeba mzigo zaidi na iweze kuwa na kasi zaidi. Tumedhamiria vilevile kubadilisha mtandao mzima wa reli ya kati kwenda kwenye *standard gauge*. Gharama za mradi huu ni dola za Kimarekani bilioni tano, tunaongea na wawekezaji mbalimbali kama vile China, Japan na Marekani kuhusu ujenzi wa reli hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, reli ya Tanga mpaka Musoma yenye kilometra 1038 na reli ya Mtwara mpaka Mbambay, imeshapata mwekezaji na mjenzi ambaye ni *China Engineering II*. Reli ya Tanga mpaka Musoma itatugharimu dola za Kimarekani bilioni 3.0 na reli ya Mtwara kwenda Mbambay itatugharimu dola za Kimarekani bilioni 3.6. Tusubiri tu haya majadiliano kwa sababu pia hii ni mikopo ambayo hatuwezi tu kuivamia bila kuangalia madhara yake kiuchumi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Gati Na.13 na 14 kuna malalamiko ya kuchelewa, Waheshimiwa Wabunge na ninyi msisahau. Katika Mkutano wa Tano, mwezi Aprili, 2013, Bunge liliagiza Wizara ya Uchukuzi kuajiri *Independent Consultant*, kuweza kupitia gharama za mradi huu, mliona kwamba ni kubwa mno. Tumefanya kazi hiyo mwishoni mwa mwaka 2012 tukaweza kupata jibu hilo. Vilevile Kampuni ya CCC iliyokuwa itakiwa ijenge hayo magati tukaiondoa tumeweka Kampuni mpya ya CHECC.

***Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)***  
**[WAZIRI WA UCHUKUZI]**

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kutoa taarifa kwamba kazi imeendelea na sasa hivi Kampuni hiyo ya CHECCimeshamaliza kile tunachokiita *Topographical Survey* na vilevile *Hydrographical Survey* ambayo imeweza kutuwezesha sasa kufahamu chini ya bahari pale kuna nini. Tumeshaonyeshwa kwamba chini ya bahari kuna mabomba ya mafuta ambayo ni lazima tuyao ndoe *immediately*, ni kazi ya kitaalam. Vilevile kwa sababu Gati Na.13 na 14 itatumika kwa meli kubwa za kisasa za *container*, kipenyo cha kugeuzi meli kubwa kwa kweli ni kidogo, inabidi tumege maeneo ya jirani kule siwezi kuyataja hapa, upenyo wetu ni mita 440 tunahitaji mita 600. Kwa hiyo, yote haya ni maandalizi na tunaweza kuanza, ni kama mchakato wa ujenzi tumeshauanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Komba suala la meli, kwa kweli tumellongelea sana, sijui nitoe ratiba. Mradi wa *DANIDA*, ujenzi wa meli mpya unaanza Juni, 2015 katika Maziwa yote matatu. Ukarabati wa *MV Serengeti*, *MV Umoja* na *MV Victoria*, unaanza Januari 2016. Vilevile tunao mradi wa South Korea ambapo ujenzi wa meli katika Maziwa yote matatu tunaanza mwaka 2014 yaani mwaka kesho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie tu kwa kusema, miradi ya miundombinu hasa reli, kwa kweli ni ya gharama kubwa sana. Nawashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa kuelewa umuhimu wa reli katika nchi yetu na kuwa tayari kujifunga mkanda kuweza kuingia katika uwekezaji huo na sisi tunaomba kuwahakikishia tu kwamba tutasimamia vizuri hii miradi na ninaelewa kabisa, Bunge hili liko tayari kutuunga mkono katika hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makof!*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, wachangiaji wamemalizika. Sasa nitamwita mtoa hoja lakini kabla a hapo inabidi tukae kama Bunge.

*(Bunge lilirudia)*

## **HOJA ZA SERIKALI**

### **Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2014/2015**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, siku ya Jumamosi, Waziri na wataalam wake walikutana na Kamati ya Bajeti kujaribu kutathmini yale miliyoyazungumza na kuona kwa namna gani inaweza kusaidia katika marekebisho ya Mpango wetu. Kwa hiyo, sasa namwita mtoa hoja, Mheshimiwa Waziri wa Nchi!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU):** Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kutoa ufanuzi kuhusu hoja ya Mapendekezo ya Mpango wa Taifa wa Maendeleo kwa Mwaka 2014/2015. Aidha, nakushukuru wewe, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa kuongoza vizuri majadiliano.

Mheshimiwa Spika, kufuatia agizo lako la Kamati ya Bajeti kukutana na Tume ya Mipango, tulikutana tarehe 2 Novemba, 2013 na kuunganisha mawazo kuhusu yaliyotiliwa mkazo katika mjadala unaoendelea. Tume ilifaidika na mjadala huo na majibu nitakayoyatoa hapa ni pamoja na maelewano yaliyopatikana baina ya Kamati ya Bajeti na Tume ya Mipango. Kwa mara nyingine, naishukuru sana Kamati ya Bajeti kwa ushirikiano.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii pia kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia hotuba hii. Jumla ya Waheshimiwa Wabunge 120 wamechangia na katika yao 72 walichangia kwa kuzungumza hapa Bungeni na Waheshimiwa Wabunge 48 wamechangia kwa maandishi. Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango, imepokea ushauri uliotolewa na itaufanyia kazi katika maandalizi ya Mpango wa Taifa wa mwaka 2014/2015. (*Makofifi*)

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU)]

Mheshimiwa Spika, vilevile naomba nitumie nafasi hii kuwashukuru sana Mawaziri na Manaibu Waziri kutoka katika sekta zinazounganisha Mpango huu kwa maelezo fasaha na ufanuzi ambao umetolewa. Wameifanya kazi yangu mimi kama Mto Hoja kuwa rahisi na naomba Waheshimiwa Wabunge wachukue maelezo yote yaliyotolewa na Mawaziri hawa, kuwa ni sehemu ya hitimisho la hoja hii.

Mheshimiwa Spika, hoja niliyoiwasilisha hapa Bungeni siyo Mpango bali ni Mapendekezo ya Mpango wa Taifa kwa mwaka 2014/2015. Hii ni kukidhi matakwa ya Kanuni ya 94 cha Kanuni za Kudumu za Bunge lako Tukufu za mwezi Aprili, 2013, linalotaka Serikali kuwasilisha mapendekezo yanayokusudiwa kutumiwa na Serikali katika kuandaa Mradi na Programu za Maendeleo, itakayo jumuishwa katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2014/2015. Lengo la kuwasilisha mapendekezo hayo, ni kupata maoni ya wananchi kuititia wawakilishi wao walioko hapa Bungeni. Kwa maneno mengine, mpango huo utakuwa shirikishi kwa njia ya kuwashirikisha Wabunge kwa maana ya kwamba mawazo wanayoyatoa hapa yanawakilishi mawazo ya wananchi. Hakuna namna ambavyo tungeweza kushirikisha vizuri zaidi kuliko hivyo.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, naomba sasa nitoe ufanuzi wa baadhi ya hoja zilizojitokeza katika mjadala. Maelezo yangu yatagawanyika katika sehemu mbili au tatu kama hivi ifuatavyo. Kwanza nitashughulika na mambo ya jumla ambayo yamejadiliwa na Wabunge wengi. Pili, nitatoa maoni mahsus yaliyotolewa na Kamati ya Bajeti au Kambi ya Upinzani. Muda ukiruhusu, nitatoa maoni na kutoa majibu kwa baadhi ya hoja mahsus zilizotolewa na Mbunge mmoja mmoja au Wabunge kadhaa lakini sina uhakika, kama muda kweli utaniruhusu.

**SPIKA:** Unayo saa moja.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA**

**URATIBU:** Mheshimiwa Spika, kitu kimoja ambacho nataka kuwaahidi Waheshimiwa Wabunge, nimeagiza Tume ya Mipango, itoe majibu kwa maswali yote nitakayotoa hapa na ambayo sitatoa ili Wabunge mgawiwe na myatumie kama rejea wakati tutakapojadili Mpango huu mwezi Juni, 2014. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sasa ni maelezo ya jumla na hoja zilizotolewa. Hoja ya kwanza ilikuwa inazungumzia juu ya mpangilio wa mapendeleko kwamba mapitio ya utekelezaji ina kurasa nyingi kuliko Mapendeleko ya Mpango kwa Mwaka 2014/2015 na kwamba Mapitio ya Utekelezaji yawasilishwe katika mfumo wa bangokitita. Katika hali ya kawaida ili kupanga vipaumbele au maeneo ya kuzingatia katika maandalizi ya Mpango, ni muhimu kuzingatia mwenendo wa uchumi wa dunia na wa kikanda, ili kujua fursa na hatua zilizopo mbele yetu na mapitio ya Hali ya Uchumi wa Taifa na hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wa miradi kwa mwaka uliotangulia na changamoto zake. Maelezo hayo, yanasaidia kuonyesha uwezo na udhaifu wetu kuelekea Mpango unaofuata. Kwa hiyo, ni maelezo muhimu kwamba huwezi kupanga Mpango bila kujua huko ulikotoka hali ilikuwaje. Kwa hiyo, inabidi lazima tuwe na kurasa ambazo zinaleza Mpango umetekelizwa namna gani, kumekuwa na changamoto zipi, ili zituwezeshe kujua huko tunakokwenda hali itakuwaje.

Mheshimiwa Spika, pamoja na umuhimu wa Sura inayorejea utekelezaji wa mwaka 2012/2013, maandalizi ya Mpango wa 2014/2015, tutazingatia ushauri wa Waheshimiwa Wabunge, kuwa na maelezo mafupi yanayoambatana na bangokitita, lenye takwimu za utekelezaji wa miradi inayoingia katika Mpango wa Maendeleo. Kwa hiyo, Mpango wetu utakaokuja Juni, 2014, utakuwa unazingatia ushauri huu wa Waheshimiwa Wabunge. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hoja ya pili, ambayo imezungumzwa na Wabunge wengi sana, inasema vipaumbele vya Mpango ni vingi mno, vipunguzwe ili kuleta

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU)]*

matokeo ya haraka. Kwanza, kipaumbele namba moja cha Mpango huu, ni kukuza uchumi. Hicho ndicho kipaumbele hasa, vingine vyote ni *sub-vipaumbele* lakini kipaumbele kikubwa ni kukuza uchumi ili ukuwaji huo utusaidie katika kujibu changamoto mbalimbali kama vile kupunguza umaskini wa wananchi. Pili, kuweka ajira kila mwaka zinazowapa ajira vijana, hayo ndiyo mambo ya msingi. Kwa sababu unapopanga Mpango, ni lazima usema ni wa nini? Unataka kupata nini, unataka ku-achieve nini. Mpango lazima uwe ni wa uchumi lakini uwe ni wa uchumi wa wananchi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, unazungumza habari ya kupunguza umaskini. Kama umaskini haupungui ni lazima tukae chini tuzungumze kwa nini haupungui na tuchukue hatua gani. Kwa maneno mengine tukuze uchumi, ili tuboreshe maisha ya wananchi wakiwemo wakulima, wafanyakazi, vijana, wanawake na makundi mengine na kuwapatia watoto wa wakulima wafanyakazi na wananchi wote elimu na afya bora zaidi. Mpango lazima ujibu hoja inayohusu maisha ya watu wa nchi hii.

Mheshimiwa Spika, wakati Mpango unaweka vipaumbele, ultazama hali ya nchi ilivyo na kubaini kwamba hatuwezi kukuza uchumi bila kuondoa vikwazo vinavyouzia ukuaji wa uchumi na hivyo kuchelewesha maendeleo ya ustawi wa wananchi na vikwazo vilivyogundulika ni kwanza miundombinu duni kama ville nishati na umeme, ambapo wote tunajua, hali ya umeme wetu huko tunakotoka na tulipo, siyo nzuri sana. Kwanza, umeme ni ghali sana na haupatikani kwa urahisi na ni watu wachache sana ndiyo wanaopata nishati ya umeme. Kwa hiyo, bado kuna tatizo katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, miundombinu ya uchukuzi ambayo Mheshimiwa Dokta Mwakyembe ameieleza vizuri hapa, reli, bandari, viwanja vyya ndege. Vilevile miundombinu ya umwagiliaji maji, pamoja na maji kwa ajili ya wananchi, ambayo kupatikana kwake kunapunguza adha na kuwapa muda zaidi wa kufanya maendeleo yao, badala ya kuishi wanayasaka maji kwa muda wa masafa marefu.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU)]

Mheshimiwa Spika, tija ndogo katika kilimo na kutegemea mvua kwa ajili ya kilimo, ni maeneo ambayo yalionekana dhahiri kuwa yana upungufu na yanahitaji mpango wa kuyaondoa pale. Ukosefu wa viwanda katika nchi ndio unaosababisha kukosekana kwa ajira na kwamba rasilimali watu vilevile ujuzi wake unahitaji kuimariswa. Tatizo lingine ni huduma hafifu za utalii, biashara na huduma za kifedha. Yote yalionekana ni matatizo ambayo yanahitaji kushughulikiwa. Ili kuondokana na hali hiyo, Mpango wa miaka mitano ulielekeza vipaumbele vitengenezwe ili kujibu matatizo hayo.

Mheshimiwa Spika, miundombinu kama bandari, reli na umeme, ikapewa kipaumbele namba moja na inaambatana na umwagiliaji na vilevile maji kwa matumizi ya wananchi. Kilimo cha mazao, mifugo na uvuvi, kikapewa kipaumbele namba mbili. Viwanda hasa vinavyoongeza thamani kwa mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi, vikapewa kipaumbele namba tatu. Rasilimali watu inayohusisha elimu, afya na kadhalika ikapewa kipaumbele namba nne na huduma za utalii biashara na fedha, zikapewa kipaumbele namba tano.

Mheshimiwa Spika, hoja kwamba vipaumbele hivi ni vingi nadhani siyo sahihi. Vipaumbele ni vitano tena vinategemeana. Reli, barabara, bandari na umeme ni lazima kwa maendeleo ya kilimo na biashara ya ndani na nje. Huwezi kuwa huna bandari, huna barabara na huna umeme lakini ukawa unategemea kilimo kitakuwa, hakiwezi kukua kwa sababu barabara ndiyo zinafikisha pembejeo kwa wakulima, barabara ndiyo zinafikisha mazao sokoni. Kwa hiyo, kama huna miundombinu hii huwezi kukuza kilimo na huwezi kukuza biashara kama una bandari lakini huna reli na huna barabara.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, unaweza ukaona jinsi vipaumbele vyenyewe vinavyohusiana. Hakuna viwanda bila umeme na bila viwanda hakuna ajira. Pia viwanda ni muhimu kwa kilimo na kilimo ni muhimu kwa upatikanaji wa malighafi kwa viwanda. Kwa hiyo, unaweza ukaona jinsi

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU)]

vipaumbele vyetu hivi vinavyoitwa vingi vilivyo na vinavyoshabihiana. Kukosekana kwa huduma nzuri za fedha kunawakosesha wazalishaji, wafanyabiashara mikopo na kudumaza uchumi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, pendekezo la Serikali hapa, siyo kupunguza vipaumbele vilivyopitishwa na Bunge lako Tukufu katika Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano mwaka 2011 badala yake tujaribu kujikita katika kupanga vizuri mtiririko wa miradi na utekelezaji katika kila kipaumbele, kuongeza jitihada za kuongeza mapato na kusimamia nidhamu ya matumizi. Mimi naamini tukisimamia nidhamu ya matumizi tutakuwa na fedha ambazo zinaweza zikasaidia kutekeleza miradi. Hili siyo mara yangu kwanza kulisema na siyo mara ya kwanza Waheshimiwa Wabunge kulisema. Nadhani tujikite katika kuona, hivi kweli fedha zetu zote zingetumika, hali yetu ingekuwaje?

Mheshimiwa Spika, wote tunajua na wote tunakubali kwamba kuna kitu kinaitwa manunuzi, kinachukua 70% na tunajua tatizo hili la mfumo wetu wa manunuzi na jinsi bei zinavyokuwa kubwa kiasi kwamba ukienda sokoni unakuta bei zipo chini lakini bei za manunuzi zipo juu. Tukiweza ku-*solve* hii *problem* na nadhani Hazina wanaijua sasa na tutasaidia nao katika ku-*solve*, inaweza ikatupa *surplus* na tukaona kumbe utekeleza unaweza ukafanyika vizuri kama fedha hizi zitakuwa *saved. (Makof)*

Mheshimiwa Spika, pendekezo la Serikali nimeshalieleza lakini pamoja na vipaumbele na miradi inayoambatana na vipaumbele, kunahitajika uwekezaji katika maeneo mengine ambayo yana uhusiano na maeneo ya kipaumbele ya kitaifa. Kwa mfano, maeneo hayo ni madiini, ardhi, nyumba, makazi na utawala bora, kwa sababu haiwezekani ukawa na vipaumbele ambavyo vinapuuza haya. Huwezi kukuza kilimo kama ardhi haikupimwa, huwezi kuondokana na mgogoro huu wa wafugaji wanagombania ardhi na wakulima bila kupima na huwezi vilevile kuwa na nchi ambayo utawala wake hauzingatii mahitaji ya wananchi na kuweka amani halafu

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU)]

ukategemea mpango utatekelezwa. Kwa hiyo, katika miundombinu na katika vipaumbele hivi, huwezi kuyaona haya lakini yana *supplement* utekelezaji wa miradi ile. Vilevile yapo mambo ambayo yalijitokeza ambayo yanachukua fedha kama ushirikiano wa kikanda, utambulisho wa taifa, Katiba Mpya na mazingira, yote ni mambo muhimu katika utekelezaji wa mpango huu. Kwa hiyo, ninachotaka ku-*urge* ni kwamba vipaumbele vipo, vinaingiliana lakini tutazame nidhamu katika matumizi, tuongeze mapato na hapo tunaweza kupiga hatua zaidi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ambayo imezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge wengi na ambayo kwa kweli hata mimi inanigusa na inanipa matatizo kidogo, ni kwamba Mpango wa Maendeleo ulenge katika kujibu matatizo ya umaskini wa Tanzania na hili ni jambo linazungumzwa sana. Wanasema uchumi unakua kwa 7% na umekuwa unakua na ukizungumza na Wachumi watakwambia uchumi wenu ni *stable* kwa sababu unakua kwa 6.5% mpaka 7% na kwa miaka kadhaa mfululizo. Kwa hiyo, kwa upande huo wa *macro*, unaweza kuona mambo ni mazuri sana. Tatizo letu lipo katika namna uchumi unavyojibu *problem* ya umaskini.

Mheshimiwa Spika, Mapendekezo ya Mpango kwa mwaka 2014 yameandaliwa kwa kuzingatia haja ya kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi lakini vilevile kupunguza umaskini. Eneo moja ambalo linaweza kutusaidia sana katika kupunguza umaskini ambalo Ndugu yangu Adam Malima amelizungumzia, ni eneo la kilimo. Ni eneo muhimu katika kukuza uchumi lakini vilevile ni eneo muhimu katika kupunguza umaskini. Katika kuendeleza kilimo, tumekaa na ndugu zetu wa kilimo, katika kutafuta jibu la swali hili na kwa kuwa Tume ndiyo inaweka rasilimali kulingana na mahitaji ya vipaumbele kwa Mpango huu, yapo mambo ambayo tumekubaliana na napenda Bunge hili lielewe tumeyaona vipi na tunataka kufanya nini.

Mheshimiwa Spika, kwanza, lazima tukuze kilimo lakini kusema hivyo tu haitoshi, tunakikuza namna gani? Una vituo

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU)]

vyatufitina ninapozungumza kilimo, naomba nitafsiriwe nazungumzia mifugo na uvuvi maana yote kwa *terminology* ni kilimo. Unakuwa na utafiti, uko ndani ya Chuo cha Utafiti lakini matokeo yake hayamfikii mkulima. Kwa hiyo, unaweza ukalipa pesa, ukatengeneza utafiti, ukaandika vitabu vikubwa kabisa lakini kama matokeo hayo ya utafiti hayafiki kwa mkulima basi mkulima atabaki hivyohivyo alivyo na matokeo ya utafiti yatabaki *separate*. Kwa hiyo, nachotaka kusema ni kwamba tumekubaliana na wenzetu wa kilimo tuunganishe suala la utafiti na huduma za ugani ili vituo vyatufitivive na uhusiano wa moja kwa moja na ugani ili maarifa yanayotoka kwenye vituo vyatufiti yaweze kuwafikia wakulima.

Mheshimiwa Spika, vilevile tumekubaliana kwamba suala la mbolea lisiwe ni suala la *Fire Bridged* kwamba wakati kilimo kinakuja lori linakimbizana na mvua kupeleka mbolea kwa wakulima. Ushauri tuliontua na tumekubaliana ni kwamba mbolea ingekuwa kama bidhaa nyingine tu kwamba wale wanaotaka kufanya biashara ya mbolea wawe na mbolea kulekule vijiji wakati wote na kwa hiyo mvua ikija itakuta mbolea iko vijijihiyo inaweza ikatusaidia. Sasa hivi hali ilivyo ni kwamba unakimbizana na lori, mbolea na mvua. Mimi nadhani tukiwa-*encourage* hawa wanaotaka kuuza mbolea wakae na mbolea, wakati wote wanawenza wakanunua mbolea na kuuza. Kuna maeneo ambayo mbolea wakati wote ina soko, hilo nalo tumelifikiria. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, suala la ushirika limekwishazungumzwa na Mheshimiwa Malima na nadhani na Sheria mpya inaweza ikatusaidia.

Mheshimiwa Spika, kuongeza fursa za mikopo kwa wakulima ndiyo jambo ambalo ni jipya kwa Tanzania. Tunatoa ruzuku kwa sababu hakuna mkopo. Mkulima wa Ludewa akitaka kwenda kukopa hana mahali anaweza kukopa. Mimi nimetembea kuangalia kilimo katika nchi ambazo zimepiga hatua kama Vietnam, suala la mikopo lipo mpaka kwenye ngazi ya Wilaya. Sasa tumeanzisha Benki

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU)]

ya Kilimo na Benki hii itafungua milango yake Januari yaani miezi michache ijayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, matumaini yetu ni kwamba ile benki itafanya kazi nzuri na itakuwa na uhusiano na *SACCOS* za wakulima wadogo ili mikopo hii iweze kufika na ili mkulima akitaka mbolea na mbegu za kisasa, akitaka jembe la plau na akitaka power tiller aweze kuweka dhamana kwa njia ya *SACCOS* yake apate mkopo kutoka Benki ya Kilimo kwa masharti nafuu zaidi kuliko masharti ambayo yapo kwenye mabenki ya sasa. Hiyo itatusaidia sana katika kuboresha kilimo. Hakuna *modernisation* kama hakuna *credit* na hakuna *modernisation* kama hakuna matumizi ya sayansi katika kilimo.

Mheshimiwa Spika, suala la masoko limezungumziwa vizuri nadhani inatakiwa kutazamwa vizuri ili kuhakikisha kwamba tunapata manufaa.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni *scheme* za umwagiliaji, Mheshimiwa Said Amour Arfi alipokuwa anajadili jambo hili alisema katika Mkoa wa Katavi kuna *scheme* sita na inayofanya kazi ni moja. Unaweza kwenda kila Mkoa, utakuta kuna *scheme* ambazo hazifanyi kazi. Tume kubaliana na Tume kwamba mwaka huu tutatoa fedha kwa ajili ya kuimarisha zile *scheme* na mwaka huo unaokuja tuhakikisha kwamba *scheme* zote zinafanya kazi kwa manufaa ya wahusika. Hiyo ndiyo itatusaidia katika kuonyesha njia ya namna ya kuweza kufika tunakotaka kwenda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuimarisha masoko na vilevile upimaji wa ardhi ya kilimo na mifugo uongezewe kasi na urasimishaji unaofanywa na MKURABITA upewe rasilimali zaidi. Kwa sababu matatizo yetu mengine haya ya wafugaji wanagombana na wakulima, yanatokana na kutopima, kule ambako tume pima kuna nafuu. Kwa sababu watu wakashajua eneo lao ni hili inakuwa ngumu sana kukaribisha wengine kama halitoshi, lakini kama watu wanachunga tu kama mbuga, watasema njoo na wewe eneo ni kubwa halifu watafika watakuta kwamba wala siyo kubwa kama

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU)]

walivyofikiria. Kwa hiyo, nafikiri tukiwekeza katika kupima na kurasimisha ardhi na vilevile upimaji na urasimishaji utawasaidia wakulima kuweka rasilimali yao ya ardhi kama dhamana ya kupata mikopo.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo tumelizungumza na ni muhimu sana tuliweke katika Mpango unaokuja wa mwaka 2014, ni juu ya usindikaji wa mazao. Hili limezungumzwa na Wabunge wengi na leo Mheshimiwa Michael Laizer amekuwa anazungumza sana kuhusu Nyama lakini mazao mengi yanahitaji usindikaji. Hili kwa kweli tumezungumza na Tume na kwa kweli tunachosema ni kwamba labda tuanze kutazama uwezekano wa namna ya kuwasaidia wawekezaji wa ndani. Tuwe na sera mahsus ambayo inawasaidia. Wapo wawekezaji wa ndani ninawajua kwa mfano ukienda kwenye pamba wako watu wana *ginneries* wangependa sasa kutoka kwenye *ginneries* waende kwenye utengenezaji wa nyazi na nguo lakini wakijaribu mtaji inakuwa ngumu sana kupata. Wengine nawajua akina Gungu wana *ginnery*, kina Njaru wa Bariadi waliwahi kujaribu, tunawajua akina Elihilary wa Shinyanga walitaka kujaribu kutengeneza kiwanda cha kutengeneza pamba ya Hospitalini lakini wakifika mahali wanakwama kwenye eneo la mtaji.

Mheshimiwa Spika, mimi nadhani tukiwa na *deliberate policy* na tujaribu na Tume tumeiambia ijaribu kupeleka mapendeleko Serikalini ili tuweke mkakati ambao utasaidia wawekezaji wa ndani waanze kutoa mchango unaoongeza thamani ya mazao kwa kuwekeza katika viwanda. Hili ni jambo ambalo tunaliweza kwa sababu nchi nyingi zimefanya. Nimekwenda China juzi, nikawauliza ninyi ubinafsishaji mliufanye, wakasema hiyo haiko kwenye *terminology* yetu, sisi tunakaribisha watu wa nje lakini tunashirikiana nao, tunafanya *joint venture*. Nilikwenda Korea, wao kabisa toka mwanzo pamoja na uhusiano wao na Marekani waliwekeza kwa kuwasaidia watu wao palepale, wakawekeza na nguvu yote ya uchumi iko mikononi mwa Wakorea. Kwa hiyo, mimi nafikiri hili jambo tunaweza tukalijaribu na tukaweza. Haya mambo yote tukifanya katika

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

*[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU)]*

sekte ya kilimo na viwanda, vitatuongezea uzalishaji wa chakula, itasaidia kupunguza mfumuko wa bei na vilevile umaskini wa kipato unaweza ukapata majibu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, mwenendo wa deni la taifa umekwishaongelewa na Naibu Waziri wa Fedha. Namshukuru kwa maelezo yake mazuri sana ya ufasaha na ameonyesha vitu ambavyo tunafanya kwa kutumia deni hilo kama barabara na hata *UDOM* hii ni deni, hatujalipa lakini ipo. Hata ukidaiwa unasema tunadaiwa lakini tumejenga *UDOM*. Kwa hiyo, hakuna namna unaweza ukakwepa mambo haya, dunia nzima inakopa hata Marekani wanakopa China. Juzi China *pressure* ya Wachina ilipanda wakati wanagombana Washington kwa sababu benki ukiikopa na wewe hutaki kulipa na huweki ukomo wa madeni benki inasikitika na Wachina nao ndiyo benki ya Amerika. Kwa hiyo, mambo haya yapo duniani, tutaendelea kukopa lakini illi mradi tusikope halafu tukafanya deni likashindwa kuhimilika tukarudi kwenye *HIPIC*.

Mheshimiwa Spika, hoja ya tano ni Mpango unaandaliwa bila kujua vyanzo vya mapato. Tulikubaliana kwamba tutatumia shilingi triliioni 8.9 kwa kila mwaka. Katika Mpango tunaoupendekeza kuna shilingi triliioni tano lakini ukweli ni kwamba hatukukusudia triliioni zote zitoke katika bajeti ya Serikali, kiasi kinachobakia tulikubaliana kwamba kitatoka kwenye sekte binafsi. Jambo ambalo tutalifanya ni kujaribu kuifanya Tume i-truck ili ijue sekte binafsi inawekeza wapi na kiasi gani. Katika Mipango yetu inayokuja na katika kueleza utekelezaji, sehemu hii itajitokeza katika tathmini. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, hoja ya sita ilisema Serikali iandae utaratibu mzuri wa kuwezesha vijana kujajiri. Hili lilikuwa ni jambo kubwa ambalo limezungumzwa sana na mimi nakubali kwamba Serikali ni lazima iwe na mkakati wa kusaidia vijana. Kulingana na sensa ya watu na makazi ya mwaka 2012, asilimia 67.1 ya nguvukazi ya Tanzania ni vijana wa umri kati ya miaka 15-35. Kundi hili la vijana ndiyo lenye kiwango kikubwa cha ukosefu wa ajira kwa 13.4% au zaidi

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU)]

ikilinganishwa na wastani wa 12.7% ya ukosefu wa ajira kwa vijana dunia nzima.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hatua mbalimbali ambazo Serikali imekuwa ikichukua kukabiliana na tatizo la ajira nchini kuititia Mifuko ya Uwezeshaji na Mifuko ya Vijana, Serikali sasa imeandaa *program* ya ajira kwa vijana itakayoelekezwa kwa kipindi cha miaka mitatu yaani 2013/2014 na mwaka 2015/2016. Baadhi ya malengo ya *program* hiyo ni kupatikana fursa za ajira 840,000 kwa kuwezesha jumla ya miradi 10,000 ya wahitimu wa elimu ya juu 30,000 kutoka vyuo mbalimbali watatoa ajira za moja kwa moja kwa wahitimu wengine 270,000 na ajira zisizo za moja kwa moja kama 540,000.

Mheshimiwa Spika, program hii itatekelezwa kwa kuzingatia maeneo makuu matatu. Inalenga kujenga uwezo wa vijana katika stadi ya kazi, ujasiriamali na kuwapatia mikopo vijana ili kupata mitaji, nyenko na vifaa vya kufanya kazi na kuwapatia vijana maeneo ya uzalishaji na biashara. Serikali inapanga kutenga fedha za kutosha katika kipindi husika ili kuwezesha utekelezaji wa program hii.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Edward alikuwa amelizungumza jambo hili na akazungumza juu ya CRDB. Mpango huu *CRDB* inashiriki kama mdau lakini ni mpango wa Serikali katika kujaribu ku-solve hii *problem* ya vijana. Vilevile kuna nafasi kama 65,000 katika sekta ya umma na sekta rasmi ambayo vilevile itatoa fursa kwa vijana wanaojiriwa moja kwa moja na ambao ni *wage earners*.

Mheshimiwa Spika, hoja ya saba ilihu sababu za kuanzisha kitengo kingine cha utekelezaji yaani hapa walikuwa wanazungumza juu ya *Big Results Now* na *Presidential Delivery Unit*. Nadhani jambo hili limeshaelezwa mara nyingi na pengine ni vizuri niokoe muda wa Bunge lako Tukufu kwa sababu jambo hili tumelizungumza lakini kama bado kuna maelezo yanayohitaji mazungumzao zaidi tutaendelea kulijadili.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU)]

Mheshimiwa Spika, tulikubaliana na Kamati ya Bajeti kwamba tutapata fursa ya hawa jamaa waliopo kwenye *Presidential Delivery Unit* walete maelezo juu ya shughuli ambazo wameanza nazo na kuonyesha *speed* gani itakuwepo. Kwa hiyo, wanaandaa na tutapata muda wa kukutana na ile Kamati. Hata hivyo, katika siku zijazo tutaweza kutoa suala hili kwa Wabunge wote ili wawewe kuelewa kitu gani hasa kinafanyika na Wabunge wakielewa Watanzania wataelewa kuitia kwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, hoja ya nane ilihu ulinzi na usalama kwamba haukuwa katika kipaumbele. Suala hili lilipigiwa debe sana na Mama Abdallah ambaye ni Mwenyekiti wa Ulinzi na Usalama. Katika suala hili nataka kusema kwa ufupi tu kwamba kwenye Mpango hatukuweka fedha kwa ajili ya ulinzi na usalama zinatolewa na hazipo katika bajeti hii. Hakuna namna unaweza ukalinyima fedha Jeshi la Polisi halafu ukasema utatekeleza Mpango, utatekeleza wapi? Ni lazima iwemo amani na utulivu katika nchi, ni lazima mipaka yetu ilindwe ndiyo Mpango huu uweze kutekelezwa kikamilifu. Kwa hiyo, nataka kuwaondolea hofu katika jambo hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lipo jambo la Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango na *capacity* ya kuweza kutekeleza mambo haya. Tume ya Mipango iliundwa kama *think tank*, haikukusudiwa kwa kweli kuwa chombo kikubwa sana. Mara nyingi kinatumia watu wengine kama *universities* na wasomi wengine katika maeneo mengine kwa ajili ya kufanya shughuli zake kwa *ku-contract*. Ukitaka kila kazi ifanywe na hii Tume, kwa kweli hii Tume itakuwa kubwa kuliko ambavyo ungeweza kufikiria kwa sababu kila fani kutakuwa na wataalam; wataalam wa gesi, wataalam wa mafuta, wawepo wa kilimo na nini, itakuwa kubwa sana lakini inapotokea suala ambalo ni *specialized*, Tume hii *ina-contract out*.

Mheshimiwa Spika, hayo ndiyo maeneo ya jumla ambayo yameongelewa katika kikao hiki na mengine yamejibowi vizuri na Waheshimiwa Mawaziri.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU)]

Mheshimiwa Spika, katika ufanuzi mdogo uliotolewa kwenye Kamati ya Bunge ya Bajeti, liko suala la matumizi ya kawaida ukilinganisha na matumizi ya maendeleo na kwamba fedha za matumizi ya kawaida zinaonekana ni nyingi. Mimi nadhani hapa nirudie tena, suala la msingi hapa ni matumizi mazuri, nidhamu katika matumizi ya fedha za Serikali. Hata hivyo, kimsingi ukifanya maendeleo, unaongeza matumizi ya kawaida, hakuna namna unaweza ukakwepa. Ukijenga shule mpya, unahitaji vitabu zaidi, unataka Walimu zaidi na kwa hiyo mshahara zaidi. Ni vigumu sana kuzuia kuongezeka kwa matumizi ya kawaida lakini unaweza ukaya- *control* kama unatumia vizuri. Kama ukitumia vizuri basi unaweza ukasema kwa kweli hakuna haja ya kuwa nazo nyingi sana kwa sababu chache zilizopo zinafanya kazi iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, fedha za maendeleo zilizotolewa katika robo ya kwanza ni asilimia ndogo zaidi ukilinganisha na zile zilizokwenda kwenye mipango ya matumizi ya kawaida. Hii ni kweli na nimezungumza na Wizara ya Fedha juu ya jambo hili na wamenieleza ni kwa nini ilitokea hivyo. Kwa sababu kuna shughuli nyingi sana ambazo zimegharamiwa katika *quarterya* kwanza. Kumekuwepo na vikao vya Bunge ambavyo vilihitaji fedha wakati uleule, kumekuwepo kwa ununuzi wa chakula kwa ajili ya Hifadhi ya Chakula kuwahi Julai ili chakula kiweze kupata soko, kwa hiyo fedha zilienda kwenye matumizi ya kawaida, mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu ilibidi lazima fedha zipatikane wakati uleule, vilevile ruzuku ya pembejeo za kilimo ili kuwahi msimu wa kilimo nazo zinatolewa wakati mmoja, kuhuisha Daftari la Wapiga Kura na kugharamia mitihani ya Darasa la Saba, Kidato cha Pili na Kidato cha Nne, yote yalihitaji fedha. Kwa hiyo, ili kuweza kuyafanya hayo kwa *quarterya* kwanza, fedha zilienda nyingi zaidi kuliko zilizoenda kwenye maendeleo. Tumekubaliana na Hazina kwamba *quarter* ya pili, *quarter* ya tatu mpaka ya mwisho, hili pengo lilitokea kwenye *quarter* ya kwanza litafidiwa ili tusiathiri mipango ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, suala lingine, Serikali haina budi

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU)]

kuhakikisha kwamba kila mdau anayehusika katika Mipango ya Maendeleo kwa nafasi yake ya kiutendaji anatimiza wajibu wake. Aidha, watendaji wanaokwamisha utekelezaji wawajibike. Hilo tunalikubali na kwa kweli tumeweza *Big Results Now*, tumeanza mfumo ambao unawajibisha watendaji ambao wanashindwa kutimiza wajibu wao na hiyo itakuwa *extended* kwenda kwenye Serikali yote baadaye.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo ya Mpango wa Taifa yanatakiwa yaanishe malengo mahsus (*defined specific targets*). Tunakubali maoni hayo na tutajaribu kuyafuatilia.

Mheshimiwa Spika, Serikali iendelee kutengeneza mipango thabiti kuendesha rasilimali watu. Tunakubali na rasilimali watu inaendelea kushughulikiwa na vyombo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, ushiriki katika sekta binafsi kwa suala la kukuza elimu na ujuzi uwe wazi. Serikali imekuwa ikishirikiana kwa karibu sana na sekta binafsi katika jambo hili na kama mnavyoju, *universities* za binafsi zote Serikali inatoa mikopo kwa wanafunzi ili watoe nafasi ya elimu kwa vijana wengi zaidi badala ya *ku-confine* mikopo kwa *universities* za Serikali.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo yaoneshe kuwa yanazingatia utekelezaji na changamoto zinazojitokeza. Ushauri huu utazingatiwa katika jambo hili.

Mheshimiwa Spika, Serikali itoe msukumo unaohitajika ili kuhakikisha mradi wa kitaifa wa kimkakati unatekelezwa kwa malengo na kwa muda tuliojiwekea. Tutajitahidi kuona jambo hili linafanyika.

Mheshimiwa Spika, malengo ya utekelezaji wa mfumo wa *Big Results Now* wanasema hayajaelewaka. Nimesema tutaendelea kuyaeleza lakini tumeanza kufanya utaratibu ambao unawapa wananchi uelewa. Kwa mfano, ushiriki wa *labs* zile ulikuwa unashirikisha sekta binafsi na ya umma.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU)]

Uzinduzi wa wazi ‘open day’ wa Mfumo wa Tekeleza kwa Matokeo Makubwa ulifanyika waziwazi. Uzinduzi rasmi na wa wazi wa mpango wa kila eneo kuu la matokeo. Taarifa kuhusu *BRN*iko kwenye tovuti. Ushiriki wa wataalam wa *PDB* na *MDU*katika mikutano ya sasa, jambo hili linafanyika. Hata Mikoani ambapo hiki kitu hakikuwa kimekusudiwa lakini Mikoa yote imeambiwa na wameanza kuunda timu za kufuatilia. Kwa sababu kuna maeneo muhimu sana ambayo yanatekelezwa Mikoani, kwa mfano, maji ya kunywa yako katika *Big Results* ambako tunataka watu milioni saba (7,000,000) waweze kupata maji safi na salama katika muda wa miaka mitatu. Suala hilo linafuatiliwa na *Presidential Delivery Unit*lakini vilevile Mikoa yenye ambayo iko karibu na utekelezaji wa miradi ya maji vijijiini itafuatilia.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni umeme hasa ule wa vijijiini ambao tunataka ifikapo mwaka 2015/2016 tuweze kuwapa umeme asilimia 30 ya wananchi wa Tanzania. Hilo jambo linahitaji usimamizi huku *centerna* vilevile katika Mikoa kufuatilia mapendekezo hayo.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2014 kutoanisha kwa kina miradi ilioibuliwa na mfumo wa *Big Results Now*. Miradi hii itakuwa katika sehemu ya Mpango ujao na tutakuja kuijadili itakapofika Juni kuonesha sekta gani *Big Results Now* watakuwa wanafanya nini, lakini iko katika maeneo yale sita tu na hayataongezeka sana.

Mheshimiwa Spika, eneo la kuondoa umasikini wa kipato nimeshalizungumza. Bajeti ya maendeleo kutolindwa, tumesema sasa tutajaribu kufanya *ringfencing* ili kuhakikisha kwamba fedha hizi haziyumbi wala hazitoki kwenye *development*.

Mheshimiwa Spika, idadi ya watu nchini imekuwa kubwa na kwa hiyo ukuaji wa uchumi unakwenda chini zaidi ukilinganisha na idadi ya watu. Hili ni jambo kubwa lakini unalifanyaje hasa maana watu wanazaa na hakuna sheria inayowazuia kufanya hiyo shughuli ya kuzaa? Kwa hiyo, wapo.

## *Hii ni Nakala ya Mtando (Online Document)*

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU)]

Jambo kubwa hapa ni kutazama utaratibu wa kukuza uchumi.

Mheshimiwa Spika, wengine wamesema hapa tunalo tatizo watu hawafanyi kazi, labda hili linaweza likatupunguzia tatizo kwamba badala ya watu kukaa tu au kukaa wanalamika, tungejiwekea utaratibu ambao utawawezesha watu hawa kufanya kazi. Wakifanya kazi na uchumi ukikua watu wataongezeka. Ziko nchi zina watu wengi kuliko sisi. Uchina wana watu 1.5 bilioni lakini wanakula wote watu wale ila wanakuna vitu vingi, lakini wapo na wanaendelea vizuri tu. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nadhani suala la msingi hapa siyo kuona ongezeko la watu kama ni *problem*, suala la msingi hapa ni kuweka taratibu za kiuchumi ambazo zitafanya ongezeko la watu liende sambamba na ukuaji wa uchumi ili ukuaji wa uchumi uweze ku-service ongezeko la watu.

Mheshimiwa Spika, hatua nyingine ni majibu kwa masuala kutoka kwenye Kambi ya Upinzani. Rafiki zangu wa Kambi ya Upinzani wametoa maneno mengi kidogo, sina mpango wa kuyajibu yote kwa sababu mengine kwa kweli walikuwa wanaauliza maswali tu. Kwa mfano, kuna mahali wanasema wamesoma llani ya Chama cha Mapinduzi (CCM) halafu wanaauliza sasa itakuwaje? Jibu lake hilo ni rahisi, llani ya CCM itafanyiwa tathmini na CCM. CCM itaenda kwa wananchi kueleza. Sasa wale ambao wana mashaka na utekelezaji wataonana na CCM kulekule vijijini. CCM itakuwa inaeleza na wenzetu wanajibu halafu mambo yatajipa tu na waamuzi ni Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, sikuona kama kuna tatizo na ndiyo maana tulikuwa na ndugu Hamad pale *TBC* nikasema kwa nini mnataka kupakua kabla ya kupika? Maji yakichemka ndiyo unaweka unga, lakini ukianza kuweka unga na maji hayajachemka badala ya kupika ugali unakuwa uji. Sasa nadhani tujipe *time* tu mambo haya yataeleweka. Bado tuna miaka miwili, tumetekeleza mitatu

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU)]

na maelezo mmeyasikia namna utekelezaji utakavyokwenda. Kwa hiyo, tusubiri.

Mheshimiwa Spika, lakini kuna mambo wamesema ambayo yanahitaji majibu. Kwa mfano, Serikali itoe tathmini ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya kipaumbele sambamba na taarifa za matumizi ya fedha. Hili litafanyika, kwenye Mpango unaokuja kufika Juni tutakapokuwa tunazungumza Mpango utakuwaje tutazungumza utekelezaji wa mwaka uliopita umekuwaje na fedha kiasi gani zimetumika. Kwa hiyo, ni jambo linakubalika.

Mheshimiwa Spika, hakuna umakini katika kuhakikisha Mpango wa Miaka Mitano kwa kuwa kifungu (c) katika kitabu cha mapendekezo ya Mpango kinasema miradi imeibuliwa mwaka 2012/2013. Labda hiyo ni *error*, lakini miradi yote inayotekelawa iliibuliwa chini ya Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano mwaka 2011.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ambayo imesemwa ni kwamba wananchi hawashirikishwi. Mimi nataka kusema kwa maana ya Mpango huu na kwa maana ya *level*/hii ya kitaifa, tunashirikisha. Tunazungumza na Kamati za Bunge, tunapata mawazo ya Wabunge wote na mawazo yale ndiyo tunaenda kuyatafsiri katika kutengeneza Mpango. Matumaini yangu ni kwamba Halmashauri za Wilaya katika ngazi ya chini na yenyewe itakuwa vilevile inafanya kama tunavyofanya sisi kwa kuwashirikisha wananchi ili miradi yao iwe inakuwa sehemu ya mpango wa Halmashauri. Tusipofanya hivyo kwa kweli itakuwa mipango hii inapangwa na *bureaucrats*, lakini kwa kuwashirikisha viongozi na wawakilishi wa wananchi tunawashirikisha wananchi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, Serikali imeshindwa kutekeleza matakwa ya Mpango kwa kushindwa kufufua reli. Nadhani Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe, ameeleza vizuri. Kwanza, nataka niseme kwamba ile reli ya kati lazima tutaifufua, lazima tufufue reli na pengine siyo vizuri sana ku-*complain*, sijui nani wamekutana, wanataka kujenga ya kwao! Wacha wajenge ya kwao na sisi tujenge ya kwetu. Kwani nani

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU)]*

amemzuia mtu kujenga reli yake? Halafu wafanyabiashara hawa ni *rational*, ukijenga reli kutoka Dar es Salaam mpaka Kabanga na mfanyabiashara yuko Burundi na pale ni kilomita 125, hawezi kupeleka mzigo wake kilomita 2700. Watakaopeleka ni wale ambaو wanafuata siasa, lakini biashara ya faida atakwenda kwa reli fupi. Kwa hiyo, sisi tutajenga reli na ukijenga mpaka pale Kabanga na ile *Nikel* iliyokuwa inazungumzwa na Mheshimiwa Mbunge kutoka Kagera, *Nikel* yenye ile ikichimbwa inatosha kufanya ile reli kuwa *viable*.

**SPIKA:** Waziri tumia *microphone* maana naona unaongelea pemberi. (*Makofii*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU):** Ilikuwa imenoga kidogo. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nasema tujenge reli, tuache kulalamika. Reli imefanyiwa *feasibility study*, Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe ametueleza na kinachobakia ni kuamua kwa kutazama nani ambaye tunaweza kushirikiana naye kujenga kwa gharama kiasi gani na kwa manufaa yapi. Nadhani hilo ndiyo jambo la msingi. Kwa hiyo, hilo nalo limekwishapata ufumbuzi wake.

Mheshimiwa Spika, maeneo ya kipaumbele yaliyotajwa na Serikali katika Mpango wa Miaka Mitano yanahitaji kufanyiwa mabadiliko na tuyaelekeze kwenye maeneo mapya. Hili kwa kweli nasikitika kwamba hatutaweza kwenda hivyo. Mwakani tunaanza kufanya tathmini ya Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano na tathmini ile itatusaidia kuona vipaumbele vya Mpango unaofuata viweje. Hapo ndipo tunaweza kuzungumza vipyta, lakini kwa sasa tuendelee na hivihivi. Utaacha kipi maana hatujatekeleza mambo makubwa? Tunataka umeme, hauwezi kusimamisha umeme. Tunataka reli, hauwezi kusimamisha reli. Tunataka barabara tena za llani ya CCM, lazima zijengwe na Waziri ametueleza pale kwamba ziko *committed* na zimeandikwa. Hizo ndiyo hoja zilizotolewa na wenzetu wa Upinzani, tunawashukuru sana.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU)]

Mheshimiwa Spika, tumejitahidi sana, *actually* hata ukitumia hotuba yako ukanung'unika bado utaacha manung'uniko halafu towa nawe *point* inayosaidia Mpango. Katika suala hili la kupanga na kutekeleza, nafikiri tuwe *nationalistic* kwa sababu Mpango wenyewe ni wa nchi yetu wote.

Mheshimiwa Spika, liko suala la ajira nimeishalizungumzia, la reli nimeishalizungumzia na lilikuwa limesemwa na wadau wengi vilevile. Liko suala la barabara na lenyewe limeelezwa vizuri sana, usafiri wa anga umezungumzwa vizuri tu na Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe. Nishati, Maji, Kilimo nacho nimekizungumza na mimi pamoja na Mheshimiwa Malima amezungumzia. Mawasiliano, suala la mifugo, ardhi, yote haya yamezungumzwa.

Mheshimiwa Spika, suala la elimu halikupata mtu wa kulizungumza lakini kwa kweli kwenye *BRN* tumekubaliana suala kubwa la msingi ni kuboresha mfumo wetu wa elimu. *BRN* ina maelezo mengi sana ambayo inatakiwa itekeleze ili kuifanya elimu iweze kuboreka. Sasa tunazungumza matumizi ni makubwa, juzi Waziri Mkuu alinituma kwenda kufungua mkutano wa Walimu kule Arusha, nikaenda kuwasikiliza wala hawana hoja nyngine isipokuwa mshahara tu, tunataka mshahara zaidi. Nikawaambia nitaenda kumwambia aliyenituma, lakini ukiongeza mshahara wa Walimu ndiyo unaongeza matumizi ya kawaida vilevile. Kwa hiyo, yako mambo ambayo huwezi kuyakwepa.

Mheshimiwa Spika, nihitimishe maelezo haya kwa kusema kwamba tumefaidika kwa kiwango kikubwa tu na maelezo ambayo yametolewa na wadau mbalimbali katika suala hili na wengine ambaao wamelieleza kutoka katika Wizara husika, wamenisaidia sana ili kupunguza maelezo yanayotakiwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *BRN* kuna wengine wanakosea kwa kweli, wanafikiri *BRN* ni Mpango, wanasema mpango huu mpya. Wengine wanasema mlisema Kilimo Kwanza, mmeacha tena mnasema Matokeo Makubwa Sasa,

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MAHUSIANO NA URATIBU)]

jamani! Matokeo Makubwa Sasa siyo Mpango wa Maendeleo, ule ni mfumo wa kufuatilia maendeleo ili yaweze kutekelezwa kama yaliwyopangwa. Mpango ni ule wa miaka mitano, hata zile *labs* hazingezi mipango, zinatafsiri utekelezaji wa mipango iliyopo. Unasema nishati tufikie MW 2780 ifikapo mwaka 2015/2016. Zile *labs* zinasema miradi gani tufanye kuweza kufikia lengo. Mpango unasema tujenge reli ya katilabina sema mambo ya kufanya ili reli ya katilabina sema kuimarkika ni moja, mbili, tatu. Pale haufanyi Mpango, pale unatafsiri Mpango halafu baada ya kutafsiri kwenye mpango *BRN* wana fuatilia sasa kuona ya kwamba ile kazi ambayo wamefanya kwenye lab katika kutafsiri Mpango wa Maendeleo wa Miaka Miatano inatekelezwa namna gani. Hiyo, ndiyo shughuli lakini siyo kwamba tukisema Tekeleza kwa Matokeo Makubwa Sasa, basi hiyo ni sawasawa na Kilimo Kwanza, aah bwana! Hilo nalo ni jina la mfumo, lakini mambo mengine yanakwenda kama yaliwyopangwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, nikushukuru tena kwa kunipa nafasi na nimalize kwa kusema tumefaidika na maelezo yaliyotolewa na ufanuzi ule nadhani unatuweka katika mazingira mazuri ya kupanga Mpango wa Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba kutoa hoja. (*Makofii*)

**MHE. WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:**  
Mheshimiwa Spika, naafiki!

**SPIKA:** Hoja imeungwa mkono, sasa nawahoji kuhusu hoja hii.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)  
(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

(*Mapendekazo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2014/2015 yalipitishwa na Bunge*)

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, Kamati yetu ya Mipango tumetoa maoni yetu kwa Serikali ili kuboresha Mpango ule utakaohusika. Kwa hiyo, wataendelea na shughuli zao na sisi itakapofika mwezi Machi tunaendelea na mzunguko wetu wa bajeti. Kwa hiyo, kwa sababu ya Katiba tunakusudia kuwa na Bunge karibuni kusudi tumalize shughuli zetu halafu tuachie ukumbi kwa ajili ya Bunge. Kwa hiyo, Mpango huu kama alivyosema ni mapendekezo ambayo mmetoa na wataendelea kuyafanyia kazi katika kuimarisha Mpango ambao utatengenezewa bajeti katika mwaka unaokuja.

Kwa hiyo, tuwashukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi na wataalam wako wote wa Tume ya Mipango, kwa kazi nzuri na muendelee kufanya hivyo kusudi hatimaye tuweze kuboresha namna ya kupanga mipango yetu na kuweza kusimamia bajeti yetu kama inavyostahilli tuwe na vitu ambavyo kila mtu anaweza kuelewa ni kitu gani tunafanya, tunakwenda wapi na tunamalizia wapi. Kwa hiyo, tunawapongeza kwa hatua hii ya kwanza, muendelee vizuri huko mnakoendelea. Huu ni mwanzo wa kazi na ndiyo mwanzo wa *budget cycle*, kwa hiyo, tunawatakieni hheri.

Waheshimiwa Wabunge, ilipaswa siku ya kwanza tumeanza Bunge kutangaza haya lakini kidogo tulighafirika. Katika Mkutano wa Kumi na Mbili, Bunge lilipitisha Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba (*The Constitutional Review Amendment Bill 2013*.

Kwa taarifa hii, napenda kuliarifu Bunge hili Tukufu kwamba Muswada huo umekwishapata kibali cha Mheshimiwa Rais na kuwa Sheria iitwayo Sheria ya Mabadiliko ya Katiba Na.6 ya Mwaka 2013 (*The Constitutional Review Amendment Act No. 6 of 2013*). (Makofi)

Kwa hiyo, Mheshimiwa Rais alisaini na kwa maana hiyo haizuii kufanya mabadiliko, lakini Sheria kama ilivyopitishwa na Bunge imeishasainiwa. Kama kuna haja ya

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[SPIKA]

mabadiliko basi yanaweza kuja, lakini sheria ile ilisainiwa. Kwa hiyo, naomba niseme hivyo. (*Makofii*)  
Mheshimiwa Waziri wa Nchi, hoja ya kuahirisha Bunge.

### **KUAHIRISHA BUNGE**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, UWEKEZAJI NA UWEZESHAJI:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 28(7), naomba kutoa hoja ya kuahirisha Kikao cha Bunge hadi kesho tarehe 5 Novemba, 2013.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:**  
Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja illitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Hoja imeungwa mkono, Mheshimiwa Ester Bulaya.

### **MAELEZO YA BINAFSI**

Maelezo ya Mheshimiwa Ester A. Bulaya Kuitaka Serikali Kufanya Mabadiliko ya Sheria ya Dawa za Kulevyaa na Kuanzisha Mahakama Maalum ya Kushughulikia Wahalifu wa Dawa za Kulevyaa

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, Kanuni 28(8), napenda kutoa Maelezo Binafsi.

Mheshimiwa Spika, lakini pia naomba maelezo yangu yote yarekodiwe kama ambavyo nimeyawasilisha, kutohana na muda nimetengeneza *summary* ambayo nitaisoma, inaendana na maelezo ambayo nimewasilisha katika ofisi yako.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 28(8) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la mwaka 2013,

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. E A. BULAYA]

napenda kutoa Maelezo Binafsi ya juu ya tatizo sugu la uagizaji, uuzaaji na usafirishaji wa dawa za kulevyia linaloongezeka kwa kasi kubwa nchini, lengo likiwa ni kuitaka Serikali ifanye mabadiliko/marekebisho ya Sheria ya Dawa za Kulevyia na Kuanzisha Mahakama Maalum kushughulikia wahalifu wanaojihuisha na usafirishaji na biashara ya dawa za kulevyia.

Mheshimiwa Spika, nimeona ni wakati muafaka kutoa maelezo haya, ili Bunge lako Tukufu na Serikali ipate fursa ya kuona uzito wa tatizo hili kutokana na ukweli kwamba katika miaka ya karibuni tatizo la dawa za kulevyia katika nchi yetu limeongezeka kwa kasi ya ajabu hali inayopelekea athari kubwa za kiuchumi, kijamii na kifaya. Mbaya zaidi kundi kubwa linaloathirika ni kundi la vijana ambao ndio nguvu kazi ya Taifa letu. Mbaya zaidi, sasa hivi, wafanyabiashara hawa wa dawa hizi haramu wameanza kuwatumbua watoto wa shule za msingi chini ya falsafa yao mpya "wapate wakiwa wadogo... wafanye watumwa wa dawa za kulevyia ...na kupata uhakika wa soko la baadaye pale ambapo watakuwa wameajiriwa au wamejajiri". (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tafiti za hivi karibuni za Umoja wa Mataifa (*World Drug Report, United Nations Office on Drugs and Crime (UNODC), 2013*) zinaonyesha kwamba kuna ongezeko kubwa na la kutisha katika matumizi ya dawa za kulevyia aina ya *Heroin* na kwa njia ya kujidunga katika nchi za Kenya, Libya, Mauritius, Shelia Sheli na Tanzania (*Chris Beyrer and others. "Time to Act: a call for comprehensive responses to HIV in people who use Drugs ", The Lancet, Vol .376. No. 9740 (14th August 2010) pp 551-563*). Halikadhalika, Ripoti ya mpya ya hivi karibuni ya ofisi ya Umoja wa Mataifa ya kupambana na miadarati na uhalifu (UNODC), imetamka bayana kwamba Tanzania ni kinara wa kupitisha dawa za kulevyia katika nchi za Afrika Mashariki na Mkoa wa Tanga ukitajwa kama Mkoa hatari zaidi!

Mheshimiwa Spika, ripoti hiyo inasema jumla ya Tani 64 za dawa za kulevyia aina ya *Heroin* ilisafirishwa bila kukamatwa kwenda au kupitia Afrika Mashariki ikiwamo

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. E.A. BULAYA]

Tanzania kati ya 2010 na 2013. Kwa Mkoa wa Tanga, ambao umetajwa wazi kama eneo hatari zaidi Afrika Mashariki wastani wa ukamataji wa shehena za dawa za kulevyta eneo hilo umefikia kilogram 1,011 mwaka 2013 toka kilogram 145 mwaka 2010 na kwamba Dola za Kimarekani takriban milioni 160 zinatumiwa na Watanzania na Wakenya kila mwaka kwa utumiaji na usafirishaji kwa mwaka! Hili sio jambo la kufumbia macho, lazima tuchukue hatua sasa.

Mheshimiwa Spika, lazima tuchukue hatua sasa, kwa sababu kama nilivyoainisha hapo juu kwamba kwa kipindi cha miaka mitatu tu (2010-2013), wakati Tani 64 za dawa za kulevyta zilipita bila kukamatwa...zikiwa mtaani zikiharibu vijana na watoto wetu katika kipindi hicho hicho, kiasi kilichowenza kukamatwa ni tani 1.6 tu! Takwimu hizo za kutisha zinatoa picha kwamba sehemu kubwa ya shehena za dawa za kulevyta hupitishwa bila kugundulika au kukamatwa na vyombo vyanya dola!

Mheshimiwa Spika, taswira ya nchi katika Jumuia ya Kimataifa. Maelfu ya Watanzania wanatumikia vifungo mbali mbali ikiwamo vifungo vyaa maisha nje ya nchi, wengine wengi wamepoteza maisha kwa kunyongwa. Nitatoa mifano michache; China peke yake inasemekana kuna wafungwa 176 (99% - dawa za kulevyta). Taarifa kwa mujibu wa Msemaji wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Ndugu Mkumbwa Ally. Brazil kuna wafungwa zaidi ya 103 (Takwimu za Tume ya Kuratibu udhibiti wa Dawa za Kulevyta nchini na Hong Kong kuna zaidi ya Watanzania 200 wenye kesi za dawa za kulevyta, ambapo 130 zimeshakwisha hukumiwa na kesi 70 zikiwa zinaendelea!

Mheshimiwa Spika, aibu ya hivi karibuni, ambayo hatuvezi kuikwepa ni meli iliyosajiliwa Tanzania (upande wa Zanzibar- MV *Gold Star*) iliyoripotiva kukamatwa nchini Italia ikiwa imesheheni tani 30 za dawa za kulevyta zenye thamani ya pauni milioni 50 (sawa na bilioni 123 za Kitanzania).

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. E.A. BULAYA]

Mheshimiwa Spika, uhalifu huu unaofanywa na mtandao huu wa watu wachache, lakini wenye nguvu umewafanya Watanzania wanaokwenda nje ya nchi kudhalilika kutokana na upekuzi unaofanywa dhidi yao kwa hofu kwamba yawezekana na wao wamebeba dawa hizo haramu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hali ya dawa za kulevyia. Changamoto ya dawa za kulevyia sio tatizo letu peke yetu ni tatizo ambalo hata Jumuiya ya kimataifa imekuwa ikipambana nalo kwa kipindi kirefu kwani tafiti zinaonyesha kwamba asilimia tano ya idadi ya watu wazima duniani (watu takribani milioni 230) wanakadiriba kutumia dawa za kulevyia.

Mheshimiwa Spika, tukiwa sehemu ya Jumuiya hii ya Kimataifa, Waheshimiwa Wabunge mtakumbuka kuwa tarehe 19 Desemba, 1988 Jumuiya ya Kimataifa ilipitisha Mkataba wa kupambana na dawa za kulevyia yaani *United Nations Convention Against Illicit Traffic in Narcotic Drugs and Psychotropic Substances*. Tanzania ni sehemu ya Mkataba huo na hili limewekwa wazi hata kwenye kifungu cha 55 cha Sheria ya Kuzuia Dawa za Kulevyia [sura 95 ya sheria zetu kama zilivyorekebisha mwaka 2002]. Mkataba wa mwaka 1988 ulikuwa unakazia zaidi Mkataba wa mwaka 1961 (*Single Convention on Narcotic Drugs, 1961*), Itifaki (*Protocol*) za 1972 zilizofanyia marekebisho Mkataba wa mwaka 1971 (*Convention on Psychotropic Substances, 1971*). Licha ya juhudzi zote, tatizo la uuzaji na usafirishaji wa dawa za kulevyia, limezidi kuwa kubwa.

Mheshimiwa Spika, hali ya dawa za kulevyia nchini na madhara kwa afya ya biandamu. Mwaka 1995 tulitunga Sheria ya Kuzuia Biashara ya Dawa za Kulevyia ambayo ilianza kufanya kazi mwaka 1996 kupitia GN.No.10/1996. Sheria hiyo inatumika Bara na Zanzibar. Kabla ya Sheria hiyo tulikuwa tuna Sheria iitwayo *The Dangerous Drugs Ordinance (Cap.95)*. Pamoja na kutungwa kwa Sheria mpya, tatizo la dawa za kulevyia limeendelea kuwa kubwa zaidi hapa nchini. Ukamataji wa dawa za kulevyia kwa miaka ya nyuma ilikuwa

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. E.A. BULAYA]

kidogo na idadi ya walioathirika (wateja) ilikuwa ni ndogo kulinganisha na sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, ni kwa bahati mbaya sana, licha ya ukubwa wa tatizo, pamoja na athari zake kwa jamii ya Watanzania, hakuna tafiti zinazoonyesha ukubwa wa tatizo kwa nchi nzima, tafiti nyingi zilizofanywa zimejikita katika maeneo machache yaliyoathirika zaidi na dawa za kulevy. (Kwa mwaka 2012 kumekuwa na huduma za kijamii kwa watumiaji wa dawa za kulevy ambapo waaathirika 27,176 walionwa katika asasi zilizo chini ya *Tanzania Aids Prevention Programme (TAPP)*. Kwa mwaka 2013 hadi mwezi Septemba, 2013, mpaka sasa kuna *clinic* mbili zinazotoa huduma za dawa za kulevy ambapo Muhimbili ina waathirika 576 na Mwananyamala 376. Idadi ya waathirika walioonwa na kupata huduma hadi mwezi Septemba, 2013 ni waathirika 15,106 kwa Mkoa wa Dar es Salaam).

Mheshimiwa Spika, tafiti zinaonyesha kwamba dawa zinazotumika kwa wingi ni bangi, mirungi, heroine, mihadarati, vidonge na *cocaine*. Tafiti iliyofanywa na Shirika la Umoja wa Mataifa linalohusika na mapambano dhidi ya dawa za kulevy UNODC (*United Nations Office on Drugs and Crime*) zinaonyesha kwamba 0.2% ya Watanzania, ambao ni karibia watu milioni 1.2 wameshawahi kutumia dawa za kulevy aina ya *heroine*.

Mheshimiwa Spika, halikadhalika, Shirika la Afya Duniani (*World Health Organisation -WHO*) linaripoti kuwa takribani 0.2% ya Watanzania wameathirika na Ugonjwa wa *TB* na takwimu za kitaifa katika program ya Kifua Kikuu na Ukoma Tanzania zinaonyesha maambukizi ya *TB* ni 0.4% wakati tafiti katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili inaonyesha kwamba maambukizi ya *TB* kwa wanaotumia dawa za kulevy ni 11% ambayo ni mara 44 zaidi ya kiwango cha maambukizi kwa watu ambao hawatumii dawa za kulevy.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa maambukizi ya UKIMWI, takwimu za mwaka 2011/2012 za *TACAIDS*, zinaonyesha kwamba 5.1% ya Watanzania wameathirika na

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. E A. BULAYA]

virusi vya UKIMWI wakati tafiti ndogondogo zinaonyesha maambukizi ya virusi ya UKIMWI kwa watu wanaotumia dawa za kulevyta ni mara 10 zaidi ya maambukizi ya kawaida. Kwa mfano 51.9% ya wanaotumia dawa za kulevyta kwa njia kujidunga sindano, 37% wanaotumia dawa za kulevyta kwa njia ya kuvuta na kufanya biashara ya ngono na 22.6% kwa wanaotumia dawa za kulevyta kwa njia ya kuvuta.

Mheshimiwa Spika, madhara ya kiafya kwa utumiaji wa dawa za kulevyta sio tu katika magonjwa ya *TB* na maambukizi ya virusi vya UKIMWI, bali pia katika homa ya ini. Japokuwa hakuna tafiti za kitaifa zilizofanyika kuhusiana na mchango wa matumizi ya dawa katika homa ya ini, tafiti ndogondogo za mwaka 2012 zinaonyesha kati ya 65% mpaka 75.6% ya watumiaji wa dawa za kulevyta wameathirika kwa homa ya ini, hasa homa ya ini aina ya *Hepatitis*. Homa ya ini ni hatari sana katika kupata magonjwa suga ya ini ikiwepo kansa ya ini na ini kushindwa kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, ukubwa wa tatizo na utendaji wa vyombo vya dola. Kesi kubwa ya kwanza inayohusu dawa za kulevyta ni ile ya mfanyabiashara NURDIN AKASHA @HABAB V.R [1995] TLR. 227 (CAT) ambaye tarehe 20/7/1993 alikamatwa nyumbani kwake *Msasani Village* akiwa na paketi 105 za *menthaqualone (mandrax)* alizozingiza nchini kutoka Mombasa akitumia malori yake. Sasa hivi tunaongelea uingizaji wa kilo kadhaa za dawa za kulevyta na siyo paketi tena.

Mheshimiwa Spika, mwezi Machi, 2010 kilo 92 za dawa za kulevyta aina ya *Heroine* zilikamatwa maeneo ya Kabuku, Mkoani Tanga na tayari washitakiwa watano wanatumikia kifungo. Tarehe 19/12/2010, kilo 50 za dawa za kulevyta aina ya *Heroine* zilikamatwa tena Wilayani Handeni, Mkoa wa Tanga. Mwezi Septemba, 2011, kilo 179 za dawa za kulevyta aina ya *Heroine* zilikamatwa Dar es Salaam. Tarehe 14/6/2011, kilo 35 za dawa za kulevyta aina ya *Heroine* zilikamatwa Mkoani Mbeya na tarehe Januari kilo 211 za dawa za kulevyta zilikamatwa Mkoani Lindi.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

*[MHE. E.A. BULAYA]*

Mheshimiwa Spika, utendaji wa Ofisi ya *DPP*. Natambua jitihada zinazofanywa na baadhi ya watendaji wa Serikali ya Awamu ya Nne katika vyombo nya dola kwa kufanikisha jitihada za kuwakamata watuhumiwa wanaojihusisha na dawa za kulevy. Kutokana na jitihada hizo, kuanzia mwaka 2008 mpaka mwaka huu wa 2013, watuhumiwa wa dawa za kulevy ni kama ifutavyo:-

(i) Cocaine kilo 395 zilikamatwa na washitakiwa waliokamatwa ni 1074.

(ii) *Heroine* kilo 768.8 na washitakiwa waliokamatwa ni 1130.

(iii) Mirungi kilo 56,562 na washitakiwa waliokamatwa ni 3,712.

(iv) Bangi kilo 487,472 sawa na tani 487 na washitakiwa waliokamatwa ni 20,255.

(v) *Mandrax* kilo 5 na gramu 9 na washitakiwa waliokamatwa ni 20.

Mheshimiwa Spika, licha ya juhud za baadhi ya watendaji waaminifu kuwakamata watu walioko katika mtandao huu hatari kumekuwa na hujuma za dhahiri dhidi ya wanaopambana na dawa za kulevy. Moja kati ya ofisi inayoshutumiwa kuwa na maafisa wanaoshirikiana na wanamtandao, ni ofisi ya *DPP*.

Mheshimiwa Spika, mtandao katika Ofisi ya *DPP* na Mahakama. Natambua kazi nzuri na jitihada zinazofanywa na baadhi ya watumishi wazalendo kwa upande kwa Ofisi ya Muendesha Mashtaka, Majaji na Mahakimu waaminifu. Hata hivyo, katika ofisi hizo za umma, kumekuwa na baadhi ya watumishi ambao wamekuwa wakihujumu kesi za dawa za kulevy kwa kushirikiana na watuhumiwa katika kupanga jinsi ya kuwasaidia washinde kesi kwa kuwapatia taarifa za siri zinazohusiana na ushaidi na jinsi ya kuharibu ushahidi nzima.

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. E A. BULAYA]

Mheshimiwa Spika, kutokana na kupanuka kwa mtandao huu wa kuhujumu, licha ya kushirikiana na washtakiwa, mtandao uliopo katika Ofisi hiyo ya DPP umekuwa ukituhumiwa kufanya njama za kushirikiana na baadhi ya watumishi wa Mahakama hasa Majaji kuhamisha kesi kupeleka kwa Majaji ambao wanadaiwa kuhusika na mtandao huu (sihitaji kutaja majina ya Majaji hapa, baadhi yao wanafahamika na wengine wametajwa mara kadhaa na vyombo vya habari).

Mheshimiwa Spika, kwa kutumia mtandao huo, baadhi ya Majaji wamekuwa wanatafsiri sheria kwa jinsi wanavyotaka na kuwapa dhamana watuhumiwa wa kesi za dawa za kulevyaa ambazo hazina dhamana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mfano mzuri ni kesi Na.6/2011, Jamhuri dhidi ya Fred William Chonde na wenzake ambaa walikutwa na kilo 179 za *Heroine* yenye thamani ya shilingi bilioni 6.5. Washtakiwa hawa wanashitakiwa kwa kosa la kusafirisha dawa za kulevyaa ambalo kwa mujibu wa kifungu cha 148(5)(a)(ii) cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai pamoja na kifungu cha 27(1)(a) cha Sheria ya Kuzuia Usafirishaji wa Dawa za Kulevyaa halina dhamana.

Kwa tafasiri yoyote ile aliyokuwa nayo Mheshimiwa Jaji, bado asingewapa dhamana kwani kifungu cha 148(5)(a)(iii) cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai na kifungu cha 27(1)(b) cha Sheria ya Kuzuia Usafirishaji wa Dawa za Kulevyaa kinazuia dhamana kwa kosa ambalo thamani ya dawa za kulevyaa inazidi shilingi milioni kumi. Kutohama na Mahakama kutoa dhamana, washtakiwa wawili raia ya Pakistani wametoroka na hawapo tena nchini.

Mheshimiwa Spika, aidha, katika kesi ya R. v. Mwinyi Rashid Ismail @Mkoko, (KLR /IR 4143/2011), mshtakiwa aliomba dhamana Mahakama Kuu wakati kesi ilikuwa bado ipo Mahakama ya Kisutu ndipo Wakili wa Serikali akamwambia Jaji kuwa anaomba kuifuta. Mheshimiwa Jaji, huku akifahamu kuwa kesi hiyo imefika mbele yake kwa ajili ya kusikiliza maombi ya dhamana tu na kuwa ilikuwa

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. E.A. BULAYA]

haijafikishwa Mahakama Kuu kwa taratibu wa sheria, aliamua kumfutia kesi mshtakiwa na kuamuru kuwa yuko huru.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, katika kesi No. 794/2011, katika Mahakama ya Wilaya ya Ilala, Mheshimiwa Hakimu aliwafunga kifungo cha nje kwa miezi kumi na tano washtakiwa Abdurahman Shaban Sindanema, Said Nassoro Khamis na Abdurahim Haroub Said waliokiri kosa la kuuza na kusambaza dawa za kulevyaa aina ya *Heroine*. Adhabu iliyotolewa na Hakimu huyu, haipo kwa mujibu wa sheria. Kwa mujibu wa kifungu cha 16 cha Sheria ya Kuzuia Dawa za Kulevyaa, adhabu iliyowekwa kwa wauzaji au wasambazaji wa dawa za kulevyaa ni kifungo cha maisha na si chini ya miaka ishirini (20) jela kwa kipindi hicho.

Mheshimiwa Spika, kesi nyingine ni Na. 274/2005 Jamhuri dhidi ya Yusuph Hashim Nyose aliyekamatwa na kilo 1.3 za dawa za kulevyaa aina ya *Heroine* alizokuwa amemeza na kisha kuzitoa kupitia njia ya haja kubwa baada ya kukamatwa na zilikuwa na thamani ya shilingi milioni kumi na mbili na laki sita (12,600,000/=). Pamoja na ushahidi uliotolewa Mahakamani na mashahidi sita (6) wa upande wa Jamhuri ikiwa ni pamoja na Mkemia aliyethibitisha kuwa ni dawa za kulevyaa na mashahidi walioshuhudia mshtakiwa akizitoa kwa njia ya haja kubwa, Hakimu alimuachilia huru.

Mheshimiwa Spika, katika hukumu yake Hakimu alisema kuwa ameridhika kuwa hizo ni dawa za kulevyaa na zina madhara kwa binadamu na kuwa hana ubishi kuwa mshtakiwa alikutwa nazo. Hata hivyo, alimuachilia huru kwa kuwa upande wa mashtaka umeshindwa kuelezea mbinu walizotumia kungundua mshtakiwa kuwa alikuwa amebeba dawa za kulevyaa kabla ya kumkamata.

Mheshimiwa Spika, mfano mwengine ni hukumu iliyotolewa tarehe 4/5/2007 inayoihusisha Jamhuri dhidi ya Chriswell Simon Mobini (561/2007) ambapo mtuhumiwa alikamatwa tarehe 9/4/2007 katika uwanja wa JKNA akiwa na pipi 93 aina ya *Heroine* yenye thamani ya zaidi ya shilingi

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. E.A. BULAYA]

milioni 30 za Kitanzania. Watuhumiwa hawa walifikishwa Mahakama ya Kisutu na kufunguliwa mashtaka chini ya kifungu 16 (1) (b) (i) cha dawa za kulevya.

Mheshimiwa Spika, katika shauri hili, Hakimu alimwachia huru baada ya mshtakiwa kulipa faini ya shilingi milioni moja za Kitanzania kwa maelezo kwamba kwa kumtazama tu mtuhumiwa, anaonekana ni mgonjwa wa vidonda vya tumbo na hivyo hawezi kupata huduma nzuri iwapo atapelekwa rumande! Hii ni mifano michache tu kati ya mingi iliopo! (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kesi zilizopo Mahakamani. Kama nilivyoainisha hapo juu na ili kuonyesha msisitizo, naomba nirejee takwimu husika kama ifuatavyo, kwamba kati ya watuhumiwa 26,191 waliokamatwa mpaka sasa, kuna jumla ya kesi 89 tu zinazosubiri kusikilizwa Mahakamani. Katika vikao vya Mahakama Kuu vilivyokaa kuanzia mwezi Agosti hadi Oktoba, 2013 hakuna kesi hata moja ya dawa za kulevya iliyosikilizwa na kutolewa hukumu, japo zilikuwa zimepangwa.

Mheshimiwa Spika, dhana ya uhuru wa Mahakama. Natambua kuwa Mahakama ni mhimili unaojitegemea katika kutenda shughuli zake na iko huru. Natambua pia kuwa Bunge haliwezi kuingilia shughuli za Serikali au Mahakama lakini pamoja na uhuru huo, Bunge hili limekuwa linakosoa Serikali pale linapoona imekosea. Kwa ujumla, lazima kuwe na *checks and balance*. Pamoja na upungufu niliyoelezea hapo juu kuhusiana na mwenendo wa Mahakama katika kusikiliza kesi za dawa za kulevya, Mahakama imekuwa inafanya kazi zake bila kukosolewa na chombo kingine na ndio maana baadhi ya watumishi wamekuwa wakitumia dhana ya uhuru wa Mahakama vibaya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kutokana na matumizi mabaya ya uhuru wa Mahakama kwa baadhi ya watumishi wa Mahakama, ni mapendekezo yangu kwamba Serikali iunde Tume Maalumu ya Kiuchunguzi kuchunguza mwenendo wa kesi hizi za dawa za kulevya ili watakaobainika kuwa

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. E.A. BULAYA]

wametumia nafasi/wadhifa/madaraka yao vibaya wachukuliwe hatua za kisheria ikiwa ni pamoja na kuvuliwa madaraka walijonayo. Kwa kufanya hivyo, itaonyesha kuwa hakuna aliye juu ya sheria na itakuwa ni fundisho kwa wengine na taarifa ya Tume iletwi katika Bunge lako Tukufu kwa hatua zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kesi kusikilizwa na Mahakimu wasio na mamlaka. Kwa ujumla watuhumiwa wote wanaokamatwa wakisafirisha dawa za kulevyta hutakiwa kufunguliwa mashtaka chini ya kifungu 16(1)(b)(i) cha Sheria ya Dawa ya Kulevyta. Kosa hili halina dhamana na husikilizwa na Mahakama Kuu peke yake. Hata hivyo baadhi ya Mahakimu wamekuwa wakilisikiliza kesi hizo na wengine kushirikiana na Waendesha Mashtaka hubadilisha Hati ya Mashtaka na kufanya wawe na mamlaka ya kusikiliza kesi hizo. Mfano ni shauri la Jamhuri dhidi ya Shirima (CC 433/2009).

Mheshimiwa Spika, katika shauri hili, mtuhumiwa alikamatwa tarehe 2/05/2009 katika Bandari ya Dar es Salaam akiwa na kilo moja ya *Heroine* yenye thamani ya Tshs.18,000,000/=...Tarehe 5/05/2009 alifikishwa Mahakamanu na kufunguliwa mashtaka chini ya kifungu cha 16(1)(b)(i) cha Sheria ya Dawa ya Kulevyta. Tarehe 9/05/2009 Hati ya Mashtaka ilibadilishwa na mashtaka kuwa chini ya kifungu 12(d) ya Sheria ya Dawa za Kulevyta. Tarehe 14/7/2009 aliamriwa kulipa faini ya Tshs.4, 000,000. Ubadilishwaji wa vifungu vyta sheria katika hati ya mashtaka hulenga kuwasaidia watuhumiwa washtakiwe na makosa madogo badala ya yale makubwa yenye adhabu kubwa kisheria.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 16(1)(b)(i) cha Sheria ya Dawa za Kulevyta kinataja kosa la dawa za kulevyta kuwa kosa ambalo halina dhamana. Hivyo Waendesha Mashtaka kwa kushirikiana na watuhumiwa, hupendelea kuwafungulia mashtaka madogo chini ya kifungu cha 12(d) cha Sheria ya Dawa za Kulevyta. Katika kesi ambazo watuhumiwa walifunguliwa mashtaka chini ya vifungu ambavyo haviendani na makosa yao halisi, Mahakama zimekuwa

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. E A. BULAYA]

zikitoa adhabu ndogo ya faini na kuwaachia huru! Tena katika mazingira mengine, kutoa hukumu ndogo kuliko ambayo imeainishwa katika sheria.

Mheshimiwa Spika, upungufu wa Sheria. Sheria ya Kuzuia Dawa za Kulevyta haina adhabu kwa mtu anayesafirisha au anayekutwa na kemikali bashirifu (*chemical precursors*). Kemikali hizi ni muhimu sana katika kutengeza dawa za kulevyta aina ya *Heroina* na *Cocaine, crystal-methamphetamine*. Muathirika wa dawa *crystal-methamphetamine* hawezu kutibika maishani mwake (*permanent brain damage*). Kwa sasa hivi kuna wimbi kubwa la uingizaji wa kemikali hizo zinazoenda kuangamiza nguvu kazi ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, mionganoni mwa matukio ya uingizaji na usafirishaji wa kemikali hizo ni kesi ya Saada Ally Kilongo aliyejamii wa uwanja wa ndege wa J.K. Nyerere akiwa na 10 kilo za *Ephedrine*. Nyingine ni kesi ya Agnes Gerald Delwaya (Masogange) na mwenzake waliojamii Afrika Kusini wakiwa na kilo 150 za *Ephedrine*. Aidha, Rumishaeli Mamkuu Shoo na mwenzake wamejamii kwenye Kiwanda cha kutengeneza *Ephedrine* nchini Kenya na tayari alikuwa na kilo hamsini (50) za kemikali hizo. Hawa watu licha ya madhara makubwa waliolitelea Taifa, wako mtaani wanapeta na kujipongeza! (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kama hatutarekebisha sheria mapema iwezekanavyo, tutajikuta tunakuwa na kiwanda au viwanda vya kutengeneza dawa za kulevyta hapa nchini. Hivyo, wauzaji badala ya kuagiza dawa hizo nje ya nchi, wataanza kutengeneza hapa na kuna taarifa kwamba pindi dawa za kulevyta zinapokosekana, wafanyabiashara huuza kemikali hizo na watumiaji wanatengeza wenyewe na kutumia.

Mheshimiwa Spika, kutokana na upungufu uliojitekeza kama hoja yangu ilivyoeleza, naomba Serikali ifanye mambo yafuatayo:-

## *Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

[MHE. E.A. BULAYA]

1. Iunde Mahakama Maalum, haraka iwezekanavyo itakayokuwa na jukumu la kushughulikia kesi za dawa za kulevyta tu kama ilivyo Mahakama ya Biashara na iliyokuwa Mahakama ya Ardhi. (*Makofi*)

2. Ifanye marekebisho ya Sheria ya Dawa za Kulevyta kwa kuongeza makosa ya kusafirisha, kuuza au kukutwa na kemikali bashirifu. (*Makofi*)

3. Lundwe Tume ya kuchunguza baadhi ya watendaji wa Mahakama na Serikali ambao kwa makusudi wamekuwa wakihujumu kesi za dawa za kulevyta pamoja na jitihada za Serikali katika kupambana na biashara hii haramu na kuleta taarifa katika Bunge hili Tukufu. (*Makofi*)

4. Kiundwe haraka chombo huru chenye nguvu na mamlaka kamili kitakachokuwa na dhamana ya kupambana na dawa za kulevyta nchini.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

*(Hapa baadhi ya Wabunge walismama kuunga mkono Maelezo Binafsi ya Mheshimiwa Ester A. Bulaya)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Maelezo Binafsi husimami wala hatujadili. Ndiyo ameshajieleza hivyo basi. Someni kifungu kinachohusika, ameshajieleza, ndivyo alivyoomba na amemaliza. (*Makofi*)

Kulikuwa na hoja ya Kuahirisha Bunge na ndiyo ninayowahoji sasa. Hoja ilitolewa na Waziri wa Nchi kuhusu Kuahirisha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)*

**SPIKA:** Hamwezi kulala, hatuna hoja nyingine, naahirisha Bunge mpaka Kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa. 1.35 Usiku Bunge ililahirishwa Mpaka Siku ya Jumanne, Tarehe 5 Novemba, 2013, Saa Tatu Asubuhi)*